# TAATHIRA ZA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE KWA UTHABITI WA KIISIMUJAMII WA LUGHA ZA MAMA MIJINI NAIROBI, KIAMBU NA THIKA: MFANO WA KIKUYU


**NA**

**STEPHEN NJIHIA KAMAU**


**TASNIFU YA UZAMIFU (PhD)**


**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**IDARA YA KISWAHILI**


**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**AGOSTI 2015**

ii

## IKIRARI

**MTAHINIWA:**

Tasnifu hii ya uzamifu ni kazi yangu asilia wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kingine.

**JINA: Stephen Njihia Kamau**

**SAHIHI:** ........................................ **TAREHE:** 4.08.2015

**WASIMAMIZI:**

Tasnifu hii ya uzamifu imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**JINA: Prof: Ireri Mbaabu**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**SAHIHI:** ........................................ **TAREHE:** 17/8/2015

**JINA: Dkt. Peter Karanja**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

**SAHIHI:** ........................................ **TAREHE:** 17/08/15

**TA**

# TABARUKU

Kwa marehemu babangu mzazi.

**Joseph Kamau Mwangi**

## SHUKRANI

Namshukuru Mungu Muumba kwa kunipa neema zake katika kiwango hiki cha masomo yangu na kuniwezesha kuimaliza kazi hii.

Shukrani maalum kwa wasimamizi wangu Prof. Ireri Mbaabu na Dkt. Peter Karanja.

Shukrani zangu za dhati pia ziwaendee wote waliohusika kwa njia moja au nyingine katika kutoa msaada anuai nilipokuwa nikitafiti na kuitayarisha tasnifu hii.

Kwenu nyote, Mungu awabariki.

# YALIYOMO

IKIRARI ..... ii
TABARUKU ..... ii
SHUKRANI ..... iv
YALIYOMO ..... v
ORODHA YA MICHORO ..... xix
ORODHA YA VIAMBATISHO ..... xx
UFAFANUZI WA ISTILAHI ..... xxi
ORODHA YA VIFUPISHO ..... xxii
IKISIRI ..... xxiii
ABSTRACT ..... xxv
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**MSINGI WA UTAFITI ..... 1**
1. 1 Utangulizi ..... 1
1.2 Usuli wa Utafiti ..... 1
1.3 Suala la Utafiti ..... 6
1.3.1 Malengo ya Utafiti ..... 8
1.3.2 Maswali ya Utafiti ..... 9
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ..... 10
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 12
1.6 Msingi wa Nadharia. ..... 15
1.7 Hitimisho ..... 16
**SURA YA PILI ..... 18**
**YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA ..... 18**
2.1 Utangulizi ..... 18

2.2 Maana, Umuhimu, Uimarishaji na Uthabiti wa Lugha za Mama (Kijamii). .......... 19
2.2.1 Asili na Maana ya Lugha ya Mama. .......... 19
2.2.2 Umuhimu wa Lugha za Mama .......... 21
2.2.3 Juhudi za Kuimarisha Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha za Mama. .......... 24
2.2.4 Uimarishaji wa Lugha za Mama kupitia Elimu. .......... 25
2.2.5 Uangamiaji wa Lugha za Mama Nchini Kenya. .......... 30
2.3 Lugha ya Kikuyu .......... 32
2.3.1 Tafiti Kuhusu Lugha ya Kikuyu kwa Jumla .......... 33
2.3.2 Tafiti Kuhusu Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ya Kikuyu. .......... 38
2. 4 Mielekeo ya Lugha .......... 41
2.4.1 Upimaji wa Mielekeo ya Lugha. .......... 44
2.4.2 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha .......... 46
2.4.3 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha Barani Afrika. .......... 47
2.4.4 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha Nchini Kenya .......... 50
2.5 Umilisi wa Lugha .......... 55
2.5.1 Dhana ya Umilisi wa Mawasiliano. .......... 56
2.5.2 Upimaji wa Umilisi wa Mawasiliano. .......... 61
2.5.3 Mitihani ya Umilisi wa Mawasiliano ya Moja kwa Moja. .......... 64
2.5.4 Mitihani ya Umilisi wa Mawasiliano isiyo ya Moja kwa Moja. .......... 65
2.6 Dhana ya vijana .......... 67
2.6.1 Vijana ni akina nani? .......... 68
2.6.2 Vijana na Matumizi ya Lugha Mijini Barani Afrika. .......... 73
2.7 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Nchini Kenya. .......... 75
2.8 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Mijini Nchini Kenya. .......... 79
2.8.1 Ruwaza za Matumizi ya Lugha za Mama nchini Kenya .......... 80

2.8.2 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha za Mama Nchini Kenya ..................................... 82

2.8.3 Lugha ya Kiswahili ........................................................................................ 83

2.8.4 Ruwaza za Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya ...................................................... 85

2.8.5 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya ............................... 87

2.8.6 Lugha ya Kiingereza ........................................................................................ 88

2.8.7 Ruwaza za Matumizi ya Kiingereza nchini Kenya ..................................................... 89

2.8.8 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha ya Kiingereza Nchini Kenya ............................. 90

2.8.9 Lugha Msimbo ya Sheng ................................................................................ 91

2.8.10 Ruwaza za Matumizi ya Sheng nchini Kenya.......................................................... 92

2.8.11 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha ya Sheng Nchini Kenya .................................. 93

2.9 Hitimisho ........................................................................................................ 95

**SURA YA TATU ........................................................................................ 96**

**MSINGI WA NADHARIA NA MAELEZO YA KINADHARIA KUHUSU UTHABITI WA LUGHA ........................................................................ 96**

3.1 Utangulizi ........................................................................................................ 96

3.2 Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha. ................................................. 96

3.2.1 Umbali wa Jamii Lugha kutoka kwa ama Vijiji au Miji. ............................................ 97

3.2.2 Maeneo ya Kijamii ambamo Lugha inatumiwa na Wanajamii Lugha.......................... 98

3.2.3 Viwango na Aina ya Uhamishaji Msimbo. ................................................................ 99

3.2.4 Idadi ya Wanajamii Lugha Wanaozungumza Lugha Husika. .................................... 100

3.2.5 Mtawanyiko wa Wazungumzaji Lugha katika Mtandao wao wa Kijamii. ................. 101

3.2.6 Mtazamo wa Kijamii wa Wanajamii Lugha na Wanajamii Wengine Kuhusu Lugha Husika. ................................................................................................ 101

3.2.7 Hadhi ya Lugha katika Jamii. ................................................................................ 102

3.2.8 Msingi Imara na Halali wa Kiuchumi wa Jamii Lugha. ........................................... 103

3.3 Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa. ...................... 104

3.4 Maelezo ya Kinadharia kuhusu Uthabiti wa Lugha katika Mazingira ya Ulumbi 109

3.4.1 Vigezo vya Upokezanaji Lugha Baina ya Vizazi. .................................................. 113

3.4.2 Vigezo vya Kubaini Uthabiti wa Lugha vya Ethnologue (2000).............................. 116

3.4.3 Vigezo vya Kupima ama Viwango vya Uthabiti au Uangamiaji wa Lugha vya UNESCO. ........................................................................................................ 117

3.4.4 Vigezo vya Upokezanaji Lugha Baina ya Vizazi Vilivyopanuliwa.......................... 118

3.5 Lugha za Mama katika Mazingira ya Wingilugha: Dhana ya Diglosia na Triglosia…........................................................................................ 124

3.5.1 Dhana ya Diglosia.................................................................................................. 125

3.5.2 Dhana ya Triglosia.................................................................................................. 127

3.6 Hitimisho........................................................................................................ 128

**SURA YA NNE........................................................................................ 130**

**MBINU ZA UTAFITI.............................................................................. 130**

4.1 Utangulizi........................................................................................................ 130

4.2 Muundo wa Utafiti ......................................................................................... 130

4.3 Mbinu Changamano ya Utafiti......................................................................... 131

4.3.1 Faida za Mbinu Changamano ya Utafiti ................................................................. 134

4.3.2 Udhaifu wa Mbinu changamano ya Utafiti............................................................. 135

4.3.3 Mpangilio Sambamba wa Mbinu Changamano ya Utafiti....................................... 137

4.4 Mahala pa Utafiti............................................................................................. 137

4.4.1 Maelezo kuhusu Jiji la Nairobi .............................................................................. 139

4.4.2 Maelezo kuhusu Mji wa Kiambu........................................................................... 140

4.4.3 Maelezo kuhusu Mji wa Thika................................................................................ 142

4.5 Jumuiya Lengwa ............................................................................................. 143

4.6 Vigezo vya Kuteua Sampuli............................................................................ 144

4.7 Idadi ya Sampuli ........ 148

4.7.1 Mchakato wa Kuteua Idadi ya Sampuli ........ 150

4.8 Vifaa vya Utafiti ........ 152

4.8.1 Hojaji za Matumizi na Mielekeo ya Lugha ........ 152

4.8.2 Mijadala ya Kimakundi ........ 153

4.8.3 Mazoezi ya Uandishi na Usomaji ........ 154

4.8.4 Vigezo vya Kupima Umilisi. ........ 155

4.9 Utafiti Awali ........ 156

4.9.1 Uhalali ........ 157

4.9.2 Utegemevu ........ 158

4.10 Utaratibu wa Kukusanya Data ........ 159

4.11 Uchanganuzi wa Data ........ 160

4.12 Uwasilishaji wa Data ........ 162

4.13 Hitimisho ........ 162

**SURA YA TANO ........ 163**

**UWASILISHAJI WA DATA ........ 163**

5.1 Utangulizi ........ 163

5.2 Mielekeo ya Vijana Mijini Kuhusu Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. ........ 163

5.3 Uchanganuzi wa Data ya Kibinafsi ya Wahojiwa ........ 164

5.3.1 Kidato cha Wahojiwa ........ 164

5.3.2 Umri wa Wahojiwa. ........ 165

5.3.3 Jinsia ya Wahojiwa. ........ 166

5.4 Mielekeo ya Lugha kuhusu Shughuli Mbalimbali za Kijamii. ........ 167

5.4. 1 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kupata Elimu au Mafunzo Shuleni. ........ 167

5.4.2 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu katika Shughuli za Biashara......... 168

5.4.3 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu katika Kupata Kazi za Kitaaluma baada ya Shule. ........................................................................................... 170

5.4.4 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuzungumza na Wazazi na Watu Wazima Nyumbani.......................................................................... 171

5.4.5 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuzungumza na Wenzao Mijini.............................................................................................................. 172

5.4.6 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kutangamana Mijini........ 173

5.4.7 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuwasiliana Nyumbani. .. 174

5.4.8 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kufahamu Utamaduni. .... 175

5.5 Mielekeo Zaidi ya Vijana Mijini Kuhusu Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng Kupitia Mizani ya Likati. ........................................................................ 176

5.5.1 Ni Muhumu kwa Vijana Kufahamu Lugha ya Kikuyu............................................. 178

5.5.2 Sababu za Vijana Mijini Kufahamu au Kutofahamu Lugha ya Kikuyu. .................... 179

5.5.3 Kikuyu Hutumika Nyumbani Kwetu Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng .......... 181

5.5.4 Sababu za Vijana Mijini za Kutumia Kikuyu Nyumbani Kwao Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng. ......................................................................................... 183

5.5.5 Hatutumii Kikuyu hata Kidogo Shuleni.................................................................... 186

5.5.6 Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Shuleni. ................................................. 188

5.5.7 Ni Muhimu Kufahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu. ................. 190

5.5.8 Sababu za Kufahamu au Kutofahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu192

5.5.9 Nahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu .................................................. 193

5.5.10 Sababu za Kuwahurumia au Kutowahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu.195

5.5.11 Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu Kuliko wale Wanaozungumza Kikuyu. ................................................................. 197

5.5.12 Sababu za Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuwa naHadhi ya Juu Kuliko wale Wanaozungumza Kikuyu Mijini................................................. 199

5.5.13 Kuna Wenzangu ambao Hawakipendi Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha zaKiswahili, Kiingereza au Sheng ..... 201

5.5.14 Sababu za Vijana Wengine Kutokipenda Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng ..... 202

5.6 Maeneo ya Matumizi ya Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana Mijini. ..... 205

5.6.1 Kidato cha Wahojiwa. ..... 205

5.6.2 Umri wa Wahojiwa ..... 206

5.6.3 Jinsia ya Wahojiwa ..... 206

5.7 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha. ..... 207

5.7.1. Lugha Unayoitumia Unapozumgumza na Marafiki Zako Darasani pale Shuleni ..... 207

5.7.2 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki Zako Nje ya Darasa Shuleni. ..... 208

5.7.3 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Walimu Darasani ..... 209

5.7.4 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Wafanyakazi Shuleni ..... 209

5.7.5 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki zako Nyumbani ..... 210

5.7.6 Lugha Unayoitumia Unapowazungumzia Wazazi Wako Nyumbani ..... 211

5.7.7 Lugha Wanayoitumia Wazazi Wanapokuzungumzia Nyumbani ..... 212

5.7.8 Lugha ambayo Wazazi Wako Wanatumia Wanapowasiliana Nyumbani ..... 212

5.7.9 Lugha Unayoitumia Unapozungumzia Watu Wazima Mtaani ..... 213

5.7.10 Lugha Wanayoitumia Watu Wazima Wanapokuzungumzia Mtaani. ..... 214

5.7.11 Lugha Unayoitumia Unapomzungumzia Babu au Nyanya Yako. ..... 215

5.7.12 Lugha Anayoitumia Nyanya au Babu Anapokuzungumzia ..... 215

5.7.13 Watoto Kwanza Hujifunza Lugha Gani Mtaani ..... 216

5.7.14 Lugha Inayotumiwa Kuhubiri Kanisani au Msikitini Nyumbani ..... 217

5.8 Umilisi wa Lugha Miongoni mwa Vijana Mijini. ..... 217

5.8.1 Kuandika kwa Kikuyu. ..... 218

5.8.2 Kusoma kwa Kikuyu. 219

5.8.3 Kuongea kwa Kikuyu 220

5.8.4 Kuandika kwa Kiswahili. 221

5.8.5 Kusoma kwa Kiswahili. 221

5.8.6 Kuongea kwa Kiswahili 222

5.8.7 Kuandika kwa Kiingereza. 223

5.8.8 Kusoma kwa Kiingereza. 224

5.8.9 Kuongea kwa Kiingereza 225

5.8.10 Kuandika kwa Sheng. 226

5.8.11 Kusoma kwa Sheng. 227

5.8.12 Kuongea kwa Sheng 228

5.8.13 Ulinganisho wa Viwango vya Umilisi katika Miji ya Nairobi, Kiambu na Thika 229

5.9 Hitimisho. 233

**SURA YA SITA 234**

**MIJADALA KUTOKANA NA DATA YA KIJARABATI NA KIMAELEZO 234**

6.1 Utangulizi 234

6.2 Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. 235

6.2.1 Mielekeo Kuhusu Lugha za Kufundishia Shuleni. 237

6.2.2 Mielekeo Kuhusu Lugha za Kufanyia Biashara. 240

6.2.3 Mielekeo Kuhusu Lugha ya Kutafuta Kazi za Kitaaluma Baada ya Masomo. 242

6.2.4 Mielekeo Kuhusu Lugha za Mawasiliano Mitaani na Nyumbani Baina ya Vijana na Wazazi na Baina ya Vijana Wenyewe. 244

6.2.5 Mielekeo Kuhusu Lugha iliyo na Hadhi Kimatumizi Miongoni mwa Vijana Mijini. 246

6.2.6 Mielekeo ya Kijumla Kuhusu Lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa Vijana Mijini. 249

6.2.7 Mielekeo Chanya Kuhusu Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana Mijini. ............. 251

6.2.8 Hitimisho kuhusu Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu Lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. ........................... 253

6.3 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika . ..........................................................................................................255

6.3.1 Miktadha Mbalimbali ya Matumizi ya Lugha katika Eneo la Kijamii la Shuleni. ..... 255

6.3.1.1 Lugha ya Mawasiliano Darasani................................................................ 256

6.3.1.2 Lugha ya Mawasiliano Nje ya Darasa. ...................................................... 257

6.3.2 Miktadha Mbalimbali ya Matumizi ya Lugha katika Eneo la Kijamii la Nyumbani.. 258

6.3.2.1 Lugha ya Mawasiliano Miongoni mwa Vijana katika Kiwango cha Familia. ......... 259

6.3.2.2 Lugha ya Mawasiliano Miongoni mwa Wazazi na Vijana Nyumbani. .................. 259

6.4 Umilisi wa Lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ........................... 260

6.4.1 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ............................................................. 262

6.4.2 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kiswahili Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ................................................................ 264

6.4.3 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kiingereza Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ............................................................... 265

6.4.4 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ............................................................. 266

6.4.5 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.268

6.5 Viwango vya uthabiti wa Kiisimujamii na hali ya Kijumla ya Kiisimujamii ya Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika. ....................................................................................... 269

6.6 Hitimisho...................................................................................................... 273

**SURA YA SABA ........................................................................................ 275**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.......................................... 275**

7.1 Utangulizi ........ 275
7.2 Muhtasari wa Kila Sura ........ 275
7.3 Hitimisho ........ 280
7.3.1 Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini kuhusu Lugha ya Kikuyu. ........ 281
7.3.2 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii yaKikuyu ........ 283
7.3.3 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha Miongoni mwa Vijana wa Jamii yaKikuyu Mijini ........ 284
7.3.4 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini ........ 285
7.4 Mapendekezo ........ 285
7.4.1 Uimarishaji wa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha. ........ 286
7.4.2 Juhudi za Uimarishaji wa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha. ........ 287
7.4.2.1 Matumizi ya Lugha ya Kikuyu katika Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha. 287
7.4.2.2 Uhusiano wa Vijana wa Mijini na jamii za Mashambani. ........ 290
7.4.2.3 Miradi ya kufundisha Vijana wa Mijini Lugha ya Kikuyu. ........ 290
7.4.2.4 Nafasi ya Serikali za Kaunti katika Kukuza Lugha za Mama. ........ 291
7.5 Tamati ........ 293
Marejeleo ........ 294
Viambatisho ........ 308
Kiambatisho I ........ 308
UMILISI WA LUGHA ........ 308
Kiambatisho II ........ 309
MAZOEZI YA KUPIMA UMILISI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUONGEA ........ 309
Kiambatisho III ........ 310
HOJAJI YA WANAFUNZI KUHUSU MIELEKEO NA MATUMIZI YA LUGHA. ........ 310

Kiambatisho IV ........................................................................................................ 313

HOJAJI YA WANAFUNZI KUHUSU MAENEO YA KIJAMII YA MATUMIZI YA LUGHA. ........................................................................................................ 313

Kiambatisho V........................................................................................................ 315

MJADALA WA KIMAKUNDI ........................................................................................ 315

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali 1: Fasili ya Lugha ya Mama........................................................................ 21

Jedwali 2: Umri wa Vijana kwa Mujibu wa Mashirika Mbalimbali Ulimwenguni. 72

Jedwali 3: Makundi ya Lugha Nchini Kenya........................................................... 77

Jedwali 4: Vigezo vya GIDS....................................................................................... 115

Jedwali 5: Vigezo vya Uthabiti wa Lugha vya Ethnologue (2000)......................... 116

Jedwali 6: Vigezo vya EGIDS..................................................................................... 120

Jedwali 7: Jumuiya ya Utafiti....................................................................................... 144

Jedwali 8: Mgawanyiko wa Shule katika Eneo la Utafiti…………………………148

Jedwali 9: Umri wa Wahojiwa...................................................................................... 165

Jedwali 10: Lugha iliyo Muhimu katika Kupata Elimu au Mafunzo Shuleni............ 167

Jedwali 11: Lugha iliyo Muhimu katika Shughuli za Biashara................................ 169

Jedwali 12: Lugha iliyo Muhimu Kupata Kazi ya Kitaaluma Baada ya Shule.......... 170

Jedwali 13: Lugha iliyo Muhimu katika Kuzungumza na Wazazi na Watu Wazima Nyumbani na Mitaani.............................................................................. 171

Jedwali 14: Lugha iliyo Muhimu katika Kuzungumza na Wenzako Mijini.............. 172

Jedwali 15: Lugha iliyo Muhimu katika Kufanya Urafiki Mijini.............................. 173

Jedwali 16: Lugha iliyo Muhimu katika Kuwasiliana nayo Nyumbani .................... 174

Jedwali 17: Lugha iliyo Muhimu Kufahamu kuhusu Utamaduni Wako................... 175

Jedwali 18: Sababu za Kuwepo ama Kutokwepo Umuhimu wa Kufahamu Kikuyu. 180

Jedwali 19: Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Nyumbani........................... 184

Jedwali 20: Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Shuleni..............................  188

Jedwali 21: Sababu za Kufahamu au Kutofahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuliko Kikuyu.......................................................................................... 192

Jedwali 22: Sababu za Kuwahurumia au Kutowahurumia Vijana Wasiofahamu Kikuyu ……………………………….……………………………..195

Jedwali 23: Sababu za Kuunga au Kupinga Suala kuwa Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu kuliko Wanaozungumza Kikuyu……………………………….……………199

Jedwali 24: Sababu za Vijana Wengine Kutokipenda Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng............................................ 203

Jedwali 25: Umri wa Wahojiwa.................................................................................. 206

Jedwali 26: Lugha Unayoitumia Unapozumgumza na Marafiki Darasani pale Shuleni ............................................................................................................ 207

Jedwali 27: Lugha Unayozungumza na Marafiki Zako Nje ya Darasa pale Shuleni. 208

Jedwali 28: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Walimu Darasani.................. 209

Jedwali 29: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Wafanyakazi Shuleni............ 210

Jedwali 30: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na marafiki zako Nyumbani........211

Jedwali 31: Lugha Unayoitumia Unapozungumzia Wazazi Nyumbani....................211

Jedwali 32: Lugha Wanayoitumia Wazazi Wanapokuzungumzia Nyumbani........... 212

Jedwali 33: Lugha ambayo Wazazi Wako Wanaitumia Wanapowasiliana Nyumbani……………………………………………………….213

Jedwali 34: Lugha Unayoitumia Unapozungumzia Watu Wazima Mtaani............... 213

Jedwali 35: Lugha Wanayoitumia Watu Wazima Wanapokuzungumzia Mtaani...... 214

Jedwali 36: Lugha Uanayoitumia Unapomzungumzia Babu au Nyanya Yako........ 215

Jedwali 37: Lugha Anayoitumia Nyanya au Babu Anapokuzungumzia................... 216

Jedwali 38: Watoto Hujifunza Lugha gani Kwanza pale Mtaani.............................. 216

Jedwali 39: Lugha Mnayoitumia Mnapoenda Kanisani au Msikitini pale Nyumbani ……………………………………………………………………………..217

Jedwali 40: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Kikuyu......................................... 219

Jedwali 41: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kikuyu............................................ 219

Jedwali 42: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kikuyu.......................................... 220

Jedwali 43: Matokeo ya Stadi ya kuandika kwa Kiswahili....................................... 221

Jedwali 44: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kiswahili........................................ 222

Jedwali 45: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kiswahili....................................... 223

Jedwali 46: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Kiingereza.................................... 224

Jedwali 47: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kiingereza...................................... 225

Jedwali 48: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kiingereza..................................... 225

Jedwali 49: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Sheng........................................... 227

Jedwali 50: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Sheng.............................................. 227

Jedwali 51: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Sheng............................................ 228

Jedwali 52: Viwango vya Umilisi wa Lugha Jijini Nairobi.......................................230

Jedwali 53: Viwango vya Umilisi wa Lugha Mjini Kiambu.................................... 231

Jedwali 54: Viwango vya Umilisi wa Lugha Mjini Thika........................................ 232

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1: Vijenzi vya Mielekeo.................................................................................. 42

Mchoro 2: Ramani ya Jamii za Kiasili na Lugha zao Nchi Kenya............................. 78

Mchoro 3: Mpangilio wa Nadharia ya Vitendo Vilivyopangwa............................. 107

Mchoro 4: Utaratibu wa Vitendo katika Uchaguzi wa Lugha................................. 108

Mchoro 5: Mpangilio Sambamba wa Mbinu Changamano ya Utafiti................... 137

Mchoro 6: Kidato cha Wahojiwa.............................................................................. 164

Mchoro 7: Jinsia ya Wahojiwa.................................................................................. 166

Mchoro 8: Ni Muhumu kwa Vijana Kufahamu Lugha ya Kikuyu.......................... 178

Mchoro 9: Kikuyu Hutumika Nyumbani Kwetu Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng........................................................................................................182

Mchoro 10: Hatutumii Kikuyu hata Kidogo Shuleni................................................ 187

Mchoro 11: Ni Muhimu Kufahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuliko Kikuyu……………………………………………………………..……190

Mchoro 12: Nahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu................................ 194

Mchoro 13: Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu Kuliko Wale Wanaozungumza Kikuyu........................................... 197

Mchoro 14: Kuna Wenzangu ambao Hawakipendi Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili,Kiingereza au Sheng......................................................... 201

Mchoro 15: Kidato cha Wahojiwa.............................................................................. 205

Mchoro 16: Jinsia ya Wahojiwa.................................................................................. 206

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Mwongozo wa Maswali ya Mijadala ya Kimakundi................. 308

Kiambatisho II: Mazoezi ya Kupima Umilisi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuongea………......................................................................... 309

Kiambatisho III: Hojaji ya Wanafunzi kuhusu Mielekeo na Matumizi ya Lugha. 310

Kiambatisho IV Hojaji ya Wanafunzi kuhusu Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha...........................................………........................... 313

Kiambatisho V Mjadala wa Kimakundi ........................................................... 315

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Asilimia | - Idadi Kamili kutoka kwa Mia Moja. |
| Mirudio | - Urudufu wa Visa |
| Mizani ya Likati | - Mizani ya kupima mielekeo ya lugha. |
| Mwelekeo chanya wa lugha | -Hali ya kuipenda lugha |
| Mwelekeo hasi wa lugha | - Hali ya kutoipenda lugha |
| Sheng | - Ni msimbo ambao hutumiwa hasa na vijana katika sehemu za mijini kama vile Nairobi. Sheng haijapewa utambuzi rasmi nchini Kenya na katika utafiti huu inatumika kwa maana ya msimbo wa vijana mjini wala sio kama lugha halisi. |
| Upeo chini | - Alama ya Chini Miongoni mwa Visa Vyote |
| Upeo juu | - Alama ya Juu Miongoni mwa Visa Vyote |
| Uthabiti wa Kiisimujamii | - Dhana hii katika utafiti huu imetumika kurejelea ile hali ya wazungumzaji wa lugha kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha yao. |
| Uwililugha | - Matumizi ya lugha mbili na mtu binafsi ama jamii |
| Wastani | - Alama ya Kati |
| Wingilugha | -Matumizi ya lugha mbili au zaidi na mtu binafsi au jamii |

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| EGIDS | - | Extended Graded Intergenerational Disruption Scale. |
| GIDS | - | Graded Intergenerational Disruption Scale. |
| KIE | - | Kenya Institute of Education. |
| KNBS | - | Kenya National Bureau of Statistics. |
| $L_1$ | - | Lugha ya kwanza. |
| $L_2$ | - | Lugha ya pili. |
| SPSS | - | Statistical Package for the Social Sciences. |
| UNESCO | - | United Nations Education Scientific and Cultural Organization. |

## IKISIRI

Utafiti huu ni wa kiisimujamii ulioangazia suala la mtagusano wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Utafiti wenyewe umejikita katika kuchunguza iwapo lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zinaathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Lugha ya Kikuyu huonekana kama lugha iliyo na viwango vya juu vya uthabiti wa kiisimujamii kutokana na idadi yake kubwa ya wazungumzaji nchini Kenya. Hata hivyo, huenda lugha hii si thabiti katika mazingira mengine kama yale ya mijini miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu, ambako kuna hali ya mtagusano wa lugha na wingilugha. Utafiti huu umetathmini athari za lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kupitia stadi za lugha za kuongea, kusoma na kuandika kama nyenzo ya kubaini uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Data ya utafiti huu ilikusanywa nyanjani miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa kutumia mtindo wa mbinu changamano ya utafiti. Mtindo wa mbinu changamano ya utafiti unahusu matumizi ya mbinu za kimaelezo na kijarabati kwa pamoja katika utafiti mmoja. Tulitumia hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha na mijadala ya kimakundi ili kubaini mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.  Aidha, vijana hawa walihusishwa katika mazoezi ya kuongea, kuandika na kusoma katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ili kubaini viwango vyao vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Data ya utafiti huu ilichanganuliwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia za Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na nadharia ya Vitendo Vilivyopangwa na Vitendo Vilivyofikiriwa. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kupitia njia za maelezo, majedwali na chati ili kuweka wazi viwango vya umilisi wa Kikuyu walio nao vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Utafiti huu uliweza kubaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu. Kutokana na mielekeo hasi na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu, utafiti huu ulibaini kuwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu ni vya chini ikilinganishwa na viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Aidha, utafiti huu ulizua tasnifu kuwa kuna mpangilio mpya wa matumizi ya lugha kitriglosia miongoni mwa vijana mijini unaohusisha lugha za Kiingereza, Kiswahili na Sheng huku lugha za mama kama vile Kikuyu zikitengwa na basi kuziweka katika hatari ya kuanza kuangamia. Utafiti huu ni muhimu katika uwanja wa isimujamii kwa

vile umetambulisha hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Tunatarajia kuwa matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika kuanzisha shughuli za kuimarisha na kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama kwa jumla miongoni mwa vijana mijini nchini Kenya.

## ABSTRACT

This is a sociolinguistic study that focused on the language contact situation between Kikuyu, Kiswahili, English and Sheng among Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika towns. The study aimed at investigating whether Kiswahili, English and Sheng languages might be affecting the ethnolinguistic vitality of Kikuyu language among the Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika towns. Kikuyu language seems to have high ethnolinguistic vitality due to its large number of speakers in Kenya. However, maybe Kikuyu language lacks sociolinguistic vitality in some areas like the urban regions among the Kikuyu youth, where language contact and bilingualism situations exists. This study investigated the effects of Kiswahili, English and sheng on the levels of Kikuyu ethnolinguistic vitality among the Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika towns based on the speaking, reading and writing language skills as a means of determining Kikuyu ethnolinguistic vitality. The data for the study was collected from the Kikuyu youth living in Nairobi, Kiambu and Thika towns using the mixed research design. Mixed research design uses both quantitative and qualitative data collection and analysis methods in the same research. Language use and attitude questionnaires and focused group discussions were used to indentify the attitudes of Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika towns towards Kikuyu language in comparision with Kiswahili, English and Sheng languages. The study also engaged the Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika in speaking, reading and writing language skills competence tests to determine their level of linguistic competency in Kikuyu, Kiswahili, English and Sheng languages. The collected data was analyzed in line with the research objectives guided by the ethnolinguistic vitality and planned action and reasoned action language theories tenents. The results of the analyzed data was presented in a descriptive and statistical way using explanations, summary tables and charts so as to show clearly the levels of Kikuyu competency among the Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika. This study was able to establish that Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika have a negative attitude and low levels of linguistic competence in Kikuyu language. Due to the negative attitude and low linguistic competence in the Kikuyu languge, this study discovered that the levels of ethnolinguistic vitality of Kikuyu language compared to the levels of ethnolingustic vitality of Kiswahili, English and Sheng among Kikuyu youth in Nairobi, Kiambu and Thika is low. This study argues that there is a new triglosia order of language use among the urban youth that involves the use of English, Kiswahili and Sheng while sidelining mother tongues like Kikuyu and thus exposing them to the onset of their endangerment. This study is important in the sociolinguistics field as it gives a good analysis of Kikuyu sociolinguistic situation among the urban youth and especially its ethnolinguistic vitality. The findings of this research are expected to be of importance in the revitalization and maintenance of mother tongues among the urban youth in Kenya.

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1. 1 Utangulizi

Sura ya kwanza ina maelezo kuhusu usuli wa utafiti kwa jumla ambapo suala la mtugasano wa lugha na baadhi ya athari zake zimefafanuliwa. Pia, sura hii imeweka wazi suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Hatimaye, sura hii imegusia kuhusu nadharia zilizouongoza utafiti na ambazo zimejadiliwa kwa kina katika sura ya 4.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Tasnifu hii inahusu athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Lengo moja kuu la utafiti huu lilikuwa kubaini jinsi mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng inavyoathiri umilisi wao wa lugha za mama kama vile Kikuyu. Aidha, utafiti huu pia ulilenga kubaini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambako kuna hali ya wingilugha na mtagusano wa lugha mbalimbali.

Sehemu hii ya utafiti imelifafanua suala la mtagusano wa lugha kwa kina ili kuonyesha matokeo mbalimbali ya mtagusano wa lugha kama vile uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ambalo ni suala la kimsingi lililochunguzwa katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu, kama asemavyo Craystal (2010), mtagusano wa lugha ndicho chanzo mojawapo cha mielekeo

tofauti ya lugha miongoni mwa wazungumzaji ambapo nayo mielekeo ya lugha huathiri viwango vya umilisi wa lugha miongoni mwa wazungumzaji kama utafiti huu ulivyodhihirisha.

Mtagusano wa lugha hutokea pale ambapo lugha mbili au zaidi zinapoingiliana kimatumizi. Kwa mujibu wa Kremnitz na wenzake (1997:23), "mtagusano wa lugha kama hali ambayo hutokea wakati lugha mbili au zaidi zinaingiliana kimatumizi katika taifa moja na pale ambapo mzungumzaji anachagua, kutoka kwa lugha hizi tofauti, lugha ya matumizi katika mazingira maalum". Aidha, Thomason (2005) anaeleza kuwa mtagusano wa lugha ni ile hali ya matumizi ya lugha zaidi ya moja katika eneo moja kwa wakati mmoja. Naye Crystal (2010:17) anasema kuwa "katika ulimwengu ambao una takriban lugha elfu tano, mtagusano wa lugha hauna budi kutokea katika kiwango cha kitaifa na kijamii" na kwa hivyo kama asemavyo Sankoff (2001) mtagusano wa lugha umekuwa sehemu ya maisha ya kijamii ya kila siku kwa mamia ya mamilioni ya watu ulimwenguni kote.

Frawley (2003:5) anasema kuwa "mtagusano wa lugha katika jamii huibua hali ya uwililugha na wingilugha yaani yale matumizi ya lugha mbili au zaidi". Eneo la utafiti huu lilikuwa miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ambako kuna hali ya wingilugha. Hii ni kwa sababu katika miji hii mitatu kuna matumizi ya lugha mbalimbali zinazozungumzwa nchini Kenya. Baadhi ya lugha zinazozungumzwa katika miji hii mitatu ni lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu ulijihusisha na uchunguzi wa kina wa jinsi lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zinavyoathiri umilisi wa lugha ya

Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Lengo kuu lilikuwa kuweza hatimaye kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini katika mazingira ya wingilugha.

Frawley (2003:8) anasema kuwa "uwililugha ni ule uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi katika mawasiliano". Kwa mujibu wa Crystal (2010:25), "mojawapo ya matokeo yasiyoepukika ya mtagusano wa lugha ni hali ya wingilugha na ambayo hujitokeza katika kiwango cha mzungumzaji binafsi kama uwililugha". Crystal anafafanua zaidi kuwa dhana ya uwililugha imeenea sana katika jamii za sasa ikilinganishwa na jamii za zamani. Hali ya kuenea kwa uwililugha imetokana na athari za teknolojia ya kisasa ya mawasiliano, elimu ya sasa na uhamaji wa watu kutoka eneo moja hadi lingine kati ya sababu nyingine. Hatimaye, maenezi haya ya wingilugha huwa na athari kadhaa mojawapo ya athari hizi ikiwa uibukaji wa mielekeo ya lugha".

Katika mazingira ya wingilugha, kama asemavyo Batibo (2005), kunayo mazoea ya kuchipuka kwa mielekeo tofauti kuhusu kila mojawapo ya lugha zinazotumika katika jamii ile. Suala la mielekeo ya lugha basi ni la kimsingi katika jamii zenye wingilugha na hasa athari za mielekeo hii kwa umilisi wa lugha hizi husika. Kartz (1960:48) anaelezea mielekeo ya lugha kuwa "ile hali ya mtu kuipenda au kuichukia lugha. Kartz anaendelea kufafanua kuwa "mielekeo ya lugha ni kule kupenda au kutoipenda lugha fulani unapokabiliwa na mazingira ambamo kuna mtagusano wa lugha na basi hali ya wingilugha". Akilifafanua zaidi suala hili la mielekeo ya lugha, Baker (1992:43) anarai kuwa "wazungumzaji wa lugha wanaweza kuwa na mielekeo chanya (kule kuipenda)

ama mielekeo hasi (kule kutoipenda) kuhusu lugha yao”. Aidha, Ajzen na Fishbein (2005:52) wanasema kuwa mielekeo chanya au hasi kuhusu lugha ndiyo sababu moja ambayo hufanya wazungumzaji wa lugha kuwa na viwango tofauti vya umilisi wa lugha husika.

Bussman (1996:54) ana maoni kuwa “mielekeo ya lugha huwa na athari za moja kwa moja kwa umilisi wa lugha husika yaani mzungumzaji anaweza kuwa na viwango vya juu au vya chini vya umilisi wa lugha kutegemea jinsi anavyoipenda au kutoipenda lugha”. Crystal (2010:45) anaeleza kuwa “katika mazingira ya wingilugha, wazungumzaji wa lugha huonyesha viwango tofauti vya umilisi wa lugha zinazotumiwa au idadi kubwa ya wazungumzaji wenye uwililugha huwa hawana umilisi sawa wa lugha zile mbili. Mzungumzaji huwa na ufasaha na umilisi zaidi katika lugha anayoipendelea zaidi kwa vile lugha hii ndiyo lugha anayoitumia kwa wingi katika maeneo mengi ya kijamii ya matumizi ya lugha”. Basi inatokea kuwa, katika hali ya wingilugha, watumiaji lugha hawana budi kuchagua, baina ya lugha nyingi, lugha watakayoitumia katika maeneo mbalimbali ya kijamii ya matumizi ya lugha katika jamii yao. Uchaguzi huu hudhibitiwa na mielekeo walio nayo wazungumzaji kuhusu lugha mbalimbali katika jamii yao. Mielekeo ya lugha nayo huwa na athari kwa umilisi wa lugha husika katika jamii.

Mielekeo ya lugha vile vile huathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha nyingi za mama hata zile zilizo na idadi kubwa ya wazungumzaji. Kwa mujibu wa Landweer (2000), kuna lugha nyingi za mama ambazo zina idadi kubwa ya wazungumzaji na hivyo huonekana

kama lugha thabiti. Hata hivyo, lugha hizi zinapochunguzwa kwa makini huwa si thabiti kwa vile, kutokana na mielekeo ya wazungumzaji wake, wazungumzaji hawa huwa wamechagua kuzitumia lugha nyingine katika jamii yao wanazoziona kuwa na hadhi zaidi ya ile lugha yao na hivyo kupungukiwa na umilisi wa lugha zao.

Mfano mzuri wa lugha kubwa iliyokabiriwa na hatari ya kungamia ni lugha ya Yoruba nchini Nigeria. Brenzinger (1998:23) anaeleza kuwa "lugha ya Yoruba ikiwa na zaidi ya wazungumzaji milioni 20 imo katika orodha ya lugha zilizo katika hatari ya kuangamia kutokana na ushindani mkubwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza hasa katika sekta ya elimu". Kama wasemavyo Fabummi na Salawu (2005:392-393), "lugha ya Yoruba licha ya kuwa mojawapo ya lugha yenye wazungumzaji wengi nchini Nigeria, ikizungumzwa na asilimia 35 ya watu na vile vile ikizungumzwa katika mataifa ya Togo, Benin, Ghana, Siera Leone na Ivory Coast, bado imekabiliwa na hatari ya kuangamia kutokana na ushindani wa lugha za matumizi mapana kama vile Kiingereza". Mfano huu wa Yoruba unaonyesha kuwa kuna uwezekano wa lugha zenye wazungumazaji wengi duniani kuwa katika hatua mbalimbali za uangamiaji pindi wakati unavyopita licha ya kuzungumzwa na idadi kubwa ya watu.

Makisio yaliyoongoza utafiti huu ni kuwa licha ya Kikuyu kuwa ndio lugha iliyo na wazungumzaji wengi zaidi nchini Kenya ikiwa na wazungumzaji takriban milioni 6.6 (KNBS 2010) na ambayo ni kama asilimia 22 ya idadi yote ya watu nchini Kenya, huenda lugha hii inaanza kupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii miongoni mwa vijana

wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kutokana na ushindani wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Sehemu hii ilijihusisha na maelezo kuhusu mtagusano wa lugha katika jamii na matokeo mbalimbali ya mtagusano wa lugha. Baadhi ya matokeo ya mtagusano wa lugha ni mielekeo ya lugha ambako wazungumzaji wanaweza wakawa na mielekeo chanya au hasi kuhusu lugha. Mielekeo chanya na hasi kuhusu lugha nayo kwa upande wake huathiri viwango vya umilisi wa lugha vya mzungumzaji. Lugha zilizoangaziwa katika utafiti huu ni lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu ulichunguza jinsi mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng inavyoathiri umilisi wao wa lugha ya Kikuyu na hatimaye kutatiza uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu mijini.

**1.3 Suala la Utafiti**

Nchini Kenya kuna mtagusano wa lugha ambao umeleta hali ya wingilugha. Hii ni kwa sababu kuna lugha mbalimbali zinazotumiwa katika mawasiliano. Lugha hizi pia zimepewa majukumu tofauti yanayozifanya kuwa na hadhi mbalimbali hapa nchini Kenya. Kuna lugha rasmi kama vile Kiswahili na Kiingereza, lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili na lugha za mama (kijamii au kiasili) kama vile Kikuyu. Kutokana na majukumu yake, lugha za Kiswahili na Kiingereza zina hadhi ya juu kuliko lugha za mama kama vile Kikuyu. Hadhi na majukumu ya lugha hizi huibua mielekeo chanya au hasi miongoni mwa wazungumzaji. Mielekeo ya lugha kwa upande wake nayo huenda

ikawafanya wazungumzaji kuwa na viwango tofauti vya umilisi wa lugha wanazozitumia katika jamii yenye wingilugha.

Tukichukulia kuwa huenda lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng zina hadhi ya juu na umaarufu kimatumizi miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika kuliko lugha ya Kikuyu, basi kuna uwezekano kuwa vijana hawa wanazipendelea lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng na hivyo kuathiri mielekeo na umilisi wao wa lugha ya Kikuyu. Aidha, hata ingawa Kikuyu ndiyo lugha kubwa zaidi hapa Kenya, huenda hadhi na umaarufu wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng unaathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hatimaye, hali ya kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu isipodhibitiwa pindi miaka inavyopita huenda ikasambaa na kuiingiza lugha ya Kikuyu katika ramani ya lugha kubwa ulimwenguni ambazo tayari zimeanza kuangamia licha ya kuwa na idadi kubwa ya wazungumzaji.

Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo hadhi na umaarufu wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng unachangia katika kudidimiza viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na hivyo hatimaye kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu.

Haya yalifanywa kwa kuchunguza vile mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji teule ya Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng

kwa upande mmoja na lugha ya Kikuyu kwa upande ule mwingine inavyoathiri umilisi wao wa lugha za mama kama vile Kikuyu.

Tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu lugha ya Kikuyu zinahusu masuala mengine ya lugha ya Kikuyu kama vile mofolojia na sintaksia ya Kikuyu, maneno miiko ya Kikuyu, lahaja za Kikuyu, maneno mkopo ya Kikuyu miongoni mwa mengine. Ni tafiti chache tu ambazo kufikia sasa zimechunguza kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Kwa mfano, Gachiri (2009) amechunguza jinsi uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu unavyoathiriwa na sera za kiserikali kuhusu mpango wa lugha hapa Kenya. Naye Muchemi (2011) ametafiti kuhusu vile mtagusano wa lugha ya Kiingereza na Kikuyu umepelekea kupotea kwa vipengele fulani vya kiisimu katika lugha ya Kikuyu kama vile nyakati na mpangilio wa maneno katika sentensi miongoni mwa vijana mashambani. Kadri ya ujuzi wetu, hakuna utafiti mwingine ambao umechunguza na kueleza athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Utafiti huu ulilenga kujaza pengo hili. Ili kulifikia azimio hili, utafiti wetu uliongozwa na malengo yafuatayo katika sehemu ya 1:3:1.

### 1.3.1 Malengo ya Utafiti

1. Kuchunguza na kubainisha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

2. Kubaini maeneo ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hupendelea kutumia lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.
3. Kubaini viwango vya umilisi wa Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu waishio mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.
4. Kwa mujibu wa 1, 2 na 3, kubaini athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu na kutambulisha hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu mijini.

### 1.3.2 Maswali ya Utafiti

1. Je, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo ipi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na mielekeo yao ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng?
2. Ni katika maeneo yapi ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hupendelea kutumia Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng?
3. Je, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vipi vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na umilisi wao wa Kiswahili, Kiingereza na Sheng?
4. Kwa mujibu wa 1, 2 na 3 lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zina athari zipi kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu na hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu iko vipi mijini?

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Sababu mojawapo ya kuchagua mada hii ilitokana na makisio ya utafiti huu kuwa lugha za mama kama vile Kikuyu huenda zikawa katika hatari ya kuangamia miongoni mwa kizazi cha vijana mijini licha ya umuhimu mkubwa wa lugha hizi katika jamii yoyote ile duniani. Umuhimu huu, kwa mujibu wa Tsunoda (2006), ni kama vile kuwa kitambulisho cha jamii husika; kuibua hisia za uzalendo na mshikamano katika jamii na kuwa hifadhi ya tamaduni za jamii mbalimbali na kuzipitisha kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Kama ilivyo katika sehemu nyingine za ulimwengu, hapa nchini Kenya, umilisi na umaarufu wa lugha za mama kama vile Kikuyu hasa miongoni mwa vijana mijini huenda ukawa wa viwango vya chini ikilinganishwa na lugha nyingine za kimataifa kama vile Kiswahili na Kiingereza. Kuna haja basi ya kuziimarisha lugha za mama kama vile Kikuyu miongoni mwa vijana mijini ili wapate kufaidi matumizi ya lugha hizi kikamilifu.

Utafiti huu pia ulichochewa na makisio yetu kuwa vijana katika sehemu za mijini huenda hawapendelei matumizi ya lugha za mama kama vile Kikuyu katika mawasilano bali hupendelea kutumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kulikuwepo basi na umuhimu wa kutathmini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ili kuweza kubaini vile uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu ulivyoathiriwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu uliweza kuweka wazi viwango vya umilisi na mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Aidha, tafiti nyingi ambazo zimefanywa na ambazo tulizipitia kuhusu lugha ya Kikuyu zinahusu nyanja nyingine za lugha hii. Miongoni mwa tafiti hizi ni kama vile Mofolojia ya Maneno Mkopo ya Kikuyu (Waithaka 2010), Maneno Miiko ya Kikuyu (Githaiga 2010), Ujifunzaji wa Miundo ya Kisintaksia wa Sentensi za Kikuyu miongoni mwa Watoto (Wangechi 1991), Mofolojia ya Kikuyu (Gathenji 1981,Wanyoike 2002), Lahaja za Kikuyu (Mutahi 1977) miongoni mwa tafiti nyingine. Hata hivyo, ni tafiti chache ambazo kufikia wakati wa utafiti huu zilikuwa zimechunguza kuhusu athari za lugha nyingine kwa lugha ya Kikuyu lakini zikiangazia masuala tofauti na utafiti wetu (taz. Muchemi 2011, Gachiri 2009). Utafiti huu ni muhimu kwa vile umeweka wazi athari za lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa lugha ya Kikuyu hasa kule kuibua mielekeo inayoathiri moja kwa moja viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Kwa njia hii, tuliibua data muhimu ambayo itaweza kutumiwa na wanaisimujamii katika kuziimarisha lugha za mama kama vile Kikuyu nchini Kenya katika siku za usoni.

Matokeo ya utafiti huu yametoa changamoto kwa wadau mbalimbali kama vile wanaisimujamii, serikali na jamii husika ya kuzijua mbinu na mikakati ya kuinua viwango vya umilisi wa lugha za mama miongoni mwa vijana nchini Kenya. Kwa kuanzisha mikakati ya kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama, lugha hizi zitaimarika na manufaa yake kuwafikia vijana mijini na vizazi vijavyo.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza kuhusu athari za mtagusano wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hata ingawa mtagusano wa lugha ambao ulilengwa zaidi katika utafiti huu ni ule wa lugha ya Kikuyu na Kiswahili pekee, utafiti huu haungezipuuza lugha za Kiingereza na Sheng. Hii ni kwa sababu lugha za Kiingereza na Sheng pia ni lugha zinazotumiwa kwa wingi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika maeneo mbalimbali ya kijamii katika mawasiliano yao ya kila siku. Kulingana na Mugenda (2008:119-120), "kuna vigezo vingine ambavyo huwa si sehemu ya vigezo halisi vya utafiti lakini haviwezi kupuuzwa iwapo utafiti unatakiwa kuwa na matokeo ya kutegemeka".

Basi ilikuwa vigumu katika utafiti wetu kupuuza athari za Kiingereza na Sheng kwa Kikuyu hata ingawa kimsingi utafiti wenyewe ulilenga athari za Kiswahili kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Utafiti huu hata hivyo haukujihusisha na lugha nyingine ambazo zilikuwa zikitumiwa katika eneo la utafiti mbali na hizi nne pekee. Sababu ya kuzichagua lugha hizi za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ni kuwa lugha hizi ndizo ambazo zinatumika kwa wingi katika mawasiliano ya vijana mijini na huenda zikawa na athari nyingi kwa lugha ya Kikuyu kuliko lugha nyingine zile. Lugha hizi tatu ndizo hutumika na vijana katika maeneo mengi ya kijamii kama vile shuleni, nyumbani, ibadani, katika biashara, kazini n.k.

Kulingana na Batibo (2005:67), “mtagusano wa lugha huwa na athari mbalimbali katika jamii kama vile uhamishaji msimbo, mielekeo ya lugha, kuchanganya msimbo, ukopaji wa maneno, athari za lugha moja kwa umilisi wa lugha nyingine, athari za lugha moja kwa viwango vya uthabiti wa lugha nyingine, mwingiliano wa $L_1$ na $L_2$ , uhamaji wa lugha na uangamiaji wa lugha baadhi ya athari nyingine”. Hata hivyo, utafiti huu ulichunguza tu suala la mielekeo ya lugha za Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng na athari zake kwa umilisi na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Pia, utafiti wetu ulijihusisha na kuchunguza jinsi mielekeo ya lugha inavyoathiri umilisi na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana pekee na wala sio makundi mengine katika eneo la utafiti kama vile watoto au watu wazima. Hii ni kwa sababu rika la vijana kama asemavyo Kerswill (2000: 182), “ limo katika kipindi cha umri ambamo mtu hukubana na matumizi ya lugha mbalimbali katika maeneo mengi zaidi ya kijamii ya matumizi ya lugha maishani kuliko rika lingine lolote lile”. Hii ina maana kuwa kati ya marika ya watoto, vijana, watu wazima na wazee katika jamii, rika la vijana ndilo huhusika zaidi na matumizi ya lugha kwa kiwango cha juu kuliko marika mengine. Aidha, Eckert (2003:117) anasema kuwa “vijana kote ulimwenguni huwa na sifa ya kutaka kufanya uvumbuzi mwingi katika matumizi ya lugha wanazozizungumza na kwa hivyo masuala mengi ya mabadiliko, ubunifu na mielekeo ya lugha hujidhihirisha vyema miongoni mwa rika la vijana kuliko rika lingine lolote lile katika jamii za ulimwengu”.

Utafiti huu basi ulitumia sampuli ya vijana na wala sio kundi lingine kwa vile vijana ndio wangedhihirisha vyema zaidi masuala ya mielekeo na matumizi ya lugha hizi nne, yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, kuliko kundi la watoto au wazee. Vijana waliolengwa na utafiti huu ni wale waliokuwa na umri wa kati ya miaka kumi na tatu hadi kumi na sita waliokuwa wakisoma katika shule za sekondari mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Kikundi hiki cha vijana kilichaguliwa kwa vile tayari kilikuwa na tajiriba za kutosha za matumizi ya lugha hizi nne na tena kilikuwa rahisi kukifikia ili kuteua sampuli kwa vile wako shuleni. Vijana hawa ililazimu pia wawe wameishi mijini tangu utotoni ili wawe wametangamana na lugha hizi nne kwa muda mrefu.

Aidha, utafiti huu uliwahusisha vijana kutoka shule za upili za wasichana na wavulana kutoka sehemu za mijini pekee ili kuhakikisha kulikuwa na usawa wa kijinsia. Shule hizi za mijini ziliteuliwa kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika wala sio kutoka miji mingine yeyote ile. Hii ni kwa sababu miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ina idadi tosha ya wakaazi wa jamii ya Kikuyu na ambayo ilitosheleza uteuzi wa sampuli ya utafiti huu. Kwa kifupi, utafiti huu ulijihusisha na suala la athari za lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na wala sio mashambani.

Vile vile, utafiti huu ulilishughulikia suala la mielekeo ya lugha inavyoathiri viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na hatimaye kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Umilisi wa lugha hizi za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ulichunguzwa kupitia

stadi za lugha ya kuongea, kusoma na kuandika, ambavyo ni vipengele vya umilisi wa kiisimu wa lugha, bali sio kupitia vipimo vinginevyo vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa mbinu za mawasiliano na umilisi wa uchanganuzi usemi. Umilisi wa kiisimu wa lugha huwa ni ujuzi wa sheria za lugha alionao mzungumzaji na unahusu mambo kama vile uwezo wa mzungumzaji wa kuunda na kutambua miundo ya sentensi sahihi na isiyo sahihi katika lugha, kufahamu msamiati mbalimbali wa lugha, kuwa na matamshi bora na kufahamu maana ya maneno.

Umilisi wa kiisimu (taz. 2.5.1) ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana. Brown (2005:77) anasema kuwa "ufahamu wa sheria za lugha humwezesha mzungumzaji kushiriki kikamilifu katika mazungumzo". Brown anaendelea kufafanua kuwa "hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano, umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano". Kama asemavyo Nicuolo (1991:52), "umilisi wa mawasiliano huanza kwa umilisi wa kiisimu wa lugha yaani kufahamu na kuzimudu sheria za lugha".

### 1.6 Msingi wa Nadharia.

Nadharia zilizotumiwa katika utafiti huu ni Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa. Tulitumia Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa ili kuyaelekeza masuala muhimu katika utafiti huu kama vile:-

i) Suala la mielekeo ya lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

ii) Suala la athari za mielekeo ya lugha za Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu na

iii) Suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Kwa upande mmoja, Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ilijikita zaidi katika kuyaongoza masuala yaliyohusiana na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Kwa upande ule mwingine, Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa iliyaongoza masuala yaliyohusiana na ubainishaji na ujenzi wa mielekeo ya lugha miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Maelezo ya kina ya Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa yametolewa kwa kina katika sura ya tatu.

**1.7 Hitimisho**

Sura hii imeyabaini na kuyafafanua masuala ya kimsingi katika utafiti huu na ambayo yaliongoza utafiti wenyewe kutoka mwanzo hadi mwisho. Baadhi ya masuala haya ni

pamoja na suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Aidha, sura hii imedokeza kuhusu nadharia zilizouongoza utafiti ambazo ni Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa. Nadharia hizi mbili zilitumiwa kama dira ya kuongoza utafiti huu hasa katika sehemu ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Sura inayofuata ilijihusisha na upitiaji wa maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada yetu ya utafiti.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imejihusisha na maelezo ya masuala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Masuala haya ni kama vile maelezo kuhusu dhana ya lugha ya mama (kijamii) kupitia mada kama vile asili na maana ya lugha ya mama, manufaa ya lugha za mama na juhudi mbalimbali za uimarishaji wa lugha za mama barani Afrika na nchini Kenya. Sura hii vile vile ina maelezo kuhusu tafiti mbalimbali ambazo tayari zimefanywa kuhusu lugha ya Kikuyu kwa jumla katika nyanja tofauti na pia mapitio ya tafiti kuhusu suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Haya yalifanywa ili kuliweka suala la utafiti wazi zaidi kwa kubainisha pengo la utafiti huu (taz 1.3). Lugha ya Kikuyu imefafanuliwa katika sura hii ya pili kwa vile utafiti huu ulijihusisha na uchunguzi wa athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Pia, katika sura hii kuna mapitio ya tafiti ambazo zinaangazia kuhusu mielekeo ya lugha na jinsi ya kupima mielekeo ya lugha. Zaidi, sura hii ina maelezo kuhusu umilisi wa lugha na suala la umilisi wa mawasiliano na jinsi ya kupima umilisi wa mawasilano kupitia stadi mbalimbali za lugha. Aidha, sura hii ina maelezo kuhusu dhana ya vijana na maelezo kuhusu matumizi yao ya lugha hasa katika sehemu za mijini barani Afrika na nchini Kenya. Hatimaye, sura hii imeangazia kuhusu hali ya kiisimujamii ya lugha nchini Kenya na ruwaza za matumizi na mielekeo ya kijumla ya lugha za Kikuyu, Kiingereza, Kiswahili na Sheng mijini nchini Kenya.

### 2.2 Maana, Umuhimu, Uimarishaji na Uthabiti wa Lugha za Mama (Kijamii).

Hata ingawa kila lugha duniani ni lugha ya mama ya mtu au kundi fulani la watu, kuna migawanyiko mbalimbali ya lugha ulimwenguni kutokana na viwango vya matumizi na hadhi zilizopewa lugha hizi katika jamii husika. Kwa mfano, kuna migawanyiko ya lugha kama vile lugha za kimataifa, lugha za kitaifa, lugha rasmi, lugha za mama (kijamii) na kadhalika. Katika sura hii, utafiti huu ulijadili kuhusu lugha za mama kama lugha zilizotengewa jukumu la mawasiliano na wanajamii mashinani ama vijijini katika taifa ambalo bila shaka lina matumizi ya lugha mbalimbali katika viwango vingine kama vile kiwango cha kitaifa na kimataifa.

#### 2.2.1 Asili na Maana ya Lugha ya Mama.

Kwa mujibu wa Pokorn (2005:54), "asili ya neno lugha ya mama imetokana na dhana kuwa mama mzazi ndiye mara nyingi huwa mtu wa kwanza kabisa kumfundisha mtoto stadi mbalimbali za lugha pale nyumbani anapomlea. Hivyo basi, kuna uwezekano mkubwa kuwa lugha anayoizungumza mamake mtoto ndiyo ambayo naye mtoto wake atakayoizungumza". Hata hivyo, dhana hii ya asili ya lugha ya mama baadaye imekuja kukosolewa na wanaisimu mbalimbali ambao wamejaribu kuelezea maana ya lugha ya mama kwa misingi mingine tofauti.

UNESCO (1953:46) inaelezea lugha ya mama kama "lugha ambayo mtu yeyote yule hupokea katika miaka yake ya awali na ambayo kwa kawaida huwa chombo chake cha mawasiliano". Kulingana na Skutnabb-Kangas (1981:17) "lugha ya mama ni lugha

ambayo mtu anajifunza kutoka utotoni ama lugha ambayo mtu anaizungumza kwa ufasaha zaidi na inayompa utambulisho wa kiisimujamii". Naye Varennes (2001:54) anaeleza kuwa "lugha ya mama ni lugha ya jamii alimozaliwa mtu bali sio lugha ya kwanza anayoizungumza na hivyo lugha ya mama ni lugha pana inayozungumzwa na jamii ya mtu binafsi". Kwa upande mwingine, KIE (2011:150) inafafanua kuwa lugha ya mama ni lugha ya kwanza kabisa ambayo mtoto hujifunza katika mazingira ya shule yake. Aidha, Pokorn (2005) anafafanua kuwa lugha ya mama ni lugha ambayo mtu anajifunza kama mtoto pale nyumbani mara nyingi kutoka kwa wazazi wake. Basi kunao uwezekano kuwa watoto wanaozaliwa katika familia zilizo katika mazingira ya uwili lugha huenda wakawa na zaidi ya lugha moja ya mama.

Utata katika kuelezea maana ya dhana lugha ya mama umepelekea wanaisimujamii kudai kuwa kuna maana zaidi ya moja ya dhana hii. Skutnabb-Kangas (1981:18) anaeleza kuwa "lugha ya mama inaweza ikafafanuliwa kupitia vigezo vitatu vikuu yaani:-

i. **Asili:** Lugha ambayo mtu alijifunza kwanza.

ii. **Umilisi:** Lugha ambayo mtu anaifahamu vyema kabisa

iii. **Matumizi**: Lugha ambayo mtu anaitumia kwa wingi zaidi".

Naye Pokorn (2005:57) anafafanua kuwa "dhana ya lugha ya mama inaweza kueleweka vyema kupitia vigezo vinne vifuatavyo:-

i. **Asili**: Lugha ambayo mtu alijifunza kwanza na ambayo ina athari za kudumu kwake kimatumizi.

**ii. Umilisi**: Lugha ambayo mtu anaifahamu vyema kabisa na ambayo ana umilisi wa juu kabisa kushinda lugha nyingine anazozifahamu.

**iii. Matumizi**: Lugha ambayo mtu anaitumia kwa wingi zaidi katika shughuli zake mbalimbali za kila siku.

**iv.Utambuzi**: a) Lugha ambayo mtu anajitambulisha nayo kama mmoja wa wazungumzaji wa lugha hiyo.

b) Lugha ambayo mtu anatambulishwa nayo na watu wengine katika jamii".

Katika jedwali, Pokorn (2005:58) anaziainisha lugha za mama ifuatavyo:-

**Jedwali 1: Fasili ya Lugha ya Mama**

| | KIGEZO | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Asili | Lugha ambayo mtu alijifunza kwanza na ambayo ina athari za kudumu kwake kimatumizi. |
| 2. | Umilisi | Lugha ambayo mtu huifahamu vyema kabisa na ambayo ana umilisi wa juu kabisa kushinda lugha nyingine anazozifahamu. |
| 3. | Matumizi | Lugha ambayo mtu anaitumia kwa wingi zaidi katika shughuli zake mbalimbali za kila siku. |
| 4. | Utambuzi | **a)** Lugha ambayo mtu anajitambulisha nayo kama mmoja wa wazungumzaji wa lugha hiyo. |
| | | **b)** Lugha ambayo mtu anatambulishwa nayo na watu wengine katika jamii au nchi. |

### 2.2.2 Umuhimu wa Lugha za Mama

Lugha za mama, kama vile Kikuyu, zina umuhimu mwingi katika jamii yoyote ile. Ruhlen (1996:112) anafafanua kuwa lugha za mama katika jamii zina umuhimu ufuatao:-

i. Kumsaidia mtu kufahamu kuhusu utamaduni wake na historia ya jamii yake.
ii. Kumwezesha mtu kujitambulisha na jamii yake na kujifunza asili yake.
iii. Kusaidia mtu katika ujifunzaji wa lugha ya pili kwa vile tayari amezifahamu sheria bia za kujifunza lugha.
iv. Kupitisha elimu vyema zaidi kuliko lugha za pili kwa sababu ndiyo lugha inayoeleweka vyema kabisa na mwanafunzi na kwa hivyo inamwezesha kuwasiliana na kujieleza vyema.

Aidha, Vigdis (2003:77) anaeleza kuwa lugha za mama ni muhimu kwa vile zinatekeleza majukumu ya kimsingi katika jamii kama vile:-

i. Kumpa mtoto tajriba za kipekee kuihusu jamii yake.
ii. Kuhifadhi utamaduni wa jamii mbali na kule kupitisha utamaduni kwa vizazi tofauti kupitia hadithi simulizi, methali, vitendawili n.k.
iii. Kumsaidia mtoto kujifunza na kuyaelewa maadili ya kijamii na matarajio ya jamii yake.
iv. Humpa kila mtu utambulisho wa pekee miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Tsunoda (2006:197) anaeleza kuwa “lugha za mama huwa na umuhimu mwingi katika jamii kama vile kuwa kitambulisho cha jamii husika, kuibua hisia za uzalendo na mshikamano katika jamii na zaidi kuwa hifadhi ya tamaduni za jamii mbalimbali na

kuzipitisha kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine”. Ngugi wa Thiong’o (2004) ana msimamo kuwa wakati jamii inapoipoteza lugha yao ya mama, huwa haipotezi tu nyenzo muhimu ya kuelezea, kuunda na kuhifadhi utamaduni wao bali hulazimika kujieleza na kuelezewa kupitia lugha na kumbukumbu za wageni. Hivyo, kulingana naye, kupoteza umilisi wa lugha ya mama ni sawa na kuupoteza utamaduni wako.

Hata ingawa lugha za mama zina umuhimu katika jamii, bado lugha hizi zinapuuzwa na kutazamwa kama lugha duni na watu wengi (Vigdis 2003). Kulingana na Vigdis, sababu kuu ya kupuuzwa kwa lugha za mama zinachangiwa na mambo kama vile mifumo ya elimu, masuala ya kisayansi, vyombo vya habari, kupata ajira na kujipatia nguvu za kisiasa. Nyanja hizi zote katika jamii nyingi husisitiza matumizi ya lugha za mawasiliano mapana kama vile Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na nyinginezo huku lugha za mama kama vile Kikuyu zikipuuzwa. Hivyo basi, kama asemavyo Cummins (2009:18) “jinsi utandawazi unavyozidi kuongezeka miongoni mwa jamii za ulimwengu, ndivyo lugha za mawasiliano mapana duniani zinavyozidi kupata umaarufu huku lugha za mama nazo zikiendelea kupoteza uthabiti wake huku nyingine zikiangamia ama kufa”.

Utafiti huu ulichunguza kuhusu suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama kwa kuzingatia lugha ya Kikuyu. Makisio ya utafiti yalikuwa huenda vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu kutokana na athari za matumizi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hatimaye, viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika huenda navyo vinasababisha lugha hii

kuwa na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii na hivyo kuingiza lugha ya Kikuyu katika ramani ya lugha kubwa ulimwenguni zilizo katika hatari ya kuangamia pindi wakati unavyopita. Iwapo lugha za mama zitaangamia, basi manufaa yote yaliyofafanuliwa katika sehemu ya 2.2.2 yatakosa kuwafikia wazungumzaji husika.

### 2.2.3 Juhudi za Kuimarisha Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha za Mama.

Umoja wa mataifa kupitia shirika la UNESCO umehusika katika juhudi za kuimarisha na kuhifadhi lugha za mama kote ulimwenguni. Lengo kuu la UNESCO ni kuweza kuimarisha na kuhifadhi lugha za mama kwa wingi iwezekanavyo ili hatimaye kuweza kuhifadhi tamaduni tofauti tofauti za jamii mbalimbali duniani (UNESCO 2005). Ili kufanikisha lengo hili, UNESCO hutilia mkazo mambo muhimu yafuatayo:-

i. Kuhimiza ushirikiano wa kimataifa katika uimarishaji na uhifadhi wa lugha za mama kote ulimwenguni.

ii. Kuweka sera thabiti zitakazohakikisha kuwa lugha za mama zimeimarishwa kwa wingi iwezekanavyo na kwa njia hiyo kuziondoa katika hatari ya kuangamia.

iii. Kuhamasisha jamii mbalimbali ulimwenguni kuhusu umuhimu wa lugha zao za mama na haja ya kuziimarisha sawia na tamaduni zao.

Kikao maalum cha umoja wa mataifa cha Septemba 2007 (UNESCO 2007), kilipitisha azimio la pamoja la kuzikinga na kuzihifadhi haki za jamii za kitamaduni kupitia lugha zao za mama. Azimio hili lilipitishwa ili kuhakikisha kuwa jamii za kitamaduni zimepewa haki za kuimarisha, kuhifadhi na kupitisha historia, tamaduni na filosofia zao kupitia lugha zao za mama. Pia azimio hili lililenga kuhakikisha kuwa serikali mbalimbali ulimwenguni zimehakikisha kuwa jamii za kitamaduni katika nchi zao zimepewa fursa na haki ya kuzihifadhi tamaduni zao hasa kupitia lugha zao za mama. Azimio hili basi lilikuwa juhudi za moja kwa moja za Umoja wa Mataifa za kuhakikisha kuwa lugha za mama za jamii mbalimbali zimeimarishwa na kuhifadhiwa kwa wingi iwezekanavyo.

### 2.2.4 Uimarishaji wa Lugha za Mama kupitia Elimu.

Hata ingawa tatizo la kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama barani Afrika linaendelea kuongezeka, inasikitisha kuona kwamba bado serikali nyingi za Afrika hazina sera madhubuti zinazolenga kuimarisha na kudumisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama na kwa hivyo kila uchao lugha hizi zinazidi kuanguka katika viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii. Akilifafanua suala hili, Sheik (2011) ana maoni kuwa ili kuweza kuziimarisha lugha za mama hapa Afrika, lazima serikali za Afrika zitilie maanani haja ya kutekeleza mapendekezo ya UNESCO (2007) ya kujaribu kuinua uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama kwa kuzifanya lugha za kufundishia katika mifumo ya elimu ya mataifa mbalimbali ulimwenguni.

Kulingana na UNESCO (2005), njia moja kuu ya kuziimarisha lugha za mama ulimwenguni ni kwa kuzifanya lugha za kufunzia katika mifumo ya mataifa wanachama ulimwenguni kote. Kipengele cha 14 cha azimio la umoja wa mataifa la mwaka wa 2007 (U.N 2007:19-21) kilisisitiza haja ya kuzifanya lugha za mama kuwa lugha za mafunzo hasa katika madarasa yote ya shule za msingi. Baadhi ya masuala yaliyotiliwa mkazo ni pamoja na:-

i. Jamii za kitamaduni kote ulimwenguni zina haki ya kuhakikisha kuwa lugha zao za mama zimetumika katika kufunza shuleni kwa njia inayoambatana na mifumo ya elimu iliyopo.

ii. Watoto wa jamii za kitamaduni lazima wapewe fursa ya masomo kupitia tamaduni zao jambo ambalo lingewezeshwa tu na matumizi ya lugha za mama katika elimu.

iii. Serikali mbalimbali ulimwenguni zina wajibu wa kushauriana na kushirikiana na jamii za kitamaduni na kupitia mifumo ya elimu hasa kwa kutumia lugha zao za mama.

Nacho kipengele cha 6 cha azimio hili kinapendekeza matumizi ya lugha za mama katika masomo ya daraja za juu kama vile vyuo vikuu.

Sheik (2011) anapendekeza kuwa lugha za mama barani Afrika zafaa pia kushirikishwa katika mawasiliano ya kiteknolojia ili zipate maeneo mapya ya kijamii ya kuzituimia na basi kuiimarisha uthabiti wake wa kiisimujamii. Lugha hizi basi zafaa kufanywa lugha za tarakilishi ili ziweze kutumika katika mtandao kwa wingi iwezekanavyo. Kama

anavyofafanua Sheik, matumizi ya mtandao katika mawasiliano yameongezeka kwa kiasi kikubwa katika enzi hii ya utandawazi na kwa hivyo lugha za mama hazina budi kushirikishwa kama hatua mojawapo ya kuiimarisha uthabiti wake wa kiisimujamii.

Juhudi za umoja wa mataifa kupitia UNESCO zimeyafanya mataifa mbalimbali ulimwenguni kuanzisha harakati za kuziimarisha lugha zao za mama kwa kuzifanya lugha za kufunzia hasa katika madarasa yote ya shule za msingi katika mifumo yao ya elimu. Matumizi ya lugha za mama katika elimu kwa mujibu wa UNESCO yanamaanisha sio tu kufundisha kuhusu lugha hizi bali kuzitumia kama lugha za kufunzia masomo mbalimbali shuleni (Sheik 2011).

Desai (2012) anaeleza kuwa mojawapo ya nchi ambazo tayari zimeanzisha sera ya kufunza kwa kutumia lugha za mama hapa Afrika ni nchi ya Afrika Kusini. Kwa mujibu wa Adams (1999:24), “nchi ya Afrika Kusini ina sera ya lugha ambayo ni ya kipekee duniani kwa vile inatoa uhuru mkubwa wa matumizi ya lugha nyingi katika kiwango cha kitaifa. Hii ni kwa sababu sera ya lugha ya Afrika Kusini ina jumla ya lugha 11 zinazotumika kama lugha rasmi nyingi zikiwa lugha za mama. Lugha hizi ni pamoja na Kiingereza, Kiafrikaans, isiZulu, isiXhosa, sePedi, seTswana, seSotho, xiTsonga, siSwati, tshiVenda na isiNdebele”.

Licha ya sera ya lugha  nchini Afrika Kusini kuwa na matumizi ya lugha hizi zote kama lugha rasmi, bado lugha nyingi za mama hazijapata fursa ya kuimarishwa ipasavyo (Deumert na wenzake 2005). Zaidi, hata ingawa sera ya lugha ya Afrika Kusini kuhusu

elimu, ya Julai 1997, imetoa kibali kwa shule zote za msingi kuchagua lugha za kufunzia, bado ukweli ni kuwa shule nyingi, hasa katika sehemu za mjini, zinapendelea kutumia Kiingereza pekee na hivyo kuzipuuza lugha za mama. Katika sehemu za mashambani, lugha za mama hutumika mafunzoni hadi darasa la tatu na kwa hivyo kama asemavyo Murray (2002), kuwanyima watoto fursa ya kuzifahamu lugha zao za mama kikamilifu. Kulingana na Dessai (2012) mbali na kuwanyima watoto fursa ya kujifunza lugha zao za mama kikamilifu, matumizi ya Kiingereza kama lugha pekee ya kufunzia katika shule nyingi pia huwafanya wanafunzi kutatizika katika kuzielewa vyema dhana zinazofunzwa katika masomo mbalimbali katika shule za msingi hali ambayo huendelezwa katika shule za upili na hata vyuo vikuu.

Kutokana na hali hii ya kupuuzwa kwa matumizi ya lugha za mama, kuna juhudi ambazo zimeanzishwa nchini Afrika Kusini za kujaribu kuzitumia lugha za mama kama lugha za kufunzia katika madarasa yote ya shule za msingi na wala sio tu katika madarasa ya miaka mitatu ya mwanzo. Kwa kufanya hivyo, Dessai (2012) ana maoni kuwa lugha hizi za mama zitakuwa kwa wakati ule ule zikiimarishwa kwa kuinua viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii. Mojawapo wa lugha ya mama ambayo imeanza kutumiwa kufundishia katika gredi zote za shule za msingi ni lugha ya Xhosa katika mji wa Khayelitsha. Juhudi hizi zilianzishwa na idara ya elimu ya mji wa Western Cape ambayo iliazimia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuunga mkono matumizi ya lugha za mama kama lugha ya kufunzia kuanzia darasa la kwanza hadi la sita.

ii. Kuwahusisha wazazi katika masuala ya matumizi ya lugha za mama katika elimu. Wazazi wangehakikisha kwamba watoto wao wamepokezwa lugha zao za mama kikamilifu katika eneo la kijamii la nyumbani kabla ya kujiunga na shule za msingi.

iii. Kusambaza masomo kupitia lugha za mama kwa shule nyingi iwezekanavyo za mji wa Western Cape.

iv. Kuhimiza wanafunzi wawe na umilisi mzuri wa lugha ya Xhosa ambayo ni lugha mojawapo rasmi inayotumika katika mji wa Western Cape.

Kwa mujibu wa Desai (2012), malengo makuu ya kutumia lugha ya Xhosa katika elimu ya shule za msingi yalikuwa kuwawezesha wanafunzi kuzifahamu dhana za kimasomo kwa urahisi na vile vile kuwapa fursa ya kuifahamu lugha yao ya mama (Xhosa) na basi kuiimarisha uthabiti wake wa kiisimujamii kwa miaka mingi ijayo.

Juhudi nyingine za kuimarisha lugha za mama kupitia elimu barani Afrika ni zile zinazohusu lugha ya Yoruba katika mkoa wa Ife nchini Nigeria. Katika mkoa huu wa Ife, lugha ambayo imekuwa ikitumiwa katika kufunzia ni Kiingereza katika gredi za juu za shule za msingi, shule za upili na vyuo vikuu (Afolayan 1976). Mfumo huu ulikuwa na wanafunzi wengi ambao walikamilisha darasa la 6 bila kufahamu asilimia kubwa ya masuala yaliyofundishwa katika madarasa mbalimbali. Ili kutatua shida hii, ilipendekezwa kuwa lugha ya Ife ingetumika kufunzia katika miaka yote 6 ya shule za msingi.

Afolayan (1976) anaeleza kuwa mradi huu, ulioanzishwa kwa njia ya majaribio katika miaka ya sabini, ulionyesha kuwa wanafunzi waliofunzwa kwa lugha ya mama (Yoruba), walifaulu zaidi masomoni ikilinganishwa na wale waliofunzwa kwa Kiingereza. Mbali na faida hii, Afolayani anaendelea kusema kuwa mradi huu pia ulihakikisha kuwa lugha ya Yoruba, ambayo ni mojawapo wa lugha za mama za Ife, imeimarishwa kwa kiwango kikubwa na uthabiti wake wa kiisimujamii kudumishwa.

Naye Heugh (2011) anaeleza kuwa mnamo mwaka wa 1994 nchi ya Ethiopia, kupitia wizara ya elimu, ilianzisha sera ya kitaifa ya elimu iliyolenga matumizi ya lugha za mama kama lugha za kufunzia kwa kipindi chote cha miaka 8 ya shule za msingi. Mbali na kuthibitisha kuwa matumizi ya lugha za mama masomoni yaliinua kiwango cha weledi miongoni mwa wanafunzi, sera hii pia ilihakikisha kuwa lugha mbalimbali za mama kama vile Amhara, Harari, Tigray, Oromifa, Oromiya na Tingirinya zimeimarishwa kwa kupitishwa kwa watoto wengi iwezekanavyo na kwa kipindi kirefu hasa mijini ambako Kiingereza kilikuwa kikitumika kwa wingi.

### 2.2.5 Uangamiaji wa Lugha za Mama Nchini Kenya.

Kama ilivyo katika sehemu nyingine za ulimwengu, hapa nchini Kenya lugha nyingi za mama zimo katika viwango tofauti vya kuangamia kutokana na mtagusano wake na lugha nyingine za matumizi mapana. Mfano wa lugha moja iliyo katika hatari ya kuangamia nchini Kenya ni lugha ya Suba. Kulingana na ramani ya UNESCO (2009) ya lugha zilizo katika hatari ya kuangamia kwa mujibu wa Moseley (2010), lugha ya Suba imekabiliwa na athari kubwa za mtagusano wake na lugha kama vile Dholuo, Kiswahili na

Kiingereza. Idadi kubwa ya watu wa jamii ya Suba hawana tena ufasaha katika lugha hii bali miongoni tu mwa kizazi cha babu na nyanya.

Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama usipodumishwa hatimaye huleta vifo au uangamiaji wa lugha husika. Kwa mujibu wa ramani ya UNESCO (2009) ya lugha zilizo katika hatari ya kuangamia, nchi ya Kenya ndiyo yenye idadi kubwa zaidi ya lugha zilizoangamia katika eneo la Afrika Mashariki. Lugha hizi ni pamoja na Yaaku (Mukogodo), Lorkoti, Sogoo (Okieki), El Molo, Kinare na Kore. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa katika nchi ya Kenya kunayo haja kubwa ya kuziimarisha lugha za mama zinazoendelea kushuka katika viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii. Uimarishaji wa lugha hizi za mama utaanza punde tu viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha mbalimbali za mama vitakavyotambulishwa wazi kupitia tafiti mbalimbali zinazolenga kuchunguza hali ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama. Hata ingawa lugha hizo zote zina idadi ndogo ya wazungumzaji, utafiti huu umebaini kuwa hata lugha zilizo na idadi kubwa ya wazungumzaji nchini Kenya kama vile Kikuyu pia zimeanza kuonyesha dalili za kuingia katika orodha ya lugha maarufu ulimwenguni zinazoangamia hatua kwa hatua pindi miaka inavyopita.

Lengo la nne la utafiti wetu lilikuwa kuchunguza kuhusu hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni vya chini kutokana na mtagusano wa Kikuyu na lugha za Kiswahili, Kiingereza

na Sheng. Hii ina maana kuwa, hata ingawa lugha ya Kikuyu ni mojawapo wa lugha zilizo na wazungumzaji wengi zaidi nchini Kenya inatokea kuwa lugha hii iko katika hatari ya kuingia katika orodha ya lugha zinazonagamia pole pole ulimwenguni kutokana na ushindani wa lugha nyingine kimatumizi bali sio kutokana na uhaba wa wazungumzaji. Iwapo lugha za mama kama vile lugha ya Kikuyu nchini Kenya hasa miongoni mwa vijana mijini zimo na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii, basi kuna haja ya kuanzisha mikakati ya kuiimarisha na kudumisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama nchini Kenya kama vile Kikuyu ili zisije zikaangamia pindi miaka inavyoendelea kupita. Maelezo kuhusu lugha ya Kikuyu yametolewa katika sehemu ya 2.3 inayofuata.

### 2.3 Lugha ya Kikuyu

Lugha ya Kikuyu ndio lugha iliyo na wazungumzaji wengi zaidi nchini Kenya. Haya ni kwa mujibu wa hesabu ya kitaifa ya idadi ya watu nchini Kenya ya 2009 ambayo ilionyesha kuwa lugha ya Kikuyu ina idadi ya takribani watu milioni 6.6. Idadi hii ni kama asilimia 22 ya idadi yote ya watu nchini Kenya (Kenya National Bureau of Statistics 2010). Kulingana na Muriuki (1974), makaazi ya jadi ya jamii ya Kikuyu ni sehemu ya kati ya nchi ya Kenya. Lugha ya Kikuyu huzungumzwa kwa wingi kama lugha ya mama katika eneo la kati la nchi ya Kenya hasa katika kaunti za Nyeri, Murang'a, Kiambu na Nyandarua. Pia, lugha hii huzungumzwa katika maeneo mengine nchini Kenya kunako wakaazi wa jamii ya Kikuyu kama vile katika kaunti ya Nairobi na katika sehemu mbalimbali za bonde la ufa kama vile mjini Nakuru na Eldoret.

Aidha, Muriuki (1974) anafafanua zaidi kuwa lugha ya Kikuyu ni lugha maarufu nchini Kenya, sio tu kutokana na idadi kubwa ya wazungumzaji, bali kwa sababu lugha hii hutumika katika shughuli muhimu za kijamii kama vile biashara, elimu na utangazaji. Kwa jumla lugha ya Kikuyu huleta taswira ya mojawapo ya lugha iliyo thabiti na imara kiisimujamii nchini Kenya.

Gikuyu ni lugha ya Kibantu iliyo kwenye tawi la Bantu ya kati na katika familia lugha ya Niger-Congo. Hii ndiyo lugha asilia ya jamii ya Agikuyu nchini Kenya. Kulingana na Muriuki (1976), jina halisi la lugha hii ni Gigikuyu na wazungumzaji wake Gikuyu. Hata hivyo, jina Kikuyu ndilo linalofahamika zaidi kimatumizi likirejelea lugha na pia wazungumzaji wake. Kwa mujibu wa Muriuki, Kikuyu ni mojawapo wa lugha zinazounda kijikundi cha Thagicu ambacho kina makundi mengine kama vile Mbeere, Embu, Chuka, Mwimbi, Igoji, Tharaka, Igembe, Tigania, Ameru na Kamba. Zaidi, Kikuyu ni lugha ambayo ina lahaja tatu kuu yaani Gaaki (Nyeri), Metumi (Murang’a) na Kabete (Kiambu).

### 2.3.1 Tafiti Kuhusu Lugha ya Kikuyu kwa Jumla

Watafiti wengi wamechunguza kuhusu masuala mbalimbali kuhusu lugha ya Kikuyu kufikia sasa. Tafiti hizi ni kama vile utafiti wa Waithaka (2010) ambaye ameshughulikia suala la utohozi wa maneno mkopo ya Kikuyu ambayo yamekopwa kutoka lugha ya Kiswahili. Waithaka hasa ameangazia taratibu za kimofolojia zinazojitokeza katika mchakato wa utohozi wa maneno kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi Kikuyu. Katika utafiti huu ametumia mtazamo wa fonolojia leksia. Utafiti wa Waithaka ni tofauti na

utafiti wetu kwani tulichunguza kuhusu athari za Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika.

Naye Mwihaki (1998) alitafiti kuhusu utohozi wa kifonolojia wa manenomkopo ya Kikuyu kutoka Kiingereza hadi Kikuyu. Yeye alilenga kuonyesha mabadiliko ya kifonolojia yanayopatikana katika maneno haya kwa kutumia nadharia ya fonolojia zalishi. Utafiti huu umebainisha kuwa fonimu ndicho kipengele kinachotegemewa katika utohozi wa kifonolojia. Utafiti huu umejikita katika nyanja ya maneno mkopo ya lugha ya Kikuyu ilhali utafiti wetu ulishughulikia suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Wangechi (1991) alishughulikia suala la upokezi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa watoto wa kati ya miaka 3 hadi 5. Wangechi amejikita katika upokezi wa miuundo ya kisintaksia miongoni mwa watoto. Katika utafiti huu, Wangechi alichunguza matamshi mbalimbali ya watoto ili kupima ufasaha wa kimazungumzo na aliweza kupata kuwa katika kiwango hiki, watoto huwa na ufasaha wa kisintaksia katika umri huu mchanga sawa na watu wazima. Wangechi ametumia nadharia ya Krashen (1973, 1988) kuelezea suala hili la upokezi wa lugha na nadharia ya Chomsky ya sarufi geuza maumbo zalishi kuelezea masuala ya sentensi na uzalishaji wake miongoni mwa watoto. Utafiti wa Wangechi, hata ingawa ni tofauti na wetu, ni muhumu kwa vile unaangazia suala la upokezi wa lugha ya Kikuyu ambalo pia ni suala lililoangaziwa na utafiti wetu lakini

miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika bali sio watoto.

Gathigia (2010) kwa upande wake alitafiti kuhusu matumizi ya maneno miiko katika lugha ya Kikuyu. Katika utafiti huu, Gathigia, alilenga kuonyesha jinsi lugha ya Kikuyu inavyotambulisha na kutumia taratibu za kisemantiki na kileksia katika uundaji wa maneno miiko. Vile vile, utafiti wake Gatihigia ulidhamiria kuonyesha athari za kijinsia katika matumizi ya maneno miiko miongoni mwa wanajamii ya Kikuyu. Utafiti wa Gathigia ni tofauti na wetu ambao ulilenga suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Wanyoike (2002) alifafanua suala la mofofonolojia ya lugha ya Kikuyu kwa kuthibitisha na kueleza mabadiliko mbalimbali ya kifonolojia kwa mizizi ya vitenzi vya Kikuyu. Pia, Wanyoike ametalii mabadiliko haya katika viambishi awali na tamati katika lugha hii kwa mujibu wa nadharia ya fonolojia leksia. Utafiti huu wa Wanyoike ni wa kiisimu na ambao ni tofauti na utafiti wetu ambao ni wa kiisimujamii.

Katika utafiti wake, Njoroge (1978) amechunguza kuhusu suala la mofolojia ya lugha ya Kikuyu kwa mujibu wa nadharia ya sarufi geuza maumbo zalishi. Katika utafiti huu, Njoroge ameangalia taratibu za uundaji wa nomino kutokana na vitenzi katika lugha ya Kikuyu kupitia unyambuaji. Pia, Njoroge amejaribu kuainisha nomino hizi katika makundi mbalimbali. Utafiti wetu ulijikita katika suala la uthabiti wa kiisimujamii wa

lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini tofauti na utafiti huu wa Njoroge ambao ni wa kiisimu unaohusu uundaji wa maneno ya Kikuyu.

Mutahi (1977), ametafiti kuhusu uainishaji wa lahaja za Kikuyu zinazozungumzwa kusini mwa mlima Kenya na hasa zilizo karibu na mlima huu. Uainishaji wa Mutahi wa lahaja hizi ulitumia misingi ya kiisimu, kisiasa, kijiografia na kiuchumi. Mutahi alifaulu katika kuziainisha lahaja za Kikuyu hata ingawa hakushughulikia eneo la Nyandarua kwa sababu, kulingana na yeye, hili ni eneo lililo na mchanganyiko wa wakazi kutoka lahaja mbalimbali za Kikuyu. Hata ingawa utafiti wa Mutahi ni wa kiisimujamii, kuna tofauti ya utafiti wake na huu wetu kwani Mutahi alilenga lahaja za lugha ya Kikuyu huku utafiti wetu ukilenga suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Mwingine aliyetafitia lugha hii ya Kikuyu ni Mugane (1996). Mugane ameshughulikia suala la unominishaji katika lugha za Kibantu lakini akijikita katika mifano kutoka kwa miundo ya nomino za lugha ya Kikuyu miongoni mwa lugha nyingine za Kibantu. Katika utafiti huu, Mugane ana maoni kuwa vitenzi jina vya lugha ya Kikuyu huchukua viambishi na kwa hivyo vinaweza kunyambulika.

Aidha, Kamau (1996) amechukua mtazamo linganuzi ambapo amelinganisha mifanyiko ya kifonolojia kati ya lahaja za Kindia na Kigichugu za lugha ya Kikuyu. Katika utafiti huu, Kamau ameweka wazi tofauti zilizopo kati ya lahaja hizi kifonolojia katika

vipengele vingi kama vile katika irabu na konsonanti kwa mujibu wa nadharia ya fonolojia zalishi.

Mbugua (1998) amejikita katika kuchunguza jinsi lugha ya Kikuyu inavyotumiwa katika kuweka bayana majukumu ya kijinsia katika jamii. Utafiti wa Mbugua umedhihirisha kuwa matumizi ya lugha katika jamii ya Kikuyu huwaweka wanawake katika nafasi ya chini katika jamii ikilinganishwa na wanaume. Utafiti wa Mbugua ni wa kiisimujamii ambao umetumia nadharia ya simiotiki ya kijamii kuonyesha jinsi lugha ya Kikuyu inavyoainisha majukumu kijinsia katika jamii ya Kikuyu.

Baada ya kuzipitia tafiti za kijumla kuhusu lugha ya Kikuyu katika sehemu hii ya 2.3.1, imebainika kuwa tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu lugha ya Kikuyu zinahusu nyanja nyingine za lugha kama vile isimu na fasihi. Miongoni mwa tafiti hizi ni kama vile Mofolojia ya Maneno Mkopo ya Kikuyu (Waithaka 2010), Maneno Miiko ya Kikuyu (Githaiga 2010), Ujifunzaji wa Miuundo ya Kisintaksia wa Sentensi za Kikuyu miongoni mwa Watoto (Wangechi 1991), Mofolojia ya Kikuyu (Gathenji 1981,Wanyoike 2002), Lahaja za Kikuyu (Mutahi 1977) miongoni mwa tafiti nyingine. Tofauti na tafiti hizi, utafiti wetu ulilenga masuala ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu kwa kuangazia suala la athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Aidha, utafiti huu ulibaini vile mielekeo hasi na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika

unavyoathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu tofauti na tafiti hizi zilizopitiwa katika 2.3.1.

### 2.3.2 Tafiti Kuhusu Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ya Kikuyu.

Hata ingawa tafiti nyingi zilizofanywa kufikia sasa kuhusu lugha ya Kikuyu zinaangazia masuala ya kiisimu na fasihi kuhusu lugha hii, kuna tafiti chache ambazo zinaangazia kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu suala ambalo limechunguzwa kwa kina katika utafiti huu. Hinton na Hale (2001) wana maoni kuwa Kikuyu ni lugha ambayo inazungumzwa na marika yote lakini inaonyesha dalili za kupungua kwa idadi ya watoto wanaojifunza lugha ya Kikuyu katika mazingira ya nyumbani katika sehemu za mijini na aidha kuna dalili za kupungua kwa maeneo ya kijamii ambamo lugha hii inatumika. Maoni kama haya kuhusu lugha ya Kikuyu, na kwa jumla lugha za mama, yanazua haja ya kuchunguza viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hii hasa katika sehemu za mijini ili baadaye kuweka mikakati mwafaka ya kuimarisha lugha hii ya mama hasa miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Gachiri (2009), alifanya utafiti ambao ulilenga kuonyesha jinsi sera za serikali ya Kenya kuhusu uzalendo, elimu na maendeleo zinavyochangia katika kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu na ambayo ni mojawapo ya lugha kuu hapa nchini Kenya. Gachiri anaeleza kuwa matumizi ya lugha ya Kiingereza yanahimizwa sana katika elimu na maendeleo ya nchi huku lugha za mama kama vile Kikuyu zikionekana kama lugha ambazo hazina nafasi yoyote katika masuala rasmi ya kiserikali. Lugha ya

Kiswahili nayo huhimizwa na serikali kama lugha ya kuleta umoja wa nchi na kama ishara ya uzalendo huku matumizi ya lugha za mama, Kikuyu kikiwemo, yakionekana kama njia ya kuendeleza ukabila.

Kwa mujibu wa Gachiri (2009), sera za serikali kuhusu uzalendo, elimu na maendeleo nchini Kenya zinapelekea kuwe na hali ya msisitizo wa kiwango cha juu cha matumizi ya Kiingereza na Kiswahili huku lugha ya Kikuyu na lugha nyingine za mama zikipuuzwa na hivyo basi kuathiri uthabiti wake wa kiisimujamii. Gachiri alifanya utafiti wake katika wilaya ya Kirinyaga ambapo alitumia nadharia ya kuchanganya msimbo ya Myers-Scotton kutafiti kuhusu vile vijana katika shule za sekondari wanavyohama kutoka kwa matumizi ya lugha ya Kikuyu ambayo waliipokea utotoni na kuanza kuzitumia lugha za Kiingereza, Kiswahili na hata Sheng katika maeneo mengi ya kijamii ya matumizi ya lugha.  Tofauti na utafiti wa Gachiri, utafiti huu hauchunguzi kuhusu uhamaji wa lugha kwa vile vijana wanaounda sampuli ya utafiti wetu hawakupata fursa ya kujifunza lugha ya Kikuyu utotoni kama ilivyo na sampuli ya utafiti wa Gachiri. Aidha, utafiti wa Gachiri umetumia sampuli ya vijana kutoka sehemu za mashambani tofauti na utafiti huu ambao umetumia sampuli ya vijana kutoka mijini ili kubaini vile lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng zinavyoathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vjiana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu pia limechunguzwa na Muchemi (2011). Yeye ametafiti kuhusu vile vijana wa jamii ya Kikuyu mashambani wanavyoathirika kutokana na mtagusano wa lugha ya Kikuyu na lugha ya Kiingereza na

hivyo kuathiri umilisi wao wa lugha ya Kikuyu. Katika utafiti huu, Muchemi anasema kuwa sababu kuu ya vijana wa jamii ya Kikuyu mashambani ya kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ni msisitizo wa matumizi ya lugha ya Kiingereza katika shule za upili nchini Kenya na hatimaye msisitizo huu unachangia katika kupotea kwa vipengele vya kiisimu vya lugha ya Kikuyu kama vile leksia na mofosintaksia.

Kwa mujibu wa utafiti wa Muchemi (2011), mtagusano wa lugha ya Kiingereza na Kikuyu umepelekea kule kupotea kwa vipengele fulani vya kiisimu katika lugha ya Kikuyu kama vile nyakati na mpangilio wa maneno katika sentensi. Hivyo, ni kama vijana wa jamii ya Kikuyu mashambani wameanza kuhama kutoka kwa matumizi ya lugha ya Kikuyu hadi kwa matumizi ya Kiingereza na hivyo kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Utafiti huu nao ulikuwa muhimu kwetu kwa vile umeshughulikia suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu.

Hata hivyo, tofauti na utafiti huu, utafiti wetu ulichunguza jinsi mielekeo kuhusu lugha ya Kikuyu inavyoathiri viwango vya umilisi wa lugha hii katika stadi za kuongea, kusoma na kuandika miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na hatimaye kutatiza uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu. Kama asemavyo Karanja (2009), mielekeo ya jamii kuhusu lugha yao huwa mojawapo ya kipimo cha kubaini uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ile. Vile vile, utafiti wetu ulichunguza jinsi matumizi ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng, na wala sio Kiingereza pekee, yanavyoathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Aidha, utafiti huu ulichunguza

athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu kiisimujamii na wala sio kwa kuzingatia vipengele vya kiisimu kama vile leksia na mofosintaksia kama vile alivyofanya Muchemi katika utafiti wake.

## 2. 4 Mielekeo ya Lugha

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kuchunguza na kubainisha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hivyo ilikuwa muhimu kulifafanua suala la mielekeo ya lugha kwa kina. Kwa mujibu wa Kartz (1960), mielekeo ni ile hali ya mtu kuweza kutathmini ishara, kitu au jambo fulani katika mazingira yake iwapo ni nzuri au ni mbaya na iwapo analipenda au halipendi. Hii ina maana kuwa wakati mtu anakabiliwa na uchaguzi wa vitu viwili au zaidi yeye huwa hana budi kupendelea kitu kimoja dhidi ya kile kingine. Katika muktadha wa lugha, wazungumzaji wanapojikuta katika mazingira ya wingilugha huwa hawana budi kupendelea matumizi ya lugha moja huku labda wakichukia lugha ile nyingine.

Mielekeo ya lugha, kama asemavyo Triandis (1971), ni ile hali ya kuipenda au kutoipenda lugha moja au zaidi katika mazingira ya wingilugha. Triandis anafafanua zaidi kuwa mielekeo ya lugha hutegemea nguzo mbili kuu ambazo ni:-

i. Mielekeo ya lugha kama mtazamo wa kiakili yaani dhana iliyo ndani ya fikra za mtu kuhusu lugha.

ii. Mielekeo ya lugha kama mtazamo wa kitabia yaani vitendo vya mtu vinaonyesha mielekeo yake kuhusu lugha.

Akirejelea nguzo hizi mbili, Fasold (1984:67) anaeleza kuwa "mielekeo ya lugha huanza katika akili za mtu binafsi na huwa katika hatua tatu. Hatua hizi ni pamoja na:-


**i.** **Hatua ya Utambuzi** - Hii ni hali ya kuwa na fikira na imani fulani kuhusu lugha husika. Hii ina maana kuwa mielekeo chanya au hasi kuhusu lugha huanza kwenye utambuzi wa kifikira wa mtu binafsi.

**ii.** **Hatua ya Athari** - Katika hatua hii, mielekeo ya mtu binafsi kuhusu lugha fulani huanza kuathiri hisia zake kwa njia ya kuipenda au kutoipenda ile lugha.

**iii.** **Hatua ya Utendaji** - Mtu katika hatua hii huwa tayari kutenda kwa njia ambayo itaonyesha mielekeo yake halisi kuhusu lugha fulani. Vitendo hivi ni kama vile kuitumia lugha katika maeneo mengi au machache ya kijamii, kutoitumia lugha kabisa, kuihama lugha kabisa kati ya vitendo vingine".

Mchoro ufuatao unaonyesha jinsi hatua hizi tatu zinavyohusiana katika ujenzi wa mielekeo ya lugha.

**Mchoro 1: Vijenzi vya Mielekeo**




(Fasold 1984: 68)

Kwa mujibu wa Fasold (1984), hatua hizi tatu za ujenzi wa mielekeo hufuatana hadi mtu anapopata mielekeo halisi kuhusu lugha fulani.

Baker (1992:13) anaeleza kuwa "mielekeo ya lugha ni mawazo ama hisia ambazo humfanya mtu afanye uamuzi wa kuipenda au kutoipenda lugha moja au zaidi anapokabiliwa na hali ya wingilugha katika jamii". Baker anaendelea kusema kuwa mielekeo ya lugha inaweza kugawanywa katika makundi mawili mapana kama ifuatavyo:-

i. **Mielekeo ya Kibinafsi ya Lugha** - Hii ni mielekeo inayotokana na mtu binafsi kuhusu lugha husika. Mielekeo ya kibinafsi inaweza ikawa chanya au hasi.

ii. **Mielekeo ya Kijamii ya Lugha** - Hii ni mielekeo inayopatikana katika kundi la watu au jamii nzima kuhusu lugha. Mara nyingi, mielekeo ya lugha katika kiwango hiki hufanya jamiilugha moja kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya jamii nyingine na hivyo hutaka iwezekanavyo kujitambulisha na lugha hiyo na tamaduni zake huku jamii ile ikipuuza lugha yao.

Mielekeo ya lugha ya kibinafsi na kijumla ikiwa chanya au hasi huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuinua au kushusha viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Iwapo mtu au jamii ina mielekeo chanya kuhusu lugha, kuna uwezekano mkubwa kuwa lugha ile itakuwa na viwango vya juu vya uthabiti wa kiisimujamii. Aidha, mielekeo hasi

ya mtu au jamii nayo itachangia katika lugha kuwa na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii kama utafiti huu ulivyobaini katika sura ya tano na sita.

### 2.4.1 Upimaji wa Mielekeo ya Lugha.

Upimaji wa mielekeo ya lugha ni ule utaratibu unaofuatwa katika kupima mielekeo ya watu kuhusu lugha yoyote ile katika jamii. Kama asemavyo Fasold (1984), katika upimaji wa mielekeo ya lugha, lazima mtafiti atilie maanani sababu mbalimbali ambazo husababisha watu kuwa na mielekeo tofauti kuhusu lugha. Sababu hizi ni kama vile, kuwepo kwa lugha nyingi katika jamii, hadhi za lugha mbalimbali katika jamii, jinsia, umri, maeneo ya kijamii lugha inamotumika n.k.

Kulingana na Baker (1992), upimaji wa mielekeo ya lugha unaweza kuwa wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja. Upimaji wa mielekeo ya lugha wa moja kwa moja huhitaji watafitiwa kuyajibu maswali ya hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha au mahojiano. Majibu yao baadaye hutumika na mtafiti kubaini mielekeo yao ya lugha husika. Baker anaeleza zaidi kuwa mtafiti anapotumia hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha, anafaa kutumia mizani ya likati ambayo hutoa majibu kwa mpangilio maalumu ili watafitiwa wachague jibu moja kati ya zile zilizotolewa kwenye mizani. Mizani ya likati hupanga majibu ifuatavyo:-

**(1) Nakubali kabisa. (2) Nakubali. (3) Sikubali au Sikatai. (4) Sikubali.(5) Sikubali kabisa.**

Upimaji mielekeo ya lugha usio wa moja kwa moja nao hupima mielekeo kwa kutumia njia ambazo hazitajulikana na watafitiwa. Njia hizi ni kama vile kutumia mijadala isiyo rasmi na uchunguzi shiriki na usoshiriki.

Walker (1982) alipendekeza kuwa mbinu zisizo za moja kwa moja za kupima mielekeo ya lugha zafaa kutumiwa kwanza na mtafiti kabla ya kutumia mbinu za moja kwa moja. Hii ni kwa sababu watafiti watatoa data ya kuaminika zaidi kuhusu mielekeo kwa vile hawafahamu kuwa wanatafitiwa. Baadaye mbinu za moja kwa moja hutumiwa ili kudhibitisha data hii zaidi. Hata hivyo, Baker (1992) anapendekeza kuwa, hata ingawa ni vizuri kufuata utaratibu huu wa Walker, ni muhimu sana kutumia mbinu zote mbili katika utafiti mmoja ili kupata matokeo ya kuaminika zaidi kuhusu mielekeo ya wahojiwa kuhusu lugha wanazozitumia.

Utafiti huu, ulilenga kuchunguza na kubainisha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Katika kupima mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, utafiti huu ulitumia mbinu za kupima mielekeo za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Tulitumia hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha ambazo zilikuwa katika mfumo wa mizani ya likati kama njia ya kupima mielekeo ya sampuli kwa njia ya moja kwa moja huku tukitumia mijadala isio rasmi ya kimakundi kama mbinu ya kupima mielekeo ya sampuli kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Matumizi ya mbinu za upimaji mielekeo ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja ilihakikisha kuwa utafiti huu uliweza kupima

mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa njia ya kina ili kupata matokeo ya kuaminika.

### 2.4.2 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha

Batibo (2005) anaeleza kuwa mielekeo ya lugha ni jambo la kawaida katika jamii. Batibo anafafanua kuwa mielekeo ya lugha hupatikana katika jamii iliyo na lugha moja au wingilugha. Katika jamii inayotumia lugha moja, mwelekeo wa lugha huwa mmoja tu kuhusu lugha yao wakati mwingi ukiwa mwelekeo chanya. Hata hivyo, katika mazingira ya jamii yenye wingilugha, mielekeo mbalimbali kuhusu lugha hujitokeza kutokana na hadhi ambazo zimeambatanishwa na lugha hizi. Kulingana na Batibo, mielekeo ya lugha hufuata ruwaza za mifumo ya kijamii na kiuchumi. Hii ina maana kuwa wanajamii huwa na mielekeo chanya kwa lugha ambazo zina hadhi ya juu kijamii na kiuchumi huku wakiwa na mielekeo hasi kuhusu lugha za hadhi ya chini katika jamii.

Maoni haya, ya kuunda mielekeo ya lugha kutokana na hadhi za lugha, yalikuwa muhimu kwa utafiti wetu. Hii ni kwa vile, kwa kutumia hojaji za mielekeo na matumizi ya lugha pamoja na mijadala isiyo rasmi ya kimakundi, maoni haya yalituongoza katika kutambua jinsi lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng zilivyopewa hadhi tofauti kimatumizi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hadhi mbalimbali za lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng nazo ziliibuwa mielekeo tofauti kuhusu lugha hizi nne kama matokeo ya utafiti huu yalivyobaini katika sura ya 5 na 6.

### 2.4.3 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha Barani Afrika.

Kwa vile mojawapo wa lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza kuhusu athari za mielekeo ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu hapa Kenya, ilikuwa muhimu kuzipitia tafiti nyingine za mielekeo ya lugha barani Afrika ili kuelewa zaidi jinsi tafiti za mielekeo ya lugha zilivyoendeshwa kwingineko Afrika. Kulingana na Adegbija (1994:1), "ni utafiti mchache tu ambao umefanywa barani Afrika kuhusu mielekeo ya lugha, hasa katika eneo la Sahara la Afrika, ikilinganishwa na bara nyingine ulimwenguni". Hivyo basi kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kuhusu mielekeo ya lugha na matokeo yake mbalimbali kwa kurejelea lugha za Kiafrika kama utafiti huu ulivyofanya.

Adegbija (1994) alifanya utafiti kuhusu mielekeo ya wakaazi wa mataifa ya Afrika kuhusu lugha zao za mama ikilinganishwa na lugha za kikoloni zilizokuwa zikitumiwa kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kibelgiji na kadhalika. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa mataifa mengi ya Kiafrika hasa katika eneo la Sahara yana mwelekeo chanya kuhusu lugha za kikoloni ikilinganishwa na lugha zao za mama. Lugha za kikoloni katika mataifa mengi ya Kiafrika zimepewa majukumu rasmi katika maeneo mengi ya kijamii huku lugha zao za mama zikiachiwa majukumu yasio rasmi na muhimu sana.

Kwa mujibu wa Adegbija (1994:21), "kupewa majukumu rasmi kwa lugha za kikoloni barani Afrika ndiyo sababu moja kuu ambayo huwafanya Waafrika kuzihama lugha zao za mama na kuanza kuzitumia lugha za kikoloni kwa wingi kwa vile lugha hizi za

kikoloni huonekana kuwa na manufaa mengi kiuchumi”. Hata hivyo, Adegbija anafafanua kuwa bado kuna jamii za Kiafrika kama vile jamii ya Wamaasai nchini Kenya ambazo zimeweza kudumisha utamaduni wao pamoja na lugha yao kwa wakati mrefu hata ingawa hakuna juhudi zozote zile zilizofanywa kuchunguza kuhusu suala kama hili.

Thiba (2000) ametafiti kuhusu historia ya sera ya lugha nchini Afrika Kusini na mielekeo ya lugha inayoibuliwa na sera hizi za lugha. Anaeleza kuwa mnamo miaka ya sabini serikali ya wakati ule ilianzisha sera ya lugha iliyohusu lugha mbili pekee yaani Kiafrikaans na Kiingereza kama lugha rasmi. Sera hii ya lugha kwa mujibu wa Thiba ilikabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa Waafrika na ambao ulifikia kilele kwa kufanyika maandamano yaliyohusisha walimu na wanafunzi wa Kiafrika ya kupinga sera hii ya lugha. Hatimaye, sera hii ya lugha ilifanyiwa mabadiliko kwa kuzinduliwa sera ya elimu kuhusu lugha nchini Afrika Kusini ambapo sera mpya ya lugha yenye lugha 11 rasmi ilianzishwa. Lugha hizi ni pamoja na Kiingereza, Kiafrikaans, isiZulu, isiXhosa, sePedi, seTswana, seSotho, xiTsonga, siSwati, tshiVenda na isiNdebele.

Hata ingawa nchi ya Afrika Kusini ina sera ya lugha inayohusisha lugha 11 nyingi zikiwa lugha za asili ya Kiafrika, Thiba (2000:23) anasema kuwa “walimu na wanafunzi wengi wa Kiafrika wana mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza kwa vile wanaiona kama lugha iliyo katika nafasi bora zaidi ya kuwawezesha kupata kazi baada ya kumaliza masomo”. Hata hivyo, Thiba anaendelea kufafanua kuwa bado kuna baadhi ya wazazi ambao wana mielekeo chanya kuhusu lugha zao za mama na wangependa watoto wao wajifunze lugha hizi ili kuhifadhi historia ya jamii yao na kuendeleza utamaduni wao.

Ennaji (2005) naye alitafiti kuhusu mielekeo ya lugha nchini Morocco kuhusu Kiarabu – kistandard, Kiarabu cha Kimorocco na Kifaransa. Ennaji anadai kuwa lugha ya Kifaransa na Kiarabu – Kistandard ndizo lugha zilizopewa hadhi ya juu kimatumizi ikilinganishwa na Kiarabu cha Morocco ambacho ndicho huonekana kama hifadhi ya uasili na utamaduni wa Wamorocco. Zaidi, Wamorocco wengi pia wana mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza kwa vile wanaiona kama lugha muhimu katika kiwango cha mawasiliano ya kimataifa kati ya Morocco na mataifa mengine ulimwenguni.

Sprenger – Tasch (2003) amechunguza kuhusu mielekeo ya lugha nchini Uganda kuhusu lugha ya matumizi katika elimu. Sprenger – Tasch amefanya hivyo kwa kuangalia mielekeo walionayo wenyeji wa Uganda kuhusu lugha ya Kiingereza, Kiganda, Kiswahili na lugha nyingine za mama kama lugha za kufunzia shuleni. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha kuwa lugha ya Kiingereza ndiyo ambayo inapendelewa zaidi na watu wengi kama lugha ya mafunzo shuleni. Hata hivyo, wazazi wengi walionyesha uzalendo na mwelekeo chanya kuhusu lugha zao za mama kwani ndizo lugha walizozitegemea kutumia ili kuwafikishia watoto wao masuala ya utamaduni na historia yao. Vile vile lugha ya Kiswahili ilichukiwa na watu kutoka jamii ya Baganda kama lugha ya mafunzo kwa vile ilionekana kama inayotoa ushindani kwa lugha yao ya Kibaganda. Hata hivyo, jamii nyingine pale Uganda zilikipendelea Kiswahili kama lugha ya mafunzo shuleni kwa vile ni mojawapo wa lugha mashuhuri kimatumizi katika eneo nzima la Afrika Mashariki.

Tafiti hizi zote zilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwa vile zilitufahamisha kuhusu matokeo mbalimbali ya utafiti kuhusu mielekeo ya lugha barani Afrika. Matokeo haya ya tafiti za mielekeo ya lugha barani Afrika yamebaini kuwa hata katika mataifa mengine ya Kiafrika, wazungumzaji wana mielekeo hasi kuhusu lugha za mama huku wakiwa na mielekeo chanya kuhusu lugha za kikoloni kama tu utafiti huu ulivyobaini katika sura za 5 na 6. Matokeo ya utafiti huu kama vile katika nchi nyingine za Afrika yalionyesha kuwa kwa jumla kuna mielekeo hasi kuhusu lugha za mama na mielekeo chanya kuhusu lugha za kikoloni kama vile Kiingereza.

### 2.4.4 Tafiti Kuhusu Mielekeo ya Lugha Nchini Kenya

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa nchini Kenya kuhusu mielekeo ya lugha. Baadhi ya tafiti hizi zimeelezewa hapa katika sehemu hii. Brenzinger (1992) anaeleza kuwa lugha nyingi nchini Kenya bado zina uthabiti na uhai mwingi kimatumizi kwa vile bado zina idadi kubwa ya wazungumzaji ambao wanazitumia katika maeneo mbalimbali ya kijamii katika shughuli zao za kila siku. Hata hivyo, kwa mujibu wa Brenzinger, kuna baadhi ya lugha nchini Kenya kama vile Suba ambazo zimo katika hatari ya kuangamia kutokana na ukweli kuwa zina idadi ndogo sana ya wazungumzaji wanaozitumia kimawasiliano katika maeneo tofauti ya kijamii.

Kwa mujibu wa Brenzinger (1992), kizazi cha watoto na vijana katika lugha ya Suba huwa hakina umilisi wowote wa lugha ya Suba kutokana na matumizi yao ya lugha nyingine kama vile Luo, Kiswahili na Kiingereza. Ni kizazi cha babu na nyanya tu ambacho kina umilisi wa kuridhisha katika lugha ya Suba. Hali kama hii ya vijana

kukosa umilisi wa lugha ya Suba ndiyo ile ile inayowakabili vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambao wana umilisi wa chini wa lugha ya Kikuyu kutokana na matumizi yao ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kama utafiti huu ulivyobainisha. Sababu nyingine ni kuwa wazungumzaji wa lugha kama vile Suba wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Suba jambo linalowapelekea kuihama kimatumizi na kuanza kutumia lugha nyingine wanaziona kuwa na hadhi kuliko lugha yao kama vile Luo, Kiswahili na Kiingereza.

Kuna tafiti kadhaa nchini Kenya ambazo zimefanywa kuhusu mielekeo ya lugha. Kioko na Muthwii (2001) walichunguza kuhusu mielekeo ya Wakenya kuhusu aina tatu za Kiingereza yaani Kiingereza cha Kenya, Kiingereza 'Standard' na Kiingereza cha Uingereza. Aina ya Kiingereza kilichopendelewa sana na Wakenya wengi ni Kiingereza Standard ambacho kilitokea kuwa marufu kwa Wakenya wengi mijini na vijijini. Hii ni kwa sababu, kama wanavyofafanua Kioko na Muthwii, aina hii ya Kiingereza ndiyo hutumika katika taaluma nyingi nchini Kenya kama lugha rasmi.

Muaka (2009) ametafiti kuhusu mielekeo ya lugha miongoni mwa vijana nchini Kenya. Muaka ameonyesha jinsi sera ya lugha nchini Kenya inavyoathiri matumizi ya lugha miongoni mwa vijana. Alifanya hivi kwa kubainisha mielekeo ya vijana mjini Nairobi na Kangundo kuhusu lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama kama vile Kikamba na jinsi mielekeo hii inavyotegemea sera ya lugha nchini Kenya. Sera ya lugha nchini Kenya inafanya lugha ya Kiingereza kuwa na majukumu mengi rasmi jambo linalowafanya vijana wengi mijini na vijijini kuwa na mwelekeo chanya kuhusu

Kiingereza ikilinganishwa na Kiswahili na lugha za mama. Aidha, Vijana wana mwelekeo chanya kuhusu Kiswahili ikilinganishwa na lugha za mama hapa nchini Kenya. Hata ingawa Muaka amezungumzia kuhusu mielekeo ya lugha miongoni mwa vijana, utafiti wake ni tofauti na utafiti huu kwa vile Muaka haonyeshi jinsi mielekeo ya lugha inavyoathiri viwango vya umilisi wa lugha na hatimaye viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha miongoni mwa vijana kama utafiti huu ulivyofanya. Aidha, utafiti wa Muaka umeegemea zaidi katika suala la uhamaji wa lugha bali sio suala la umilisi na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kama utafiti wetu ulivyofanya.

Babusa (2010) kwa kutumia mtazamo linganuzi, amelinganisha mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili kuhusu lugha ya Kiswahili na vile mielekeo hii inavyoathiri viwango vya umilisi wa lugha hii miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili mikoani Mombasa na Nairobi. Pia utafiti wa Babusa umeangalia tofauti za viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili kijinsia katika mikoa hii miwili. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa wanafunzi wa mkoa wa pwani walikuwa na mielekeo chanya zaidi kuhusu lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wale wa mkoa wa Nairobi. Wasichana nao walionyesha kuwa na viwango vya juu vya umilisi wa Kiswahili kuliko wavulana. Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi waliokuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiswahili walikuwa na viwango vya chini vya umilisi ilhali wengine wenye mielekeo hasi wakiwa na viwango vya juu vya umilisi.

Utafiti wa Babusa ni mwafaka kwa utafiti wetu kwani umechunguza kuhusu mielekeo ya lugha na athari zake kwa viwango vya umilisi wa lugha. Jambo hili ndilo tulilolichunguza

katika utafiti wetu lakini tofauti ikiwa tuliangalia lugha ya Kikuyu. Hata hivyo. Utafiti wa Babusa haujaligusia suala la jinsi mielekeo na umilisi wa lugha huathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha na hatimaye kuiingiza katika hatari ya kuangamia. Aidha, utafiti wetu haukulinganisha masuala ya mielekeo ya lugha na viwango vya umilisi kwa misingi ya kijinsia bali ulilenga kubaini athari za umilisi wa lugha kwa uthabiti wa lugha kama suala linalojikita katika jinsia zote za kike na kiume.

Furaha (1991) amechunguza jinsi mielekeo ya lugha inavyoathiri uteuzi wa lugha ya matumizi ya kila siku mjini Malindi. Utafiti huu umeonyesha kuwa uteuzi wa lugha ya matumizi mjini Malindi kwa kiasi kikubwa hutegemea mielekeo walionayo wazungumzaji wa lugha zile kuhusu kila lugha. Utafiti wenyewe uliangazia lugha nne zinazotumika kwa wingi mjini Malindi. Lugha hizi ni Kitaliano, Kiswahili, Kijerumani na Kiingereza. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa wakazi wa Malindi hupendelea Kitaliano kuliko lugha zile nyingine tatu. Lugha ya Kiswahili nayo inafuata huku lugha za mama zinazozungumzwa hapa zikionyesha hali ya kutopendelewa katika mazungumzo ya kila siku kutokana na usasa uliowaathiri wakazi wa Malindi.

Utafiti wa Furaha (1991) ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwani ulionyesha nafasi ya mielekeo ya lugha katika uchaguzi wa lugha ya matumizi ya kila siku katika jamii. Utafiti wetu pia ulionyesha jinsi mielekeo ya lugha inavyoathiri matumizi ya lugha miongoni mwa vijana katika jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Tofauti na utafiti wa Furaha, utafiti wetu ulilenga kuonyesha jinsi mielekeo ya lugha inavyoathiri umilisi

wa lugha za mama miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika na hatimaye kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu.

Okwany (1993) naye alitafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya kuhusu ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Sampuli yake ilikuwa wanafunzi 483 kutoka shule tatu za upili ambayo ilikuwa karibu idadi sawa na sampuli ya utafiti wetu uliokuwa na sampuli ya vijana 300 kutoka shule za upili katika kaunti za Nairobi na Kiambu. Utafiti wa Okwany uliweza kubainisha kuwa wanafunzi wengi wana mwelekeo chanya wa kijumla kuhusu lugha ya Kiswahili. Jambo hili kwa mujibu wa Okwany (1993) labda limechangiwa na Kiswahili kufanywa somo rasmi na linalotahiniwa kwenye mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na upili nchini Kenya. Tofauti na utafiti huu, utafiti wetu ulichunguza mielekeo ya vijiana wa jamii ya Kikuyu kuhusu lugha za mama tukizingatia lugha ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Vile vile, tofauti na utafiti wa Okwany, utafiti wetu uliegemea zaidi katika kubaini jinsi mielekeo ya lugha inavyoweza kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha kama vile Kikuyu miongoni mwa vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Kwa kifupi, tafiti tulizozipitia kuhusu mielekeo ya lugha nchini Kenya kama vile utafiti wa Babusa (2010), Muaka (2009), Muthwii (2001), Okwany (1993) na Furaha (1991) zimelijadili suala la mielekeo ya lugha bila kuhusisha mielekeo ya lugha na suala la uthabiti wa kiisimujamii wa lugha walizozitafitia. Tofauti na tafiti hizi, utafiti wetu mbali na kujihusisha na suala la mielekeo ya lugha, umepiga hatua zaidi ya kuonyesha jinsi mielekeo ya lugha huathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Hakika lengo la kijumla la

utafiti huu likuwa kule kuonyesha jinsi mielekeo na viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika inavyochangia katika kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu na uwezekano wa lugha ya Kikuyu kuwa katika hatari ya kuingia katika orodha ya lugha za mama zinazokabiliwa na hatari ya kuangamia pindi miaka inavyopita.

## 2.5 Umilisi wa Lugha

Utafiti huu pia katika lengo lake la tatu ulichunguza kuhusu viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na viwango vya umilisi wao wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Suala la mielekeo ya lugha huenda sambamba na suala la umilisi wa lugha. Hii ina maana kuwa iwapo wazungumzaji wana mielekeo hasi kuhusu lugha yao basi huenda ikawa pia hata viwango vyao vya umilisi wa lugha hii viko chini. Kama asemavyo Krauss (1992), idadi ya watu ambao wana umilisi kamili wa lugha zao za mama inazidi kupungua huku idadi ya watu walio na viwango vya chini vya umilisi wa lugha za mama ikizidi kuongezeka na hivyo kurudisha chini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama ulimwenguni.

Utafiti huu wetu mbali na kubaini mielekeo ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika, pia ulilenga kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu walivyo navyo vijana wa jamii ya Kikuyu. Katika kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika, utafiti huu ulitumia mitihani ya umilisi wa mawasiliano

na mijadala ya kimakundi. Aidha, utafiti huu ulilenga kutambua viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa kuhusisha zaidi kipengele cha umilisi wa kiisimu katika lugha na kwa kiasi fulani kipengele cha umilisi wa mbinu za lugha na wala sio vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii. Suala la upimaji wa viwango vya umilisi wa mawasilano limeelezewa zaidi katika sehemu ya upimaji wa umilisi wa mawasiliano katika sehemu 2.5.2.

### 2.5.1 Dhana ya Umilisi wa Mawasiliano.

Umilisi wa mawasiliano ni suala ambalo limejadiliwa na wanaisimu na wanaisimujamii kwa muda mrefu kufikia sasa. Mjadala huu zaidi umejikita katika kule kujaribu kutambulisha hasa ni vipengele vipi mzumgumzaji anafaa kuvimudu ili isemekane kuwa ana umilisi tosha wa lugha anayoizungumza na hatimaye kuelezewa kuwa ana umilisi wa mawasiliano. Baadhi ya wale ambao wamechangia pakubwa mjadala huu ni wataalamu kama vile Hymes (1972) na Canale na Swain (1980) na Nicuolo (1991). Wengine ni kama vile Nunn (2005), Flutcher na Davidson (2007), Lehaman (2009) na Chapelle na Brindley (2010).

Chomsky (1965) alizua dhana ya umilisi wa lugha. Kulingana naye, umilisi wa lugha ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kufahamu vyema sheria za kiisimu za lugha anayoizungumza. Sheria hizi ni kama vile kufahamu kuhusu leksia, fonetiki na othografia, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ya lugha husika. Mbali na kuzifahamu sheria za lugha, mzungumzaji anafaa kuwa na ule uwezo wa kutumia lugha

ile kwa njia sahihi anapozungumza na watu wengine. Hivi ni kusema kuwa mzungumzaji anafaaa kuwa na uwezo wa kutumia lugha ile kwa njia sahihi katika tukio halisi la uzungumzi.

Mtazamo huu wa Chomsky (1965) kuhusu umilisi wa lugha uliegemea katika masuala ya kiisimu pekee. Kulingana na Hymes (1972), mtazamo huu ulikuwa finyu kwa vile kulingana naye, kuzifahamu sheria za kiisimu za lugha pekee hakutoshi kumwezesha mtu kuweza kuitumia lugha kikamilifu katika jamii yake. Hivyo basi Hymes (1972) na wanaisimu wengine kama vile Savignon (1972) waliyapanua mawazo ya Chomsky kuhusu umilisi wa lugha kwa kuanzisha dhana ya umilisi wa mawasilano. Mbali na kuhusisha umilisi wa sheria za lugha, Hymes alifafanua kuwa umilisi wa mawasiliano pia huhusisha masuala ya kiisimujamii ya lugha yaani utendaji wa lugha ama kule kuweza kutumia lugha kwa ufaafu katika miktadha mbalimbali ya kijamii.

Nunn (2005) naye anaeleza kuwa suala la umilisi wa mawasiliano ni pana kuliko kufahamu sheria za kiisimu pekee za lugha husika. Zaidi ya kufahamu sheria za lugha, mzungumzaji lazima awe na kipengele cha utendaji katika lugha ambacho atakipata pindi anavyozidi kutangamana na wazungumzaji wengine katika jamii yake. Hii ni kwa sababu utendaji wa lugha hutegemea masuala yaliyo nje ya ujuzi wa kiisimu wa mzungumzaji katika lugha. Maoni haya yanalingana na ya Lehaman (2009:67) anapoelezea kuwa “umilisi wa mawasiliano haujifungi tu katika masuala ya kiisimu pekee. Kipengele cha umilisi wa kiisimu huwa tu kama msingi wa mfumo mzima wa umilisi wa mawasiliano”. Hivyo, kulingana na Lehman, ili mzungumzaji awe na umilisi kamili wa mawasiliano

lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kutumia lugha ile katika miktadha tofauti ya kijamii kwa usahihi.

Hymes (1972) , alihoji kuwa lazima kila mzugumzaji wa lugha aweze kufahamu jinsi ya kutumia lugha husika katika miktadha mbalimbali ya kijamii. Hymes aliongezea kipengele muhimu kuhusu umilisi wa mawasiliano ambacho kilikuwa kile cha umilisi wa kiisimujamii. Hata hivyo Hymes alikubaliana na Chomsky (1965) kuwa ni jambo la kimsingi kwa kila mzungumzaji wa lugha kuwa na umilisi wa kiisimu (sheria za lugha) wa lugha husika. Kwa kifupi, mtazamo wa Hymes kuhusu umilisi wa mawasilano ulihusisha vipengele viwili muhimu ambavyo ni:-

i. umilisi wa kiisimu ambao ulihusu uwezo wa mzungumzaji wa kuzifahamu vyema sheria za lugha na
ii. umilisi wa kiisimujamii ambao ulihusu uwezo wa mzungumzaji wa kuwa na utendaji wa lugha yaani kujua jinsi ya kutumia lugha ipasavyo katika miktadha tofauti ya kijamii.

Mchango wa Chomsky, Hymes na Savignon ni muhimu kwa utafiti wetu kwa vile tulipima viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kupitia vigezo vya kiisimu na kiisimujamii kupitia stadi za kuongea, kuandika na kusoma (taz. sehemu 5.6).

Wanaisimujamii wengine waliochangia masuala zaidi kuhusu umilisi wa mawasiliano ni Canale na Swain (1980, 1981). Mbali na vipengele vya umilisi wa kiisimu na umilisi wa kiisimujamii, Canale na Swain waliongezea kipengele cha tatu cha umilisi wa mawasiliano ambacho ni kipengele cha umilisi wa mbinu za mawasiliano. Kulingana na Canale na Swain "ili mzungumzaji awe na umilisi wa mawasilano, anahitajika vile vile kuweza kuwa na mbinu za kimazungumzo na zisizo za kimazungumzo za kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki kwa vile labda ana upungufu katika vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano kama kile cha kiisimu. Mzungumzaji basi lazima afahamu mbinu anazoweza kutumia ili mawasiliano yasivunjike kama vile kurudia rudia jambo, kutumia maelezo wakati amekosa neno la dhana fulani, kukwepa kutumia maneno asioyafahamu vyema kati ya mbinu nyingine". Mzungumzaji vile vile lazima afahamu matumizi ya ishara mbalimbali anazoweza kutumia kuhakikisha kuwa mawasiliano hayavunjiki. Kipengele hiki kwa mujibu wa Canale (1983) ni tofauti sana na vipengele vile viwili vya awali vya umilisi wa mawasiliano. Hii ni kwa sababu kipengele hiki kinategemea mambo kama vile ukakamavu wa mzungumzaji anapozungumza na hutumika tu wakati mzungumzaji amepungukiwa katika kipengele cha kiisimu na kile cha kiisimujamii anapozungumza.

Katika utafiti wetu ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika hawana ujuzi wa kipengele hiki cha umilisi wa mbinu za mawasiliano. Hii ni kwa sababu katika stadi ya kuongea kwa lugha ya Kikuyu, mazungumzo yalikatika tu pindi waliposhindwa kuyatamka maneno ya Kikuyu ama walipokosa msamiati mwafaka wa lugha ya Kikuyu katika mazungumzo. Ukosefu wa ujuzi wa kipengele cha

mbinu za mawasiliano miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kilipelekea mawasiliano kuvunjika jambo ambalo halikutokea walipokuwa wakizungumza kwa kutumia lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Canale (1984) aliongezea kipengele cha nne cha umilisi wa mawasiliano. Kulingana naye, mzungumzaji pia anahitajika kuwa na umilisi wa uchanganuzi usemi. Hii ina maana kuwa kila mzungumzaji katika kitendo cha mawasiliano anafaa kuwa na uwezo wa kuchanganua maana na miundo mbalimbali ya lugha husika ili kuweza kuunda vipashio vyenye ruwaza sahihi katika lugha andishi na lugha ongezi. Canale anapendekeza kuwa kila mzungumzaji lazima awe na uwezo wa kutumia vipashio kama vile viwakilishi, viunganishi na visawe vya maneno kati ya vingine kwa njia yenye muwala na muumano ili apate kushiriki kikamilifu katika mazungumzo. Zaidi, lazima mzungumzaji aweze kufahamu kaida nyingine za matumizi ya lugha kama vile kufahamu jinsi ya kuanzisha na kukomesha mazungumzo na kupokezana zamu katika mazungumzo. Kwa hivyo, vipengele vinne vya umilisi wa mawasiliano kwa mujibu wa Canale na Swain (1980,1981) na Canale (1984) ni:-

i. Umilisi wa kiisimu.
ii. Umilisi wa kiisimujamii.
iii. Umilisi wa mbinu za mawasiliano.
iv. Umilisi wa uchanganuzi usemi.

Utafiti huu, hata ingawa umejihusisha na suala la umilisi wa mawasiliano, umejikita zaidi katika kipengele cha kwanza cha umilisi wa mawasiliano ambacho ni umilisi wa kiisimu

wa lugha na kwa kiasi fulani kipengele cha umilisi wa mbinu za mawasiliano. Umilisi wa kiisimu wa lugha kama asemavyo Verhoeven (1992) hurejelea ufahamu ama kuwa na ujuzi wa sheria za lugha. Vipengele vya umilisi wa kiisimu wa lugha ni kama vile uwezo wa mzungumzaji wa kuunda na kutambua miundo ya sentensi sahihi na isiyo sahihi katika lugha husika (sintaksia), kufahamu msamiati mbalimbali wa lugha (leksimu), kuwa na matamshi bora (fonolojia) na kufahamu maana ya maneno (semantiki) na uundaji wa maneno na sentensi sahihi (mofolojia na sintaksia). Ujuzi huu wote kulingana na Verhoeven ndio msingi wa kufahamu vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano.

Kwa kifupi, umilisi wa kiisimu ni ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria hizi za lugha kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki katika mazungumzo. Haingewezekana kupima umilisi wa mawasiliano kupitia kipengele cha kiisimujamii kwa vile ingelazimu kuwatazama vijana waliounda sampuli ya utafiti katika miktadha tofauti ya matumizi ya lugha jambo ambalo lingechukuwa muda mrefu nje ya muda uliotengewa utafiti wetu.

### 2.5.2 Upimaji wa Umilisi wa Mawasiliano.

Utafiti huu ulilenga kutambua viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Upimaji wa umilisi wa mawasiliano unaelezewa kama,

> ‘***kitendo cha kutathmini ujuzi alio nao mzungumzaji wa lugha fulani katika sheria za lugha na uwezo wake wa kutumia lugha hii katika miktadha mbalimbali ya kijamii. (Tafsiri yetu)***
>
> (Chapelle na Brindley 2010:247)

Katika kupima viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng, utafiti huu ulihusisha kipengele cha umilisi wa kiisimu katika lugha na kipengele cha umilisi wa mbinu za lugha na wala sio vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii.

Mitihani mingi ya upimaji wa umilisi wa mawasiliano zaidi huegemea katika kipengele cha umilisi wa kiisimu na wala sio vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano kama vile umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa mbinu za mawasiliano na umilisi wa uchanganuzi usemi. Hii ni kwa sababu, kama asemavyo Rubin (1992:44), “sio muhimu kila mara kupima vipengele vyote vya umilisi wa mawasiliano ili kufahamu kama mzungumzaji ana umilisi wa mawasiliano ama la”. Hakika, kama anavyoendelea kuelezea Rubin, “ni nadra sana kupata vipengele vyote vya umilisi wa mawasiliano vikipewa uzito sawa katika utafiti iwapo vyote vitahusishwa katika upimaji wa umilisi wa mawasilano”.

Hata ingawa umilisi wa kiisimu haumaanishi kuwa mzungumzaji ana umilisi wa kutosha katika mawasiliano, umilisi huu wa kiisimu ndio msingi ama nguzo ya umilisi wa mawasiliano. Kama asemavyo Nicuolo (1991), umilisi wa mawasiliano huanza kwa umilisi wa kiisimu wa lugha yaani kufahamu na kuzimudu sheria za lugha. Akifafanua zaidi, Nicuolo anasema kuwa hii labda ndio sababu mara nyingi mitihani mingi ya

kupima umilisi wa mawasiliano huegemea zaidi katika umilisi wa kiisimu kwa kupima uwezo wa mzungumzaji wa kutumia sheria za lugha sana sana kupitia stadi za lugha zinazolenga maandishi na mazungumzo yaani stadi za kuongea, kusoma na kuandika. Aidha, Nicuolo anadai kuwa vipengele vile vingine vya umilisi wa mawasiliano, kama vile umilisi wa kiisimujamii, huhitaji kipindi kirefu cha wakati kupimwa kwani vimejikita zaidi katika masuala ya tamaduni za jamii na tabia lugha za mzungumzaji.

Mcmanara (2000) naye anasema kuwa kimsingi, mitihani ya umilisi wa mawasiliano yafaa kupima uwezo wa mzungumzaji katika kiwango cha sheria za lugha na vile vile katika kiwango cha utendaji wa lugha. Hata hivyo, mitihani mingi ya umilisi wa mawasiliano hujikita katika kupima umilisi wa kiisimu ambao huchukuliwa kama msingi wa kufahamu lugha yoyote ile.

Kulingana na Brown (2005), mitihani ya umilisi wa mawasiliano inafaa kuzingatia masuala manne muhimu yaani:-

i. Iweze kupima uwezo wa kimawasiliano wa mzungumzaji kwani hili ndilo jambo la kimsingi katika mawasiliano.
ii. Ijikite katika maeneo na miktadha ya kijamii ambayo mzungumzaji inaifahamu vyema.
iii. Iweze kuibua ubunifu wa mzungumzaji katika lugha husika wala si kutoa kile alichoulizwa pekee.

iv. Ihusishe stadi za kimsingi za lugha husika kama vile kuandika, kusoma na kuzungumza.

Nicuolo (1991), Rubin (1992), Verhoeven (1992) na Mcmanara (2000) wana msimamo wa pamoja kuwa suala la upimaji wa umilisi wa mawasiliano ni tata na ambalo linandelea kuibua hisia mbalimbali za wanaisimu tofauti katika mjadala unaoendelea hadi sasa. Hii ni kwa sababu mitihani mingi ya kupima umilisi wa mawasiliano huegemea zaidi katika upimaji wa umilisi wa kiisimu hata ingawa hiki sicho kipengele pekee kinachohusishwa na umilisi wa mawasiliano.

Verhoeven (1992) hata hivyo anasema kuwa kuna aina mbili kuu za upimaji wa umilisi wa mawasiliano ambazo zote hutumika na wanaisimujamii. Aina hizi mbili ni pamoja na:-

i. Mtihani ya umilisi wa mawasiliano ya moja kwa moja.
ii. Mitihani ya umilisi wa mawasiliano isiyo ya moja kwa moja.

**2.5.3 Mitihani ya Umilisi wa Mawasiliano ya Moja kwa Moja.**

Mitihani ya umilisi wa mawasiliano ya moja kwa moja hulenga kupima umilisi wa mawasiliano wa mzungumzaji kwa kuzingatia vipengele vyote vinne vya umilisi wa mawasiliano (Verhoeven 1992). Vipengele hivi ni pamoja na umilisi wa kiisimu, umilisi wa kiisimujamii, umilisi wa mbinu za mawasiliano na umilisi wa uchanganuzi usemi.

Kama asemavyo Ingram (1985), mitihani ya umilisi wa mawasiliano ya moja kwa moja hujikita katika kupima utendaji halisi wa mzungumzaji wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali ya mazungumzo na vile vile huchunguza tabia lugha za mzungumzaji. Basi, mitihani ya aina hii ya umilisi wa mawasiliano bali na kupima umilisi wa kiisimu wa mzungumzaji pia hupima masuala ya viziada lugha katika mazungumzo. Kwa vile mitihani hii hujihusisha na tabia lugha za mzungumzaji, huchukua muda mrefu na labda jambo hili huelezea ni kwa nini mitihani hii si maarufu katika upimaji wa umilisi wa mawasiliano. Zaidi, kama asemavyo Rubin (1992), mitihani ya aina hii ni ngumu kutekelezwa kwa vile inalazimu kumtazama na kumchunguza mzungumzaji katika miktadha halisi ya matumizi ya lugha, jambo ambalo ni ngumu kupima, hutumia wakati mwingi kutekeleza na ni ngumu kudhibiti.

**2.5.4 Mitihani ya Umilisi wa Mawasiliano isiyo ya Moja kwa Moja.**

Aina hii ya upimaji wa umilisi wa mawasiliano ndiyo ambayo hutumika kwa wingi katika kupima umilisi wa mawasiliano. Mitihani hii hupima umilisi wa mawasiliano kwa kuegemea kipengele cha umilisi wa kiisimu wa lugha na hivyo basi hupuuza vipengele vingine vya umilisi wa mawasiliano. Msisitizo hapa ni kuwa umilisi wa kiisimu wa lugha ndio msingi na nguzo ya umilisi wa mawasiliano (Nicuolo 1992). Naye Mcmanara (2000) anaongeza kuwa upimaji wa mawasiliano usio wa moja kwa moja hujikita katika kupima masuala ya kiisimu kama vile uwezo wa kutumia msamiati mbalimbali wa lugha, matamshi na masuala ya sarufi ya lugha.

Tunapotumia mitihani ya umilisi wa mawasiliano isiyo ya moja kwa moja, lugha hugawanyishwa katika vipengele mbalimbali vya kiisimu vinavyoweza kupimika kwa uwazi zaidi na kwa njia isiyo na mapendeleo (Rubin 1992). Vipengele vinavyotumika kwa wingi ni stadi za lugha kama vile kuzungumza, kuandika, kusoma na kusikiliza. Nicuolo (1992) na Mcmanara (2000) wana maoni kuwa kati ya stadi hizi nne za lugha, stadi ya kusikiliza ni ngumu kupima kwa vile imejificha katika stadi nyingine za lugha kama vile kuzungumza na kuandika. Kwa hivyo, stadi zinazohusishwa zaidi na upimaji wa umilisi wa kiisimu wa lugha ni stadi za kuongea, kuandika na kusoma. Uwezo wa mzungumzaji wa L2 katika stadi hizi za lugha ndio hutumiwa kama kigezo cha kupima kiwango cha umilisi alionao katika lugha hiyo na ndio msingi wa kuelezea kama ana umilisi wa mawasiliano ama la. Kwa mujibu wa Rubin, upimaji wa aina hii wa umilisi wa mawasiliano si wa moja kwa moja kwa vile unapima tu kipengele kimoja cha umilisi wa mawasiliano ambacho ni umilisi wa kiisimu.

Utafiti wetu ulitumia mitihani ya umilisi wa mawasiliano isiyo ya moja kwa moja katika kupima viwango vya umilisi wa vijana wa jamii ya Kikuyu katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Haya yalifanywa kupitia stadi za kuzungumza, kusoma na kuandika (taz 5.8). Vijana waliounda sampuli ya utafiti huu walikuwa vijana 300 kutoka shule mbalimbali za upili katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Maelezo kuhusu vijana ni nani na mifano ya lugha za vijana mijini barani Afrika yametolewa katika sehemu inayofuata ya 2.6

## 2.6 Dhana ya vijana

Utafiti huu ulichunguza kuhusu athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hivyo basi kundi la vijana lilikuwa kigezo muhimu kwa utafiti huu na ilibidi dhana ya vijana ifafanuliwe kwa kina kwa kuegemea zaidi matumizi na mielekeo yao ya lugha mijini. Utafiti huu umejihusisha na sampuli ya vijana pekee wala sio marika mengine katika jamii kwa vile vijana ndio huhusika zaidi na matumizi ya lugha nyingi zinazopatikana katika jamii. Kama asemavyo Kerswill (2000:182) "kundi la vijana ndilo huonyesha sifa ya kutaka kutalii matumizi ya lugha mbalimbali katika jamii na pia ndilo kundi ambalo hupenda kufanyia lugha majaribio na mabadiliko mengi kuliko kundi lingine lile katika jamii".

Aidha, Eckert (2003:117) ana maoni kuwa "mbali na kundi la vijana kuhusika na matumizi ya lugha nyingi katika jamii, sifa nyingine kuu ya utamaduni wa vijana ulimwenguni ni ile sifa ya vijana kutaka kufanya uvumbuzi mwingi katika matumizi ya lugha hadi kiwango cha kuziunda lugha na misimbo mipya". Ni kwa misingi ya maelezo kama haya ya Kerswill (2000) na Echert (2003), ambapo utafiti huu ulitumia kikundi cha vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika utafiti huu kwa makisio kuwa vijana hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 2.6.1 Vijana ni akina nani?

Kikundi cha vijana kimekuwepo katika takriban jamii zote ulimwenguni ambapo jamii huwa imegawanyishwa katika mfumo wa rika unaotambua watoto, vijana na wazee kama wadau wa kimsingi katika kila jamii. Kulingana Keniston (1975) suala la kijana ni nani limetolewa fasili mbalimbali na watu na mashirika anuai. Fasili hizi tofauti hutumia vigezo mbalimbali kama vile misingi ya kijamii (kitamaduni), umri, kisheria, kiuchumi na kisaikolojia. Hata hivyo, kama asemavyo Clark (1992), kigezo cha kufafanua dhana ya kijana ni nani kilichotumiwa kwa wingi na watu na mashirika mengi ulimwenguni ni kile cha umri.

Katika jamii nyingi ulimwenguni, vijana huelezewa kupitia misingi ya kitamaduni na kijamii. Kwa mujibu wa Clark (1992), katika jamii nyingi kijana hutambuliwa kama binadamu ambaye amefikisha kiwango cha kuoa au kuolewa na anaweza akapashwa tohara na basi kushiriki mafunzo ya kunga za utu uzima na uzazi. Clark anaendelea kuelezea kuwa katika jamii nyingi, vijana wa kike na kiume huwekewa vigezo tofauti vya kuonyesha kuwa sasa wao wamefikia rika la kutambuliwa kama vijana. Vijana wa kike na kiume hupewa majukumu mbalimbali na jamii yao na pia hupewa mafunzo tofauti yanayoafiki majukumu yao mapya. Hata hivyo, kuna jamii ambazo humrejelea mtu kama kijana iwapo hajaoa hata umri wake ukiwa ni miaka arobaini. Aidha, kuna jamii nyingine ambazo hutilia maanani kigezo cha kubalehe kama kipimo cha kijana ni nani hata ikiwa mtu amebalehe akiwa na umri wa miaka kumi.

Kerswill (2000) analifafanua suala la ujana kisaikolojia anaposema kuwa hiki ni kipindi cha mabadiliko kutoka utotoni hadi utu uzima ama kipindi cha maadalizi ya mtu kuchukuwa majukumu ya mtu mzima katika jamii yake. Kipindi hiki humfanya mtu apitie awamu ya mabadiliko ya kimaumbile na kisaikolojia. Kwa kifupi, kwa mujibu wa Clark, kijana ni mtu yeyote aliye kati ya mtoto na mtu mzima kimaumbile na kitabia. Kielimu, Clark anasema kuwa ujana ni kipindi katika maisha ya mtu kati ya miaka ya kuachana na mfumo rasmi wa elimu rasmi na wakati mtu anapopata kazi yake ya kwanza ama anapofikisha umri wa kutafuta kazi rasmi.

Wyman (2012:217) anaeleza kuwa "jamii tofauti ulimwenguni pia huelezea dhana ya vijana kupitia kigezo cha mielekeo walionayo kuhusu kikundi hiki. Baadhi ya mielekeo hii ni kama vile:-

i. Kikundi cha watu ambao bado hawajakomaa na wasioweza kujisimamia maishani na kwa hivyo ni lazima wawe chini ya ulinzi wa watu wazima.

ii. Kikundi katika jamii ambacho kimeundwa na watu wakaidi na waasi kwa vile wanang'ang'ania uhuru wa kujitawala.

iii. Kikundi ambacho kimeundwa na watu ambao wanaweza kuitetea na kuilinda jamii yao au nchi.

iv. Kikundi cha watu ambacho ndicho tegemeo la kuendeleza jamii au nchi na ndio viongozi wa kesho".

Hata ingawa kuna vigezo tofauti vya kuelezea fasili ya dhana ya kijana, kigezo cha umri ndicho kinachotumika kwa wingi na mataifa na mashirika mbalimbali ulimwenguni. Jambo lililo wazi ni kuwa kigezo hiki cha umri kinazua utata mwingi kwani viwango tofauti tofauti vya umri vimetumika kuwawekea vijana mipaka ya umri. Wyman (2012) anasema kuwa hata ingawa ujana huchukuliwa na jamii nyingi kama kipindi cha mpito kutoka hali ya utegemevu utotoni hadi ya hali ya kujitegemea kama mtu mzima, maelezo haya hayafafanui vyema kijana ni nani na kwa hivyo kigezo mwafaka cha kutumiwa ni umri.

Kwa mujibu wa shirika la Umoja wa Mataifa, vijana ni watu katika jamii ambao wana umri kati ya miaka 15 – 24. Maelezo haya ya Umoja wa Mataifa yalitolewa mara ya kwanza katika sherehe za kuanzisha rasmi siku ya kimataifa ya vijana mnamo mwaka wa 1985. Nchi nyingi ulimwenguni zimefuata kigezo hiki cha Umoja wa Mataifa katika kuwawekea vijana mipaka ya umri katika fasili zao. Nchi hizi ni kama vile Thailand, Afrika Kusini, Tanzania na Namimbia kati ya nchi nyingine ulimwenguni ambazo huwachukulia vijana kama watu walio kati ya umri wa miaka 15 – 24. Hata hivyo, maelezo haya ya umoja wa mataifa kuhusu umri wa vijana yanakuwa na utata kwani *Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto la 1989* linaelezea kuwa mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka 18 kama mtoto ilhali nalo *Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za Binadamu* hutambua vijana kama watu walio na umri wa miaka 18 kuendelea juu.

Mashirika mengine yaliyofafanua vijana kwa kutumia kigezo cha umri ni kama vile Shirika la Afya Duniani linalosema kuwa vijana ni watu walio na umri wa kati ya miaka 15 – 24 lakini wanafafanua zaidi wanaposema kuwa kuna kundi la vijana chipukizi walio kati ya umri wa miaka 10 – 19 na watu wadogo walio kati ya umri wa miaka 20 – 24. Shirika la UNESCO (2004) nalo linaeleza kuwa fasili ya dhana ya kijana ni ya kimuktadha kwani fasili hii mara nyingi hutegemea miktadha ya jamii hizi. Hata hivyo, shirika hili linaweka mipaka ya umri wa vijana kuwa kati ya miaka 15 – 24 kukiwa na makundi mawili ya vijana. Kikundi kimoja ni cha vijana chipukizi kati ya umri wa miaka 15 – 19 na watu wakubwa wachanga walio kati ya miaka 20 – 24. Shirika la Umoja wa Afrika nalo kwa upande wake linasema kuwa kijana ni mtu yeyote katika jamii ya Kiafrika aliye na umri kati ya miaka 15 -34.

Nchini Kenya, kigezo cha umri pia kimetumiwa katika kufafanua dhana ya kijana. Katiba ya nchi ya Kenya (2010) inaeleza kijana kama mtu yeyote yule ambaye amehitimu umri wa miaka 18 na kwa hivyo ameanza kupewa haki sawa kama watu wengine katika nchi ya Kenya. Hivyo, mtu aliyehitimu umri wa miaka 18 lakini asiyezidi miaka 35 huhesabika kama kijana ilhali yeyote chini ya miaka 18 huhesabiwa kama mtoto. Hata hivyo, Wizara ya Vijana nchini Kenya kupitia sera ya kitaifa kuhusu vijana nchini Kenya ya mwaka wa 2006 inasema kuwa kijana ni mtu aliye kati ya umri wa miaka 15 – 30. Katika jedwali, umri wa vijana kwa mujibu wa mashirika mbalimbali unaonyeshwa ifuatavyo:-

**Jedwali 2: Umri wa Vijana**

| SHIRIKA | UMRI WA KIJANA |
|---|---|
| UNESCO/ILO/UN Secretariat | 15 – 24 |
| UN HABITAT | 15 – 32 |
| UNICEF/WHO/UNFPA | 15 – 24 |
| THE AFRICAN YOUTH CHARTER | 15 – 35 |
| AFRICAN UNION | 15 – 34 |
| MINISTRY OF YOUTH – KENYA | 15 – 30 |

Katika utafiti huu, ambao uliwahusisha vijana wa jamii ya Kikuyu kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika, tulitumia kigezo cha umri katika kuteua sampuli yetu ya vijana. Baada ya kutathmini vigezo mbalimbali vya umri kutoka kwa mashirika na mataifa mbalimbali taifa la Kenya likiwemo, tulipata kuwa kigezo cha umri ambacho kimetumika kwa wingi ni kile ambacho kinaweka umri wa chini wa vijana kuwa miaka 15 na ule wa juu kuwa miaka 24. Kwa hivyo, tuliteua sampuli ya vijana ambao umri wao ulikuwa kati ya miaka 15 hadi 18. Hii ni kwa sababu huu ndio umri wa vijana wengi ambao wanasoma katika shule za upili nchini Kenya na ambazo zilitumia katika kuunda jumuiya ya utafiti huu. Hasa, mtafiti aliwahusisha wanafunzi wa kidato cha 3 na 4 kwa vile alikuwa na uhakika kuwa karibu vijana hawa wote wangekuwa katika kikundi hiki cha miaka 15 -18.

### 2.6.2 Vijana na Matumizi ya Lugha Mijini Barani Afrika.

Marie (2010) anaeleza kuwa kuanzia mwishoni mwa miaka ya sabini na mwanzoni mwa miaka ya themanini kuendelea mbele, miji mingi mikuu barani Afrika imeshuhudia kuzuka kwa lugha mpya za mawasiliano ambazo anaziita lugha za mijini. Marie anaendelea kuelezea kuwa kwa vile lugha nyingi za mijini zilizozuka hapa Afrika zinatokana na vijana wanaoishi mijini basi ni mwafaka zaidi kuziita lugha za vijana mijini.

Naye Kiessling na wenzake (2004:97) wanaeleza kuwa "vijana katika miji mingi barani Afrika wanaendelea kuunda lugha zao wenyewe na kwa kufanya hivi wanajitenga mbali na matumizi ya lugha za mama na kizazi cha wazee. Vijana hufanya hivi kwa kutumia msamiati kutoka kwa lugha nyingine zilizopo katika sehemu za mijini wanamoishi. Kiessling na wenzake wanatoa mifano ya lugha zilizoundwa na vijana mijini barani Afrika kama vile lugha za:-

i. Nouchi mjini Abidjan nchini Ivory Coast.

ii. Camfranglais mijini Yaoude na Douale nchini Cameroon.

iii. Lingala ya Bayankee katika miji ya Kinshasa (Zaire) na Brazzaville (Congo).

iv. Isccimto na Tsotositaal mjini Johannesburg nchini Afrika Kusini.

v. Sheng mjini Nairobi nchini Kenya".

Kwa mujibu wa Marie (2010), lugha za vijana mijini zilipoanza kuzuka na kupata umaarufu kimatumizi zilikabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa wazazi, sekta ya elimu na wanaisimu kwa jumla kwani zilionekana kama lugha ambazo zilitatiza shughuli

za elimu hasa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha rasmi shuleni. Pia, lugha hizi za vijana mijini Afrika zilionekana kama lugha ambazo ziliwatenga vijana kutoka kwa wazazi wao na lugha za mama jambo ambalo lingewafanya wazisahau lugha zao za mama mbali na kuupoteza utamaduni wao.

Mclaughlin (2009) anaongeza kuwa hata ingawa lugha za vijana mijini hapa barani Afrika zinaendelea kukua na kupata umaarufu kimatumizi, bado lugha hizi hazijapata utambuzi rasmi kutoka kwa serikali husika. Aidha, bado watu wengi kama vile walimu na wazazi wana mielekeo hasi kuhusu lugha za vijana mijini Afrika kwani zinatatiza juhudi za elimu hasa ufunzaji na ujifunzaji wa lugha rasmi za masomo kama vile Kiingereza na Kiswahili hapa nchini Kenya. Marie (2010) anaongeza kusema kuwa baadhi ya lugha hizi za vijana mjini Afrika, kama vile Sheng nchini Kenya na Tsotsitaal nchini Afrika Kusini, huonekana kama lugha zilizotokana na magenge ya kihalifu katika vitongoji duni vya miji hii na kwa hivyo wakaazi wa miji hii bado wanaona ugumu katika kuzikubali kama lugha halali.

Hata ingawa kuna mielekeo hasi kama hii kuhusu lugha za vijana mjini barani Afrika, Kiessling (2009) anaeleza kuwa licha ya mielekeo hii hasi, lugha hizi zinaendelea kupata umaarufu miongoni mwa vizazi vyote na vile vile zimeanza kusambaa hata katika sehemu za mashambani. Marie (2010) anaongezea kuwa lugha hizi pia zimeanza kutafitiwa kwa dhati na wanaisimu kutokana na sifa zake kama vile ubunifu wa kiisimu na mabadiliko ya haraka katika msamiati wake jambo ambalo huzifanya kuwa lugha za kipekee miongoni mwa lugha nyingine katika miji mikubwa barani Afrika. Naye Githiora

(2002) ana maoni kuwa kufikia sasa lugha nyingi za vijana katika miji mikubwa barani Afrika zimeanza kusambaa kwa haraka na kuwa maarufu sio tu kwa vijana mbali hata kwa watu wazima. Anatoa mfano wa Sheng mjini Nairobi kama kielelzo kizuri cha lugha ya vijana mijini Afrika ambayo pole pole inageuka kuwa lugha ya kila mtu.

Iraki (2004) anaeleza kuwa kuna sababu mbalimbali zinazosababisha kuzuka kwa lugha za vijana mijini kama vile sheng. Mojawapo ya sababu hizi ni ile hali ya wingilugha mijini na haja ya vijana kutaka kujitenga kimawasiliano kutoka kwa wazazi wao. Hata hivyo, lugha za vijana hutofautiana kutoka mji mmoja hadi mwingine kutegemea lugha zinazozungumzwa hapo, utamaduni wa jamii katika miji hiyo na hali ya kiuchumi ya wazungumzaji. Hii ina maana kuwa

> ***"Hata ingawa kuna masuala ya kijumla ambayo yanaweza kupatikana katika lugha za vijana mijini barani Afrika, kila mji una upekee wake na hivyo kuna masuala ya kiisimu yaliyo tofauti kutokana na muundo wa kiisimu na kijamii wa miji hii, historia ya ukuaji wa miji hii, sera za utawala wa kikoloni kuhusu lugha kati ya masuala mengine."(tafsiri yetu)***
>
> (Mclaughlin 2009:2)

Marie (2010) anaeleza kuwa hata ingawa kuna miji ambayo imeshuhudia kuzuka kwa lugha za vijana hapa barani Afrika, bado kuna miji mingine mikubwa ambayo hakujapatikana uchipukaji wa lugha za vijana. Anatoa mifano ya miji kama vile Addis Ababa - Ethiopia, Monorovia - Liberia, Windhoek – Namibia na Bujumbura nchini Burudi.

### 2.7 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha Nchini Kenya.

Utafiti huu ni wa kiisimujamii ambao ulichunguza kuhusu athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa umilisi wa lugha za mama kama vile Kikuyu miongoni mwa

vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Aidha, lengo la nne la utafiti huu lilikuwa kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika mjini ya Nairobi, Kiambu na Thika. Kulikuwa na haja ya kufafanua kwa ujumla kuhusu hali ya kiisimujamii ya lugha nchini Kenya ambako kunapatikana lugha hizi nne zinazochunguzwa katika utafiti huu yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.  Maelezo kuhusu hali ya kiisimujamii ya lugha nchini Kenya ndiyo yaliyotolewa katika sehemu hii ili kutoa taswira ya makundi ya lugha zinazozungumzwa nchini Kenya (taz.jedwali 3) na migawanyiko ya lugha hizi kimaeneo nchini Kenya (taz. mchoro 2)

Nchi ya Kenya ina zaidi ya lugha 40 zenye asili ya Kiafrika zinazozungumzwa zikiwakilisha familia tatu kuu za lugha barani Afrika yaani Niger – Congo, Nilo – Sahara na Afro – Asiatic. Nchini Kenya kuna takriban asilimia 65 ya watu wanaozungumza lugha za Kibantu, asilimia 30 ya watu wanaozungumza lugha za Kinilote, asilimia 3 ya watu wanaozungumza Kicushite huku asilimia 2 ikizungumzwa na watu wengine walio nje ya makundi haya matatu ya lugha. Hivyo basi, nchini Kenya lugha nyingi zinapatikana katika makundi haya mapana nyingi ya lugha hizi zikiwa katika makundi ya Bantus, Nilotes na Cushites.

Mbali na zile lugha za kiasili nchini Kenya, kuna lugha nyingine za kigeni ambazo zimepata umaarufu kimatumizi kutoka sehemu mbalimbali duniani. Baadhi ya lugha hizi ni lugha kutoka bara Uropa kama vile Kiingereza, Kifaransa, na Kijerumani. Vile vile kuna lugha nyingine za kigeni kutoka bara Asia kama vile Kihindi na Kipakistani. Aidha,

lugha nyingine za kigeni ambazo huzungumzwa nchini Kenya ni kama vile Kichina, Kijapan na lugha ya Kiarabu. Lugha hizi zinaonyeshwa kulingana na migwawanyiko yake ya kimakundi katika jedwali hili la Moseley (2010) hapa chini.


**Jedwali 3: Makundi ya Lugha Nchini Kenya**

| | | |
|---|---|---|
| **Hunters-gatherers** | Boni, Dahalo, El-Molo, Ndorobo/Dorobo, Sanye | |
| **Bantus** | Western | Abaluhyia/Luhya, Kisii, Kuria, Gusii |
| | Central | Kikuyu, Kamba/Akamba/Wa-kamba, Meru, Embu, Tharaka, Mbeere |
| | Coastal | Mijikenda (Digo, Duruma, Rabai, Ribe, Kambe, Jibana, Chonyi, Giriama, Kauma), Taveta, Pokomo, Taita , Swahili (Bajun, Pate, Mvita, Vumba, Ozi, Fundi, Siyu, Shela, Amu) |
| **Nilotes-paranilotes** | Nilotes | Luo |
| | Teso | Iteso, Turkana |
| | Maasai | Maasai, Samburu, Njemps |
| | Kalenjin | Nandi, Kipsigis, Elgeyo, Sabaot, Marakwet, Tugen, Terik, Pokot |
| **Cushites** | Somali, Rendille, Galla, Borana/Boran, Gabbra, Orma, Sakuye | |
| **Nyingine** | Europeans, Asians (Hindus, Pakistanis), Arabs | |

Kutoka:(Moseley 2010:23)

Aidha, lugha zote za kiasili na migawanyiko yake kijiografia nchini Kenya zinaonyeshwa katika ramani ya lugha za kiasili nchini Kenya ya Lewis (2009:202) ifuatavyo:-

**Mchoro 2: Ramani ya Jamii za Kiasili na Lugha zao Nchi Kenya**




Kutoka: (Lewis 2009:202)

## 2.8 Ruwaza za Matumizi ya Lugha Mijini Nchini Kenya.

Katika miji mingi mikubwa nchini Kenya kunayo hali ya mtagusano wa lugha na basi ruwaza za matumizi ya lugha katika miji hii huashiria hali ya wingilugha (Wendo 2009) . Mifano ya miji mikubwa nchini Kenya ambayo ina hali ya wingilugha ni kama vile Nairobi, Mombasa, Kisumu, na Nakuru kati ya miji mingine. Katika miji kama hii kuna matumizi ya lugha za mama kama vile Kikuyu kwa wingi kutegemea jamii mbalimbali zinazoishi katika miji hii. Kwa mfano, mji wa Nairobi una wakaazi kutoka karibu kila jamii nchini Kenya na karibu lugha zote za mama nchini Kenya huzungumzwa hapa ijapokuwa kwa viwango vya chini kidogo ikilinganishwa na na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Iraki (2004) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili, ambayo ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya, pia hutumika na wakaazi wengi mijini kuwezesha mawasiliano baina ya jamii tofauti katika shughuli zao za kila siku. Iraki anafafanua zaidi kuwa lugha ya Kiingereza, ambayo pia ni lugha rasmi nchini Kenya, nayo ni maarufu mijini hasa katika uendeshaji wa shughuli rasmi kama vile elimu na shughuli za kiserikali. Kulingana na Muaka (2011), mbali na lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha za mama kama vile Kikuyu, lugha ya Sheng nayo hutumiwa kwa wingi kimawasiliano hasa miongoni mwa vijana katika miji mikubwa kama vile Nairobi, Kiambu, Thika, Kisumu na Mombasa na hata katika sehemu za mashambani.

Utafiti wetu ulichunguza kuhusu athari za matumizi ya Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng kwa matumizi ya lugha za mama kama vile Kikuyu miongoni

mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Sampuli ya vijana wa jamii ya Kikuyu katika utafiti huu iliteuliwa kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Miji hii mitatu imekaribiana kwa masafa huku mji wa Kiambu ukiwa takriban kilomita 20 kutoka mji wa Nairobi na mji wa Thika ukiwa karibu kilomita 40 kutoka mji wa Nairobi. Hii basi ina maana kuwa wakaazi wa miji hii mitatu huingiliana kwa wingi katika shughuli zao za kila siku. Inatokea kuwa lugha zinazotumiwa katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ni karibu sawa. Hakika katika miji hii mitatu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng hutumika kwa wingi katika mawasiliano ya kila siku miongoni mwa vizazi vyote. Katika utafiti huu tulijikita katika matumizi ya lugha nne tu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ambazo ni Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Lugha hizi nne zimetolewa maelezo ya kina katika sehemu inayofuata hasa ruwaza za matumizi yake katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika na vile vile mielekeo ya kijumla ambayo imeambatanishwa na lugha hizi na wazungumzaji wake.

### 2.8.1 Ruwaza za Matumizi ya Lugha za Mama nchini Kenya

Muaka (2009) anaeleza kuwa hata ingawa kuna karibu lugha za mama 42 au zaidi nchini Kenya, lugha hizi hazitumiki kwa wingi katika maeneo muhimu ya kijamii nje ya mipaka yake ya kijamii. Muaka anaendelea kufafanua kuwa kati ya lugha hizi za mama ni lugha chache tu ambazo zinatumika kwa wingi nje ya mipaka yake ya kijamii. Anatoa mifano ya lugha kama vile, Kikuyu, Kiswahili, Kiluhya, Kijaluo, lugha za kundi la Kalejin na Kikamba. Hakika, ni katika maeneo machache tu ya kijamii katika sehemu za vijijini

ambako lugha nyingi za mama hutumika kwa wingi huku kwingineko katika kiwango cha kitaifa zikiwa hazina majukumu yoyote rasmi isipokuwa Kiswahili, ambayo ni mojawapo wa lugha ya mama nchini Kenya.

Mbali na kuwa lugha za mawasilano katika sehemu nyingi za mashambani nchini Kenya, lugha za mama pia zimependekezwa kutumika shuleni kama lugha za kufunzia hasa katika madarasa ya kwanza matatu ya shule za msingi. Shirika la UNESCO (1953) lilihimiza matumizi ya lugha za mama shuleni kwa kusema kuwa lugha hizi ndizo lugha mwafaka zaidi katika ufundishaji shuleni. Msimamo wa UNESCO ni kuwa lugha za mama zafaa kutumika kufunzia shuleni hadi kiwango cha juu iwezekanavyo na hasa zafaa zaidi kutumika kufunzia watoto katika miaka yao ya kwanza shuleni ili kuwezesha mabadiliko laini ya kimazingira kwa mtoto kutoka nyumbani hadi shuleni.

Nchini Kenya, kulingana na Mbaabu (1996), sera ya lugha katika mfumo wa elimu huelekeza kuwa watoto wanaojiunga na shule za msingi mashambani wanafaa kufunzwa kupitia lugha za mama ambazo huzungumzwa na wakaazi wengi katika eneo lao kwa miaka ya kwanza mitatu wakati lugha ya Kiswahili ikitumika kufundisha katika sehemu za mijini. Baadaye, mafunzo yanafaa kuendeshwa kwa lugha ya Kiingereza kuanzia darasa la nne kwenda juu. Hata hivyo, kama asemavyo Khejeri (2014), sera hii ya lugha ya kufundisha kwa kutumia lugha za mama katika madarasa ya kwanza matatu katika shule za msingi imekabiliwa na upinzani mkubwa hadi sasa huku masomo katika shule za msingi mashambani na mijini yakiendeshwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kuanzia darasa la kwanza.

### 2.8.2 Mielekeo ya Kijumla Kuhusu Lugha za Mama Nchini Kenya

Khejeri (2014) anaeleza kuwa matumizi ya lugha za mama nchini Kenya yamo katika njia panda. Hii ni kwa sababu kuna mielekeo tofauti iliyoambatanishwa na matumizi ya lugha hizi hapa nchini Kenya. Kwa upande mmoja, kuna mielekeo chanya kuhusu matumizi ya lugha za mama ambapo kwanza huonekana kama lugha mwafaka zaidi katika mawasiliano katika sehemu za mashambani. Kama asemavyo Muthwii (2002), lugha za mama nchini Kenya huwa zimetengewa jukumu la kuwezesha mawasiliano katika maeneo mengi ya kijamii mashambani kama vile mawasiliano nyumbani, kanisani na katika biashara. Hii ni kwa sababu sehemu nyingi za mashambani nchini Kenya huwa zina wakaazi wengi kutoka jamii moja jambo ambalo huzipa lugha zao za mama nafasi bora kama lugha za mawasiliano katika shughuli zao za kila siku.

Aidha, lugha za mama nchini Kenya, kama ilivyo katika sehemu nyingine ulimwenguni, hutengewa jukumu la kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za jamii mbalimbali kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Basi nchini Kenya, kama asemavyo Muaka (2009) watu wengi wana mwelekeo chanya kuhusu lugha za mama kama vyombo mwafaka vya kuhifadhi utamaduni na historia za jamii zao na kuzipitisha kwa vizazi vijavyo.

Hata hivyo, kuna pia hali ya mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha za mama nchini Kenya. Kama anavyoeleza Muthwii (2002), kuna mielekeo hasi kuhusu matumzi ya lugha za mama kama lugha za kufundishia shuleni. Muthwii anafafanua zaidi kuwa kuna upinzani mkubwa nchini Kenya wa matumizi ya lugha za mama katika elimu kutoka kwa wadau muhimu katika sekta ya elimu kama vile wazazi na walimu ambao huona lugha za

mama kama lugha zisizo na faida katika elimu mbali na kuathiri ujifunzaji wa lugha za pili kama vile Kiingereza na Kiswahili.

Naye Muaka (2009) anafafanua kuwa mielekeo mingine hasi kuhusu matumizi ya lugha za mama ni kuwa lugha hizi huambatanishwa na watu wa hadhi ya chini maishani nchini Kenya. Inatokea kuwa mtu asiyefahamu lugha za matumizi mapana nchini Kenya hasa Kiingereza na Kiswahili bali huifahamu lugha ya mama huonekana kama mtu aliyepitwa na wakati na asiyestaraabika.

Aidha, kama afafanuavyo Khejeri (2014) matumizi ya lugha za mama nchini Kenya huambatanishwa na uenezaji wa ukabila kwa kuwagawanyisha wananchi katika msingi ya kikabila. Khejeri anaelezea zaidi kuwa hii ndiyo sababu moja kuu iliyofanya nchi ya Kenya kuteua lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa ili iweze kudidimiza matumizi ya lugha za mama hasa katika utekelezaji wa majukumu ya kitaifa. Muaka (2009) anaongezea kuwa nchini Kenya lugha za mama huonekana kama lugha ambazo hazihimizi utangamano wa kitaifa kwa vile watu hujiona na hufikiri kama makabila tofauti kupitia matumizi ya lugha zao za mama.

**2.8.3 Lugha ya Kiswahili**

Kiswahili, kama asemavyo Mbaabu (1996), ni lugha asili nchini Kenya ambayo imo katika familia ya lugha ya Bantu na hasa katika familia ndogo ya lugha ya Wabantu wa pwani pamoja na lugha nyingine za pwani kama vile Mijikenda, Taveta, Pokomo na Taita. Mbaabu anafafanua zaidi kuwa lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali kama vile

Kipate, Kimvita, Kiamu, Kivumba, Kisiyu, Kibajuni, Kimtang'ata kati ya lahaja nyingine ambazo huzungumzwa katika upwa wa bahari ya Hindi nyingi ya lahaja hizi zikizungumzwa nchini Kenya na Tanzania.

Muaka (2011) anaeleza kuwa hata ingawa lugha ya Kiswahili ni lugha ya kiasili nchini Kenya, lugha hii imekuwa na kusambaa kimatumizi hadi kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya mbali na kuwa lugha ya Kimataifa. Kufikia karne ya 13, lugha ya Kiswahili ilikuwa imeanza kukua na kuenea hadi kufikia kiwango hiki chake cha sasa wakati ilipoanza kutumiwa kama lugha ya kibiashara kati ya wageni wa awali wa pwani ya Afrika Mashariki kama vile Wareno na Waarabu na wenyeji wa Kiafrika wa pwani ya Afrika Mashariki. Kutokana na maingiliano ya lugha ya Kiswahili na lugha za kigeni kuanzia karne ya 13, Muaka anaeleza kuwa lugha hii imeathirika na lugha hizi kwa kukopa msamiati mbalimbali kutoka kwa lugha kama vile Kiarabu, Kireno, Kireno na hata Kiingereza kati ya lugha nyingine.

Mbali na biashara, Mwaro (2002) anaeleza kuwa wamishenari nao walipofika hapa Afrika Mashariki walisaidia sana katika kufanikisha maenezi ya Kiswahili. Wao walihakikisha kuwa lugha hii imeyafikia mataifa ya Kimagharibi kupitia uchapishaji wa vitabu kama vile kamusi na vitabu vya isimu ya Kiswahili. Mwaro anaendelea kufafanua kuwa hasa wamishenari wa Kijerumani walichangia sana katika uchapishaji na utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili.

Jambo lingine ambalo limesaidia katika kukiendeleza na kukieneza Kiswahili kimataifa kama asemavyo Amatubi (2002) ni kule kuanzishwa kwa vituo vya masomo ya Kiafrika katika vyuo vikuu vingi kule Uingereza, Marekani na Ujerumani. Katika vituo hivi, lugha ya Kiswahili huwa ni kipengele kimoja muhimu katika programu zao za kimasomo. Lugha hii huwa muhimu kwa vyuo hivi haswa vinapofanya utafiti barani Afrika. Aidha, Mwaro (2002) anaeleza kuwa shughuli za utangazaji pia zimechangia katika kukisambaza Kiswahili ulimwenguni kote na hivyo kukifanya kuwa lugha ya Kimataifa. Idhaa maarufu za utangazaji duniani kama vile *B.B.C, V.O.A, Dutche Welle, Radio China na Radio Moscow* huwa na vipindi vya matangazo kwa Kiswahili. Idhaa hizi basi huchangia katika kuikuza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa.

Vita vya kwanza na vya pili vya dunia navyo vilitoa mchango wa kipekee katika kusambaza lugha ya Kiswahili katika maeneo mapya ulimwenguni (Amatubi 2002). Lugha hii ilitumika na wanajeshi kama lugha ya mawasiliano hapa Afrika Mashariki na kati. Wanajeshi hawa walipofika katika sehemu nyingine ulimwenguni waliweza kuifikisha lugha hii huko na kuchangia katika kuifanya lugha ya kimataifa.

### 2.8.4 Ruwaza za Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya

Kwa mujibu wa Muaka (2011), lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya kiasili kutoka nchini Kenya ambayo ina matumizi mapana zaidi kuliko lugha nyingine yoyote ile. Kwanza kabisa, lugha hii hutumika kama lugha ya taifa nchini Kenya lengo kuu likiwa ni kuwaunganisha wananchi wote nchini na kujenga utaifa. Kama asemavyo Mwaro (2002),

kwa muda mrefu kuanzia enzi za uhuru, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumiwa kama lugha ya taifa nchini Kenya kuwaleta pamoja Wakenya, kujenga utaifa na kukuza uzalendo miongoni mwa Wakenya. Vile vile Kiswahili ndiyo lugha ambayo hutumiwa na serikali ya Kenya kuzifikisha sera zake za kiuongozi kwa wananchi katika pembe zote za Kenya na hutumiwa na wanasiasa na viongozi katika hotuba zao kwa wananchi.

Hivi karibuni lugha ya Kiswahili ilifanywa kuwa lugha ya rasmi nchini Kenya na kujiunga na lugha ya Kiingereza ambayo kwa muda mrefu imekuwa lugha rasmi pekee nchini Kenya. Kiswahili kimepewa hadhi yake mpya ya kuwa lugha rasmi katika katiba mpya iliyopitishwa nchini Kenya mnamo mwaka wa 2010. Kama lugha rasmi nchini Kenya, lugha ya Kiswahili sasa inaweza ikatumika kutekeleza majukumu yote rasmi kama inavyofanya lugha ya Kiingereza.

Mbali na kutumika kama lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya, lugha ya Kiswahili pia hutumika kama lingua franka ya kibiashara nchini Kenya hasa biashara ndogo ndogo miongoni mwa Wakenya Githiora (2002). Hii ni kwa sababu, kama anavyofafanua zaidi Githiora, lugha ya Kiswahili imesambaa kote nchini na basi ndiyo lugha mwafaka zaidi ya kutumiwa na Wakenya katika maingiliano yao ya kibiashara hasa mijini ambako kuna hali ya wingilugha.

Aidha, lugha ya Kiswahili inatumika kwa wingi katika vyombo mbalimbali vya habari kama lugha ya utangazaji katika idhaa za redio na runinga na uandishi wa magazeti ambayo huwa na toleo la Kiswahili. Kuhusu haya, Githiora (2002) anasema kuwa

matumizi mengine ya Kiswahili nchini Kenya ni katika utangazaji mbali na ukweli kuwa lugha ya Kiswahili pia hutumika katika masuala ya uchapishaji wa vitabu kwa wingi.

### 2.8.5 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha ya Kiswahili Nchini Kenya

Muaka (2011) anaeleza kuwa hata ingawa Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya na vile vile lugha ya kimataifa, Wakenya kwa jumla hawajakitambua Kiswahili kama lugha inayostahili kuwa na hadhi ya juu kuliko lugha ya Kiingereza nchini Kenya. Kiswahili nchini Kenya kwa upande mmoja hupewa hadhi ya juu kimatumizi kuliko lugha nyingine zote za kiasili kama vile Kikuyu. Hata hivyo, kwa upande ule mwingine, Kiswahili hupewa hadhi ya chini kimatumizi ikilinganishwa na lugha ya Kiingereza ambayo hutekeleza jukumu la lugha rasmi pekee nchini Kenya. Hii ni kwa sababu, kama asemavyo Wendo (2009), hata ingawa Kiswahili kimepewa majukumu ya lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya huku lugha ya Kiingereza ikiwa na jukumu la lugha rasmi pekee, lugha ya Kiingereza ndiyo bado lugha inayotumika kwa wingi katika maeneo yote rasmi kama vile bungeni na katika masuala ya elimu na utawala jambo ambalo lugha ya Kiswahili haijaweza kulifikia kama lugha rasmi.

Aidha, kama anavyoeleza Gachiri (2009) Wakenya wengi hawaioni lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa bali tu kama lugha moja maarufu nchini Kenya na kwa hivyo kwao sio lugha ambayo inaweza ikawaletea maendeleo kama vile lugha ya Kiingereza. Wendo (2009) anaongeza kuwa Kiswahili huchukuliwa tu kama lugha ya kuwaunganisha Wakenya na kuondoa ukabila nchini Kenya. Zaidi, lugha ya Kiswahili kama anavyoendelea kueleza Wendo huchukuliwa na watu wengi kama lugha ngumu kujifunza

na kufikia kiwango cha kuizungumza kwa usahihi kama inavyozungumzwa na wenyeji wa pwani ya Kenya ambako kuna chimbuko la lugha hii.

### 2.8.6 Lugha ya Kiingereza

Lugha ya Kiingereza imekuwa ikitumika nchini Kenya kuanzia enzi za wamishonari na wakoloni. Baada ya kongamano la Berlin la mwaka wa 1886 la ugawanyaji na unyakuzi wa bara la Afrika na mataifa ya Ulaya, Kiingereza kiliingizwa na wakoloni kwa kiwango kikubwa barani Afrika hata ingawa kilikuwa tayari kimeingizwa barani na wamishenari na walowezi.

Kulingana na Mazrui na Mazrui (1998), hata ingawa aina ya Kiingereza kinachofundishwa na kuandikiwa vitabu nchini Kenya ni ile ya Kiingereza cha Uingereza kinachozungumzwa na Malkia wa Uingereza, watu wengi nchini Kenya huzungumza aina ya Kiingereza cha Kenya na hivyo kuna aina nyingi ya Viingereza ambavyo huzungumzwa hapa nchini Kenya kutegemea sana sana asili ya Wakenya mbalimbali. Zaidi, Kiingereza cha Kenya kimegawanyika katika Kiingereza cha mijini na Kiingereza cha mashambani. Muaka (2009) naye anaeleza kuwa Kiingereza kinachozungumzwa nchini Kenya kimepewa mguso wa lugha za jamii za kiasili. Hii ina maana basi kuwa kuna aina mbalimbali za Kiingereza zinazozungumzwa nchini Kenya ambazo ni tofauti na kile Kiingereza halisi.

### 2.8.7 Ruwaza za Matumizi ya Kiingereza nchini Kenya

Kiingereza, amabayo ni lugha ya kigeni nchini Kenya huwa na hadhi ya juu kuliko lugha zote za kiasili nchini Kiswahili kikiwemo. Hii ni kwa sababu lugha hii imeambatanishwa na faida nyingi kwa wazungumzaji wake kama vile kujipatia masomo shuleni, kupata kazi baada ya masomo na kuinuka kwa hadhi ya mzungumzaji katika jamii miongoni mwa faida nyingine. Mazrui na Mazrui (1998) wanaeleza kuwa hata baada ya nchi ya Kenya kujipatia uhuru, Kiingereza kilibakia kuwa lugha rasmi na hivyo ndiyo lugha iliyotumiwa katika shughuli zote rasmi nchini Kenya kama vile utawala na elimu.

Kutokana na hali ya Kiingereza kuwa lugha rasmi nchi Kenya tangu uhuru, lugha hii ilipata hadhi ya juu ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili na lugha mbalimbali za mama. Wendo (2009) anaongezea kuwa hadhi ya juu ya lugha ya Kiingereza nchini Kenya hulazimu karibu kila mtu na hasa kizazi kile kichanga kujifunza lugha hii. Wendo anafafanua zaidi kuwa nguvu za Kiingereza kama lugha rasmi nchini Kenya ni za kiwango cha juu hivi kwamba karibu kila kitu ambacho ni rasmi huandikwa kwa lugha hii.

Kutokana na hadhi yake kama lugha rasmi nchini Kenya, lugha ya Kiingereza pia hufundishwa kama lugha ya pili kwa watoto shuleni. Lugha hii hufundishwa kama somo linalotahiniwa na vile vile ndilo somo la kufundishia masomo mengine yote shuleni isipokuwa masomo ya lugha kama vile Kiswahili. Hata ingawa Kiingereza ni lugha ya kigeni iliyoingia nchini Kenya mwishoni mwa karne ya 19, bado ndiyo lugha ambayo

inatumika katika karibu maeneo yote rasmi kama vile katika elimu, bungeni, utawala na katika biashara za kimataifa.

### 2.8.8 Mielekeo ya Kijumla Kuhusu Lugha ya Kiingereza Nchini Kenya

Ongechi (2002) anaeleza kuwa mwelekeo wa kijumla kuhusu matumizi ya lugha ya Kiingereza nchini Kenya ni chanya. Ongechi anafafanua kuwa hata ingawa ni kama tu robo moja ya Wakenya ambao inaweza kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha nchini Kenya, lugha hii bado ndiyo inayopendelewa zaidi kama lugha rasmi na lugha ya kufunzia shuleni ikilinganishwa na lugha kama Kiswahili ambayo pia ni lugha rasmi nchini Kenya. Vile vile, kama asemavyo Wendo (2009), Wakenya wengi wana mwelekeo chanya kuhusu Kiingereza kwa kuwa ni lugha ambayo inawawezesha kupata ajira za kitaaluma baada ya masomo na ilhali ni lugha ambayo humfanya mtu kuonekana kuwa na hadhi ya juu katika jamii iwapo ana ufasaha wa kutosha wa lugha hii.

Hata hivyo, kama asemavyo Muaka (2009), mwelekeo hasi kuhusu Kiingereza nchini Kenya ni kuwa Kiingereza ni lugha ambayo hutumiwa kugawanyisha Wakenya kimatabaka. Hii ni kwa sababu Kiingereza huchukuliwa kama lugha ya wasomi na watawala wanaoishi maisha ya hadhi ya juu ikilinganishwa na watu wa tabaka la chini wasiokimudu Kiingereza kikamilifu au hawakifahamu hata kidogo.

### 2.8.9 Lugha Msimbo ya Sheng

Sheng ni lugha msimbo iliyochipuka katika miaka ya 60 hasa mwishoni mwa miaka hii katika mitaa ya watu wa mapato ya chini mashariki mwa jiji la Nairobi kuanzia mtaa wa Kaloleni kabla ya kusambaa katika mitaa mingine (Iraki 2004). Iraki anaendelea kueleza kuwa chimbuko hasa la lugha msimbo ya Sheng ni mtaa wa Kaloleni jijini Nairobi na baadaye lugha msimbo hii iliweza kusambaa katika mitaa mingine mashariki mwa jiji la Nairobi kama vile Jericho na Bahati. Lugha msimbo ya Sheng ilichipuka kama mchanganyiko wa lugha mbalimbali katika mazingira changamano ya wingilugha katika jiji la Nairobi.

Mbaabu (1996) anaeleza kuwa kuchipuka kwa lugha msimbo ya Sheng kulikuwa kama suluhisho la hali ya wingilugha katika mji wa Nairobi na kulitokana na hali ya ukosefu wa uwiano na utaifa katika jamii na sera ya lugha inayowafanya Wakenya kuzungumza lugha kwa mpangilio wa Kitriglosia ambako kuna lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama. Hivyo, uchipukaji wa Sheng ulitokana na haja ya kijamii baada ya ukosefu wa mfumo thabiti wa sera ya lugha nchini Kenya. Hata hivyo, Iraki (2004) ana maoni tofauti na haya anaposema kuwa mbali na kuwepo kwa mfumo wa kitriglosia wa matumizi ya lugha nchini Kenya na ambao unasisitiza zaidi matumizi ya lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama, bado Sheng ingechipuka. Hii ni kwa sababu vijana mjini Nairobi baada ya kukabiliwa na mazingira ya wingilugha na kuwa hawakuwa na umilisi kamili wa lugha yoyote katika mazingira hayo, basi hawakuwa na budi kutumia ubunifu wao wa kiisimu kujiundia lugha yao wenyewe.

Kimuundo, kama wasemavyo Abdulaziz na Osinde (1997), Sheng ina mfumo wa sintaksia ya Kiswahili hata ingawa imekopa vipengele vingine vya kiisimu kama vile fonolojia, mofolojia na leksia kutoka kwa lugha mbalimbali zinazopatikana mijini Nairobi kama vile Kiingereza, Kiswahili na baadhi ya lugha za mama zikiwemo lugha za Kikuyu, Kimasai, Luo, Luhya na kadhalika. Hii huenda ndiyo sababu inayomfanya Iraki (2004) kudai kuwa Sheng ni kama aina ya Kiswahili na huzungumzwa na vijana hasa katika mitaa ya watu wa mapato ya chini iliyoko mashariki mwa jiji la Nairobi. Iraki anaongeza kuwa Sheng ni lugha msimbo ambayo imeundwa kwa kukopa maneno kutoka kwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha mbalimbali za mama, Kifaransa kati ya lugha nyingine nyingi ambayo yote yameunganishwa pamoja kwa kufuata sheria za kisintaksia za lugha ya Kiswahili.

Hata ingawa ni vigumu kutoa asilimia sahihi ya maneno ya lugha mbalimbali yaliyotumika kuunda msamiati wa lugha msimbo ya Sheng, Iraki (2004), akitumia kamusi ya Sheng – English yenye karibu vidahazo 800, anasema kuwa huenda asilimia 20 ya maneno ya Sheng yamekopwa kutoka kwa lugha ya Kiswahili, asilimia 13 kutoka kwa lugha ya Kiingereza huko asilimia 67 ikitoka kwa lugha nyingine mbalimbali zinazozungumzwa jijini Nairobi na vitongoji vyake.

### 2.8.10 Ruwaza za Matumizi ya Sheng nchini Kenya

Kwa mujibu wa Iraki (2004) ruwaza za matumizi ya Sheng zimefanyiwa utafiti na watafiti mbalimbali kama vile Mbaabu (1996) na Githiora (2002) miongoni mwa wengine. Kinachoibuka kutoka kwa tafiti hizi ni kuwa Sheng ni lugha msimbo ya vijana

wengi katika miji mbalimbali nchini Kenya na hasa katika mji wa Nairobi katika mitaa ya watu wa mapato ya chini. Iraki anazidi kufafanua kuwa lugha msimbo ya Sheng vile vile hutumiwa na baadhi ya watu wazima na hasa wale walio chini ya miaka 60 kwani kama anavyoeleza watu hawa walikuwa na umri wa miaka kama 20 wakati Sheng ikichipuka mjini Nairobi mnamo miaka ya sitini.

Aidha, kwa mujibu wa Githiora (2002), Sheng ni maarufu kimawasiliano miongoni mwa familia za mitaani mjini Nairobi, wafanyakazi wa kujiajiri kama vile wachuuzi, vijana wa kuegesha magari, wafanyakazi za juakali kati ya wengine. Hata hivyo, kwa sasa lugha ya Sheng imeanza kupata umaarufu mkubwa kimatumizi na imeanza kupenya na kuwa lugha ya matumizi kwa watu wa madaraja karibu yote mijini. Lugha msimbo ya Sheng, kwa mujibu wa Muaka (2011), pia imeanza kutumika hata katika vyombo mbalimbali vya habari kama vile redio, runinga na baadhi ya magazeti nchini Kenya na vile vile imeanza kusambaa kutoka mitaa ya watu wa mapato ya duni katika miji kama vile Nairobi na kuanza kutumika katika maeneo mengine mengi ya kijamii kama vile vyombo vya habari na katika sanaa kama vile muziki na uigizaji.

### 2.8.11 Mielekeo ya kijumla Kuhusu Lugha ya Sheng Nchini Kenya

Kulingana na Githiora (2002), mwelekeo wa kijumla kuhusu Sheng nchini Kenya ni hasi. Hii ni kwa sababu Sheng bado sio lugha iliyopewa utambuzi rasmi na serikali ya Kenya na kwa hivyo imebaki tu kuwa kama msimbo wa mtaani. Kwa kiasi kikubwa, lugha msimbo ya Sheng nchini Kenya huchukuliwa kama msimbo wa vijana kutoka mitaa ya

watu wa mapato ya chini katika miji mikubwa nchini Kenya kama vile Nairobi. Aidha, Sheng pia huonekana kama msimbo wa watu wa daraja la chini wanaoishi katika mitaa duni katika miji mikubwa nchini Kenya.

Mielekeo mingine hasi kuhusu Sheng ni kuwa kutoka kwa sekta ya elimu nchini Kenya. Hii ni kwa sababu msimbo huu huonekana kama lugha inayotinga ujifunzaji wa lugha rasmi nchini Kenya ambazo ni Kiingereza na Kiswahili na ambazo pia hutumika kuendesha masomo shuleni. Kulingana na Iraki (2004), umaarufu wa matumizi ya Sheng miongoni mwa vijana hasa katika sehemu za mijini nchini Kenya ni tatizo kubwa katika ujifunzaji wa sarufi sahihi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza shuleni. Zaidi, lugha msimbo ya Sheng, kama asemavyo Githiora (2011), huonekana na Wakenya wengi kama msimbo chafu na msimbo unaohusishwa na makundi ya kijambazi katika mji mikubwa nchini Kenya ili kuficha siri za matendo yao maovu. Wazazi wengi katika miji mikubwa nchini Kenya nao huiona Sheng kama msimbo unaotumiwa na vijana kuweka mpaka wa kimawasiliano kati yao na wazazi wao (Iraki 2004). Vile vile wazazi huichukulia Sheng kama msimbo wa ukaidi miongoni mwa vijana na msimbo usio na faida zozote kielimu na hatimaye kiuchumi. Hata hivyo, kwa upande wao, vijana huwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha msimbo ya Sheng. Kulingana na Iraki (2004) hii ni kwa sababu vijana wengi mijini Kenya huipenda Sheng kwa vile ni msimbo ambao wao huutumia kimawasiliano kuhifadhi siri zao na kujitenga kutoka kwa wazazi wao.

Hata ingawa lugha ambazo zimetolewa maelezo hapa ni lugha nne tu yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, kuna lugha nyingine nyingi ambazo zinazungumzwa

nchini Kenya. Sera ya lugha nchini Kenya imezipanga lugha hizi zote kulingana na majukumu yake mbalimbali zinazotekeleza nchini. Kuna lugha rasmi ambazo ni Kiswahili na Kiingereza na ambazo hutekeleza majukumu yote rasmi nchini Kenya. Pia kuna lugha ya taifa ambayo ni lugha ya Kiswahili ikiwa na jukumu kuu la kuunganisha Wakenya na kupigana na ukabila. Hatimaye kuna kikundi cha lugha za mama ambacho hujumuisha lugha mbalimbali zinazozungumzwa na makundi tofauti ya kiasili nchini Kenya. Hata hivyo, kuna vile vile lugha za kigeni zinazozungumzwa nchini Kenya hata ingawa hazijahusishwa katika sera ya lugha ya nchi ya Kenya kama vile Kifaransa, Kiarabu, Kihindi miongoni mwa lugha nyingine za kigeni.

## 2.9 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia masuala mbalimbali na hasa yanayohusu maandishi na tafiti mbalimbali ambazo tayari zimefanywa kuhusiana na mada ya utafiti huu. Baadhi ya masuala haya ni kama vile maelezo kuhusu maana, asili, umuhimu na uthabiti wa lugha za mama. Pia sura hii ina maelezo kuhusu lugha ya Kikuyu na utafiti mbalimbali uliofanywa kuhusiana na lugha ya Kikuyu hasa kuhusu uthabiti wake wa kiisimujamii. Vile vile suala la mielekeo na umilisi wa lugha limejadiliwa katika sura hii. Aidha, sura hii imetoa fasili ya dhana ya kijana na kutambulisha ruwaza za matumizi ya lugha miongoni mwa vijana barani Afrika nchi ya Kenya ikiwemo. Hatimaye sura hii imetoa maelezo kuhusu ruwaza za matumizi na mielekeo ya kijumla kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng nchini Kenya. Sura inayofuata nayo ilijihusisha na suala la nadharia za utafiti mbali na kuyajadili masuala ya kinadharia yanayohusu uimarishaji na uthabiti wa lugha kwa jumla.

# SURA YA TATU

# MSINGI WA NADHARIA NA MAELEZO YA KINADHARIA KUHUSU UTHABITI WA LUGHA

## 3.1 Utangulizi

Sura ya tatu ya utafiti huu inatoa ufafanuzi kuhusu nadharia zilizouongoza utafiti wetu hasa katika hatua za ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Nadharia hizi mbili ni Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa na ambazo zimetolewa maelezo ya kina katika sura hii. Vile vile, sura hii ina maelezo ya kinadharia yanayohusiana na uthabiti wa lugha za mama kwa jumla na juhudi za uimarishaji wa lugha za mama katika nchi mbalimbali barani Afrika.

## 3.2 Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha.

Utafiti huu ulitumia vigezo vya Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ya mwanaisimujamii Landweer (2000). Landweer amependekeza vigezo vinane kama msingi wa nadharia hii vya kupima uthabiti wa lugha. Vigezo hivi ni vifuatavyo:-

i. Umbali wa jamii lugha kutoka kwa ama vijijini au mijini.
ii. Maeneo ya kijamii ambamo lugha inatumiwa na wanajamii lugha.
iii. Viwango na aina ya uhamishaji msimbo.
iv. Idadi ya wanajamii lugha wanaozungumza lugha husika.
v. Mtawanyiko wa wazungumzaji lugha katika mtandao wao wa kijamii.
vi. Mtazamo wa kijamii wa wanajamii lugha na wanajamii lugha wengine kuhusu lugha husika.
vii. Hadhi ya lugha katika jamii.

viii. Msingi imara na halali wa kiuchumi wa jamii lugha.

### 3.2.1 Umbali wa Jamii Lugha kutoka kwa ama Vijiji au Miji.

Kwa mujibu wa Landweer (2000), jinsi jamii lugha ilivyo mbali na sehemu za miji ndivyo ilivyo thabiti zaidi kiisimujamii kwani haina maingiliano mengi na lugha nyingine. Hii ni tofauti na jamiilugha nyingine ambayo iko karibu na miji kwani haina budi kuingiliana na lugha nyingine na basi kuathiriwa kwa njia moja au nyingine. Hivi basi lugha kama hii huwa haina uthabiti mwingi wa kiisimujamii.

Aidha, Landweer (2000) anaeleza kuwa umbali wa jamii lugha kutoka kwa miji sio wa kimasafa tu bali pia hupimwa na idadi ya wanajamii lugha ambao mara nyingi huenda wakirudi kutoka mijini kwa shughuli mbalimbali kama vile biashara, kazi na elimu. Kwa njia hii huenda wakafikishia wanajamii lugha walio mbali na miji athari za lugha nyingine. Kwa mujibu wa kigezo hiki, jamii lugha inaweza kugawanywa katika makundi manne mapana ambayo ni:-

i. Jamiilugha za vijijini ambazo nadra hazina uhusiano na jamiilugha za mijini.
ii. Jamiilugha ambazo zina uhusiano wa kiwango cha chini na jamiilugha za mijini.
iii. Jamiilugha ambazo zina uhusiano wa karibu na jamiilugha za mijini.
iv. Jamiilugha zinazoishi mijini.

Utafiti huu umejihusisha na uchunguzi wa jamii lugha zinazoishi mijini. Hii ni kwa sababu vijana wote wa jamii ya Kikuyu waliohusika katika sampuli ya utafiti huu iliundwa na vijana wa jamii ya Kikuyu kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Vijana

hawa walikuwa na uhusiano wa mbali na jamii za vijijini kwa vile wengi wao walidai kuwa ilikuwa nadra sana kwao kwenda kuzuru sehemu za mashambani. Kiisimujamii basi, ni kama vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, kiambu na Thika wametengwa kutoka kwa jamii ya Wakikuyu inayoishi vijijini na umbali huu una athari kwa umilisi wao wa lugha ya Kikuyu kwa vile wanazitumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika shughuli zao za kila siku.

### 3.2.2 Maeneo ya Kijamii ambamo Lugha inatumiwa na Wanajamii Lugha.

Msingi wa kigezo hiki ni kuwa jinsi lugha inavyotumiwa katika maeneo mengi ya kijamii, ndivyo lugha ile ilivyo thabiti kimatumizi. Fasold (1984:183) anasema kuwa "maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha huwa ni miktadha ya kijamii ambapo uchaguzi wa kutumia lugha moja huwa mwafaka zaidi kuliko matumizi ya lugha nyingine katika muktadha ule". Mifano ya maeneo haya ya kijamii ya matumizi ya lugha ni kama vile nyumbani, shuleni, kazini, ibadani, sherehe za kijamii kati ya mengine. Hata hivyo, kwa mujibu wa Landweer (2000), eneo la nyumbani ndilo msingi wa maeneo mengine ya kijamii ya lugha yoyote ile kwani ndilo ambalo huhusika na matumizi ya kiwango cha juu cha lugha za mama. Kuhusu eneo la nyumbani, Karanja (2012) ana maoni kuwa kutoweka kwa matumizi ya lugha katika eneo la nyumbani ni dalili hakika ya kupungua kwa uthabiti wa lugha husika. Landweer (2000) naye anaongezea kuwa kule kuanza kupotea kwa matumizi ya lugha katika maeneo mengi ya kijamii kunakoletwa na matumizi ya lugha nyingine katika jamii, ndiko huwa mwanzo wa kupunguka kwa uthabiti wa wa kiisimujamii wa lugha.

Katika utafiti wetu tulijikita zaidi katika kuchunguza matumizi ya lugha miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha ya nyumbani na shuleni. Hii ni kwa sababu ni katika maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha ya nyumbani na shuleni ambamo vijana hupatikana wakitumia lugha kwa wingi kuliko maeneo mengine ya kijamii ya matumizi ya lugha kama vile kanisani, biashara, kazini n.k

### 3.2.3 Viwango na Aina ya Uhamishaji Msimbo.

Jinsi jamii lugha husika huwa na viwango vya chini na aina chache za uhamishaji msimbo, ndivyo lugha yao huwa na uthabiti wa juu. Landweer (2000) anasema kuwa uhamishaji msimbo wa kiwango cha juu na usiofuata ruwaza zozote huonyesha kuwa wanajamii lugha hupendelea matumizi ya lugha nyingine wala sio ile yao na basi huanza kuathiri uthabiti wake wa kiisimujamii. Uhamishaji msimbo unaweza ukawa wa aina tatu kuu kwa mujibu wa Landweer (2000). Aina hizi ni:-

**a.** Uhamishaji msimbo imara katika jamii ya kidiglosia.

**b.** Hali ya wingilugha imara ambako maeneo mbalimbali ya kijamii ndiyo hubainisha msimbo utakaotumika.

**c.** Uhamishaji msimbo usiodhibitiwa ambapo uhamishaji msimbo hutokea bila kufuata ruwaza yoyote ile.

Ubadilishaji msimbo wa aina ya tatu ndio ambao huhusika zaidi katika kupunguza uthabiti wa wa kiisimujamii wa lugha huku ule wa kwanza ukiwa hauna athari nyingi kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika.

Katika utafiti huu ni wazi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wako katika kiwango cha kubadilisha msimbo ambacho huthibitiwa kwa kiasi kikubwa na maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha hasa katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la shuleni ambako kuna sera maalum za matumizi ya lugha. Vile vile vijana hawa pia wanajikuta katika muktadha wa tatu wa ubadilishaji msimbo hasa katika eneo la nyumbani ambako ubadilishaji msimbo kutoka lugha za Kiswahili, Kiingereza, Sheng na Kikuyu zaidi ni wa kiholela. Bila shaka ruwaza kama hizi za ubadilishaji msimbo zinaathiri uthabiti wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kama utafiti huu ulivyogundua katika sura ya tano na sita.

### 3.2.4 Idadi ya Wanajamii Lugha Wanaozungumza Lugha Husika.

Kigezo hiki kinahusika na idadi ya wazungumzaji lugha ambao wanazungumza lugha husika. Sio lazima lugha iwe na idadi kubwa ya wazungumzaji ili iwe thabiti kiisimujamii. Lugha inaweza kuwa na wazungumzaji chini ya 10, 000 na bado iwe thabiti kiisimujamii kulingana na msaada inayopokea kutoka kwa asasi mbalimbali za kijamii kama vile serikali (Landweer 2000). Hata hivyo, Landweer (2000) anasema kuwa idadi ya wageni wanaoingia katika jamii lugha fulani kwa shughuli mbalimbali na kuanza kutumia lugha ile ni muhimu kwa uthabiti wa lugha husika. Iwapo jamii lugha inaweza kuwafanya wageni kutumia lugha yao wanapojiunga nao, basi lugha yao ina uthabiti wa kiisimujamii wa kiwango cha juu.

Msingi wa kigezo hiki basi ni kuwa jinsi jamiilugha inavyoweza kuhimili athari za wageni wenye lugha tofauti katika jamii yao, ndivyo lugha yao ilivyo thabiti kiisimujamii. Iwapo jamii lugha itaathiriwa sana na lugha za wageni katika jamii zao, basi lugha hiyo sio thabiti kiisimujamii.

Utafiti huu katika sura ya 5 na 6 umebaini kuwa hata ingawa lugha ya Kikuyu ni mojawapo ya lugha zilizo na idadi kubwa ya wazungumzaji, lugha hii sio thabiti tena miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hii ni kutoka na ukweli kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yameathiriwa sana na matumizi yao ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika maeneo ya matumizi ya lugha ya nyumbani na shuleni.

### 3.2.5 Mtawanyiko wa Wazungumzaji Lugha katika Mtandao Wao wa Kijamii.

Kulingana Landweer (2000) jinsi jamii ilivyo na watu wengi wanaohusiana kwa njia moja au nyingine, ndivyo lugha ile ilivyo thabiti kiisimujamii. Mtandao wa kijamii hauhusu tu wazungumzaji lugha wenye uhusiano wa kifamilia bali hata uhusiano wa kijirani, kikazi, kidini na kadhalika. Mitandao hii, ambayo hutokea kwa usambamba, ndiyo huhimiza matumizi ya lugha ya jamii fulani na kuifanya imara.

### 3.2.6 Mtazamo wa Kijamii wa Wanajamii Lugha na Wanajamii Wengine Kuhusu Lugha Husika.

Kigezo hiki hujaribu kutambulisha kama iwapo kuna utambuzi wa ndani na nje wa jamii lugha kama kundi tofauti na la kipekee katika jamii pana. Suala muhimu hapa ni iwapo

lugha inaonekana kuwa muhimu kutoka ndani na nje ya jamii lugha ile, basi lugha hii ni thabiti. Zaidi, iwapo lugha inatambulika na mashirika ya nje kama vile serikali, pia lugha hii ni thabiti. Hivyo basi lugha thabiti lazima iwe na utambuzi wa kiwango cha juu kutoka ndani na nje ya jamiilugha.

Katika matokeo ya utafiti wetu katika sura ya 5 na 6, utafiti huu ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Mielekeo hii hasi inawafanya vijana hawa kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu na hatimaye kuathiri uthabiti wa kiisimujamii miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kama utafiti huu ulivyobaini.

### 3.2.7 Hadhi ya Lugha katika Jamii.

Kulingana na Landweer (2000) jinsi lugha ilivyo na hadhi ya juu katika jamii ndivyo ilivyo thabiti. Iwapo lugha ina hadhi ya chini basi uthabiti wake huwa chini. Lugha thabiti lazima iwe na hadhi katika kiwango cha kitaifa, kimkoa na hata vijijini.

Kati ya lugha nne zilizochunguzwa katika utafiti huu yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, lugha ya Kikuyu ndiyo iliyopewa hadhi ya chini zaidi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hadhi ya chini iliyopewa lugha ya Kikuyu na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika inakifanya Kikuyu kuwa na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii miongoni mwa vijana hawa kama ilivyobainika katika sura ya 5 na 6 ya utafiti huu.

### 3.2.8 Msingi Imara na Halali wa Kiuchumi wa Jamii Lugha.

Kama asemavyo Landweer (2000), iwapo lugha ina msingi imara na halali wa kiuchumi, basi lugha kama hii huwa imara. Ili lugha iwe thabiti lazima iwe na faida za kiuchumi kwa wazungumzaji wake. Lugha kama hii lazima iwawezeshe wazungumzaji wake kupata elimu, nafasi za kazi na kuwashirikisha kikamilifu katika biashara ili waweze kujitegemea kiuchumi. Lugha ambayo haiwezi kuwanufaisha wazungumzaji wake kiuchumi huenda ikahamwa na wazungumzaji wake na hivyo kuifanya isiwe thabiti.

Katika matokeo ya utafiti huu katika sura ya 5 na 6, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wanaiona lugha ya Kikuyu kama lugha isiyo na faida kiuchumi kwa vile haiwezi kuwasaidia kupata kazi za kitaaluma. Hii ndiyo sababu mojawapo inayowafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Hata ingawa tulitumia vigezo vya Landweer (2000), nadharia hii pia imesheheni mchango wa wanaisimujamii wengine kama vile Giles, Bourhis na Taylor (1977), Lewis (2009) na Smeets (2005). Uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kwa mujibu wa Giles na wenzake (1977:78) ni

> **"*kile kinachofanya jamiilugha fulani kujitambulisha kwa njia ya kipekee na ya pamoja ndani ya mazingira yenye jamii lugha nyingi*" (tafsiri yetu)**

Basi kulingana na Giles na wenzake, uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hutegemea mambo matatu ambayo ni hadhi ya lugha katika jamii, idadi ya wazungumzaji na kuungwa mkono na asasi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali kama vile vyombo vya habari. Allard na Landry (1986) wanaongezea kuwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hutegemea mielekeo ya jamiilugha kuhusu lugha yao.

Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwa vile ilielekeza masuala yaliyohusiana na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Lengo la nne la utafiti huu lilikuwa kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu. Nadharia hii ilitufaa sana katika kulifikia lengo hili kama matokeo ya utafiti huu yanavyobaini katika sura ya sita.

### 3.3 Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa.

Utafiti huu pia ulielekezwa na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa iliyoasisiwa na Ajzen na Fishbein mnamo mwaka wa 1975. Baadaye, nadharia hii ilifanyiwa marekebisho kadhaa kutokana na mchango wa wataalam kama vile Ajzen na Fishbein (1980), Ajzen (1985), Halle na wenzake (2002), Miller (2005) na Ajzen na Fishbein (2005). Nadharia hii ya vitendo vilivyofikiriwa na vitendo vilivyopangwa ni nadharia ya saikolojia jamii kuhusu mielekeo kwa jumla (Ajzen na Fishbein 1975). Mwanzoni, nadharia hii ilijulikana kama nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa pekee kabla ya kufanyiwa marekebisho na Ajzen mnamo mwaka wa 1985 na kuanza kujulikana kama nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na vitendo vilivyopangwa (Miller 2005).

Nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ilianzishwa na Ajzen na Fishbein (1975) kama nadharia ya kutabiri nia ya utendaji inayotokana na mielekeo na vitendo lengwa. Ajzen na Fishbein (1980) wanasema kuwa nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa ina misingi yake katika dhana kuwa binadamu ni viumbe ambavyo hutafakari na kupima kuhusu matokeo ya utendaji wake kabla ya kutenda kitendo chenyewe. Hivyo, kama wanavyoelezea zaidi Ajzen na Fishbein, vitendo vyote vyenye umuhimu wa kijamii hutawaliwa na matarajio ya mtu mwenyewe au watu wengine kuhusu jambo ambalo humfanya atende au kutolitenda jambo hilo.

Kwa mujibu wa Miller (2005), nadharia hii ina vipengele vitatu muhimu yaani:-

i. Mielekeo ya mtu kuhusu kitendo yaani imani ya mtu kuhusu athari za kutenda kitendo fulani na tathmini ya mtu kuhusu kitendo hicho.

ii. Matarajio ya mtu au watu wengine kuhusu kitendo yaani maoni ya mtu au watu wengine kuhusu kitendo ambacho mtu anapanga kutenda. Matarajio haya huathiri nia ya mtu katika utendaji wa kitendo fulani.

iii. Nia ya utendaji ambayo huwa ni msukumo alionao mtu wa kutenda jambo fulani unaotokana na mielekeo yake kuhusu jambo fulani na matarajio ya wengine kuhusu utendaji wake.

Kwa hivyo, nadharia hii hushikilia kuwa nia ya utendaji ya mtu hutegemea mwelekeo wa mtu kuhusu kitendo chenyewe na matarajio yake au ya watu wengine kuhusu matokeo ya kitendo hicho. Hivi ni kusema kuwa iwapo mtu analenga kufanya jambo au kuwa na


tabia fulani, basi kuna uwezekano mkubwa kuwa atafanya hivyo hatimaye (Halle na wenzake 2002).

Ajzen (1985) aliifanyia nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa marekebisho na ikaanza kujulikana kama nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na vitendo vilivyopangwa. Aliweza kufanya hivi kwa kuongeza kipengele kingine kimoja kwa nadharia awali ya vitendo vilivyofikiriwa. Kipengele hiki ni kile cha uthibiti vya vitendo vilivyofikiriwa ambacho hueleza kuwa mtu anaweza kuwa na nia ya kutenda kitendo fulani na kwa njia fulani lakini hatimaye akakosa kufanya hivyo kutokana na mambo mengine yaliyomzuia kufanya vile. Hatimaye, nadharia ya vitendo vilivyopangwa ilikuwa na vipengele vinne vifuatavyo:-

i. Mielekeo ya mtu kuhusu kitendo.
ii. Matarajio ya mtu au watu wengine kuhusu kitendo.
iii. Uthibiti vya kitendo kilichofikiriwa.
iv. Nia ya utendaji

Kwa mujibu wa Miller (2005), nadharia hii mpya ya vitendo vilivyovikiriwa na vitendo vilivyopangwa inaelezea kuwa mielekeo ya mtu kuhusu kitendo fulani na matarajio yake na ya watu wengine kuhusu iwapo kitendo ni kizuri au ni kibaya humwelekeza mtu katika nia ya kutaka kutenda kitendo fulani. Nia ya utendaji nayo huwa kigezo muhimu cha kubashiri tabia. Katika mchoro ufuataao, nadharia ya vitendo vilivyopangwa inaweza ikawakilishwa ifuatavyo:-

**Mchoro 3: Mpangilio wa Nadharia ya Vitendo Vilivyopangwa**




(Ajzen na Fishbein 2005: 38)

Ajzen na Fishbein (2005) wanasema kuwa iwapo mtu ana mwelekeo chanya kuhusu kitendo anachopanga kutenda na ana imani kuwa watu wengine wanatarajia atende kitendo hicho, basi atakuwa na motisha ya kiwango cha juu na kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa zaidi wa kukitenda kitendo hicho. Basi kuna uhusiano kati ya mielekeo na nia ya utendaji na hatimaye utendaji wa kitendo chenyewe.

Nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na vitendo vilivyopangwa, kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (2005) na Miller (2005), imetumiwa kuongoza tafiti nyingi zinaohusiana na mielekeo katika nyanja mbalimbali kama vile saikolojia, mawasiliano, mazingira na lugha. Kwa mfano, Furaha (1991) aliitumia nadharia hii alipokuwa akitafiti kuhusu mielekeo ya matumizi ya lugha miongoni mwa wakaazi wa mji wa Malindi kuhusu lugha ya Kitaliano, Kiswahili, Kijerumani na Kiingereza. Furaha anasema kuwa mielekeo ya


lugha ni matokeo ya imani aliyo nayo mtu kuhusu lugha hiyo na matarajio ya watu wengine muhimu kwake kuhusu matumizi ya lugha hiyo.

Hivyo basi, katika mazingira ya wingilugha, mtu huunda mielekeo mbalimbali kuhusu lugha zinazozungumzwa katika mazingira yake jambo ambalo humfanya atumie au achague lugha za matumizi kutoka kwa lugha zile zilizopo. Uamuzi wa kutumia lugha moja au nyingine ni kitendo kinachotokana na hali ya kutathmini lugha hiyo na pia kutilia maanani matarajio ya watu wengine kuhusu nia yake ya kuchagua lugha hiyo. Baada ya haya yote, mtu hufikia uamuzi wa kutumia lugha moja wala sio ile nyingine katika mawasiliano. Kama wasemavyo Ajzen na Fishbein (2005:6)

> ***"kwa kawaida watu hutarajia kutenda jambo baada ya kulitathmini na kulipenda na pia wanapoamini kuwa watu wengine muhimu kwao katika jamii wanafikiri kuwa mtu huyo anapaswa kulifanya jambo hilo".***
>
> ***(Tafsiri yetu)***

Kwa mujibu wa Miller (2005) na Furaha (1991) mielekeo ya lugha pamoja na matarajio ya watu wengine kuhusu matumizi ya lugha hiyo humfanya mtu awe na nia ya kuitumia lugha hiyo na hatimaye huanza kuitumia lugha hiyo na wala sio nyingine. Mielekeo hii ya lugha hubainika kwa kuchunguza utaratibu wa vitendo vya watu katika miktadha ya kijamii. Haya yanawakilishwa katika mchoro ufuatao:-

**Mchoro 4: Utaratibu wa Vitendo katika Uchaguzi wa Lugha.**




(Ajzen na Fishbein (2005: 43)

Uteuzi wa kutumia lugha moja badala ya nyingine katika jamii ni kitendo ambacho mtu kwanza hukifikiria na kukitathmini kama kina faida au la kabla ya kuiteua lugha hiyo kuwa lugha ya matumizi katika eneo fulani la kijamii. Kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (2005), uteuzi wa lugha moja dhidi ya nyingine kwa mujibu wa nadharia hii lazima, mbali na kukubalika na mtu binafsi, vile vile lazima ukubalike na watu wengine muhimu kwa mzungumzaji katika jamii yake kama vile watu wa rika lake.

Kitendo cha vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika cha kupendelea lugha fulani dhidi ya nyingine katika matumizi yao ya lugha kinatokana na imani zao kuhusu lugha hizi na pia matarajio ya watu wengine walio muhimu maishani mwao katika jamii. Jambo hili hatimaye huwafanya wawe na mielekeo tofauti kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Nadharia hii ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa ilikuwa muhimu kwa utafiti wetu katika kuchanganua masuala ya mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hii ni kwa sababu nadharia yenyewe inafafanua mchakato anaoupitia mtu katika uchaguzi wa lugha ya matumizi katika mazingira ya wingilugha. Uchaguzi wa kutumia lugha moja dhidi ya nyingine katika mazingira ya wingilugha kwa mujibu wa nadharia hii sio kitendo cha kiholela bali ni jambo linalopitia mchakato maalum.

**3.4 Maelezo ya Kinadharia kuhusu Uthabiti wa Lugha katika Mazingira ya Ulumbi**

Lengo la nne la utafiti huu lilikuwa kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika

kupitia viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha . Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa viwango vya uthabiti wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni vya chini ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Suala la uthabiti wa lugha basi lilikuwa muhimu kwa utafiti huu na limefafanuliwa kwa kina katika sehemu hii ya 3.4.

Kwa mujibu wa Wurum (2002), uthabiti wa lugha ni kitendo cha kudumisha lugha ikiwa imara na kuiepusha kutokana na hatari zozote zile zinazotishia kuiangamiza. Hinton na Hale (2001) wanaeleza kuwa uthabiti wa lugha ni ule uwezo wa lugha iliyo na matumizi finyu katika jamii wa kujiendeleza kama lugha imara katika mazingira yenye lugha nyingine za matumizi mapana.

Aidha, uthabiti wa lugha ni

> ***"jumla ya shughuli zote zinazolengwa kuipa lugha uhai ili iendelee kuishi na kukua kwa kuiepusha na mambo yanayoweza kuiangamiza au kushusha viwango vyake vya uthabiti kwa kuhakikisha kuwa inatumiwa na marika yote katika jamii na katika maeneo mengi ya kijamii iwezekanavyo" .***
>
> ***(tafsiri yetu)***
>
> (Sallabank 2004:97)

Obiero (2010) anaeleza kuwa shughuli ya kutathmini na kuelewa uthabiti wa lugha ni changamano na yafaa kufanywa sio mara moja tu bali mara kadhaa na kwa mitazamo tofauti ili kubaini hali halisi ya uthabiti wa lugha husika. Hata hivyo, kiwango cha uthabiti wa lugha ndicho kigezo cha kimsingi ambacho hutumiwa katika kutambulisha aina ya mradi mwafaka wa kuiimarisha lugha. Naye Crystal (2002) anasema kuwa ili

kubadilisha hali ya uangamiaji wa lugha ulimwenguni, shughuli za udumishaji na uhifadhi wa lugha lazima zianzishwe kwa dhati. Shughuli hizi kwanza zitahusu hatua muhimu ya kubaini viwango vya uthabiti wa lugha kama hizi kwa sasa kisha kuweka mikakati ya kuinua uthabiti wa lugha hizi hasa kwa kuhakikisha kuwa zinatumika katika maeneo mengi na mapya ya kijamii iwezekanavyo. Grenoble na Whaley (2006) nao wana maoni kuwa kutathmini mabadiliko ya uthabiti wa lugha kwa kipindi kirefu cha wakati hutoa fursa mwafaka zaidi ya kufaulu katika jaribio la kuimarisha lugha iliyokabiliwa na hatari ya kuangamia.

Wanaisimujamii hao wote wanajaribu kutilia mkazo umuhumu wa kutambulisha viwango vya uthabiti wa lugha kama hatua ya kimsingi ya kuanzisha shughuli za kuimarisha na kuidumisha lugha. Lengo moja la utafiti huu lilikuwa kubaini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii hii mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Utafiti huu, kati ya tafiti nyingine kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu, huenda basi baadaye ukawa msingi bora wa kutegemewa katika kuanzisha miradi ya kuimarisha na kudumisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii hii mijini nchini Kenya.

Suala la uthabiti wa lugha za mama ulimwenguni limekuwa likiwashughulisha wanaisimujamii kwa muda mrefu kufikia sasa. Hii ni kutokana na idadi kubwa ya lugha za mama ulimwenguni ambazo zimo katika viwango mbalimbali vya kushuka kwa uthabiti wake huku nyingine tayari zikiwa zimeangamia kabisa kwani hazina watu wanaozizungumza tena. Kulingana na Krauss (1992), ni takribani asilimia tano tu ya

lugha za ulimwengu ambayo ni salama kutokana na tishio la kuangamia huku karibu asilimia 57 ya lugha zote ulimwenguni zikiwa katika hatari kubwa ya kuangamia. Maoni haya yanaungwa mkono na Crystal (2000) anayesema kuwa mamia ya lugha ulimwenguni kwa sasa yamo hatarini ya kuangamia. Lewis na Simons (2009:4) wanasema kuwa "picha halisi ya uangamiaji wa lugha ulimwenguni haionyeshi hali ya matumaini. Hii ni kwa sababu kati ya lugha 6,909 zilizo katika ramani ya Enthologue, 437 ya lugha hizi ziko karibu kuangamia kabisa huku lugha 3,524 zikiwa na wazungumzaji chini ya 10, 000".

Hata hivyo kulingana na Brenzinger (1998), sio lugha ndogo tu ulimwenguni ambazo zimo katika hatari ya kuangamia kama yalivyo makisio ya wengi. Hata baadhi ya lugha kubwa ulimwenguni pia zimo katika viwango mbalimbali vya kuangamia sio kutokana na uhaba wa wazungumzaji, bali kutokana na sababu nyingine kama vile kuathiriwa na mtagusano wake na lugha nyingine katika jamii. Hali hii inatokana na mambo kadhaa. Mojawapo ni suala la wingilugha linalosababishwa na hali ya mtagusano wa lugha duniani.

Sababu nyingine zinazopelekea kushuka kwa viwango vya uthabiti wa lugha za mama ulimwenguni ni kama vile kupungua kwa maeneo ya kijamii ambamo lugha za mama zinatumiwa katika jamii husika, kutopitishwa kwa lugha za mama kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, wazazi kukosa kuwapokeza watoto lugha zao za mama na mielekeo walio nayo wazungumzaji wa lugha kuhusu lugha yao ya mama (Landweer 2000). Zaidi,

uhaba wa wazungumzaji wa lugha za mama hupelekea kurudi nyuma kwa lugha hizo kimatumizi na kwa hivyo kuziingiza katika hatari ya kuangamia.

Mwanaisimujamii mwingine aliyechangia katika kufafanua suala hili la uthabiti na uangamiaji wa lugha ni Obiero (2010) anaposema kuwa hata ingawa shughuli za kubaini uthabiti wa lugha na uangamiaji wa lugha huchukuliwa kama kitu kimoja na wanaisimujamii wengi, shughuli hizi huwa shughuli mbili tofauti lakini zilizo na uhusiano wa karibu. Obiero anaendelea kufafanua kuhusu masuala haya mawili kwa kusema kuwa wanaisimujamii wengi wameegemea zaidi katika kuweka vigezo vya kubaini uangamiaji wa lugha bali sio katika kuweka vigezo vya kubaini viwango vya uthabiti wa lugha.

Kufikia sasa, kuna wanaisimujamii mbalimbali ulimwenguni ambao wameshughulikia masuala ya uthabiti wa lugha, uangamiaji (kufa) wa lugha na uimarishaji na udumishaji wa lugha. Wanaisimujamii hawa wamefanya tafiti mbalimbali za kiisimujamii kuhusu lugha duniani na kuibuka na masuala anuai ya kinadharia ambayo yamekuja kutumia kama misingi ya kufafanulia masuala ya uthabiti wa lugha, uangamiaji wa lugha, uimarishaji na udumishaji wa lugha.

### 3.4.1 Vigezo vya Upokezanaji Lugha Baina ya Vizazi.

Mwanaisimujamii mmoja aliyelishughulikia suala la uangamiaji wa lugha ni Fishman (1991, 2001) katika vigezo vyake vya upokezanaji lugha baina ya vizazi, maarufu kwa Kiingereza kama *Graded Intergenerational Disruption Scale (GIDS)*. GIDS huwa ni

mpangilio wa vigezo vinane vinavyotumika katika upimaji wa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yoyote ile ulimwenguni. Vigezo hivi basi hutumiwa na wanaisimujamii kubaini kama lugha ina kiwango cha juu ama cha chini cha uthabiti wa kiisimujamii. Aidha, mbali na kupima uthabiti wa lugha husika, vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi pia hutumika kubaini kama lugha inayochunguzwa imo katika hatari ya kuangamia au la.

Kwa kuazisha vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi, Fishman (1991), aliweka msingi ambao ulitumiwa na wanaisimujamii wengine katika kuandaa taratibu za kupima uthabiti wa lugha ulimwenguni.  Kama asemavyo Obiero (2010), vigezo vya Fishman vya GIDS vilichochea wanaisimujamii wengine kuanzisha vigezo vya kutathmini aidha viwango vya uangamiaji wa lugha ama viwango vya uthabiti wa lugha. Kwa kuviweka vigezo hivi, Fishman alijaribu kuonyesha vigezo ambavyo vinaweza kutumiwa katika kupima ama lugha ina uthabiti wa kiwango cha juu na kwa hivyo iko imara na haimo katika hatari ya kuangamia au viwango vyake vya uthabiti vipo chini na hivyo huenda ikawa imo katika hatari ya kuangamia.

Fishman (1991, 2001) ana vigezo vinane alivyovipendekeza kuwa kipimo cha kuonyesha kiwango cha uthabiti wa lugha yoyote ile duniani. Kwa mujibu wa Lewis na Simons (2009), vigezo hivi vya GIDS (Fishman 1991, 2001) vimeegemezwa katika msingi kuwa wajibu mkuu wa kupokezana lugha baina ya vizazi ni kule kudumisha lugha husika na ambalo si jukumu la wazazi tu bali jamii nzima na asasi zake. Wakifafanua zaidi kuhusu GIDS, Lewis na Simons (2009:24) wana maoni kuwa,

> “***Iwapo watoto hawatajifunza lugha yao ya mama kutoka kwa wazazi wao, kuna uwezekano mkubwa kuwa hata nao baadaye hawataipitisha lugha ile kwa watoto wao.” (Tafsiri yetu)***

Lewis na Simons (2009) wanasema kuwa vigezo hivi vya Fishman (1991, 2001) vimetumika kama msingi au tathmini bora zaidi ya kuchunguza uthabiti wa lugha ulimwenguni kwa karibu miongo miwili. Baadaye, shirika la UNESCO nalo liliasisi utaratibu wake wa kupima uthabiti wa lugha ulimwenguni uliokuwa na vigezo sita. Vile vile, jarida la *Enthologue: Languages of the World (2000)*, lilitayarisha vigezo vitano vya kupima uthabiti wa lugha.

Vigezo vinane vya GIDS vya Fishman (2001) ambavyo vilikuwa msingi wa kupima uthabiti wa lugha kwa muda mrefu vimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali 4: Vigezo vya GIDS**

| **HATUA** | **MAELEZO** |
|---|---|
| **GIDS 8** | Wazungumzaji pekee wa lugha husika ni wa rika la babu na nyanya katika jamii. |
| **GIDS 7** | Rika la wazazi linafahamu vyema lugha husika na huitumia katika mawasiliano yao na wazee lakini hawaipitishi kwa watoto wao. |
| **GIDS 6** | Lugha inatumika katika mazungumzo na marika yote na watoto wanajifunza lugha hii kama lugha yao ya kwanza. |
| **GIDS 5** | Lugha inatumika katika mazungumzo na marika yote na inatumiwa vyema kimaadishi na jamii yote. |

| | |
|---|---|
| **GIDS 4** | Maarifa ya lugha husika yanapitishwa katika elimu. |
| **GIDS 3** | Lugha inatumiwa kazini, mikoani i na mashinan na wenyeji na wageni. |
| **GIDS 2** | Lugha inatumika katika vyombo vya habari mikoani na mashinani na katika huduma za serikali. |
| **GIDS 1** | Lugha inatumika katika elimu, vyombo vya habari na serikalini katika viwango vya kitaifa. |

(Kuoka:Fishman 2001:76) (Tafsiri yetu)

Kulingana na Fishman (2001), vigezo hivi vinane vya GIDS vimepangwa kwa njia kuwa kigezo cha 8 huonyesha dalili za lugha iliyokabiliwa na tishio kubwa la kuangamia ilihali kigezo cha 1 huonyesha lugha ambayo haimo katika hatari ya kuangamia.

### 3.4.2 Vigezo vya Kubaini Uthabiti wa Lugha vya Ethnologue (2000)

Vigezo vingine vya kubaini uthabiti wa lugha ni vile vya Ethnologue (2000) vilivyotayarishwa na Grime na wenzake (2000). Ethnologue ina vigezo vitano vya kubaini viwango vya uthabiti wa lugha ambavyo vimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali 5: Vigezo vya Uthabiti wa Lugha vya Ethnologue (2000)**

| HATUA | MAELEZO |
|---|---|
| **1** | **LUGHA HAI**<br>Lugha ambazo zina idadi kubwa ya wazungumzaji asilia. |
| **2** | **LUGHA ZA PILI PEKEE**<br>Lugha ambazo huzungumzwa kama lugha za pili pekee kwa vile hazina wazungumzaji wa kwanza wanaopatikana. |

| | |
|---|---|
| **3** | **LUGHA ZILIZOKARIBIA KUANGAMIA**<br>Lugha zilizo na wazungumzaji chini ya 50 au idadi ndogo sana ya wazungumzaji wanaoendelea kutoweka. |
| **4** | **LUGHA ZILIZOLALA**<br>Lugha ambazo hazina wazungumzaji wowote wanaojulikana waliobaki lakini kuna kundi la watu wanaojitambulisha kama jamii kupitia lugha ile. |
| **5** | **LUGHA ZILIZOANGAMIA**<br>Hakuna mzungumzaji yeyote wa lugha ile aliyebaki na hakuna jamii yoyote ya watu inayojitambulisha na lugha hiyo. |

(Obiero 2010:206 -207) (Tafsiri yetu)

Kwa mujibu wa Obiero (2010), vigezo hivi vya Ethnologue vimeegemea zaidi katika kufafanua hatua za uangamiaji wa lugha bali sio katika kufafanua hatua za kubainisha uthabiti wa lugha. Obiero anaongeza kuwa vigezo hivi, vile vile ni vya kijumla mno katika kuongoza kikamilifu mpangilio wa ungamiaji wa lugha hatua kwa hatua.

### 3.4.3 Vigezo vya Kupima ama Viwango vya Uthabiti au Uangamiaji wa Lugha vya UNESCO

Juhudi nyingine za kushugulikia suala la uthabiti na uangamiaji wa lugha duniani zimefanywa na shirika la UNESCO. Juhudi za UNESCO ziliongozwa na mwanaisimujamii Brenzinger (1998) katika mkutano wa wataalam wa lugha wa UNESCO kuhusu usalimishaji wa lugha zilizokabiliwa na hatari ya kuangamia. Vigezo vilivyotayarishwa na UNESCO vya kupima uthabiti wa lugha ni hivi vifuatavyo:-

i. Kiwango cha upitishaji wa lugha baina ya vizazi katika jamii
ii. Idadi ya wazungumzaji wa lugha.
iii. Asilimia ya wazungumzaji wa lugha katika jumuiya nzima au nchi.
iv. Utowekaji wa lugha katika maeneo mbalimbali ya kijamii.
v. Ueneaji wa lugha katika maeneo mapya ya kijamii kama vile matumizi ya lugha katika vyombo vya habari.
vi. Vifaa vilivyopo vya kufundisha kuhusu lugha husika.
vii. Mielekeo na sera za serikali na asasi za kijamii kuhusu lugha husika.
viii. Mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha yao.
ix. Idadi na ubora wa maandishi ya lugha husika

### 3.4.4 Vigezo vya Upokezanaji Lugha Baina ya Vizazi Vilivyopanuliwa.

Lewis na Simons (2009) walifanya juhudi za kuviboresha zaidi vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi yaani GIDS walipoleta pamoja vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi vya Fishman (1991, 2001), vigezo vya kupima ama viwango vya uthabiti au uangamiaji wa lugha vya UNESCO (2002) na vigezo vya uthabiti wa lugha vya Ethnologue (Grime 2000). Matokeo ya juhudi hizi ni vigezo kumi na tatu vya upokezanaji lugha baina ya vizazi vilivyopanuliwa maarufu kwa Kiingereza kama *Expanded Graded Intergenerational Disruption Scale (EGIDS).* Kwa mujibu wa Lewis na Simons (2009), vigezo vya EGIDS vinaweza vikatumika kwa shughuli za kupima uthabiti wa lugha yoyote ile duniani kwa njia iliyopanuliwa na yenye uwazi zaidi kwa vile vinatathmini lugha kwa kutumia vigezo zaidi. Hivyo basi, vigezo vya EGIDS kama

vile vigezo vya GIDS ni vigezo vya kupima ama lugha ina uthabiti wa kiisimujamii au imo katika hatari yoyote ile ya kuangamia tofauti ikiwa vigezo vya EGIDS vimepanuliwa na kuwa na hatua kumi na tatu badala ya hatua nane za vigezo vya GIDS.

Lewis na Simons (2009) wana maoni kuwa hata ingawa vigezo vya GIDS (Fishman 1991, 2001) UNESCO (2002) na Ethnologue (2000) vya kupima uthabiti na uangamiaji wa lugha bado ni vya kimsingi na vinaendelea kutumiwa, kunahitajika upanuzi wa vigezo hivi kwa kuvileta pamoja ili kuwe na vigezo vipana zaidi vitakavyotumika katika tafiti mbalimbali za masuala ya uthabiti na uangamiaji wa lugha duniani.

Wataalam hawa wawili (Lewis na Simons 2009) wameasisi utaratibu mpya wa kupima uthabiti na uangamiaji wa lugha duniani. Wamefanya hivi kwa kupanua vile vigezo vinane vya GIDS na kuvipata vigezo kumi na tatu wanavyoviita EGIDS vya kupima uthabiti wa lugha. Hata hivyo, kama wasemavyo Lewis na Simons, vigezo vya EGIDS vimepanuliwa kwa njia kwamba vinaenda sambamba na vile vya Fishman (1991, 2001). Vigezo vya EGIDS vimepewa nambari mpya huku kwingineko hatua nyingine za GIDS zikigawanywa maradufu. Kwa mfano, hatua za 6 na 8 za GIDS zimetenganishwa na kuwa 6a na 6b na vile vile 8a na 8b mtawaliwa. Vigezo kumi na tatu vya EGIDS (Lewis na Simons 2009) ni hivi vifuatavyo:-

**Jedwali 6: Vigezo vya EGIDS**

| HATUA | MAELEZO |
| --- | --- |
| **EGIDS 10** | **LUGHA ZILIZOANGAMIA KABISA**<br>Hatua hii huwa haina mzungumzaji yeyote wa lugha ile aliyebaki wala hakuna yeyote katika ile jamii aliye na nia ya kujihusisha na lugha ile tena. Lugha kama hizi huwa zimengoja tu juhudi za yeyote yule atakayeanzisha mradi wa kuzifufua. |
| **EGIDS 9** | **LUGHA ZILIZOLALA**<br>Hizi ni lugha ambazo matumizi yake huwa ni kama yametoweka kabisa katika jamii husika. Hata hivyo, jamii husika bado huwa zinajitambulisha na lugha hizi na huwa na nia ya kuziimarisha kama kumbukumbu za asili zao. Basi katika hatua hii lugha hutumika tu wakati wa sherehe za kitamaduni lakini kwa ufasaha wa chini sana. |
| **EGIDS 8b** | **LUGHA ZILIZOKARIBIA KUANGAMIA KABISA**<br>Katika hatua hii wazungumzaji wa lugha huwa rika la babu na nyanya pekee. Pia kizazi hiki huwa kidogo sana kiasi kwamba nafasi za kutumia lugha kimazungumzo huwa nadra |
| **EGIDS 8a** | **LUGHA ZILIZOATHIRIKA KABISA**<br>Kizazi kinachozungumza lugha husika katika hatua hii huwa ni kile cha babu na nyanya. Hata hivyo, wazazi wanaweza kutumia lugha hii kimazungumzo lakini inapolazimu kabisa kufanya vile. Ufasaha wao wa lugha husika nao huwa umepunguka sana. |
| **EGIDS 7** | **UHAMAJI LUGHA**<br>Wazungumzaji huanza kuonyesha dalili za uhamaji lugha. Wazazi wengi huwa hawawapokezi watoto wao lugha yao ya mama. Pia maeneo ya kijamii ambamo lugha ilikuwa ikitumika hupungua sana. Hata hivyo, lugha husika huwa bado inaweza kuimarishwa kwa kuanzisha tena upokezanaji wa lugha hiyo katika mazingira ya nyumbani kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto wao. |

| | |
|---|---|
| **EGIDS 6b** | **LUGHA ZILIZOATHIRIKA.** Lugha katika hatua hii huonyesha viwango vinavyoshuka katika matumizi yake kimazungumzo. Matumizi ya lugha husika katika mazungumzo ya kila siku katika maeneo mbalimbali ya kijamii huanza kupitwa na matumizi ya lugha nyingine kimazungumzo katika jamii ile. Upokezanaji lugha baina ya vizazi hapa huwa si kamili yaani wazazi wengi huwa wanawapokeza watoto wao lugha pale nyumbani lakini idadi fulani ya wazazi haitekelezi jukumu hili. Kwa njia hii, lugha husika huanza kuingia katika hatari ya kuangamia kwani pindi vizazi vinavyopita, ndivyo idadi ya wazungumzaji wenye umilisi halisi wa lugha hii itakavyopunguka. Vile vile, maeneo ya kijamii ambamo lugha hii ilikuwa ikitumika kimazungumzo huanza kupunguka. |
| **EGIDS 6a** | **LUGHA ZA MAZUNGUMZO** Lugha katika hatua hii hutumika kwa wingi katika kiwango cha mazungumzo na jamii husika. Lugha hapa haimo hatarini kimazungumzo. Hapa lugha huwa na mpangilio imara wa kidiglosia ambapo lugha kimaandishi huwa na hadhi ya juu (H) na kimazungumzo huwa hadhi ya chini (L). |
| **EGIDS 5** | **LUGHA ZA MAANDISHI** Lugha ambazo zinatumika katika elimu isiyo rasmi katika jamii na haziungwi mkono na asasi mbalimbali za kijamii. |
| **EGIDS 4** | **LUGHA ZA ELIMU** Hizi ni lugha zinazotumiwa kama vyombo vya kufundishia katika daraja la chini. Lugha hizi zinaweza kuwa ndizo L1 za kujipatia elimu na huungwa mkono na asasi mbalimbali za kijamii. |
| **EGIDS 3** | **LUGHA ZA BIASHARA** Hizi ni lugha ambazo hazina hadhi rasmi lakini hutumika kwa wingi kama L2 na watu wengi katika jamii wenye L1 zao. Matumizi yake mengi ni katika biashara na mawasiliano baina ya makundi mbalimbali. Mara nyingi huwa na mfumo sanifu kimaandishi hata ingawa hazijasanifishwa rasmi. |

| | |
|---|---|
| **EGIDS 2** | **LUGHA ZA KIMAENEO (KIMKOA)**<br>Hapa kuna lugha ambazo zimekaribiana kimatumizi na lugha za kitaifa lakini lugha hizi zinatumika zaidi katika kiwango cha mkoa kwa shughuli kama vile elimu, utawala na katika vyombo vya habari. Si lazima ziwe zimesanifishwa. |
| **EGIDS 1** | **LUGHA ZA KITAIFA.**<br>Lugha hizi zinatumika katika kiwango cha kitaifa katika mazungumzo na maandishi. Huenda hata zimefanyiwa usanifishaji. Pia lugha hizi hutumika kama lugha rasmi kutekeleza majukumu ya kiserikali, elimu na kwenye vyombo vya habari. |
| **EGIDS 0** | **LUGHA ZA KIMATAIFA.**<br>Lugha katika hatua hii ni imara kabisa na hazimo katika hatari yoyote. Ni lugha chache tu ulimwenguni zilizofikia kiwango hiki. |

(Lewis na Simons 2009:28-29) (Tafsiri yetu)

Hata ingawa utafiti wetu ulinufaika pakubwa na kwa njia mbalimbali kutokana na vigezo hivi vyote yaani vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi vilivyopanuliwa (EGIDS) vya Lewis na Simons (2009), Vigezo vya upokezanaji lugha baina ya vizazi (*GIDS*) vya Fishman (1991, 2001), vigezo vya kupima ama viwango vya uthabiti au uangamiaji wa lugha vya UNESCO (2002) na vigezo vya uthabiti wa lugha vya Ethnologue (Grime 2000) utafiti huu uliongozwa na vigezo vya nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yake Landweer (2000) (Taz. 3.2).

Hii ni kwa sababu kama asemavyo Obiero (2010) vigezo hivi vya EGIDS, GIDS, UNESCO na Ethnologue vimeegemea zaidi katika kuonyesha hatua za kuangamia kwa

lugha ilhali vile vya Landweer vimeegemea zaidi katika kuonyesha hatua za uthabiti wa lugha. Utafiti huu ulichunguza na kutambulisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na jinsi ulivyoathirika kutokana na athari za lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng.

Suala la uthabiti wa lugha yoyote ile, na zaidi lugha za mama, ni muhimu kwa wadau mbalimbali katika masuala ya uhifadhi na uimarishaji wa lugha, kama vile wanaisimujamii. Hii ni kwa sababu viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha vikibainika vyema, wadau hawa watapata misingi ya kuanzisha mikakati mwafaka ambayo jamii husika inafaa kuanzisha ili kuzifufua, kuziimarisha au kuzihifadhi lugha zao. Obiero (2010) anafafanua kuwa shughuli zote za ufufuzi na uimarishaji wa lugha ulimwenguni huanza kwa shughuli ya kutambulisha viwango vya uthabiti vya lugha husika. Akielezea zaidi, Obiero anasema kuwa ni baada tu ya kubaini viwango vya uthabiti vya lugha husika ambapo wanaisimujamii huweza kutambulisha na kufahamu kama lugha ni thabiti ama la. Nao Grenoble na Whaley (2006) wanasema yafuatayo kuhusu uthabiti wa lugha.

> ‘***Kutathmini na kuelewa uthabiti wa lugha ni shughuli changamano ….ilihali kiwango cha kuelewa uthabiti wa lugha ndicho kigezo cha kimsingi kinachotumiwa kutambulisha aina ya programu iliyo mwafaka katika kuiimarisha lugha’. (Tafsiri yetu)***
>
> (Grenoble na Whaley 2006:104)

Sheik (2011) ana maoni kuwa lugha nyingi za mama barani Afrika zinakabiliwa na ushindani mkubwa kimatumizi kutoka kwa lugha za matumizi mapana zinazopatikana hapa. Nyingi ya lugha hizi ni lugha za kikoloni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kireno kati ya lugha nyingine. Hata hivyo, kama ilivyo hapa nchini Kenya, kuna lugha za Kiafrika za matumizi mapana kama vile Kiswahili ambazo pia zinatoa ushindani mkubwa kwa lugha za mama na hivyo kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hizi jambo ambalo lilichunguzwa katika utafiti huu.

### 3.5 Lugha za Mama katika Mazingira ya Wingilugha: Dhana ya Diglosia na Triglosia.

Utafiti huu ulijihusisha na uchunguzi wa athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Katika miji hii mitatu, yaani Nairobi, Kiambu na Thika, kuna hali ya wingilugha ambapo baadhi ya lugha zinazozungumzwa kwa wingi ni lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Lugha hizi nne zinatumika kwa hadhi tofauti katika maeneo tofauti ya matumizi ya lugha kama utafiti huu ulivyobaini.

Matumizi ya lugha katika mazingira ya wingilugha husababisha jamii kuwa na mipangilio mbalimbali ya matumizi ya lugha zile kulingana na majukumu yaliyopewa kila lugha katika jamii husika. Mara nyingi, kutokana na majukumu yanayotekelezwa na lugha katika jamii, ile lugha ama zile lugha hupata hadhi mbalimbali kimatumizi. Hii ina maana kuwa katika jamii moja kuna lugha za hadhi ya juu kimatumizi na hadhi ya chini

vile vile. Kutokana na hadhi hizi za matumizi ya lugha katika jamii, dhana za diglosia na triglosia hutumika kuelezea hali hii. Lugha za mama kama vile Kikuyu hujikuta katika mpangilio huu wa lugha huku wakati mwingi zikipewa hadhi ya chini kimatumizi ikilinganishwa na lugha nyingine hasa zile za kikoloni.

### 3.5.1 Dhana ya Diglosia

Dhana ya diglosia ilianzishwa na Ferguson mnamo mwaka wa 1959. Ferguson alianzisha dhana ya diglosia kutoka kwa neno la kifaransa *Diglossie, Di* ikimanisha mbili na *glossie* ikimanisha lugha. Kwa mujibu wa Sebba (2011), Ferguson alianzisha dhana hii kuelezea hali ya matumizi ya lugha ambapo lugha moja iliweza kutumiwa kwa njia mbili tofauti na wazungumzaji wake kukidhi mahitaji mbalimbali ya kijamii. Furaha (1991), anaongeza kuwa diglosia ni ile hali ya mzungumzaji kutumia namna moja ya lugha katika muktadha mmoja na namna nyingine ya lugha hiyo hiyo katika muktadha mwingine.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa Hudson (1980), lugha moja inaweza kuwa na hadhi mbili tofauti kimatumizi kutegemea muktadha yaani hadhi ya juu na ya chini. Hadhi ya juu ya lugha ile ingetumika katika miktadha rasmi na hadhi ya chini ya lugha ile ile ingetumika katika miktadha isiyo rasmi katika jamii hiyo hiyo. Ferguson basi, kwa mujibu wa Furaha (1991), alielezea diglosia kama tukio ambalo lingewezekana tu katika mazingira ya lugha moja pekee. Hata hivyo Fishman, kama asemavyo Hudson (1980), mnamo mwaka wa 1971 alielezea uwezekano wa diglosia kujitokeza katika lugha mbili tofauti katika jamii moja. Katika mazingira kama haya, lugha moja huwa na hadhi ya juu na nyingine hadhi ya chini kimatumizi katika jamii ile (Furaha 1991).

Akielezea zaidi kuhusu diglosia, Sebba (2011) anasema kuwa Fishman alianzisha diglosia iliyo ama isiyo na uwililugha na uwililugha ulio ama usio na diglosia. Hivi, dhana ya diglosia inazua mazingira manne tofauti ya matumizi ya lugha yafuatayo:-

**a)** Mazingira ya kwanza ni ya uwililugha ukiwa na diglosia. Hapa lugha mbili katika jamii moja hutumika lakini zikiwa zimetenganishwa kabisa na majukumu zinayoyatekeleza. Lugha moja basi huwa na hadhi ya juu kimatumizi kuliko ile nyingine

**b)** Pili, kuna mazingira ya uwililugha bila diglosia na ambayo ni nadra sana kupatikana katika jamii, ambapo lugha mbili hutumika katika jamii lakini hakuna ile iliyo na hadhi kuliko nyingine

**c)** Katika mazingira ya tatu, Sebba anasema kuwa hapa kuna diglosia bila uwililugha ambapo lugha moja tu ndiyo inayotumika katika jamii lakini hupewa hadhi tofauti katika miktadha tofauti.

**d)** Mwisho, kulingana na Sebba, ni mazingira ambamo hamna diglosia ama uwililugha. Hii ina maana kuwa ni lugha moja inayotumika katika jamii bila hadhi zozote kujitokeza katika miktadha tofauti.

Mataifa mengi ya Kiafrika yana mifumo ya uwililugha na diglosia ambapo lugha mbalimbali zinazotumika hapa hupewa hadhi tofauti kimatumizi (Hudson 1980, Sebba 2011). Lugha za kikoloni kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani huwa zimepewa hadhi ya juu kimatumizi ikilinganishwa na lugha za mama ambazo hupewa hadhi ya chini kimatumizi.

### 3.5.2 Dhana ya Triglosia

Mkilifi (1972) alizua dhana ya triglosia alipokuwa akitafiti kuhusu matumizi ya lugha nchini Tanzania. Hapa alilinganisha lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha za mama kimatumizi. Lugha ya Kiingereza ilikuwa na hadhi ya juu ikilinganishwa na Kiswahili. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili ilikuwa na hadhi ya juu ikilinganishwa na lugha za mama kimatumizi katika jamii zile zile.

Batibo (2005) anaeleza kuwa mataifa mengi ya Kiafrika yana mpangilio wa triglosia katika matumizi yake. Lugha za kikoloni (Kiingereza, Kifaransa, Kireno n.k) huwa na hadhi ya juu na hutekeleza majukumu rasmi kama vile shughuli za kielimu na kiserikali. Chini ya lugha hizi ni zile za kiasili za matumizi mapana kama vile Kiswahili na ambazo hutumika katika masuala ya kijamii na kiuchumi. Chini kabisa huwa lugha za mama ambazo huwa na hadhi ya chini kabisa na huachiwa majukumu yasio rasmi wala muhimu katika jamii. Hadhi za juu na hadhi za chini za lugha ndizo huzua mielekeo ya lugha miongoni mwa wazungumzaji kwani lugha nyingine hupendelewa zaidi kuliko nyingine kimatumizi.

Suala la diglosia na triglosia lilikuwa muhimu kwa utafiti wetu kwani liliwezesha mtafiti kuelewa bayana mpangilio ya lugha kihadhi hasa katika jamii zilizo na hali ya wingilugha. Eneo la utafiti wetu lilkuwa katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ambako tulichunguza matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu. Mipangilio ya lugha ama kidiglosia au kitriglosia katika jamii ndio huzua suala la mielekeo ya lugha. Utafiti huu ulilenga

kubaini mielekeo walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kama ilivyobainika katika matokeo ya utafiti huu, vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo chanya kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ikilinganishwa na mielekeo hasi waliyo nayo kuhusu lugha ya Kikuyu. Utafiti huu pia ulibaini kuwa mielekeo hasi ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ndiyo huathiri umilisi wao wa lugha za mama kama vile lugha ya Kikuyu jambo ambalo nalo hatimaye kuathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu mijini.

**3.6 Hitimisho**

Sura hii imejishughulisha na kuyajadili masuala mbalimbali ya kinadharia kuhusu lugha za mama. Hata hivyo, suala lililojitokeza bayana ni kuwa lugha za mama kama vile Kikuyu zimejikuta katika miktadha ya kimatumizi ambamo kuna hali ya wingilugha. Matumizi ya lugha katika mazingira ya wingilugha huzua mipangilio ya diglosia na triglosia na ambayo inaathiri mambo kadhaa kuhusu matumizi ya lugha ya mama. Kwa mfano, katika mipagilio ya matumizi ya lugha ya diglosia na triglosia, lugha za mama kama vile Kikuyu, ndizo huchukua hadhi za chini ikilinganishwa na lugha za matumizi mapana kama vile Kiswahili na Kiingereza. Hali ikiwa hivi, wazungumazaji wa lugha hizi za mama na hasa vijana huwa na mielekeo hasi kuzihusu jambo ambalo huathiri vibaya viwango vya umilisi vya wazungumzaji. Hatimaye uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama hurudi chini na zinaanza kuingia katika mkondo wa kuangamia. Sura hii

pia imeonyesha kuwa kuna juhudi mbalimbali zinazofanywa ili kuimarisha uthabiti wa lugha za mama hasa kupitia elimu. Hata hivyo, ni vigumu kuanzisha juhudi kama hizi kabla ya kubaini hali halisi ya kiisimujamii ya lugha yoyote ile. Kimsingi, sura hii imebaini kuwa lugha nyingi za mama kama vile Kikuyu huenda zinakabiliwa na tishio kwa uthabiti wake wa kiisimujamii jambo ambalo ndicho kitovu cha utafiti wetu.

# SURA YA NNE

# MBINU ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii ina maelezo kuhusu mbinu za utafiti. Maelezo haya yanahusu mbinu zilizotumiwa ili kupata majibu kwa maswali ya utafiti yaliyoulizwa katika sura ya kwanza. Sehemu hii inajumuisha vipengele kama vile muundo wa utafiti, mahala pa utafiti, jumuiya lengwa, uteuzi wa sampuli na idadi ya sampuli. Pia, kuna maelezo kuhusu vifaa vya utafiti, utafiti awali, mbinu za kukusanya data na hatimaye suala la uchanganuzi wa data.

## 4.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni mpangilio ambao mtafiti hutumia ili apate majibu ya maswali ya utafiti wake. Ritchie na Lewis (2003) wana maoni kuwa muundo wa utafiti ni ramani inayomwongoza mtafiti katika kupata majibu ya maswali yake ya utafiti. Utafiti huu ulitumia muundo wa kisoroveya. Kwa mujibu wa Mugenda (2008), muundo wa kisoroveya huwa ni kama jaribio la mtafiti la kupata data kutoka kwa jumuiya ili kubainisha hali ya sasa ya jumuiya hiyo kwa kutumia kigezo kimoja au kingine. Hivyo basi, muundo wa kisoroveya humwezesha mtafiti kupata habari katika hali halisi ya wakati wa utafiti kutoka kwa sampuli yake. Gray (2009:124) anasema kuwa “muundo wa utafiti wa kisoroveya ni utaratibu wa kukusanya data kwa kutumia hojaji ama mahojiano kutoka kwa sampuli ili kupata data”. Creswell na Clark (2011) wanasema kuwa muundo wa kisoroveya hulenga kumwezesha mtafiti kuelezea mielekeo, maoni, tabia na sifa za jumuiya nzima kwa kutumia data inayotokana na sampuli iliyoteuliwa. Akihimiza haya,

Schilling (2013:106) anasema kuwa "muundo wa kisoroveya hutumika kukusanya data kuhusu mielekeo ya watu, maoni yao na tabia zao kati ya masuala mengine". Schilling anaongezea kuwa kuna utafiti wa kisoroveya wa jumuiya nzima (unaolenga jumuiya yote) na utafiti wa kisoroveya wa sampuli (unaolenga sehemu ndogo tu ya jumuiya). Utafiti wetu ni utafiti wa kisoroveya wa sampuli kwa vile ulilenga sampuli ndogo ya vijana wa jamii ya Kikuyu wanaoishi katika miji teule ya Nairobi, Kiambu na Thika.

**4.3 Mbinu Changamano ya Utafiti**

Utafiti huu ulitumia mbinu changamano ya utafiti. Mbinu changamano ya utafiti imeanza kutumika na watafiti wengi katika nyanja mbalimbali za kiakademia na imeanza kupata umaarufu kama njia ya tatu ya kufanya utafiti hata ingawa mbinu za utafiti ambazo zimekuwa zikitumika kwa wingi hapo awali ni zile za kimaelezo na kijarabati (Johnson na Onweugbuzie 2004, Creswell na Clark 2011).

Creswell na Clark (2011) wanaeleza kuwa mbinu changamano ya utafiti ilianza kupendekezwa kutumika mwishoni mwa miaka ya themanini wakati watafiti kutoka nyanja mbalimbali za kiakademia kama vile sosholojia na lugha walipoanza kujadili uwezekano wa mbinu ya tatu ya utafiti. Watafiti hawa walikuwa kama vile Fielding na Fielding (1986) kutoka Uingereza, Brewer na Hunter (1989), Green (1989) kutoka Marekani, na Morse (1991) kutoka Canada. Baadaye watafiti kama vile Morse (1991), Rallis (1994) na Creswell (2003) walianza kufanya utafiti wakitumia mbinu changamano ya utafiti na kuandika vitabu kuhusu mbinu changamano ya utafiti kama mbinu ya tatu ya kufanya utafiti.

Denzin na Lincoln (2011:271) wanasema kuwa “mbinu changamano ya utafiti ni mtindo wa kukusanya na kuchanganua data kwa kuchanganya mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti mmoja ili kuelewa suala la utafiti vyema zaidi”. Kulingana na Green (1989), mbinu changamano ya utafiti ni mbinu ambayo huhusisha mbinu moja ya kijarabati (inayolenga kukusanya data ya kitakwimu) na mbinu moja ya kimaelezo (inayolenga kukusanya data ya kimaelezo) ambapo mbinu zote mbili zinatumika kwa pamoja katika utafiti mmoja. Johnson na Onweugbuzie (2004) wanasema kuwa mtindo wa mbinu changamano ya utafiti ni ule ambao unahusu matumizi ya mbinu za kimaelezo na kijarabati kwa pamoja katika utafiti mmoja. Naye Gray (2009) anaelezea mbinu changamano ya utafiti kama ukusanyaji au uchanganuzi wa data iliyotokana na mchanganyiko wa mbinu mbili za kimaelezo na kijarabati katika utafiti mmoja ambapo data za aina hizi mbili zimekusanywa. Aidha, Creswell (2007:4) anasema kuwa

> “***Mbinu changamano ya utafiti ni ile ambayo mtafiti hukusanya, huchanganua data, hutayarisha matokeo ya utafiti na hufikia uamuzi fulani akitumia mbinu za kijarabati na kimaelezo kwa pamoja katika utafiti mmoja .” (tafsiri yetu)***

Kulingana na Johnson (2007), uchanganyaji wa mbinu hizi mbili katika utafiti mmoja unaweza kutokea katika hatua ya ukusanyaji data, katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data au katika hatua zote za utafiti. Katika utafiti wetu, mtindo huu wa mbinu changamano ulitumiwa katika hatua ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data ambapo tulitumia mbinu mbalimbali za ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka kwa mbinu zote mbili za kimaelezo na kijarabati. Hii ni kumaanisha kuwa tulitumia mbinu hizi mbili kwa pamoja wala sio moja baada ya nyingine.

Kwa kifupi, katika matumizi ya mbinu changamano ya utafiti, mtafiti hutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Hukusanya data na kuichanganua akitumia mbinu za kijarabati na kimaelezo kwa pamoja.
ii. Huchanganya mbinu zote mbili (kijarabati na kimaelezo) kwa njia kuwa zitachangiana kwa njia sawa au isiyo sawa katika utafiti mmoja.
iii. Huhakikisha kuwa mbinu za kijarabati na kimaelezo za utafiti zimechanganywa katika muundo mahsusi ili kuelekeza mpangilio wa kufanya utafiti mzima.
iv. Anaweza akatumia mbinu changamano ya utafiti katika utafiti mzima au sehemu tu ya utafiti ule. (Creswell et al 2007:5)

Green (2008) anasema kuwa sio utafiti wowote ule ambao hutumia mbinu changamano ya utafiti hata ingawa mbinu hii imeanza kupata umaarufu katika nyanja mbalimbali za utafiti wa kiakademia. Green anaendelea kufafanua kuwa mbinu changamano ya utafiti inaweza kutumika pale ambapo matokeo ya utafiti yaliyopatikana kwa kutumia mbinu ya utafiti ya kijarabati huhitaji kufafanuliwa kimaelezo ili kupata matokeo ya kutegemeka zaidi. Hivyo basi, data ya kimaelezo iliyokusanywa kwa kutumia mahojiano na mijadala ya kimakundi itahitajika kufafanua zaidi matokeo yaliyopatika kijarabati kupitia hojaji.

Creswell (2011:272) naye anaeleza kuwa “mbinu changamano ya utafiti hutumika pale ambapo sana sana data iliyokusanywa kwa aidha mbinu ya kijarabati au kimaelezo haijitoshelezi kikamilifu na basi ni lazima ifafanuliwe zaidi kwa data nyingine iliyokusanywa kwa mbinu ya kimaelezo au kijarabati”. Creswell anatoa mfano kuwa

iwapo mtafiti anatumia mtindo wa utafiti wa kisoroveya ambapo inamlazimu kutumia mbinu ya kijarabati ya utafiti, huenda akahitaji data zaidi iliyotokana na mbinu ya kimaelezo ya utafiti. Katika mfano kama huu, mbinu changamano ya utafiti ndiyo ingekuwa mwafaka zaidi ili mbinu ya kijarabati na kimaelezo ziweze kuchangiana katika utafiti mmoja.

### 4.3.1 Faida za Mbinu Changamano ya Utafiti

Faida za kutumia mtindo wa mbinu changamano katika utafiti kwa mujibu wa Gray (2009:234) ni kama vile:-

i. Kupata matokeo ya kina zaidi kuhusu suala linaloshughulikiwa.
ii. Mbinu mbili katika utafiti mmoja hufaana au kukamilishana. Pale ambapo mbinu moja ina udhaifu ile nyingine itafidia udhaifu huu na basi utafiti kuimarika.
iii. Mbinu changamano hutumika kupima vipengele vya utafiti vinavyoingiliana bali vinatofautiana.
iv. Matokeo ya kutumia mbinu moja hutumiwa kuchangia uchunguzi kwa kutumia mbinu ile nyingine.
v. Mbinu changamano hutumika kutoa mwanga zaidi katika vipengele fulani vya utafiti.
vi. Kupanua upeo wa utafiti kwa kutafitia vifaa mbalimbali vya utafiti.

Naye Creswell (2011:276) amefafanua manufaa ya mbinu changamano ya utafiti ifuatavyo:-

i. Mbinu changamano ya utafiti huongeza uthabiti wa matokeo ya utafiti kwa kupuuzilia mbali udhaifu wa mbinu za kijarabati na kimaelezo za kukusanya na kuchanganua

data. Kwa upande mmoja, mbinu ya kijarabati hutegemea tu takwimu zinazojitokeza na kupuuza maelezo kutoka kwa wahojiwa. Kwa upande ule mwingine, mbinu ya kimaelezo hutegemea zaidi maoni ya wahojiwa kuhusu suala fulani. Udhaifu wa mbinu hizi mbili unaweza kuepukwa iwapo mbinu zote mbili zitatumika katika utafiti mmoja kama mbinu changamano.

ii. Vile vile, mbinu changamano ya utafiti inaweza ikaibua data ya kina zaidi ikilinganishwa na aidha mbinu ya kijarabati ama kimaelezo. Hii ni kwa sababu vifaa mbalimbali vya kukusanya data vitahusishwa katika utafiti mmoja.

iii. Mbinu changamano ya utafiti pia huwawezesha watafiti wa nyanja mbalimbali kutumia mbinu moja ambayo haiwatenganishi.

iv. Hatimaye mbinu changamano ya utafiti humpa mtafiti uhuru mwingi wa kutumia mbinu iliyo mwafaka zaidi kwa utafiti wake.

#### 4.3.2 Udhaifu wa Mbinu changamano ya Utafiti

Creswell (2011:279) anaeleza kuwa "mbinu changamano ya utafiti ina udhaifu kama vile:-

i. Huhitaji mtafiti ambaye ana ujuzi wa kutosha wa kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo kwa vile wakati mwingine watafiti hukabiliwa na tatizo la kuchanganua data ya kijarabati.

ii. Lazima vile vile mtafiti afahamu jinsi ya kutayarisha na kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti vinavyotumiwa na mbinu ya kijarabati kama vile hojaji na mbinu ya kimaelezo kama vile maswali ya mahojiano.

iii. Mbinu changamano hutumia wakati mwingi katika hatua ya ukusanyaji na

uchanganuzi wa data kwa vile mbinu hii hutumia vifaa vingi vya kukusanya data na data inayopatikana ni nyingi vile vile.

iv. Huwa na gharama ya juu kwa vile inatumia vifaa vingi vya utafiti na vinavyombidi mtafiti kuingiliana na wahojiwa kwa wingi".


Ili kuweza kuyajibu maswali ya utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu changamano ya utafiti kama mbinu mwafaka zaidi ya utafiti. Hii ni kwa sababu utafiti wenyewe ulihusisha data ya kijarabati na kimaelezo. Data ya kijarabati ilitokana na hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha na mtihani ya kupima umilisi katika stadi za lugha za kuandika, kuongea na kusoma ilhali data ya kimaelezo ilitokana na majibu ya mijadala ya kimakundi. Aidha, sio ama data ya kijarabati au ya kimaelezo ambayo ingeweza kuyajibu maswali ya utafiti huu kikamilifu. Basi mbinu hizi za kijarabati na kimaelezo zilitumika kwa pamoja katika utafiti wetu ili kuchangiana katika kukusanya na kuchanganua data na basi kuyajibu maswali ya utafiti kwa njia iliyo wazi iwezekanavyo.

Kwa mujibu wa Creswell (2011), mbinu changamano ya utafiti inaweza kuchukua miundo ama sura mbalimbali inapotumiwa katika utafiti. Miundo hii hutegemea jinsi mtafiti anavyopanga kutumia mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti wake. Kwa mfano, mtafiti anaweza akaanza kwa kutumia mbinu ya kijarabati na baadaye akatumia mbinu ya kimaelezo yaani kwa mfululizo. Aidha, mtafiti anaweza akatumia mbinu hizi mbili kwa njia sambamba.

### 4.3.3 Mpangilio Sambamba wa Mbinu Changamano ya Utafiti

Utafiti wetu ulitumia mpangilio sambamba wa mbinu changamano ya utafiti. Katika mpangilio huu, mtafiti alitumia mbinu ya utafiti ya kijarabati na kimaelezo kwa karibu kiwango sawa kila moja ya mbinu hizi mbili ikitumika kwa njia huru kutokana na ile nyingine katika hatua ya kukusanya na kuchanganua data. Hatimaye, data hii ililetwa pamoja na kufasiriwa kama kitu kimoja kabla ya matokeo ya mwisho kupatikana. Katika mchoro, mpangilio sambamba wa mbinu changamano ya utaftiti uliofuatwa katika utafiti huu ni huu ufuatao:-

**Mchoro 5: Mpangilio Sambamba wa Mbinu Changamano ya Utafiti**




(Mtafiti)

### 4.4 Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kaunti ya Nairobi na Kiambu ambapo mtafiti aliteua sampuli ya shule kumi na mbili kila kaunti ikiwakilishwa na shule sita. Kaunti hizi mbili zilichaguliwa kwa vile zina miji mikubwa, yaani Nairobi, Kiambu na Thika, ambako

kunazungumzwa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu ulilenga kuchunguza taathira za Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ni kati ya lugha zinazozungumzwa na idadi kubwa ya watu katika kaunti hizi za Nairobi na Kiambu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika.

Aidha, miji hii ilichaguliwa ili kutoa ulinganisho wa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika. Ulinganisho huu ulikuwa muhimu ili kuweza kubaini kama iwapo maingiliano ya jamiilugha ya Kikuyu katika sehemu za mjini na mashambani yalikuwa na athari zozote kwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini na hatimaye kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu kwa jumla. Miji hii mitatu imeachana kimasafa huko mji wa Kiambu ukiwa takriban kilomita 20 kutoka jijjini Nairobi na mji wa Thika ukiwa takriban kilomita 40 kutoka jiji la Nairobi. Pia, miji ya Kiambu na Thika nayo imepakana na sehemu za mashambani ambako kuna makaazi ya wanajamiilugha ya Kikuyu. Hii ina maana kuwa kuna maingilano mengi kati ya miji ya Kiambu na Thika na jamiilugha ya Kikuyu mashambani kuliko jiji la Nairobi. Kuhusu haya Landweer (2000) anaeleza kuwa jinsi jamiilugha ilivyo mbali kimasafa na jamii za mijini basi ndivyo lugha yao ilivyo na viwango vya juu vya uthabiti wa kiisimujamii.

Uchaguzi wa miji ya Nairobi, Kiambu na Thika basi ulielekezwa na sababu zifuatazo:-

i. Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ni kati ya lugha zinazozungumzwa na idadi kubwa ya watu katika kaunti katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika.

ii. Kuachana kimasafa na katika viwango vya maingiliano kati ya jamiilugha ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na jamiilugha ya Kikuyu mashambani.

Sababu hizi mbili zilifanya miji hii mitatu kuwa mahala mwafaka pa kufanyia utafiti huu. Maelezo kuhusu miji ya Nairobi, Kiambu na Thika yametolewa katika sehemu zifuatazo za 4.4.1, 4.4.2 na 4.4.3.

### 4.4.1 Maelezo kuhusu Jiji la Nairobi

Nairobi ndio mji mkuu wa nchi ya Kenya na ndicho kitovu cha kiuchumi na kiutawala cha Kenya. Hesabu ya watu ya mwaka wa 2009 inaonyesha kuwa mji wa Nairobi una takriban wakaazi 3,138,369. Jiji la Nairobi limejengwa katika eneo la karibu kilomita 150 mraba. Jiji la Nairobi lilipata jina lake kutokana na jina la Kimaasai *Ewaso Nyirobi* lenye maana ya mahali penye maji baridi.

Nairobi kwa sasa ni makutano ya watu kutoka karibu kila jamii nchini Kenya wengi wakija kutafuta nafasi za kazi. Hali ikiwa hivi basi, jiji la Nairobi lina hali ya wingilugha. Baadhi ya jamii moja ambayo ina idadi kubwa ya wakaazi jijini Nairobi ni jamii ya Kikuyu ambayo ni lugha mojawapo ya zile zinazochunguzwa katika utafiti huu. Jiji la Nairobi pia limeshuhudia kuzuka kwa lugha mpya kama vile Sheng miongoni mwa

vijana hasa wanaoishi katika vitongoji vilivyo mashariki mwa mji huu. Lugha ya Sheng, ambayo kwa sasa inazidi kuwa maarufu kimatumizi ndani na nje ya Nairobi, nayo ni lugha nyingine ambayo imehusishwa katika utafiti wetu. Lewis (2009) anafafanua kuwa hata ingawa jiji la Nairobi lina hali ya wingilugha, lugha zinazotumia wa wingi kama lugha za kuunganisha jamii mbalimbali kimawasiliano ni Kiswahili na Kiingereza kwani ndizo lugha rasmi nchini Kenya huku Kiswahili pia kikiwa lugha ya taifa. Lugha za Kiswahili na Kiingereza nazo vile vile zilichunguzwa katika utafiti huu.

Jiji la Nairobi lilianzishwa mnamo mwaka wa 1899 kama kituo kidogo cha reli ya Mombasa – Nairobi - Uganda iliyokuwa ikijengwa wakati ule. Kituo hiki kidogo cha reli cha Nairobi baadaye kilichomwa moto lakini kuanzia mwaka wa 1900 kilianza kujengwa upya na kufikia mwaka wa 1907 makao makuu ya British East Africa Protectorate yakahamishwa kutoka Mombasa hadi Nairobi. Baadaye jiji la Nairobi lilifanywa makao makuu ya serikali ya kikoloni ya Waingereza nchini Kenya na mji huu ukapewa hadhi ya kuwa manispaa mnamo mwaka wa 1919. Kati ya miaka ya 1920 na 1950 idadi ya waakazi wa kikoloni kutoka Uingereza ilikuwa imeongezeka kutoka 9, 000 hadi 80, 000. Mnamo mwaka wa 1954 mji wa Nairobi ulipata hadhi ya kuwa jiji na baada ya nchi ya Kenya kujinyakulia uhuru mnamo mwaka wa 1963, jiji la Nairobi likawa mji mkuu wa nchi ya Kenya.

### 4.4.2 Maelezo kuhusu Mji wa Kiambu

Mji wa Kiambu ndio makao makuu ya kaunti ya Kiambu na upo takriban kilomita 20 kutoka jiji la Nairobi. Kulingana na hesabu ya idadi ya watu nchini Kenya ya 2009, mji

wa Kiambu una takriban wakaazi 13,814 wengi wakiwa wa jamii ya Kikuyu. Mji huu umepakana na maeneo ya mashambani ambayo ni makaazi ya jamiilugha ya Kikuyu kama vile Ndumberi, Ikinu, Kanunga, Kirigiti kati ya maeneo mengine. Aidha, mji wa Kiambu una hali ya wingilugha ambako lugha maarufu zinazozungumzwa hapa ni Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng (maarufu miongoni mwa vijana)

Asili ya neno Kiambu imetolewa maelezo mengi tofauti. Moja ya maelezo haya ni kuwa neno Kiambu limetokana na jina la ukoo mmoja maarufu wa jamii ya Wakikuyu iliyoishi karibu na eneo lililojengwa mji wa Kiambu. Ukoo huu ulijulikana kama *mbari ya mbuu* na hivi neno Kiambu likapatikana. Aidha, kuna maelezo kuwa eneo la Kiambu lilikuwa likipokea mvua za rasharasha kila mara na kwa hivyo likabandikwa jina la Kikuyu la kuelezea hali hii yaani *kia mbuu* kumaanisha mahali pa mvua za rasharasha. Baadaye neno hili likawa Kiambu. Vile vile kuna maelezo kuwa eneo hilo ambamo mji wa Kiambu umejengwa zamani lilishuhundia mapigano ya kikabila ya mara kwa mara kati ya Wamaasai na Wakikuyu na kwa hivyo mara kwa mara nduru zilisika wakati wa vita hivi. Basi Wakikuyu wakaliita eneo hili *kia mbuu* kumaanisha pahala pa nduru. Maelezo ya kwanza, kuwa mji wa Kiambu ulipata jina lake kutokana na ukoo mmoja maarufu wa jamii ya Wakikuyu kwa jina *mbari ya mbuu,* kwa maoni yetu yana ukweli mwingi kuliko maelezo yale mengine mawili. Hii ni kwa sababu jamii ya Wakikuyu ina mazoea ya kupatia mahali jina kutokana na mtu mashuhuri au ukoo unaoishi katika eneo fulani.

Mji wa Kiambu una wingilugha. Lugha inayotumika kwa wingi ni lugha ya Kikuyu kwani wakaazi wengi hapa ni kutoka jamii ya Wakikuyu. Hata hivyo, lugha nyingine

maarufu hapa ni Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Lugha hizi nne ndizo zinazochunguzwa katika utafiti wetu na kwa hivyo mji wa Kiambu ulikuwa eneo mwafaka kwa utafiti wetu.

### 4.4.3 Maelezo kuhusu Mji wa Thika

Thika ni mji wa kibiashara ambao una viwanda vingi vidogo na upo karibu kilomita 40 kutoka jiji la Nairobi. Mji wa Thika ndio makao makuu ya wilaya ya Thika na makao madogo ya Kaunti ya Kiambu. Mji wa Thika kwa sasa una wakaazi kutoka jamii mbalimbali nchini Kenya na kwa hivyo kuna hali ya wingilugha. Wakaazi wengi wa mji huu ni Wakikuyu na lugha ya Kikuyu ndio lugha yenye wazungumzaji wengi hapa. Hata hivyo lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng nazo huzungumzwa hapa kwa wingi. Mji wa Thika kama vile mji wa Kiambu umepakana na maeneo ya mashambani ambayo yana idadi kubwa ya wakaazi wa jamiilugha ya Kikuyu. Maeneo haya ni kama vile Mang'u, Gatuanyaga, Kabati, Ruchu, Gatanga, Ng'araria kati ya maeneo mengine. Mji huu vile vile ulikuwa mwafaka kwa utafiti wetu kwa vile lugha zote nne zinazotafitiwa zinazungumzwa hapa.

Asili ya jina Thika ilitokana na neno la Kikuyu *thika* lenye maana ya kuzika maiti au kitu. Inasemekana kuwa wakati mmoja hapo zamani kulikuwa na kiangazi kikubwa kilichowafanya Wamaasai na Wakikuyu kupigana ili kila jamii iweze kupata umiliki na matumizi ya mito Chania na Thika. Vita hivi vilisababisha vifo vya wapiganaji wengi ambao walizikwa katika eneo ambalo mji wa Thika upo kwa sasa. Basi pahala hapa pakaitwa Thika.

## 4.5 Jumuiya Lengwa

Jumuiya lengwa ya utafiti huu ilikuwa vijana wa jamii ya Kikuyu kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika katika kaunti za Nairobi na Kiambu. Kwa mujibu wa Best na Kahn (2010), jumuiya ni kundi lolote la watu binafsi ambalo lina sifa moja au zaidi kwa ujumla. Sifa hizi ndizo mtafiti hulenga kuzichunguza katika utafiti wake (Ogula 2005). Kulingana na Mugenda na Mugenda (2003), jumuiya ya utafiti ni jumla ya watu au vitu ambavyo vina sifa za kijumla zinazotafitiwa.

Katika utafiti huu, jumuiya ya utafiti iligawanyika mara mbili yaani jumuiya pana na jumuiya finyu. Mtafiti alianza kwa kutambulisha jumuiya pana ya utafiti wake na baadaye akateua jumuiya finyu ya utafiti kutokana na ile jumuiya pana. Hatimaye, jumuiya finyu ya utafiti huu ndiyo iliyotumiwa na mtafiti katika kuteua sampuli ya utafiti huu.

Jumuiya pana ya utafiti huu ililenga vijana wa jamii ya Kikuyu katika shule zote za upili mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Kwa jumla, miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ina takribani shule 270 za upili zote zikiwa na jumla ya wanafunzi takriban 78, 800. Ni kutokana na shule hizi 270 za upili ambapo jumuiya finyu ya utafiti iliteuliwa na mtafiti kupitia sampuli kusudio (taz. 4.6).

Jumuiya finyu ya utafiti huu ilihusisha shule 12 za upili kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Jiji la Nairobi liliwakilishwa na shule 6 huku miji ya Kiambu na Thika ikiwakilishwa na shule 3 kwa kila mji. Kutokana na shule hizi 12 za upili mijini Nairobi,

Kiambu na Thika, jumuiya finyu ya wanafunzi 200 kutoka vidato vya 3 na 4 iliteuliwa kutoka kila shule na kwa hivyo jumla ya wanafunzi 2,400 ilipatakana. Ni kutokana na jumuiya finyu hii ya jumla ya shule 12 za upili na wanafunzi 2,400 ambapo sampuli ya utafiti huu iliteuliwa. Jumuiya hii finyu inaonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali 7: Jumuiya finyu ya Utafiti**

| | MJI | IDADI YA SHULE | IDADI YA WANAFUNZI |
|---|---|---|---|
| **1** | **NAIROBI** | **6** | **1 200** |
| **2** | **KIAMBU** | **3** | **600** |
| **3** | **THIKA** | **3** | **600** |
| | **JUMLA** | **12** | **2 400** |

Kwa vile jumuiya finyu ya utafiti huu bado ilikuwa pana, ilikuwa vigumu kuifanyia utafiti ikiwa kama kundi moja pana. Hivyo basi ilimbidi mtafiti kuifanya jumuiya finyu kuwa ndogo zaidi ili aweze kuitafitia kwa urahisi. Haya yalifanyika kwa kuiteua sampuli kutokana na jumuiya finyu ya wanafunzi 2,400.

### 4.6 Vigezo vya Kuteua Sampuli

Sampuli, kama wanavyofafanua Best na Kahn (2010), huwa ni sehemu ndogo ya jumuiya ambayo imechaguliwa kwa minajili ya kuchunguzwa kwa kina. Kwa kuchunguza sifa mbalimbali katika sampuli, Babbie (2014) anasema kuwa mtafiti hatimaye hupata uamuzi au matokeo fulani ambayo huyajumlisha kama matokeo ya jumuiya nzima aliyokuwa akishughulikia.

Babbie (2014) anaeleza kuwa uteuzi wa sampuli ni utaratibu wa kuchagua idadi ndogo ya wahusika binafsi kutoka kwa jumuiya pana hivi kwamba ile sampuli iliyoteuliwa ina uwezo wa kuwakilisha ile jumuiya pana kikamilifu. Babbie anaongeza kuwa sampuli haiteuliwi kiholela yaani bila kufuata utaratibu wowote ule bali sampuli yafaa kuteuliwa kwa kufuata utaratibu maalum.

Best na Kahn (2010:35) wanaeleza kuwa "njia mwafaka zaidi ya kuteuwa sampuli ya kiisimujamii ni ile ya unasibu. Hii ni kwa sababu uteuzi wa sampuli kinasibu huhakikisha kuwa kila mhusika katika jumuiya amewakilishwa katika sampuli kwa njia sawa na kwa kuepukana na mapendeleo". Hata hivyo, Best na Kahn (2010:36) wanaendelea kusema kuwa, "iwapo mbinu ya sampuli nasibu haiwezakani kwa sababu moja au nyingine, mtafiti anafaa kutumia mbinu nyingine za uteuzi wa sampuli". Babbie (2014) ana maoni kuwa tafiti nyingi za masomo ya sayansi jamii hazitumii mbinu ya sampuli nasibu kwa wingi katika uteuzi wa sampuli zao bali huegemea katika mbinu zisizo za kinasibu za kuteua sampuli kama vile sampuli kusudio. Hii ni kwa sababu mara nyingi sifa zinazotafitiwa katika masomo kama haya huwa si wazi kiasi cha kuweza kutumia unasibu.

Utafiti wetu ulitumia kwa wingi mbinu ya sampuli kusudio. Kwa mujibu wa Best na Kahn (2010), sampuli kusudio humruhusu mtafiti kuteua sampuli ambayo ina wahusika wenye sifa anazozitaka pekee na wale ambao anakisia kuwa watampa majibu anayotaka kutoka kwa sampuli yake. Kulingana na Creswell (2005), sampuli kusudio ni mbinu muhimu ya uteuzi wa sampuli ambayo si ya kubahatisha kwani inampa mtafiti uhuru wa

kuteua sampuli yake kwa kutegemea sifa anazozitafitia katika jumuiya yake. Naye Lune (2010), anasema kuwa sampuli kusudio haiizingatii ukubwa wa sampuli bali jambo muhimu ni kama sampuli yenyewe inamwezesha mtafiti kupata data ya kutosha itakayoshughulikia suala la utafiti kikamilifu. Kombo na Tromp (2006) nao wana maoni kuwa sampuli kusudio huwa mwafaka kwa mtafiti pale ambapo kundi au sehemu fulani ya sampuli inaaminika ndiyo ina data mwafaka inayoafiki malengo ya utafiti. Kwa hivyo, mbinu ya sampuli kusudio ilikuwa mwafaka kwa utafiti wetu kwa vile katika shule 12 tulizozitembelea, tayari jumuiya hii ya vijana ilikuwa na sifa zilizokuwa zikichunguzwa ambazo ni uwezo wa kufahamu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Sampuli elekezi pia ilitumiwa katika kubaini jumuiya finyu na hatimaye sampuli halisi ya utafiti. Sampuli elekezi ni mbinu ya kuteua sampuli ambapo mhusika mmoja katika jumuiya hutumiwa na mtafiti kuwafikia wahusika wengine ambao wana sifa ambazo zitafaa utafiti wake (Best na Kahn 2010). Best na Khan wanaendelea kufafanua kuwa sampuli elekezi hutumika pale ambapo wahojiwa huwa wametapakaa au kuchanganyika katika jumuiya. Hivyo basi, baada ya mtafiti kumpata mhojiwa mmoja au wawili wenye sifa anazozitaka, yeye humtumia mhojiwa huyu kuwafikia wengine wenye sifa zizo hizo katika jumuiya yake.  Jumuiya ya utafiti wetu ilikuwa na vijana kutoka jamii tofauti na kwa hivyo ili kuwafikia vijana wa jamii ya Kikuyu pekee, mbinu ya sampuli elekezi ilikuwa mwafaka.

Sampuli ya utafiti huu ilihusisha vijana wa asili ya Kikuyu wanaoishi katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika na ambao walikuwa wanafunzi katika shule za upili. Sampuli

hii ilijumuisha tu vijana ambao wameishi katika sehemu za mjini tangu utotoni ili kuhakikisha kuwa data iliyopatikana kutoka kwao ilikuwa ya kutegemeka zaidi.

Sampuli ya vijana katika utafiti huu ilichaguliwa kutoka kwa jumuiya finyu ya shule 12 za upili katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Miji hii iliteuliwa kupitia sampuli kusudio. Mtafiti alichagua miji ya Nairobi, Kiambu na Thika kwa vile kuna wakaazi wengi wa jamii ya Kikuyu na pia kwa sababu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zinatumika kwa wingi katika miji hii. Katika utafiti huu, kusudi lilikuwa kuchunguza kuhusu athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Basi miji hii mitatu (Nairobi, Kiambu na Thika) ilikuwa mwafaka kwa utafiti wetu kwani lugha hizi nne zinatumika hapa.

Vile vile, shule zilizozochaguliwa kwa utafiti huu ziliteuliwa kupitia sampuli kusudio. Hizi zilikuwa shule ambazo zina wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu na ambao wanakaa katika sehemu za mijini. Shule hizi zilikuwa 2 za wasichana, 2 za wavulana na 2 za mseto kutoka mji wa Nairobi, shule 1 ya wasichana, 1 ya wavulana na 1 ya mseto kutoka miji ya Kiambu na Thika jumla ikiwa shule 12 kutoka miji hii mitatu (taz. jedwali 8).

**Jedwali 8: Mgawanyiko wa Shule katika eneo la Utafiti**

| | SHULE ZA WASICHANA | SHULE ZA WAVULANA | SHULE ZA MSETO | IDADI |
|---|---|---|---|---|
| NAIROBI | 2 | 2 | 2 | 6 |
| KIAMBU | 1 | 1 | 1 | 3 |
| THIKA | 1 | 1 | 1 | 3 |
| | | | JUMLA | 12 |

Mbinu ya sampuli elekezi pia ilitumiwa hasa pale ambapo mwanafunzi mmoja au wawili katika kila shule waliwaelekeza watafiti kwa wanafunzi wengine wa jamii ya Kikuyu walioishi mijini tangu utotoni. Kusudi la kutumia mbinu ya sampuli elekezi lilikuwa kuweza kupata sampuli ya utafiti huu kwa haraka na kwa uhakika zaidi. Baada ya kuhakikisha kuwa vijana wote waliopatikana kwa kutumia sampuli elekezi walikuwa wa jamii ya Kikuyu na kuwa walikuwa wakaazi wa miji ya Nairobi, Kiambu na Thika hadi utotoni, mbinu ya sampuli nasibu ilitumiwa ili kuchagua sampuli ya vijana waliohusika katika sampuli ya utafiti huu. Mbinu ya sampuli nasibu ilihakikisha kuwa nafasi sawa imetolewa kwa kila mhusika katika jumuiya finyu iliyoshirikishwa katika utafiti huu.

## 4.7 Idadi ya Sampuli

Idadi ya sampuli ya utafiti ilifikiwa baada ya kutilia maanani maoni ya wataalamu mbalimbali kuhusu idadi mwafaka ya sampuli yaani sampuli itakayotoa uwakilishi halisi wa jumuiya ya utafiti. Kulingana na Best na Khan (2010) hakuna maafikiano baina ya watafiti kuhusu idadi halisi ya sampuli ambayo inafaa kuteuliwa kutoka kwa jumuiya. Hii ni kwa sababu watafiti mbalimbali hutumia asilimia na fomyula tofauti wanapoteua

sampuli yao kutoka kwa jumuiya wanayoshughulikia. Best na Khan wanaendelea kufafanua kuwa suala ambalo watafiti hawajaafikiana ni kuhusu iwapo sampuli yafaa kuwa kubwa ama ndogo na vipimo mwafaka vya sampuli kubwa na ndogo ni ipi.

Kwa mujibu wa Milroy (1987:54), "utafiti wa lugha huhitaji matumizi ya sampuli ndogo. Hii ni kwa sababu sampuli kubwa katika utafiti wa lugha husaidia tu kupata data nyingi iliyojaa urudufu". Borg na Gall (2003) nao wanapendekeza kuwa takriban asilimia 30 ya jumuiya yote ni sampuli tosha na wakilishi katika utafiti wowote ule. Maoni haya yanaendelezwa na Orodho (2009) anaposema kuwa sampuli iliyo zaidi ya wahojiwa 30 ni mwafaka kwa utafiti.

Kwa upande mwingine, Kothari (2004) anaeleza kuwa idadi ya sampuli wakilishi yafaa kuwa takribani kati ya asilimia 10 na 15 ya jumuiya yote. Naye Ngechu (2004) ana maoni kuwa idadi ya sampuli yafaa kupimwa kimaeneo. Anatoa mfano kuwa utafiti unaohusu taifa nzima unafaa kuwa na sampuli isiyopungua wahusika 1,000 ilhali tafiti zinazolenga maeneo madogo kama vile wilaya zafaa kuwa na sampuli ya wahusika 50 kuelekea juu.

Kwa mujibu wa Best na Khan (2010:79), "idadi ya sampuli iliyo mwafaka ni ile inayotoa uwakilishi mzuri zaidi wa jumuiya husika, iliyo nafuu kiwakati na kifedha na ambayo itawawezesha watafiti kujumulisha matokeo yao kwa jumuiya". Basi ni maoni ya Best na Khan kuwa hakuna idadi ama asilimia maalum ya wahusika wanaofaa kuteuliwa katika sampuli. Hivyo suala la ukubwa na udogo wa sampuli halifai kujitokeza. Hata hivyo, Best na Khan (2010) wanaeleza kuwa mara nyingi sampuli za wahusika zaidi ya 30

huchukuliwa kama sampuli kubwa na sampuli za wahusika chini ya 30 zikichukuliwa kama sampuli ndogo. Kilicho muhimu zaidi kulingana nao sio ukubwa ama udogo wa sampuli bali ni mbinu zilizotumika katika kuiteua ile sampuli wakilishi zaidi iwezekanavyo.

### 4.7.1 Mchakato wa Kuteua Idadi ya Sampuli

Hata ingawa kuna maoni tofauti kuhusu idadi mwafaka ya sampuli, utafiti wetu ulifuata mchakato maalum wa kiisimujamii ili kupata sampuli mwafaka ambayo ingeweza kutoa uwakilishi kamili wa jumuiya ya utafiti. Patrick (2009) anasema kuwa uteuzi wa idadi mwafaka ya sampuli ya utafiti wa kiisimujamii huanza kwa kubainisha idadi ya jumuiya pana ya utafiti katika eneo la utafiti. Jumuiya pana ya utafiti huu ilikuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika shule za upili mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Miji hii mitatu ina takriban shule 270 za upili ambazo kwa pamoja zina wanafunzi (vijana) takriban 78,800.

Kwa vile haiwezekani kuteua sampuli kutokana na jumuiya pana ya utafiti, Patrick (2009) anaeleza kuwa mtafiti anafaa kuteua jumuiya finyu, mara nyingi kimaksudi, kutokana na jumuiya pana ya utafiti. Ni kutokana na jumuiya finyu ambapo mtafiti atapata idadi mwafaka ya sampuli ya utafiti. Katika kubaini jumuiya finyu ya utafiti, Patrick anaendelea kufafanua kuwa mtafiti anafaa kuweka mipaka halisi ya jumuiya yake finyu. Hatua ya kuweka mipaka halisi ya jumuiya finyu huwa ni kitendo cha kubaini wahusika halisi ambao wanafaa kuhusishwa katika jumuiya finyu. Jumuiya finyu ya utafiti wetu ilikuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika kidato cha 3 na 4 kutoka shule 12

za upili mijini Nairobi, Kiambu na Thika jumla ikiwa vijana takriban 2400 ikichukuliwa kuwa kila kidato kilikuwa na takriban wanafunzi 100. Ni kutokana na jumuiya hii finyu ambapo idadi ya sampuli ya utafiti iliteuliwa.

Baada ya kubaini jumuiya finyu ya utafiti, idadi ya sampuli ya utafiti iliteuliwa. Kwa mujibu wa Schilling (2007:168), “idadi ya sampuli yafaa kuwa ndogo zaidi kuliko jumuiya finyu lakini iwe kiwakilishi halisi cha jumuiya finyu na jumuiya pana ili iweze kutoa matokeo ya kuaminika na kutegemeka”. Idadi ya sampuli ya utafiti huu ilihesabiwa kwa kutumia fomyula ya kupata idadi ya sampuli ikiwa idadi ya jumuiya finyu haizidi 10, 000 na idadi ya jumuiya pana ni zaidi ya 10, 000. Fomyula hii yake Patrick (2009) ni ifuatayo:-

$$nf = \frac{\frac{N}{n}}{(e^2) + z}$$

ambapo nf = idadi ya sampuli. e = 1.96 (utegemevu ukiwa 95%)

N = jumuiya pana z = $\pm$5.2 (kiwango kubalifu cha makosa)

n = jumuiya finyu

Basi katika kuhesabu idadi ya sampuli ya utafiti huu kwa mujibu wa fomyula hii tulipata,

$$nf = \frac{\frac{78\ 800}{2\ 422}}{(1.96^2) \pm 5.2}$$

$$nf = 297.3584 \text{ (takriban 300)}$$

Hatimaye, sampuli nzima ya utafiti huu ilikuwa vijana 300 kutoka kwa shule zote 12 kila jinsia ikiwakilishwa na vijana 150. Idadi ya vijana walioshirikishwa katika sampuli hii kutoka kila shule ilikuwa wanafunzi (vijana) 25 na kwa hivyo ikizingatiwa kuwa jumuiya pana ya utafiti ilikuwa takriban vijana 78,800 na jumuiya finyu ilikuwa vijana 2,400, basi sampuli ya wanafunzi 300 ilipatikana kuwa mwafaka kwa utafiti huu na ambayo ingehakikisha kuwa data iliyopatikana ilikuwa ya kutegemeka.

## 4.8 Vifaa vya Utafiti

Data yote katika utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia vifaa mbalimbali vya utafiti kwa mujibu wa mbinu changamano za utafiti. Vifaa hivi ni vifuatavyo:-

### 4.8.1 Hojaji za Matumizi na Mielekeo ya Lugha

Hojaji huwa ni orodha ya maswali yaliyotayarishwa awali ili kukusanya data ya aina fulani nyanjani. Hojaji huweza kukusanya data kubwa kwa kipindi kifupi cha wakati. Hata hivyo maswali ya hojaji yafaa kutungwa kwa njia kuwa yataibua data yote inayotakikana na kwa usahihi. Borg na Gall (2003:127) wanaeleza kuwa “hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha zafaa kutayarishwa kwa njia kuwa zitagusia aina tatu kuu za mielekeo kutoka kwa wahojiwa. Aina hizi za mielekeo ni pamoja na:-

i. Mielekeo inayohusu kupenda au kutopenda kitu.
ii. Mielekeo inayohusu ufahamu wa mtu kuhusu jambo au hali fulani.
iii. Mielekeo inayohusu moyo wa mtu wa kurekebisha jambo ama hali”.

Naye Baker (1992) anaeleza kuwa hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha hujaribu kubaini kutoka kwa sampuli iwapo lugha inayotafitiwa ni muhimu au si muhimu katika shughuli mbalimbali zinazohusu matumizi ya lugha. Umuhimu wa kimatumizi wa lugha husika hupimwa kutegemea viwango mbalimbali vya umuhimu kama vile muhimu sana, muhimu, si muhimu na si muhimu hata kidogo (Baker 1992). Pia, hojaji hizi hupima mielekeo ya sampuli kuhusu lugha yao kwa kuuliza maswali yanayolenga mielekeo ya kijumla au isio ya kijumla. Maswali haya ni kama vile, Je, ni muhimu kuzungumza lugha hii?, Ufahamu wa lugha hii unaweza kukusaidia kupata kazi au kupandishwa cheo kazini?, Ungetaka kuhesabiwa kama mmojawapo wa wazungumzaji wa lugha hii? (Baker 1992).

Vijana walioshirikishwa katika sampuli ya utafiti huu walipewa hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha walizotarajiwa kuzijibu. Wanafunzi hawa walitakiwa kuyajibu maswali yaliyohusiana na matumizi na mielekeo yao ya lugha za Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng. Maswali haya yalikuwa yakilenga kubaini mielekeo waliyokuwa nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu matumizi ya lugha za Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng katika maeneo mbalimbali ya kijamii ya matumizi ya lugha. (taz. kiambatisho III)

### 4.8.2 Mijadala ya Kimakundi

Mtafiti aliwashirikisha vijana 15 katika kila shule katika mijadala ya kimakundi iliyoongozwa na maswali yaliyokuwa yametayarishwa awali (taz. Kiambatisho I).

Mijadala hii ilihusu mada mbalimbali katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ikilenga kupima viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika stadi ya kuongea na ujuzi wao wa kijumla wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kulingana na Mugenda (2008), mijadala isio rasmi ya kimakundi huwa mwafaka kwa utafiti kwani sampuli huwa imetulia katika mazingira yasio rasmi jambo linalowafanya wajieleze kikawaida na bila uoga.

Mbinu ya uchunguzi ushiriki ilitumiwa na watafiti ili kupata data inayotakikana kutoka kwa sampuli katika stadi ya kuongea kupitia kusikiliza mijadala hii kwa makini. Mijadala hii ilirekodiwa na baadaye watafiti wakaichanganua data hii kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi usemi ili kutambulisha umilisi wa vijana katika lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng kupitia stadi hii ya kuongea. Kulingana na Mugenda na Mugenda (2012), mbinu ya uchanganuzi usemi inahusu kule kurekodi mazungumzo ya sampuli na baadaye mtafiti anazicheza kanda hizi huku akiyachanganua masuala mbalimbali na yaliyo muhimu kwa utafiti wake. Baadhi ya masuala haya ni kama vile kuchanganya msimbo, kuhamisha msimbo, matamshi mabaya ya maneno ya Kikuyu, kiimbo kibaya cha maneno, uwezo wa kushiriki kikamilifu katika mazungumzo katika lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng kati ya mengine.

### 4.8.3 Mazoezi ya Uandishi na Usomaji

Wanafunzi waliounda sampuli ya utafiti huu walishirikishwa katika mazoezi ya kusoma kwa sauti na kuandika katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ili

kupima viwango vya umilisi wa lugha hizi nne walivyo navyo vijana wa jamii ya Kikuyu katika stadi hizi mbili yaani kusoma na kuandika. Haya yalikuwa mazoezi mafupi ya kusoma kwa sauti na kuandika makala fupi kwa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ambayo baadaye yalisahihishwa na kuchanganuliwa na watafiti ili kuweza kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika stadi za kusoma na kuandika. Uwezo mbalimbali katika kusoma na kuandika wa watafitiwa katika shughuli hii ndio uliotumika kutofautisha viwango vyao mbalimbali vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika stadi ya kuongea na kuandika. Vigezo vilivyotumiwa vimefafanuliwa katika sehemu ifuatayo ya 4.8.4

### 4.8.4 Vigezo vya Kupima Umilisi.

Katika stadi hizi za kuongea, kusoma na kuandika, vigezo mbalimbali vilitumiwa na mtafiti ili kupima viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Vigezo hivi vilikuwa kusitasita katika mazungumzo na kusoma, kuchanganya msimbo, kuhamisha msimbo, matamshi mabaya ya maneno, maendelezo mabaya ya maneno, kiimbo kibaya na ung’amuaji wa maana ya maneno, uwezo wa kujieleza kwa ufasaha, uhaba wa msamiati katika mazungumzo na uandishi katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng kati ya vigezo vingine. Vigezo hivi vyote ndivyo vilivyotumiwa na mtafiti katika kupima na kubaini viwango vya umilisi walio nao vijana wa jamii ya Kikuyu mijini katika lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

## 4.9 Utafiti Awali

Hatua ya mwisho ya kuhakikisha kuwa vifaa vya utafiti ni vya uhakika katika ukusanyaji wa data ni ya utafiti awali (Mugenda 200). Hii ni kwa sababu utafiti awali humpa mtafiti fursa halisi ya kufanyia vifaa vya utafiti majaribio nyanjani akitumia idadi ndogo ya wahojiwa. Lengo kuu huwa ni kubaini iwapo kuna shida yoyote katika maswali ya hojaji na mahojiano kama vile maswali tata na yasiyoeleweka vyema na wahojiwa. Aidha, mtafiti hupata fursa ya kupima iwapo vifaa vyake vya utafiti vinaibua data ya kutosha au la na pia iwapo data inayopatikana kutoka kwa wahojiwa ni mwafaka katika kuyajibu maswali ya utafiti.

Kabla ya kwenda nyanjani kukusanya data, mtafiti alivifanyia majaribio vifaa vya utafiti ili kuwa na uhakika kuwa vifaa hivi vingetegemewa katika kukusanya data ambayo ilikuwa na uhalali na utegemevu. Hatua hii ya utafiti awali ilitekelezwa baada ya wasimamazi kuvipitia vifaa vya utafiti huu, kutoa ushauri na mapendekezo yao na mtafiti kutilia maanani masuala yote kutoka kwa wasimamizi ili kuhakikisha kuwa vifaa hivi vingetumika kukusanya data ya utafiti huu kwa utegemevu wa hali ya juu. Vifaa vilivyofanyiwa majaribio ni pamoja na hojaji za mielekeo na matumizi ya lugha, maswali ya mahojiano ya makundi na vifungu vya ufahamu vilivyotumika kupima umilisi wa lugha. Vifaa hivi vya utafiti vilifanyiwa majaribio kwa awamu mbili katika shule ya upili ya mseto ya Kasarani Academy ambayo haikuhusishwa tena katika utafiti wenyewe. Jumla ya wanafunzi waliohusishwa katika awamu hizi mbili za utafiti awali walikuwa wanafunzi 30 kukiwa na wasichana 15 na wavulana 15 kutoka kidato cha 3 na 4.

Katika awamu ya kwanza, watafiti waliteua kimaksudi wanafunzi kumi kutoka kidato cha 3 na 4 miongoni mwao wakiwa wasichana 5 na wavulana 5. Baada ya kufanya utafiti awali katika awamu hii ya kwanza, ilitokea kuwa baadhi ya maswali ya kuelekeza mijadala ya kimakundi yalifaa kubadilishwa ili kuweka maswali mengine ambayo yangetoa maelezo zaidi yaliyokuwa yameachwa na maswali katika hojaji za mielekeo na matumizi ya lugha. Awamu ya pili ya utafiti awali ilihusisha jumla ya wanafunzi 20 (wasichana 10 na wavulana 10). Lengo la utafiti awali huu wa pili lilikuwa kupima iwapo shida zilizokuwa zimepatikana katika utafiti awali katika awamu ya kwanza zilikuwa zimesuluhishwa baada ya marekebisho yaliyofanywa. Matokeo ya utafiti awali katika awamu ya pili yalimhakikishia mtafiti kuwa vifaa vya utafiti vilikuwa na kiwango cha juu cha uhalali na utegemevu kwani hakuna shida yoyote iliyopatikana na vifaa hivi katika ukusanyaji wa data.

### 4.9.1 Uhalali

Kulingana na Mbwesa (2006:14) “uhalali wa vyombo vya utafiti hurejelea kiwango cha kifaa cha utafiti cha kuweza kupima kile ambacho kimelengwa kupima”. Uhalali wa vifaa vya utafiti ulihakikishwa kupitia kwa wasimamizi wa utafiti huu. Wasimamizi waliyapitia maswali ya hojaji ya mielekeo na matumizi ya lugha, maswali ya kuongoza mijadala ya kimakundi na mitihani ya kupima umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika stadi za kusoma, kuandika na kuongea miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ili kuhakikisha uhalali wake. Marekebisho yaliyotolewa na wasimamizi yalifanywa na mtafiti ili kuhakikisha kuwa data itakayokusanywa nyanjani ilikuwa halali. Data hii kwa upande wake ilihakikisha

kuwa matokeo yaliyopatikana ni yakutegemeka na yalitoa picha halisi kuhusu sampuli na kwa jumla jumuiya nzima ya utafiti huu.

**4.9.2 Utegemevu**

Mugenda na Mugenda (2012) wanaeleza kuwa utegemevu wa vifaa vya utafiti ni kile kiwango ambacho vifaa hivi humwezesha mtafiti kupata data ya aina moja hata ukusanyaji wa data ukirudiwa tena mara kadhaa kwa kutumia vifaa vile vile na wahojiwa wale wale. Naye Patton (2002) anaeleza kuwa utegemevu wa vifaa vya utafiti ni ule uwezo wa vifaa vya utafiti wa kutoa matokeo sawa katika majaribio mawili au zaidi kwa kutumia wahojiwa sawa.

Kwa mujibu wa Patton (2002:55), "njia moja maarufu ya kubaini utegemevu wa vifaa vya utafiti ni kwa kutumia mbinu ya jaribio maradufu. Katika mbinu hii, majaribio mawili hufanywa lakini kwa awamu mbili tofauti na kwa wakati tofauti yakihusisha wahojiwa wale wale. Iwapo mtafiti atapata matokeo sawa ama yaliyotofautiana kwa kiasi kidogo tu, basi vifaa vyake vya utafiti vina utegemevu wa kiwango cha juu". Akielezea zaidi, Patton anasema kuwa njia hii ya kupima utegemevu wa vifaa vya utafiti ni rahisi na iliyo wazi.

Ili kupima utegemevu wa vifaa vyetu vya utafiti, mtafiti alitumia mbinu ya jaribio maradufu katika shule ya upili ya mseto ya Kasarani Academy. Majaribio mawili yalifanyiwa vifaa vya utafiti lakini kwa vipindi viwili tofauti kiwakati. Matokeo yaliyotokana na jaribio la kwanza yalifanana na matokeo ya jaribio la pili na kwa hivyo

kwa jumla vifaa vyetu vya utafiti vilikuwa na utegemevu wa kiwango cha juu na vingetegemewa kutoa matokeo ya kuaminika katika utafiti wenyewe.

### 4.10 Utaratibu wa Kukusanya Data

Baada ya uteuzi wa sampuli, mtafiti alitumia kibali cha Chuo Kikuu cha Kenyatta cha kufanya utafiti nyanjani kumweshesha kupata kibali cha utafiti kutoka kwa shirika la National Council for Science and Technology shirika ambalo husimamia masuala ya kiutafiti nchini Kenya. Kibali hiki ndicho alichokitumia mtafiti kupata idhini ya kutangamana na wanafunzi wa shule za upili ambazo zilikuwa sehemu ya sampuli yake katika kaunti za Nairobi na Kiambu.

Katika kukusanya data, watafiti walitembelea shule 12 za upili zilizoteuliwa kila shule ikiwa na sampuli ya wanafunzi 25 na kwa jumla sampuli kamili ya utafiti huu ilikuwa wanafunzi 300 katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Miji hii ilichaguliwa kwa vile ilikuwa na wakaazi wengi wa jamii ya Kikuyu wanaoishi humo.

Katika kila shule, mtafiti alihakikisha kuwa amejitambulisha vyema kwa wahojiwa na kisha kuwaeleza lengo la utafiti huu na umuhimu wa utafiti wenyewe kwa vijana kama wao. Vile vile matafiti aliwaelezea vyema utaratibu wa kuyajibu maswali ya hojaji ya mielekeo na matumizi ya lugha, jinsi ya kufanya mtihani ya kupima umilisi katika stadi za lugha na hatimaye kuhusu utaratibu wa kushiriki katika mijadala ya kimakundi. Haya

yote yalifanywa ili kuhakikisha kuwa wahojiwa wote walifahamu kile walichotarajiwa na mtafiti kukifanya na pia kuhakikisha kuwa wote waliupata umuhimu wa zoezi hilo.

Aidha, mtafiti alielekeza kila hatua ya ukusanyaji data hii kwa kuwasomea kila swali katika hojaji moja baada ya lingine. Hata ingawa utaratibu huu ulichukuwa muda mrefu, mtafiti alikuwa na uhakika kuwa kila swali limejibiwa na kuwa kila mhojiwa amerudisha hojaji yake. Vikao vya mahojiano ya kimakundi viliendeshwa kwa utaratibu kama ule katika hojaji huku mtafiti akirekodi mahojiano haya kwa uchanganuzi baadaye. Mithani ya kupima umilisi wa stadi za kuongea, kusoma na kuandika nayo ilikuwa na ufupi wa kadri ili isichoshe wahojiwa na kwa wakati ule ule iweze kupima kikamilifu umilisi wao katika stadi hizi za kuongea, kusoma na kuandika.

### 4.11 Uchanganuzi wa Data

Uchanaganuzi wa data ni ule uchunguzi wa data iliyokusanywa nyanjani na kufanya uamuzi fulani kuihusu. Kwa mujibu wa Mbwesa (2006:18), “uchanganuzi wa data ni jumla ya shughuli na taratibu zote ambazo mtafiti huifanyia data yake ili kufikia uamuzi na matokeo fulani kutokana na data hii. Basi shughuli nzima ya uchanganuzi wa data itahusu mambo kama vile kuainisha, kupanga upya, kuiweka data katika makundi sawa kati ya shughuli nyingine”.

Kwa kuzingatia malengo ya utafiti na nadharia za utafiti huu, data iliyokusanywa nyanjani ilichanganuliwa ili kubaini athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini

Nairobi, Kiambu na Thika na basi kubaini hali ya kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana hawa.

Data kutoka kwa hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kijarabati. Uchanganuzi huu ulifanywa kwa kutumia programu za uchanganuzi wa data ya SPSS. Kabla ya uchanganuzi huu, data katika hojaji hizi ilikaguliwa huku watafiti wakijaribu kutenga data yenye upungufu fulani kama vile kujazwa maswali visivyo. Ilikuwa muhimu kuondoa data kama hii ili isije ikapotosha matokeo ya utafiti wetu. Data iliyobaki ilipangwa kulingana na maswali mbalimbali yaliyoulizwa na kisha kuchanganuliwa kwa kutumia programu ya SPSS.

Data ya hojaji hizi zaidi ilihusu kubaini ruwaza za matumizi na mielekeo ya lugha walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Data kutokana na mijadala ya kimakundi iliyokuwa imerekodiwa ilifafanuliwa kimaelezo. Mtafiti alicheza kanda zilizorekodiwa data hii huku akichanganua masuala muhimu yaliyojitokeza kuhusu umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Mazoezi ya kusoma na kuandika pia yalisahihishwa na matokeo kuchanganuliwa kimaelezo nia ikiwa kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika stadi za kusoma na kuandika.

### 4.12 Uwasilishaji wa Data

Data ya utafiti huu iliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo na kijarabati. Mbinu za kijarabati za uwasilishaji data zilizotumiwa ni kama vile chati za mduara, histogramu na majedwali ili kuonyesha mielekeo walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha za Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng na maeneo ya kijamii ambako vijana wa jamii ya Kikuyu hutumia lugha hizi. Hatimaye, matokeo ya utafiti yalijikita zaidi katika kutimiza malengo ya utafiti na kuyajibu maswali ya utafiti kwa mujibu wa nadharia zilizoongoza utafiti huu. Mapendekezo hatimaye yalitolewa (taz. sura ya saba).

### 4.13 Hitimisho

Sura hii kwa jumla ilijihusisha na maelezo kuhusu mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Baadhi ya masuala yaliyofafanuliwa ni pamoja na muundo wa utafiti uliotumiwa katika utafiti huu na hasa mbinu changamano ya utafiti, jumuiya lengwa ya utafiti, mbinu za kuteua sampuli na idadi ya sampuli. Mengine yaliyogusiwa ni kama vile maelezo kuhusu vifaa vya utafiti na suala la utafiti awali.

# SURA YA TANO

# UWASILISHAJI WA DATA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ni ya uwasilishaji wa data iliyokusanywa nyanjaji kwa kutumia vifaa vya ukusanyaji data ambavyo vilikuwa hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha na mitihani ya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Data hii ilikusanywa kutokana na sampuli ya vijana wa jamii ya Kikuyu wanaoishi katika miji ya Nairobi, Thika na Kiambu katika kaunti za Nairobi na Thika. Utafiti huu ulitumia mbinu changamano ya utafiti katika kuwasilisha na baadaye kuchanganua data iliyokusanywa. Data kutokana na hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha na mitihani ya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingreza na Sheng imewasilishwa kwa njia ya kijarabati kupitia histogramu na majedwali.

## 5.2 Mielekeo ya Vijana Mijini Kuhusu Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Kama ilivyobainishwa awali katika mbinu za utafiti, hojaji ya mielekeo ya lugha ilitumiwa ili kukusanya data muhimu ambayo ingeonyesha mielekeo ambayo wahojiwa walikuwa nayo kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hojaji hii iligawanyika katika sehemu mbili kuu zote zikiwa na maswali yaliyolenga kubaini mielekeo ya wahojiwa kuhusu lugha hizi nne. Sehemu ya kwanza ililenga kubaini umuhimu uliopewa kila lugha na wahojiwa katika shughuli na miktadha tofauti tofauti ya kijamii. Sehemu hii ilikuwa na kauli 13 zilizolenga shughuli na miktadha kama vile kupata elimu, kufanya biashara, kupata kazi, kuzungumza na watu wazee na wale wa rika moja na wahojiwa, kufanya urafiki, kuabudu (kanisani au


miskitini), kufahamu kuhusu masuala ya kitamaduni na kuwasiliana katika eneo la nyumbani. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

## 5.3 Uchanganuzi wa Data ya Kibinafsi ya Wahojiwa

### 5.3.1 Kidato cha Wahojiwa

Ubainishaji wa kidato cha wahojiwa ulikuwa muhimu katika utafiti huu ili kuhakikisha kuwa kundi hili la wahojiwa liliweza kuwakilisha vyema jumuiya lengwa iliyohusisha vijana wa shule za upili katika kidato cha tatu na nne.

**Mchoro 6: Kidato cha Wahojiwa.**




Matokeo hapa yanaonyesha kuwa asilimia 51 ya vijana waliohojiwa ilikuwa ya wanafunzi wa kidato cha nne huku asilimia 49 ikiwa ya wanafunzi wa kidato cha tatu. Kwa hivyo, kila kidato kiliwakilishwa kwa karibu idadi sawa ya wahojiwa ijapokuwa wahojiwa kutoka kidato cha nne walikuwa wengi kidogo ikilinganishwa na wale wa kidato cha tatu. Hata hivyo, tofauti hii haikuwa na athari zozote zile kwa utafiti huu kwa jumla kwa vile wote walikuwa katika kundi moja katika umri.

### 5.3.2 Umri wa Wahojiwa.

Kundi la vijana lilikuwa kigeu muhimu kwa utafiti huu. Ili kubaini umri wa kila mhojiwa aliyeshiriki katika kujaza hojaji hii, wahojiwa wote waliombwa kujaza umri wao katika miaka. Jambo hili lilisaidia katika kuhakikisha kuwa vijana waliohojiwa walikuwa wa kidato cha tatu na nne ambao kwa jumla huwa na umri wa kati ya miaka 15 hadi 18.

**Jedwali 9: Umri.**

| | **Miaka** |
|---|---|
| **Wastani** | **17.33** |
| **Kati** | **17.00** |
| **Modi** | **17.00** |
| **Upeo chini** | **14.00** |
| **Upeo juu** | **20.00** |

Matokeo katika jedwali 8 yanaonyesha kuwa umri wa wastani wa wahojiwa wote ulikuwa miaka 17 yule mdogo zaidi katika umri akiwa na miaka 14 na yule mkubwa zaidi katika umri akiwa na miaka 20.


Utafiti huu umejihusisha na sampuli ya vijana pekee wala sio marika mengine katika jamii kwa vile vijana ndio huhusika zaidi na matumizi ya lugha nyingi zinazopatikana katika jamii. Kama asemavyo Kerswill (2000: 182) "kundi la vijana ndilo huonyesha sifa ya kutaka kutalii matumizi ya lugha mbalimbali katika jamii na pia ndilo kundi ambalo hupenda kufanyia lugha majaribio na mabadiliko mengi kuliko kundi lingine lile katika jamii".

Aidha, Eckert (20003:117) ana maoni kuwa "mbali na kundi la vijana kuhusika na matumizi ya lugha nyingi katika jamii, sifa nyingine kuu ya utamaduni wa vijana ulimwenguni ni ile sifa ya vijana kutaka kufanya uvumbuzi mwingi katika matumizi ya lugha hadi kiwango cha kuziunda lugha na misimbo mipya". Ni kwa misingi ya maelezo kama haya ya Echert (2003) na Kerswill (2000), ambapo utafiti huu ulitumia kikundi cha vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika utafiti huu kwa makisio kuwa vijana hawa walikuwa na weledi wa kutosha wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 5.3.3 Jinsia ya Wahojiwa.

Utafiti huu pia ulitilia maanani kigezo cha jinsia ya wahojiwa ili kuhakisha kuwa kulikuwa na ushiriki sawa wa wahojiwa kijinsia. Kwa kufanya hivi, jinsia zote mbili za kike na kiume zingewakilishwa kwa njia sawa.

**Mchoro 7: Jinsia ya Wahojiwa**




Ni wazi kuwa kutokana na mchoro huu, jinsia zote mbili zilihusishwa kwa kiwango sawa. Wahojiwa wasichana walikuwa asilimia 50 na wavulana asilimia 50. Basi utafiti

wetu ulikuwa na usawa wa kijinsia. Hata hivyo, utafiti huu haukuzingatia tofauti za kijinsia kama kigezo cha kuchunguza athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

## 5.4 Mielekeo ya Lugha kuhusu Shughuli Mbalimbali za Kijamii.

Katika sehemu hii, hojaji hii ililenga kubaini mielekeo ambayo vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa nayo kuhusu lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kijamii. Matokeo yalikuwa ifuatavyo:-

### 5.4. 1 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kupata Elimu au Mafunzo Shuleni.

Kuhusu mielekeo ya vijana kuhusu lugha ambayo waliiona kuwa na umuhimu katika shughuli ya kupata elimu au mafunzo shuleni, matokeo yalikuwa yafuatayo kama inavyoonyeshwa katika jedwali 10 :-

**Jedwali 10: Lugha iliyo Muhimu Katika Kupata Elimu au Mafunzo Shuleni.**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| Lugha | Kiingereza | 297 | 61.0% | 99.0% |
| | Kiswahili | 183 | 37.6% | 61.0% |
| | Sheng | 7 | 1.4% | 2.3% |
| | Kikuyu | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | | 487 | 100.0% | 162.3% |

Kutokana na matokeo katika jedwali hili, ni dhahiri kuwa asilimia 61 ya vijana walionyesha mwelekeo chanya kwa lugha ya Kiingereza kwa kuichagua kama lugha

waliyoiona muhimu zaidi katika kupata elimu shuleni nayo asilimia 38 ya vijana walionekana kukipendelea Kiswahili kama lugha muhimu katika masuala ya elimu. Hata hivyo, asilimia 1 ya vijana wote waliohojiwa ilikuwa na mwelekeo hasi kuhusu Sheng kama lugha ya matumizi katika shughuli za kielimu huku kukiwa hakuna kijana yeyote aliyehojiwa ambaye alichagua lugha ya Kikuyu kama lugha ya matumizi katika shughuli za elimu.

Hii inamaanisha kuwa vijana wana mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Sheng na Kikuyu kuhusu shughuli za elimu ikilinganishwa na mielekeo yao chanya kuhusu lugha za Kiingereza na Kiswahili. Katika shule zote tulizozitembelea, kulikuwa na sera ya matumizi ya lugha ambayo ilihimiza matumizi ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili pekee huku lugha za Kikuyu na Sheng zikiwa zimepigwa marufuku kwa matumizi shuleni. Hali hii ilichangia pakubwa katika kuwafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha za Kikuyu na Sheng kama lugha za matumizi katika elimu.

### 5.4.2 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu katika Shughuli za Biashara

Vijana waliohojiwa walikuwa na mielekeo tofauti kuhusu lugha iliyo muhimu katika shughuli za kibiashara mijini kama inavyodhihirika katika jedwali 11 hapa chini.

**Jedwali 11: Lugha iliyo Muhimu katika Shughuli za Biashara**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| **Lugha** | **Kiswahili** | **208** | **38.8%** | **69.6%** |
| | **Kiingereza** | **167** | **31.2%** | **55.9%** |
| | **Sheng** | **102** | **19.0%** | **34.1%** |
| | **Kikuyu** | **59** | **11.0%** | **19.7%** |
| **Jumla** | | **536** | **100.0%** | **179.3%** |

Uchanganuzi wa matokeo katika suala la mielekeo ya vijana kuhusu lugha ya matumizi katika biashara mijini ulionyesha kuwa lugha ya Kiswahili ilipendelewa na asilimia 39 ya vijana kama lugha ya kuendesha biashara mijini, asilimia 31 ya vijana wakachagua Kiingereza kama lugha ya kibiashara mijini, asilimia 19 ya vijana waliipendelea Sheng kama lugha ya biashara mijini nayo asilimia 11 ya vijana wakichagua Kikuyu kuwa lugha ya biashara mijini.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya kuendesha biashara mijini. Maoni ya vijana hawa ni kuwa lugha zinazofaa kutumika kwa wingi katika uendeshaji wa biashara mijini ni lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hii ina maana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo chanya kuhusu Kiswahili, Kiingereza na Sheng kama lugha za kuendesha shughuli za kibiashara mijini.

### 5.4.3 Mielekeo ya Vijana kuhusu Lugha iliyo Muhimu katika Kupata Kazi za Kitaaluma baada ya Shule.

Kulikuwepo na haja ya kubaini mielekeo waliyokuwa nayo vijana kuhusu lugha waliyofikiria ingewafaa zaidi katika shughuli za kutafuta kazi za kitaaluma baada ya kumaliza masomo shuleni na vyuoni. Jedwali 12 linaonyesha matokeo haya ifuatavyo:-

**Jedwali 12: Lugha iliyo Muhimu Katika Kupata Kazi za Kitaaluma Baada ya Shule.**

| | | Majibu | | Asilimia ya visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| **Lugha** | **Kiingereza** | **286** | **66.2%** | **96.3%** |
| | **Kiswahili** | **136** | **31.5%** | **45.8%** |
| | **Kikuyu** | **6** | **1.4%** | **2.0%** |
| | **Sheng** | **4** | **0.9%** | **1.3%** |
| **Jumla** | | **432** | **100.0%** | **145.5%** |

Kutokana na jedwali 12 hapo juu lugha ya Kiingereza ilichaguliwa na asilimia 66 ya vijana kama lugha ambayo ingewafaa zaidi katika shughuli za kutafuta kazi za kitaaluma baada ya kumaliza masomo. Nayo asilimia 32 ya vijana walikiona Kiswahili kama lugha muhimu ya kuwasaidia kupata kazi baada ya masomo. Lugha ya Kikuyu ilichaguliwa na asilimia 1 pekee ya vijana kama lugha ya kutafuta kazi za kitaaluma baada ya masomo huku lugha ya Sheng nayo ilichaguliwa na asilimia 1 ya vijana.

Kwa upande mmoja, matokeo haya yanabaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama lugha mwafaka za kuwasaidia kupata kazi za kitaaluma baada ya masomo. Kwa upande ule mwingine, vijana mijini wana mielekeo hasi kwa lugha za Kikuyu na Sheng kama lugha za kuwapatia kazi za kitaaluma baada ya masomo.

### 5.4.4 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuzungumza na Wazazi na Watu Wazima Nyumbani.

Utafiti huu pia ulilenga kubaini mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha waliyoiona kuwa muhimu katika kuzungumza na wazazi na watu wazima nyumbani. Matokeo ya suala hili yanabainika wazi kama jedwali 13 linavyoonyesha.

**Jedwali 13: Lugha iliyo Muhimu Katika Kuzungumza na Wazazi na Watu Wazima Nyumbani.**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| Lugha | Kiswahili | 215 | 44.3% | 72.9% |
| | Kiingereza | 123 | 25.4% | 41.7% |
| | Kikuyu | 105 | 21.6% | 35.6% |
| | Sheng | 42 | 8.7% | 14.2% |
| Jumla | | 485 | 100.0% | 164.4% |

Matokeo katika jedwali 13 yalionyesha kuwa, asilimia 44 ya vijana mijini walipendelea Kiswahili kama lugha iliyofaa zaidi kutumiwa katika kuzungumza na wazazi na watu wazima nyumbani. Asilimia 25 nayo ilipendelea kutumia Kiingereza katika mawasiliano baina yao na wazazi na watu wazima nyumbani na mitaani pale mijini huku asilimia 22 ya vijana waliohojiwa wakichagua lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano kati yao na wazazi na watu wazima nyumbani pale mijini. Hii ni licha ya kuwa vijana wote waliohojiwa walikuwa wa jamii ya Kikuyu. Lugha ya Sheng nayo ilichaguliwa na asilimia 9 tu ya vijana wote waliohojiwa.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo chaya kuhusu lugha za Kiswahili na Kiingereza kama lugha ya

mawasiliano nyumbani huku wakionyesha mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu na Sheng kama lugha za mawasiliano katika eneo la nyumbani. Basi lugha za Kiswahili na Kiingereza zinonekana kutoa ushindani mkubwa kwa lugha ya Kikuyu ambayo kwa kawaida yafaa kuwa ndiyo lugha inayotumika kwa wingi zaidi katika eneo la nyumbani kwani familia yote ni Wakikuyu.

### 5.4.5 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuzungumza na Wenzao Mijini.

Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika waliulizwa kutoa maoni yao kuhusu lugha waliyoiona kuwa muhimu katika kuzungumza na wenzao pale mijini. Matokeo haya yanaonyeshwa katika jedwali 14 hapa chini.

**Jedwali 14: Lugha iliyo Muhimu katika Kuzungumza na Wenzako Mijini**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| **Lugha** | **Sheng** | **260** | **53.3%** | **86.7%** |
| | **Kiswahili** | **118** | **24.2%** | **39.3%** |
| | **Kiingereza** | **94** | **19.3%** | **31.3%** |
| | **Kikuyu** | **16** | **3.3%** | **5.3%** |
| **Jumla** | | **488** | **100.0%** | **162.7%** |

Matokeo katika jedwali 14 hapa juu yanabaini kuwa asilimia 53 ya vijana wote waliohojiwa walikuwa na mwelekeo chanya kwa lugha ya Sheng kama lugha ambayo walipendelea kuitumia zaidi katika mawasiliano baina yao, Kiswahili kilichaguliwa na asilimia 24 ya vijana kama lugha ya mawasiliano baina yao mijini huku asilimia 19 ya vijana wakipendelea Kiingereza kama lugha ya mawasiliano baina yao. Hata hivyo, ni asilimia 3 tu ya vijana mijini ambao walikichagua Kikuyu kama lugha ya mawasiliano baina yao pale mijini.

Matokeo haya yanaweka wazi mielekeo hasi walio nayo vijana kwa lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano baina yao. Hakika, vijana hawa wana mielekeo chanya kuhusu lugha za Sheng, Kiswahili na Kiingereza kama lugha za mawasiliano baina yao kwani ndizo lugha ambazo wanaonekana kuzipendelea zaidi dhidi ya lugha ya Kikuyu ambayo ndiyo yafaa kuwa lugha yao ya mama.

### 5.4.6 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kutangamana Mijini

Katika jaribio la kubaini lugha ambayo vijana mijini hupendelea zaidi katika shughuli ya kutangamana, utafiti huu uliwauliza vijana kutoa maoni yao kuhusu suala hili kama inavyoonyeshwa katika jedwali 15 hapa chini.

**Jedwali 15: Lugha iliyo Muhimu Katika Kutangamana Mijini**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| Lugha | Sheng | 221 | 45.2% | 74.4% |
| | Kiingereza | 148 | 30.3% | 49.8% |
| | Kiswahili | 115 | 23.5% | 38.7% |
| | Kikuyu | 5 | 1.0% | 1.7% |
| Jumla | | 489 | 100.0% | 164.6% |

Matokeo ya swali hili yanaonyesha kuwa asilimia 45 ya vijana mijini walipendelea kutumia lugha ya Sheng katika masuala ya kutangamana pale mijini, Kiingereza nacho kilipendelewa na asilimia 30 ya vijana kama lugha ya kutangamana mijini huku asilimia 24 ya vijana nao wakichagua Kiswahili kama lugha ya kutangamana mijini. Ni asilimia 1 pekee ya vijana mijini ambao walikipendelea Kikuyu kama lugha ya kutangamana mijini.

Katika matangamano ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika na watu wengine, ilitokea kuwa vijana hawa wana mielekeo hasi kwa lugha ya Kikuyu kama lugha ya kutangamana mijini ikilinganishwa na mielekeo yao chanya kuhusu lugha za Sheng, Kiswahili na Kiingereza.

### 5.4.7 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kuwasiliana Nyumbani.

Vile vile utafiti huu ulilenga kubaini lugha ambayo vijana waliiona kuwa muhimu katika mawasiliano yao na wanafamilia pale nyumbani. Matokeo ya suala hili yanabainika katika jedwali 16 lifuatalo:-

**Jedwali 16: Lugha iliyo Muhimu Katika Kuwasiliana Nyumbani**

| | | **Majibu** | | **Asilimia ya Visa** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Mirudio** | **Asilimia** | |
| **Lugha** | **Kiswahili** | **220** | **41.6%** | **74.3%** |
| | **Kikuyu** | **136** | **25.7%** | **45.9%** |
| | **Kiingereza** | **97** | **18.3%** | **32.8%** |
| | **Sheng** | **76** | **14.4%** | **25.7%** |
| **Jumla** | | **529** | **100.0%** | **178.7%** |

Matokeo ya jedwali 16 kuhusu lugha ya matumizi pale nyumbani miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yalionyesha kuwa asilimia 42 ya vijana mijini hutumia lugha ya Kiswahili nyumbani kwao kuwasiliana, asilimia 26 ya vijana nao walisema kuwa wao hutumia Kikuyu kuwasiliana pale nyumbani kwao, Kiingereza kilitumiwa na asilimia 18 ya vijana kama lugha ya mawasiliano nyumbani kwao pale mijini huku asilimia 14 ya vijana wakisema kuwa wao hutumia lugha ya Sheng katika mawasiliano yao na wanafamilia wengine pale nyumbani.

Matokeo katika jedwali la 16 yanaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili inatoa ushindani mkubwa kwa lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano katika eneo la nyumbani la matumizi ya lugha. Ikitiliwa maanani kuwa wanafamilia wote ni Wakikuyu basi lugha ya Kikuyu ndiyo inayofaa kutumika kwa wingi katika eneo la nyumbani. Basi vijana wa jamii ya Kikuyu wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano nyumbani badala ya kuwa na mielekeo chanya kwa lugha ya Kikuyu. Aidha, kuna asilimia kubwa ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambao nao wanazipendelea lugha za Kiingereza na Sheng kama lugha za matumizi nyumbani na basi kutoa ushindani zaidi kwa lugha ya Kikuyu.

### 5.4.8 Mielekeo ya Vijana Kuhusu Lugha iliyo Muhimu Katika Kufahamu Utamaduni.

Aidha, utafiti huu ulilenga kubaini mielekeo ya vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha waliyofikiria kuwa muhimu zaidi katika kufahamu utamaduni wao kama jedwali 17 linavyoonyesha.

**Jedwali 17: Lugha iliyo Muhimu Kufahamu Kuhusu Utamaduni.**

| | | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|---|
| | | Mirudio | Asilimia | |
| Lugha | Kikuyu | 241 | 63.4% | 82.0% |
| | Kiswahili | 75 | 19.7% | 25.5% |
| | Kiingereza | 55 | 14.5% | 18.7% |
| | Sheng | 9 | 2.4% | 3.1% |
| Jumla | | 380 | 100.0% | 129.3% |

Matokeo katika jedwali 17 yalibaini kuwa asilimia 63 ya vijana wote waliohojiwa walichagua Kikuyu kama lugha iliyo muhimu zaidi katika kuhifadhi utamaduni

ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Lugha ya Kiswahili nayo ilichaguliwa na asilimia 20 ya vijana kama lugha muhimu ya kuhifadhi utamaduni wao, lugha ya Kiingereza ikachaguliwa na asilimia 15 ya vijana huku asilimia 2 ya vijana wakichagua Sheng kama lugha muhimu ya kuhifadhi utamaduni wao.

Hata ingawa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kikuyu katika shughuli mbalimbali ya kijamii, vijana hawa walionyesha mielekeo chanya kwa lugha ya Kikuyu kama lugha ya muhimu ya kuwawezesha kufahamu kuhusu utamanduni wao. Jambo hili ni muhimu kwa utafiti wetu kwa vile linaonyesha kuwa bado kwa kiasi fulani vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika bado wanaithamini lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya mama.

## 5.5 Mielekeo Zaidi ya Vijana Mijini Kuhusu Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng Kupitia Mizani ya Likati.

Katika sehemu ya pili ya hojaji hii utafiti huu ulilenga kubaini zaidi kiwango cha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza. Aidha, utafiti huu ulilenga kubaini baadhi ya sababu zinazowafanya vijana katika miji hii mitatu kuwa na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha hizi nne. Vijana mijini waliulizwa kuyajibu maswali kuhusu mielekeo ya lugha iliyokuwa katika mfumo wa mizani ya likati. Mizani hii ya likati ilikuwa na kauli 8 ambazo zililenga vipengele mbalimbali vya mielekeo ya vijana

waliohojiwa kuhusu lugha ya Kikuyu kwa upande mmoja na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa upande ule mwingine.

Wahojiwa basi walitakiwa kuyajibu maswali kwa kuchagua jibu moja kutoka kwa mizani ya likati. Baker (1992), kama ilivyofafanuliwa katika ukurasa ufuatao, anasema kuwa unapotumia hojaji za matumizi na mielekeo ya lugha, mtafiti anafaa kutumia mizani ya likati ambayo hutoa majibu kwa mpangilio maalumu ili watafitiwa wachague jibu moja kati ya majibu yaliyotolewa kwenye mizani ya likati. Kauli zote za mizani ya likati zilikuwa na majibu 4 ya kuchagua ambayo yalikuwa ni:

1) Nakubali kabisa

2) Nakubali

3) Nakataa

4) Nakataa kabisa


Wahojiwa walielekezwa jinsi ya kuyajibu maswali haya kwa kuchagua jibu mojawapo ya zile 4 katika kila swali. Maswali haya ya likati yalilenga kutambulisha aidha wahojiwa walikuwa na mwelekeo chaya au hasi kuhusu lugha hizi nne. Kama alikubaliana na kauli iliyotolewa, basi mhojiwa alikuwa na mwelekeo chanya ulionyeshwa na majibu *Nakubali Kabisa* na *Nakubali* na kama mwelekeo ulikuwa hasi majibu yalionyeshwa na *Nakataa* na *Nakataa Kabisa.* Yafuatayo ndiyo matokeo yaliyotokana na majibu ya wahojiwa katika maswali ya hojaji ya likati.

Aidha, katika kila swali la sehemu hii, wahojiwa walitakiwa kufafanua sababu za kuchagua jibu walilolichagua katika mizani ya likati. Wahojiwa walihimizwa kutoa sababu zote ambazo ziliwafanya kuchagua jibu fulani. Maelezo haya yangesaidia mtafiti katika uchaganuzi wa data hii.

### 5.5.1 Ni Muhumu kwa Vijana Kufahamu Lugha ya Kikuyu

Wahojiwa hapa waliulizwa kueleza kama kuna umuhimu wowote kwao wa kuifahamu lugha ya Kikuyu. Lengo kuu lilikuwa kubaini umuhimu ambao vijana mijini waliambatanisha na lugha ya Kikuyu ambayo ni mojawapo wa lugha zilizozungumzwa pale mijini. Matokeo hapa yalikuwa kama yanavyoonyeshwa katika mchoro 8.

**Mchoro 8: Ni Muhumu kwa Vijana Kufahamu Lugha ya Kikuyu**




Kulingana na matokeo haya ni wazi kuwa, asilimia kubwa ya vijana wanaamini kuwa kuna umuhimu wa kuifahamu lugha ya Kikuyu kwa vile asilimia 37 ya vijana walikubaliana kabisa na kauli hii huku asilimia 43 ya vijana walikubaliana na kauli hii.

Hata hivyo, kuna idadi ndogo ya vijana mijini ambao hawakuona umuhimu wowote wa kufahamu lugha ya Kikuyu kwa vile asilimia 13 ya vijana mijini hawakukubaliana na kauli hii nayo asilimia 6 ya vijana mijini hawakukubaliana kabisa na kauli kuwa ni muhimu kwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuifahamu lugha ya Kikuyu.

Kwa jumla, asilimia 80 ya vijana wote waliohojiwa walikubali kuwa kuna umuhimu wa vijana mijini kuifahamu lugha ya Kikuyu. Nayo asilimia 20 ya vijana mijini hawakuona umuhimu wowote wa kuifahamua lugha ya Kikuyu. Jambo hili ni muhimu kwa utafiti wetu ambao unajaribu kutambulisha hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hii ni kwa sababu iwapo shughuli za uimarishaji wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika zitaanzishwa, basi shughuli hii huenda ikawa na ukubalifu miongoni mwa vijana hawa.

### 5.5.2 Sababu za Vijana Mijini Kufahamu au Kutofahamu Lugha ya Kikuyu.

Mbali na kusema kama Kikuyu ni muhimu au si muhimu, vijana waliohojiwa walitakiwa kutoa sababu zilizowafanya kufikia uchaguzi walioufanya kuhusu suala la umuhimu wa kufahamu lugha ya Kikuyu. Sababu zilizotolewa na vijana waliohojiwa zimeonyeshwa katika jedwali 18 lifuatalo:-

**Jedwali 18: Sababu za Kuwepo ama Kutokuwepo Umuhimu wa Kufahamu Kikuyu.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1. Kufahamu utamaduni na asili ya jamii yao. | 134 | 37.3% | 45.6% |
| 2. Kuwasiliana na wazee, wazazi na watu wasiofahamu lugha nyinginezo pale mijini | 121 | 33.7% | 41.2% |
| 3. Sio lazima au muhimu kujifunza Kikuyu | 26 | 6.1% | 8.8% |
| 4. Kikuyu hakitumiki katika maeneo mengi ya kijamii | 24 | 6.7% | 8.2% |
| 5. Kukuza uzalendo wa kijamii | 22 | 3.3% | 7.5% |
| 6. Ili isitoweke au kufa | 12 | 7.2% | 4.1% |
| 7. Hueneza ukabila | 11 | 3.1% | 3.7% |
| 8. Hawakufunzwa Kikuyu na yeyote | 5 | 1.4% | 1.7% |
| 9. Ni lugha iliyopitwa na wakati | 4 | 1.2% | 1.4% |
| Jumla | 359 | 100.0% | 122.1% |


Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kuwa idadi kubwa ya vijana waliohojiwa waliuona umuhimu wa kufahamu lugha ya Kikuyu. Hii ni kwa sababu asilimia 37 ya vijana walisema Kikuyu ni muhimu kwa kufahamu utamaduni na asili ya jamii yao ya Kikuyu, asilimia 34 wakasema kuwa lugha ya Kikuyu kitawafaa katika kuwasiliana na wazee, wazazi na watu wasiofahamu lugha nyingine kama Kiingereza na Sheng, asilimia 6 ya vijana mijini nao walisema kuwa Kikuyu ni lugha muhimu katika kukuza uzalendo wa kijamii huku asilimia 3 ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wakisema kuwa ni muhimu kwa vijana kufahamu lugha ya Kikuyu ili isitoweke au kufa.

Hata hivyo, kuna vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika waliofikiria kuwa hakuna umuhimu wowote kwao wa kuifahamu lugha ya Kikuyu. Asilimia 7 ya vijana mijijni walisema kuwa sio lazima mtu kujifunza lugha ya Kikuyu kwa vile hawakuona umuhimu au faida ya kujifunza lugha hii pale mjini. Nayo asilimia 7 ya vijana mijini hawakuona umuhimu wowote wa kujifunza Kikuyu kwa vile lugha hii huwa haitumiki katika maeneo mengi ya kijamii ya matumizi ya lugha pale mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Asilimia 3 ya vijana mijini walisema kuwa lugha ya Kikuyu hueneza ukabila pale mijini ambako kuna watu kutoka jamii tofauti na kwa hivyo hawakuona umuhimu wa kujifunza Kikuyu. Aidha, asilimia 2 ya vijana mijini walisema kuwa hawakufunzwa lugha ya Kikuyu na yeyote pale mjini Nairobi, Kiambu na Thika na kwa hivyo hata nao hawakuona umuhimu wa kujifunza lugha ya Kikuyu vile vile. Hatimaye, asilimia 1 ya vijana mijini walisema kuwa si muhimu kwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kujifunza lugha ya Kikuyu kwa vile ni lugha iliyopitwa na wakati ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 5.5.3 Kikuyu Hutumika Nyumbani Kwetu Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng

Utafiti huu pia ulitaka kuchunguza kuhusu matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika eneo la nyumbani. Lengo hapa lilikuwa kubaini iwapo lugha za mama kama vile Kikuyu hutumika kuwasiliana nyumbani ikilinganishwa na lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Matokeo ya swali hili la utafiti yanaonyeshwa katika mchoro 9 ufuataao:-

**Mchoro 9: Kikuyu Hutumika Nyumbani Kwetu Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng.**




Kulingana na matokeo haya ni wazi kuwa, ni asilimia ndogo ya vijana waliosema kuwa lugha ya Kikuyu hutumika nyumbani kwao kuwasiliana. Asilimia 20 ya vijana walikubaliana na kauli hii huku asilimia 19 ya vijana wakikubaliana kabisa na kauli hii kuwa lugha ya Kikuyu hutumika nyumbani kwao kuliko lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hata hivyo, kuna asilimia kubwa ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika waliosema kuwa lugha ya Kikuyu haitumiki katika mawasiliano nyumbani kwao. Matokeo katika mchoro 9 hapa juu yanaonyesha kuwa asilimia 37 ya vijana mijini hawakukubaliani na kauli hii huku asilimia 24 ya vijana mijini ikiwa hawakukubaliana kabisa na kauli hii.

Kwa jumla, asilimia 39 ya vijana wote waliohojiwa ndio waliokubali kuwa lugha ya Kikuyu hutumika nyumbani kwao kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Nayo zaidi ya nusu ya vijana waliohojiwa mijini Nairobi, Kiambu na Thika yaani asilimia 61 walisema

kuwa hawaitumii lugha ya Kikuyu kuwasiliana pale nyumbani bali hutumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Matokeo katika mchoro wa 9 yanasisitiza zaidi ukweli kuwa kwa jumla vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la nyumbani. Hii ina maana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapati fursa mwafaka ya kupokezwa lugha yao ya mama (Kikuyu) pale nyumbani hali inayoathiri umilisi wao wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 5.5.4 Sababu za Vijana Mijini za Kutumia Kikuyu Nyumbani Kwao Kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Vijana waliohojiwa katika miji teule walitoa sababu mbalimbali za kuwepo au kutokuwepo kwa matumizi ya Kikuyu nyumbani kwao ilikilinganishwa na matumizi ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Sababu zilizotolewa na vijana hawa zimeonyeshwa katika jedwali 19 lifuatalo:-

**Jedwali 19: Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Nyumbani.**

| Sababu zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1. Kikuyu kinafahamika tu na wazazi | 129 | 41.3% | 43.3% |
| 2. Kkuyu kinafahamika na wazazi na watu wengine kama lugha yao ya mama | 71 | 22.8% | 23.8% |
| 3. Vijana wapendelea kutumia lugha nyingine kama Kiswahili na Kiingereza | 49 | 15.7% | 16.4% |
| 4. Ili kuwe na mawasiliano nyumbani | 24 | 7.7% | 8.1% |
| 5. Ili watoto wafahamu lugha ya Kikuyu | 19 | 6.1% | 6.4% |
| 6. Ni lugha ngumu kujifunza | 10 | 3.0% | 3.4% |
| 7. Haisaidii maishani kama vile kupata kazi za kitaaluma | 3 | 1.0% | 1.0% |
| 8. Kikuyu kimepitwa na wakati na wanakichukia | 3 | 1.0% | 1.0% |
| 6. Sio lugha ya elimu na hivyo haihimizwi na Wazazi | 2 | 0.6% | 0.7% |
| 10. Huathiri ujifunzaji wa L2 | 2 | 0.6% | 0.7% |
| Jumla | 312 | 100.0% | 104.7% |

Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kuwa ni idadi ndogo ya vijana mijini waliohojiwa waliosema kuwa wao hutumia lugha ya Kikuyu kwao nyumbani ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Asilimia 23 ya vijana hawa walisema kuwa lugha ya Kikuyu hutumika kwao nyumbani kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa vile ndiyo lugha inayofahamika na wazazi na watu wazima pale mijini. Nayo asilimia 8 ya vijana mijini walisema kuwa lugha ya Kikuyu ilitumika kwao nyumbani ili kuwezesha mawasiliano baina ya wanafamilia hasa wale wasiofahamu

lugha kama vile Kiingereza na Sheng. Aidha, asilimia 6 ya vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika walisema kuwa Kikuyu hutumika nyumbani kwao pale ili watoto wapate fursa ya kuifahamu lugha ya Kikuyu na waweze kukitumia katika mawasiliano yao ya kila siku.

Hata hivyo, kuna idadi kubwa ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambao walisema kuwa wao hawatumii lugha ya Kikuyu kuwasiliana pale nyumbani. Asilimia 41 ya vijana mijijni walisema kuwa lugha ya Kikuyu haitumiki nyumbani kwao kwa vile ni lugha ambayo inafahamika tu na wazazi. Hivyo, ili kuwasiliana pale nyumbani inabidi kutumike lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na hata Sheng.


Asilimia 16 ya vijana mijini nao walisema kuwa wao hawatumii lugha ya Kikuyu pale nyumbani kwao kwa vile wao na hata wazazi wao hupendelea kutumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko Kikuyu. Asilimia 3 ya vijana mijini walisema kuwa Kikuyu huwa lugha ngumu kujifunza ilkilinganishwa na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng na kwa hivyo hawapendi kutumia lugha ya Kikuyu pale nyumbani. Pia, asilimia 1 ya vijana mijini walisema kuwa hawakitumii Kikuyu pale nyumbani kwao kwa vile sio lugha inayotumika katika elimu na kwa hivyo hata wazazi wao pale nyumbani hawawahimizi wajifunze Kikuyu bali husisitiza zaidi wajifunze lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

Asilimia nyingine 1 ya vijana mijini walisema kuwa hawakitumii Kikuyu hata kidogo pale nyumbani kwao kwa vile lugha ya Kikuyu haisaidii mtu maishani kwa mfano katika kujipatia kazi za kitaaluma baada ya masomo. Aidha, asilimia 1 ya vijana mijini waliiona lugha ya Kikuyu kama lugha iliyopitwa na wakati na kwa hivyo wanaichukia na hawaoni haja ya kuitumia kuwasiliana pale nyumbani. Hatimaye, asilimia 1 ya vijana waliohojiwa walisema kuwa hawapendi kutumia lugha ya Kikuyu kuwasiliana pale nyumbani kwani lugha hii huathiri matumizi yao ya L2 kama vile Kiswahili na Kiingereza na ilhali lugha hizi mbili ndizo wanazozitumia shuleni.

### 5.5.5 Hatutumii Kikuyu hata Kidogo Shuleni.

Sera za matumizi ya lugha katika shule mijini, ambamo vijana wote waliojiwa husomea, pia zilichunguzwa katika sehemu hii ya utafiti huu. Lugha zilizochunguzwa hapa ni Kikuyu, Kiswahili, Kiingreza na Sheng ambazo ni baadhi ya lugha zinazotumika kwa wingi kuwasiliana mijini. Lengo kuu lilikuwa kubinisha jinsi lugha hizi nne zinavyotumika shuleni na hasa lugha za mama kama vile Kikuyu na iwapo kuna mielekeo yoyote inayotokana na sera za lugha miongoni mwa vijana mijini shuleni katika miji teule. Ilibainika kuwa katika shule nyingi mijini Nairobi, Kiambu na Thika sera za shule haziruhusu matumizi ya lugha za mama kama Kikuyu miongoni mwa wanafunzi. Haya yanadhihirika wazi katika mchoro 10:-

**Mchoro 10: Hatutumii Kikuyu hata Kidogo Shuleni.**




Mchoro 10 unaonyesha kuwa kwa kiasi kikubwa vijana mjini hawatumii Kikuyu hata kidogo shuleni. Jambo hili ni wazi katika matokeo ya mchoro 10 kwa vile asilimia 19 ya vijana walikubaliana na kauli hii huku asilimia 53 ya vijana wakikubaliana kabisa na kauli hii kuwa hawakitumii Kikuyu hata kidogo shuleni. Hata hivyo, kuna idadi ndogo ya vijana mijini ambao walisema kuwa walikuwa wanaitumia lugha ya Kikuyu shuleni hata ingawa ilikuwa kinyume cha sheria za shule. Ukweli huu unadhihirika vyema katika mchoro 11 kwa vile asilimia 13 ya vijana mijini hawakukubaliana na kauli hii huku asilimia 15 ya vijana mijini wakiwa hawakukubaliana kabisa na kauli hii.

Kwa jumla, asilimia 72 ya vijana wote waliohojiwa walisema kuwa hawaitumii kabisa lugha ya Kikuyu shuleni pale mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hii ni asilimia kubwa ikilinganishwa na asilimia 28 ya vijana ambao walisema kuwa wao hutumia lugha ya Kikuyu kuwasiliana pale shuleni kinyume cha sheria za matumizi ya lugha ambako matumizi ya Kiswahili na Kiingereza huhimizwa huku matumizi ya Kikuyu na Sheng yakiwa yamepigwa marufuku. Kutokana na hali ya kuhimiza matumizi ya lugha za Kiingereza na Kiswahili pekee katika shughuli za elimu, basi inatokea kuwa vijana wa

jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha za mama kama vile Kikuyu kama lugha zinazoweza kutumiwa katika shughuli za kielimu. Aidha, uhimizaji wa matumizi ya lugha za Kiingereza na Kiswahili pekee shuleni kunawanyima vijana fursa ya kuongeza viwango vyao vya umilisi wa lugha za mama kama vile Kikuyu.

### 5.5.6 Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Shuleni.

Mbali na wahojiwa kusema kama walitumia au kutotumia Kikuyu shuleni pale mijini, wahojiwa pia walitoa sababu zao za kuelezea msimamo wao zaidi. Sababu walizotoa za kutumia au kutotumia Kikuyu shuleni zimeonyeshwa katika jedwali 20 lifuatalo:-

**Jedwali 20: Sababu za Kutumia au Kutotumia Kikuyu Shuleni.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1. Si lugha rasmi shuleni, imepigwa marufuku na ukiizungumza utaadhibiwa. | 122 | 34.1% | 40.8% |
| 2. Haiwezeshi mawasiliano kwa vile kuna wanafunzi wa jamii tofauti. | 103 | 28.8% | 34.4% |
| 3. Haitahiniwi shuleni kama vile Kiswahili na Kiingereza. | 25 | 7.0% | 8.4% |
| 4. Ili kupata fursa ya kujifunza lugha nyingine kama Kiswahili na Kiingereza. | 24 | 6.7% | 8.0% |
| 5. Si lugha ya taifa na huenda ilete ukabila shuleni. | 24 | 6.7% | 8.0% |
| 6. Huathiri ujifunzaji wa L2 kama vile Kiswahili na Kiingereza kwa mfano katika matamshi. | 20 | 5.6% | 6.7% |
| 7. Kikuyu hutumiwa kama njia ya kujitenga na vijana wa jamii nyingine kimawasilano. | 15 | 4.1% | 5.0% |
| 8. Hutumika kisirisiri kujifurahisha tu na kama njia ya kukaidi sheria za shule kwa vile ni marufuku miongoni mwa wanafunzi. | 14 | 3.9% | 4.7% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **9. Kuwasiliana na wafanyakazi wengine wa shule wa asili ya Kikuyu** | **11** | **3.1%** | **3.7%** |
| **Jumla** | **258** | **100.0%** | **119.7%** |

Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kuwa ni idadi kubwa ya vijana mijini waliohojiwa walisema kuwa wao hawatumii lugha ya Kikuyu shuleni bali kwa wingi wao hutumia lugha za Kiswahili na Kiingereza. Asilimia 34 ya vijana walisema kuwa hawatumii Kikuyu shuleni kwa vile si lugha rasmi shuleni yaani imepigwa marufuku na ukipatikana ukiizungumza utaadhibiwa, asilimia 29 ya vijana mijini nao walisema kuwa haitumii lugha ya Kikuyu kwani lugha hii haiwezeshi mawasiliano pale shuleni mjini Nairobi, Kiambu na Thika kwa vile kuna wanafunzi kutoka jamii tofauti nchini Kenya huku asilimia 7 wakisema kuwa Kikuyu hakitumiki shuleni ili kuwezesha wanafunzi wapate fursa ya kujifunza lugha za Kiswahili na Kiingereza ambazo ndizo lugha rasmi za masomo nchini Kenya.

Aidha, asilimia 7 ya vijana walikuwa na maoni kuwa Kikuyu hakitumiki pale shuleni kwa vile lugha hii haitahiniwi shuleni kama vile Kiswahili na Kiingereza**,** asilimia 7 ya vijana mijini hawatumii lugha ya Kikuyu pale shuleni kwa vile si lugha ya taifa na huenda ilete ukabila pale shuleni na hatimaye asilimia 6 ya vijana mijini walisema kuwa Kikuyu hakitumiwii shuleni kwani huathiri vibaya ujifunzaji wa L2 kama vile Kiswahili na Kiingereza.


Hata hivyo, kuna vijana ambao walisema kuwa wao hutumia lugha ya Kikuyu kuwasiliana pale shuleni katika sehemu za mijini. Asilimia 4 ya vijana mijini walisema

kuwa vijana wachache hutumia lugha ya Kikuyu pale shuleni kisirisiri kujifurahisha tu na kama njia ya kukaidi sheria za shule kwa vile imepigwa marufuku. Asilimia nyingine 4 ya vijana mijini walisema kuwa wao hutumia lugha ya Kikuyu miongoni mwao kama njia ya kujitenga na vijana wa jamii nyingine kimawasiliano pale shuleni. Kisha asilimia 3 ya vijana mijini walisema kuwa wao hutumia Kikuyu pale shuleni ili kuwasiliana na wafanyakazi wengine wa shule wenye asili ya Kikuyu na ambao hawafahamu vyema lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 5.5.7 Ni Muhimu Kufahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu.

Utafiti huu pia ulilenga kubaini mwelekeo halisi wa vijana mijini kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha nyingine pale mijini kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Ili kubaini mwelekeo wao halisi kuhusu lugha za mama kama vile Kikuyu, vijana waliulizwa kama ni muhimu kufahamu Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko kufahamu Kikuyu. Matokeo ya swali hili yanadhirika vyema katika mchoro 11 ifuatavyo:-

**Mchoro 11: Ni Muhimu Kufahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu**




Katika mchoro 11, ni wazi kuwa idadi kubwa ya vijana mijini iliunga mkono kauli hii kwa kusema kuwa ni muhimu kufahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko

kuifahamu lugha ya Kikuyu. Hii ni kwa sababu asilimia 35 ya vijana mijini walikubaliana na kauli hii huku asilimia 31 ya vijana mijini wakikubaliana kabisa na kauli hii kuwa kuna umuhimu wa kuzifahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, ni idadi ndogo ya vijina mjini waliokuwa na maoni kuwa kuna umuhimu wa kufahamu lugha ya Kikuyu kuliko kufahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kati ya wahojiwa wote, asilimia 23 ya vijana walikukubaliana na kauli hii ilhali nayo asilimia 11 ya vijana hawakukubaliana kabisa na kauli hii pia.

Kwa jumla, asilimia 66 ya vijana wote waliohojiwa walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko kufahamu lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, asilimia 34 ya vijana walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na kuzifahamu lugha nyingine zinazotumika mijini kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Matokeo ya mchoro 11 yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wanaziona lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuwa lugha zilizo na hadhi ya juu kimatumizi kuliko lugha za mama kama vile Kikuyu. Hali hii pia inachangia katika kuwafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu na hatimaye kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa Kikuyu.

### 5.5.8 Sababu za Kufahamu au Kutofahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu

Vijana waliopinga au kukubaliana na kauli kuwa ni muhimu kuzifahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko lugha ya Kikuyu walitoa sababu mbalimbali kama jedwali 21 linavyoonyesha.

**Jedwali 21: Sababu za Kufahamu au Kutofahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng Kuliko Kikuyu.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1. Lugha hizi zinatumika na watu wengi kwa mawasiliano mapana | 155 | 47.7% | 52.4% |
| 2. Kikuyu huendeleza utamaduni | 49 | 15.1% | 16.6% |
| 3. Kiswahili na Kiingereza husaidia kupata Kazi za kitaaluma | 40 | 12.3% | 13.5% |
| 4. Hukuza uzalendo wa kijamii | 28 | 8.6% | 9.5% |
| 5. Huleta umoja na kuondoa ukabila | 24 | 7.4% | 8.1% |
| 6. Ni lugha ya mawasiliano ukizuru sehemu za mashambani. | 22 | 6.8% | 7.4% |
| 7. Mtu huonekana ameendelea (ni wa kisasa) | 7 | 2.1% | 2.4% |
| Jumla | 325 | 100.0% | 109.8% |

Matokeo katika jedwali hili yanaonyesha kuwa ni idadi kubwa ya vijana waliohojiwa mijini Nairobi, Kiambu na Thika walisema kuwa ni vyema kufahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko Kikuyu. Kwa upande mmoja, kati ya wahojiwa wote, asilimia 48 ya vijana walisema kuwa ni afadahli kufahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuliko Kikuyu kwa vile lugha hizi ndizo hutumika na watu wengi kwa mawasiliano mapana mijini wanakoishi. Nayo asilimia 12 ya vijana mijini walisema

kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza husaidia mtu kupata kazi za kitaaluma na hii ndiyo maana wanafaa kuzitumia na kuzifahamu zaidi ikilinganishwa na lugha ya Kikuyu. Aidha, asilimia nyingine 7 ya vijana waliohojiwa walisema kuwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng huleta umoja na huondoa ukabila katika jamii na ndio maana wanafaa kuzifahamu na kuzitumia kwa wingi kuliko Kikuyu pale mijini. Hatimaye, asilimia 2 ya vijana walikuwa na maoni kuwa mtu huonekana ameendelea ama ni wa kisasa anapotumia Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuliko anapotumia lugha ya Kikuyu.


Kwa upande mwingine, kuna vijana ambao walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha ya Kikuyu kuliko lugha ya Kiswahili, Kiingereza au Sheng. Kati ya vijana hawa asilimia 15 walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha ya Kikuyu kuliko Kiswahili, Kiingereza au Sheng kwa vile lugha ya Kikuyu huendeleza utamaduni wa jamii yao ya Wakikuyu. Asilimia 9 ya vijana mijini nao walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha ya Kikuyu kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa vile lugha ya Kikuyu hukuza uzalendo wa kijamii. Hatimaye, asilimia 7 ya vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika walisema kuwa ni muhimu kufahamu lugha ya Kikuyu zaidi kuliko lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa vile lugha ya Kikuyu ni muhimu katika kuendesha mawasiliano wakati wanapozuru sehemu za mashambani.

### 5.5.9 Nahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu

Utafiti huu pia ulilenga kufahamu mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuhusu vijana wenzao ambao hawakifahamu Kikuyu. Swali hili basi lilitaka kupima iwapo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hujionea fahari au huona umuhimu wowote wa kuifahamu

lugha ya Kikuyu. Jambo hili lilisaidia kubaini zaidi mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuhusu lugha ya Kikuyu. Mchoro 12 unaonyesha matokeo haya kama ifuatavyo:-

**Mchoro 12: Nahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu**




Katika mchoro 12, inatokea kuwa tofauti kati ya vijana mijini ambao walikubaliana au kutokabiliana na swali hili haikuwa kubwa sana. Hata hivyo, asilimia kubwa ya vijana walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao ambao hawaifahamu lugha ya Kikuyu. Hii ni kwa sababu asilimia 31 ya vijana walikubaliana na kauli hii huku asilimia 24 nyingine ya vijana walikubaliana kabisa na kauli hii. Hata hivyo, kuna vijana mijini ambao hawakukubaliana na suala hili kwa kusema kuwa hawana huruma kwa vijana wenzao mijini ambao hawafahamu lugha ya Kikuyu. Kati ya vijana, hawa asilimia 19 hawakukubaliana na kauli hii huku asilimia 25 wakiwa hawakukubaliana kabisa na kauli hii. Kwa jumla, asilimia 55 ya vijana wote waliohojiwa walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao ambao hawakifahamu Kikuyu. Nayo asilimia 45 ya vijana wote waliohojiwa mijini walisema kuwa hawahurumii vijana wenzao mijini ambao hawafahamu lugha ya Kikuyu.

Matokeo haya yanaoonyesha wazi kuwa zaidi ya nusu ya vijana wote wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana hamu ya kuifahamu lugha ya Kikuyu. Hii inatokana na ukweli kuwa asilimia 55 ya vijana hawa wanajihurumia kwa kutoifahamu lugha ya Kikuyu. Jambo hili ni muhimu kwa shughuli ya udumishaji na uimarishaji wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Shughuli hii hujihusisha na miradi ya kufunza watu kuhusu lugha yao kama mojawapo ya hatua za kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha.

### 5.5.10 Sababu za Kuwahurumia au Kutowahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu.

Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walipoulizwa sababu zilizowafanya wawahurumie au kutowahurumia vijana wenzao wasiokifahamu Kikuyu, walitoa sababu zifuatazo kama inavyoonyeshwa katika jedwali 22:-

**Jedwali 22: Sababu za Kuwahurumia au Kutowahurumia Vijana ambao Hawakifahamu Kikuyu.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1.Kwa sababu hawawezi kuwasiliana na wazee na watu wazima | 94 | 28.4% | 31.8% |
| 2.Kuna lugha nyingine zinazotumika zaidi kama Kiswahili, Kiingereza na Sheng pale mijini. | 72 | 21.8% | 24.3% |
| 3.Hawafahamu utamaduni/asili yao | 67 | 20.2% | 22.6% |
| 4.Kikuyu hakina maana na kimepitwa na wakati | 56 | 16.9% | 18.9% |
| 5.Wanadharauliwa kwa kutofahamu Kikuyu waendapo mashambani | 23 | 6.9% | 7.8% |
| 6.Kikuyu kinaathiri ujifunzaji wao wa L2 | 10 | 3.0% | 3.4% |
| 7.Watasengenywa bila kujua | 5 | 1.5% | 1.7% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **8.Wanaichukia lugha yao ya mama** | **4** | **1.2%** | **1.4%** |
| **Jumla** | **331** | **100.0%** | **111.8%** |

Kutokana na jedwali 22 hapa juu, vijana waliosema kuwa wanawahurumia vijana wenzao pale mijini ambao hawakifahamu Kikuyu walitoa sababu mbalimbali. Asilimia 28 ya vijana mijini walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao ambao hawakifahamu Kikuyu kwa sababu hawawezi kuwasiliana kwa ufasaha na wazee na watu wazima pale mijini. Asilimia 20 ya vijana mijini nao walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao ambao hawakifahamu Kikuyu kwa vile hawatapata fursa ya kufahamu utamaduni na asili yao. Asilimia 7 ya vijana waliohojiwa walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao wasiofahamu Kikuyu kwa vile wanadharauliwa wanapoenda mashambani kwa kutofahamu lugha ya Kikuyu.

Aidha asilimia 2 ya vijana mijini walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao wasiofahamu Kikuyu kwa vile wanaweza wakasengenywa na watu kwa kutumia Kikuyu bila kujua. Hatimaye asilimia 1 ya vijana mijini nao walisema kuwa wanawahurumia vijana wenzao wasiofahamu lugha ya Kikuyu kwa vile hii ni kama dalili ya kuonyesha kuwa wanaichukia lugha yao ya mama.


Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambao walisema kuwa wao hawawahurumii vijana wenzao wasiofahamu lugha ya Kiswahili nao walitoa sababu zao za kutowahurumia. Asilimia 22 ya vijana mijini walisema kuwa hawahurumii vijana

wenzao ambao hawafahamu Kikuyu kwa vile kuna lugha nyingine zinazotumika kwa wingi kama Kiswahili Kiingereza na Sheng pale mijini na kwa hivyo hawaoni haja ya kufahamu Kikuyu. Asilimia 17 ya vijana mijini walisema kuwa hawawezi kuwahurumia vijana wenzao ambao hawafahamu Kikuyu kwani hawaoni haja ya kujifunza Kikuyu kwa vile ni lugha ambayo haina maana na imepitwa na wakati. Asilimia 2 ya vijana mijijni nao walisema kuwa hawawezi kuwahurumia wenzao ambao hawafahamu Kikuyu kwa vile sio lazima kufahamu lugha hii kwani inaathiri ujifunzaji wao wa L2 kama vile Kiswahili na Kiingereza.

### 5.5.11 Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu Kuliko wale Wanaozungumza Kikuyu.

Utafiti huu pia ulilenga kubainisha hadhi mbalimbali ambazo vijana mijini wamezipea vijana wenzao wanaozizungumza lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ikilinganishwa na lugha ya Kikuyu. Kwa kufanya hivi, mielekeo ya vijana kuhusu lugha hizi nne ingebainika wazi zaidi. Matokeo ya suala hili yameonyeshwa katika mchoro 13 kama ifuatavyo:-

**Mchoro 13: Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu Kuliko wale Wanaozungumza Kikuyu**



Katika matokeo ya mchoro 13, ni wazi kuwa asilimia kubwa ya vijana mijini wana fikra kuwa vijana wanaozungumza lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana hadhi ya juu kuliko wale wanaozungumza Kikuyu. Hii ni kwa vile asilimia 26 ya vijana walikubaliana na kauli hii huku asilimia 40 ya vijana wakikubaliana kabisa na kauli hii. Hata hivyo, kuna vijana mijini ambao hawakukubaliana na suala hili kwa kusema kuwa vijana wanozungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng hawana hadhi kuliko wale ambao wanazungumza Kikuyu. Kati ya vijana hawa, asilimia 11 ya vijana mijini hawakukubaliana na kauli hii huku asilimia 22 ya vijana mijini hawakukubaliana kabisa na kauli hii.

Kwa jumla, asilimia 67 ya vijana wote waliohojiwa walisema kuwa vijana wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi ya juu kuliko wale wanaozungumza Kikuyu. Ni asilimia 33 tu ya vijana wote waliohojiwa mijini waliosema kuwa vijana wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng hawana hadhi ya juu kuliko wenzao wanaozungumza lugha ya Kikuyu.

Data hii inaonyesha kuwa kwa jumla, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo kuwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zina hadhi ya juu kuliko lugha za mama kama vile Kikuyu. Hali hii inachangia kuwepo kwa viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu na hatimaye viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kama inavyofafanuliwa zaidi katika sura ya sita.

### 5.5.12 Sababu za Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuwa na Hadhi ya Juu Kuliko wale Wanaozungumza Kikuyu Mijini.

Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika pia walitakiwa kutoa sababu zao za kuuunga mkono au kutounga mkono kauli hii kuwa vijana wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana hadhi ya juu kuliko wale wanaozungumza Kikuyu. Vijana waliounga mkono au kupinga suala hili walitoa sababu mbalimbali kama inavyojitokeza katika jedwali 23 hapa chini:-

**Jedwali 23: Sababu za Kuunga au Kupinga Suala kuwa Vijana Wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana Hadhi ya Juu Kuliko Wanaozungumza Kikuyu.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1.Wanaweza kuwasiliana na watu wa jamii zote pale mijini. | 70 | 22.0% | 23.8% |
| 2.Hawawezi kuwasiliana na wenzao waendapo mashambani. | 68 | 21.4% | 23.1% |
| 3.Wanaonekana wamesoma na wameheshimika zaidi katika jamii. | 52 | 16.4% | 17.7% |
| 4.Watapata kazi haraka kwa kufahamu lugha kama Kiswahili na Kiingereza | 50 | 15.7% | 17.0% |
| 5.Wanafahamu lugha za kisasa na za kiteknolojia. | 43 | 13.6% | 14.6% |
| 6.Hawafahamu kuhusu utamaduni wao kama wale wanaofahamu Kikuyu. | 27 | 8.4% | 9.2% |
| 7.Wana matamshi mazuri na ufasaha wa kuzungumza kuliko wanaofahamu Kikuyu | 8 | 2.5% | 2.7% |
| Jumla | 318 | 100.0% | 108.2% |

Kutokana na jedwali hili, vijana mijini ambao walisema kuwa wenzao wanaozungumza kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza

Kikuyu walitoa sababu kadhaa. Asilimia 22 ya vijana mijini walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wanaweza kuwasiliana na watu wa jamii zote pale mijini. Asilimia 16 ya vijana mijini nao walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wanaonekana wamesoma na wanaheshimika zaidi katika jamii. Vile vile asilimia nyingine 16 ya vijana mijini walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile watapata kazi haraka kutokana na kufahamu kwao kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza. Aidha, asilimia 14 ya vijana mijini walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wanafahamu lugha za kisasa na za kiteknolojia. Hatimaye asilimia 3 ya vijana mijini walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wana matamshi mazuri na ufasaha mwingi wa kuzungumza kuliko vijana wanaofahamu Kikuyu.


Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambao walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng hawana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu walitoa sababu zao ifuatavyo. Asilimia 21 ya vijana mijini walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng hawana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile hawawezi kuwasiliana kwa ufasaha na wenzao waendapo mashambani. Asilimia 9 ya vijana mijini nao walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng hawana hadhi kuliko

wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile hawafahamu kuhusu utamaduni wao kama wale wanaofahamu Kikuyu.

### 5.5.13 Kuna Wenzangu ambao Hawakipendi Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng

Vijana wa jamii ya Kikuyu wanoishi mijini Nairobi, Kiambu na Thika waliulizwa kuhusu msimamo wao kuhusu kupenda au kutokipenda Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Swali hili lililenga kupima mwelekeo wa kijumla walio nao vijana mijini kuhusu lugha hizi nne. Ni wazi kuwa idadi kubwa ya vijana mijini hawapendi lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kama mchoro 14 hapa chini unavyoonyesha.

**Mchoro 14: Kuna Wenzangu ambao Hawakipendi Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng.**




Matokeo ya mchoro 14 hapo juu yanaonyesha kuwa vijana wengi wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawaipendi lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa asilimia 17 ya vijana walikubaliana na kauli hii huku asilimia 80 ya vijana wakikubaliana kabisa na

kauli hii. Hata hivyo, asilimia ndogo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ilionekana kuipenda lugha ya Kikuyu zaidi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Matokeo ya utafiti yanavyoonyesha kuwa asilimia 2 ya vijana mijini hawakukubaliana na kauli hii huku asilimia 1 pekee ya vijana mijini wakikosa kukubaliana kabisa na kauli hii.

Kwa jumla, asilimia 97 ya vijana wote waliohojiwa walionyesha kuwa vijana wengi mijini hawaipendi lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na vile wanavyozipenda lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Ni asilimia 3 tu ya vijana mijini walioonekana kukipenda Kikuyu. Matokeo haya yanaonyesha kuwa kwa jumla vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo chanya kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng huku wakiwa na mielekeo hasi kuhusu lugha za mama kama vile Kikuyu jambo linalochangia lugha ya Kikuyu kuwa na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 5.5.14 Sababu za Vijana Wengine Kutokipenda Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng

Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walitoa sababu kadhaa za aidha kukipenda au kutokipenda Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng kama jedwali 24 linavyoonyesha.

**Jedwali 24: Sababu za Vijana Wengine Kutokipenda Kikuyu ilhali Wanazipenda Lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng.**

| Sababu Zilizotolewa | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| 1. Hawakitumii mara nyingi na katika maeneo mengi kama vile elimu kwa hivyo si lugha muhimu. | 175 | 53.0% | 63.6% |
| 2.Wataonekana kama ni washamba yaani wasiostaarabika wakizungumza Kikuyu. | 50 | 15.2% | 18.2% |
| 3.Wanaiona lugha duni kwa hivyo hawajifunzi | 49 | 14.8% | 17.8% |
| 4.Hawapendi kujifunza Kikuyu kwani ni Kigumu | 32 | 9.7% | 11.6% |
| 5.Vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wana matamshi mazuri na ufasaha wa kuzungumza kuliko wanaofahamu Kikuyu. | 21 | 6.4% | 7.6% |
| 6.Wanakienzi na kukipenda Kikuyu kwa vile ni lugha ya wazazi wao. | 2 | 0.6% | 0.7% |
| 7.Mara kwa mara wao hutembea mashambani na kutamani sana kuzungumza kwa Kikuyu. | 1 | 0.3% | 0.5% |
| **Jumla** | **330** | **100.0%** | **120.0%** |

Kutokana na jedwali 24, vijana wengi mijini walisema kuwa hawaipendi lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na jinsi wanavyozipenda lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Vijana hawa walitoa sababu tofauti tofauti za kutoipenda lugha ya Kikuyu. Asilimia 53 ya vijana mijini walisema kuwa hawaipendi lugha ya Kikuyu jinsi wanavyozipenda lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hii ni kwa sababu hawakitumii Kikuyu mara nyingi na katika maeneo mengi ya kijamii ya matumizi ya lugha kama vile elimu na kwa hivyo si lugha muhimu. Asilimia 15 ya vijana mijini nao

walisema kuwa hawakipendi Kikuyu kwa vile wakizungumza Kikuyu mijini wataonekana kama ni washamba ama wasiostaarabika.

Asilimia 15 ya vijana mijini nao walisema kuwa vijana hawapendi kukitumia Kikuyu pale mijini kwa vile wanaiona kama lugha duni na kwa hivyo haina haja kujifunza**.** Aidha, asilimia 10 ya vijana walisema kuwa hawapendi kujifunza Kikuyu kwani ni kigumu kufahamu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hatimaye, asilimia 6 ya vijana mijini nao walisema kuwa vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wana matamshi mazuri na ufasaha wa kuzungumza kuliko vijana wanaofahamu Kikuyu.

Kwa hakika, ni idadi ndogo tu ya vijana mijini ambao walisema kuwa wanakipenda Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Vijana hawa nao walitoa sababu zao mbalimbali za kukipenda Kikuyu.  Asilimia 1 ya vijana mijini Nairobi, Kiambu na Thika walisema kuwa wanakipenda Kikuyu kwa vile ni lugha ya wazazi wao. Nayo asilimia 1 ya vijana mijini walisema kuwa wanakipenda Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa vile mara kwa mara wao hutembea mashambani na kutamani sana kuzungumza kwa Kikuyu jinsi vijana wenzao kule mashambani wanavyofanya**.**


## 5.6 Maeneo ya Matumizi ya Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana Mijini.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubaini maeneo ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu hutumia lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika miji teule ya Nairobi, Kiambu na Thika. Katika kujaribu kubaini maeneo ya kijamii ambamo vijana katika miji hii hutumia lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, utafiti huu uliwahusisha wanafunzi wa Kidato cha 3 na cha 4 katika shule 12 kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika.

### 5.6.1 Kidato cha Wahojiwa.

Utafiti huu uliwahusisha wanafunzi wa kidato cha 3 na 4 kwa karibu idadi sawa kama mchoro 15 unavyoonyesha hapa chini.

**Mchoro 15: Kidato Cha Wahojiwa.**




Mchoro 15 unaonyesha kuwa kati ya vijana wote waliohojiwa katika shule 12 zilizoteuliwa katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika, asilimia 49 ilikuwa ni wanafunzi wa kidato cha 3 huku asilimia 51 ikiwa ni ya wanafunzi wa kidato cha 4. (taz. pia 5.3.1)

### 5.6.2 Umri wa Wahojiwa

Umri wa wahojiwa pia ulitiliwa maanani katika utafiti huu kama jedwali 24 hapa chini linavyoonyesha.

**Jedwali 25: Umri**


| | Miaka |
|---|---|
| Wastani | 17.33 |
| Kati | 17.00 |
| Modi | 17.00 |
| Upeo chini | 14.00 |
| Upeo juu | 20.00 |

Matokeo katika mchoro huu yanaonyesha kuwa umri wa wastani wa vijana waliohojiwa ulikuwa miaka 17 huku umri wa chini kabisa ukiwa miaka 14 na wa juu zaidi miaka 20. (taz pia 5.3.2)

### 5.6.3 Jinsia ya Wahojiwa

Jinsia ya wahojiwa pia ilitiliwa maanani katika utafiti huu ili kuhakikisha kuwa jinsia zote mbili zilihusishwa kwa kiwango sawa.

**Mchoro 16: Jinsia ya Wahojiwa**



Matokeo katika mchoro 16 hapo juu yanaonyesha kuwa jinsia zote mbili ziliwakilishwa kwa njia sawa. Kulikuwa na asilimia 50 ya wasichana na asilimia 50 ya wavulana waliohusishwa katika utafiti huu. (taz pia 5.3.3)

## 5.7 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha.

Katika juhudi za kubaini lugha wanazozitumia vijana wa jamii ya Kikuyu katika maeneo mbalimbali ya kijamii mijini Nairobi, Kiambu na Thika, vijana waliulizwa kutoa majibu sahihi kuhusu lugha walizozitumia katika maeneo mbalimbali mijini walimoishi kama ifuatavyo:-

### 5.7.1. Lugha Unayoitumia Unapozumgumza na Marafiki Zako Darasani pale Shuleni.

Utafiti huu kwanza ulilenga kubaini lugha iliyotumiwa na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wanapozungumza na marafiki wao darasani pale shuleni kama jedwali 26 linavyoonyesha.

**Jedwali 26: Lugha Unayoitumia Unapozumgumza na Marafiki Darasani pale Shuleni.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 213 | 34.1% | 71.0% |
| Sheng | 207 | 33.1% | 69.0% |
| Kiingereza | 205 | 32.8% | 68.3% |
| Kikuyu | 0 | 0% | 0% |
| Jumla | 625 | 100.0% | 208.3% |

Vijana walipoulizwa kuhusu lugha wanayoitumia wanapozungumza na marafiki zao wakiwa darasani pale shuleni, ilibainika kuwa Kiswahili na Sheng ndizo lugha zilizotumiwa zaidi kwa asilimia 34 na 33 mtawaliwa. Asilimia 33 ya vijana nao walitumia Kiingereza huku Kikuyu kikiwa hakitumiwi hata kidogo na vijana wanpozungumza na wenzao darasani pale mijini.

### 5.7.2 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki Zako Nje ya Darasa Shuleni.

Utafiti huu pia ulilenga kubaini lugha zinazotumiwa na vijana nje ya eneo la darasani pale shuleni kwa kuwauliza vijana hawa kuchagua lugha walizopendelea kutumia nje ya darasa kama jedwali 27 linavyoonyesha.

**Jedwali 27: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki Zako Nje ya Darasa Shuleni.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Sheng | 259 | 49.7% | 86.3% |
| Kiswahili | 170 | 32.6% | 56.7% |
| Kiingereza | 82 | 15.7% | 27.3% |
| Kikuyu | 10 | 1.9% | 3.3% |
| Jumla | 521 | 100.0% | 17.7% |

Ni wazi kuwa kutokana na matokeo haya, asilimia kubwa ya vijana ambayo ni asilimia 50 hutumia Sheng nje ya darasa huku asilimia 33 wakitumia Kiswahili. Lugha ambazo huwa na matumizi ya kiwango cha chini nje ya darasa miongoni mwa vijana ni Kiingereza na Kikuyu ambazo zilitumiwa na asilimia 16 na 2 mtawaliwa.

### 5.7.3 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Walimu Darasani

Vile vile utafiti huu ulijaribu kubainisha lugha ambazo vijana na walimu wao hutumia wanapowasiliana pale darasani kama jedwali 28 linavyoonyesha.

**Jewali 28: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Walimu Darasani.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiingereza | 293 | 53.1% | 97.7% |
| Kiswahili | 250 | 45.3% | 83.3% |
| Sheng | 9 | 1.6% | 3.0% |
| Kikuyu | 0 | 0% | 0% |
| Jumla | 552 | 100.0% | 184.0% |

Ilibainika kuwa mawasiliano mengi kati ya vijana na walimu huwa katika Kiingereza kwa asilimia 53 na Kiswahili kwa asilimia 45. Ni asilimia 2 tu ya vijana ambao walisema kuwa wao huwasiliana na walimu wao kwa kutumia Sheng pale darasani huku lugha ya Kikuyu ikiwa haitumiki kamwe.

### 5.7.4 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Wafanyakazi Shuleni

Lugha zinazotumiwa na vijana kuwasiliana na wafanyakazi pale shuleni nazo zilibainishwa katika jedwali 29.

**Jedwali 29: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Wafanyakazi Shuleni.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 254 | 57.3% | 85.2% |
| Sheng | 80 | 18.1% | 26.8% |
| Kikuyu | 71 | 16.0% | 23.8% |
| Kiingereza | 38 | 8.6% | 12.8% |
| Jumla | 443 | 100.0% | 148.7% |

Matokeo hapa yanaonyesha kuwa idadi kubwa ya vijana, yaani asilimia 57 hutumia Kiswahili kuwasiliana na wafanyakazi wa shule. Hata hivyo, asilimia 18 hutumia Sheng, 16 Kikuyu na 9 hutumia Kiingereza katika kuwasiliana na wafanyakazi pale shuleni.

### 5.7.5 Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki zako Nyumbani

Eneo lingine muhimu la matumizi ya lugha na ambalo lilichuinguzwa na utafiti huu ni lile la nyumbani. Utafiti huu ulilenga kubaini jinsi vijana wanavyotumia lugha hizi nne yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng wanapotangamana wao kwa wao pale mitaani mwao. Jedwali 30 linaonyesha matokeo haya ifuatavyo:-

**Jedwali 30: Lugha Unayoitumia Unapozungumza na Marafiki zako Nyumbani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Sheng | 265 | 47.3% | 88.9% |
| Kiswahili | 146 | 26.1% | 49.0% |
| Kiingereza | 95 | 17.0% | 31.9% |
| Kikuyu | 54 | 9.6% | 18.1% |
| Jumla | 560 | 100.0% | 187.9% |

Kutokana na jedwali 30, ilibainika kuwa asilimia 47 ya vijana hutumia lugha ya Sheng. Kiswahili hutumiwa na asilimia 26 ya vijana huku Kiingereza kikitumiwa na asilimia 17 ya vijana. Lugha ya Kikuyu ndiyo iliyotumiwa na idadi ndogo zaidi ya vijana kwa asilimia 10.

### 5.7.6 Lugha Unayoitumia Unapowazungumzia Wazazi Wako Nyumbani

Utafiti huu pia ulilenga kutambulisha lugha zinazotumiwa na vijana wanapozungumzia wazazi wao pale nyumbani kama jedwali 31 linavyoonyesha.

**Jedwali 31: Lugha Unayoitumia Unapowazungumzia Wazazi Wako Nyumbani**

| | Majibu | | |
|---|---|---|---|
| **Lugha** | **Mirudio** | **Asilimia** | **Asilimia ya Visa** |
| **Kiswahili** | **244** | **45.5%** | **82.4%** |
| **Kikuyu** | **127** | **23.7%** | **42.9%** |
| **Kiingereza** | **102** | **19.0%** | **34.5%** |
| **Sheng** | **63** | **11.8%** | **21.3%** |
| **Jumla** | **536** | **100.0%** | **181.1%** |

Matokeo katika jedwali 31 yanaonyesha kuwa asilimia 46 ya vijana wanatumia Kiswahili wanapowazungumzia wazazi wao pale nyumbani. Nayo asilimia 24 wanatumia lugha ya Kikuyu wanapowazungumzia wazazi wao. Asilimia 19 ya vijana wanawazungumzia wazazi wao lugha ya Kiingereza huku asilimia 12 ikitumia Sheng.

### 5.7.7 Lugha Wanayoitumia Wazazi Wanapokuzungumzia Nyumbani

Mbali na kutaka kujua lugha ambazo vijana wanazitumia wanapowazungumzia wazazi wao, utafiti huu pia ulitaka kufahamu lugha walizozitumia wazazi wanapowazungumzia vijana pale nyumbani kama jedwali 32 linavyoonyesha.

**Jedwali 32: Lugha Wanayoitumia Wazazi Wanapokuzungumzia Nyumbani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kikuyu | 210 | 39.3% | 70.7% |
| Kiswahili | 194 | 36.3% | 65.3% |
| Kiingereza | 101 | 18.9% | 34.0% |
| Sheng | 29 | 5.4% | 9.8% |
| Jumla | 534 | 100.0% | 179.8% |

Ilibainika kuwa asilimia 39 ya wazazi walipendelea kutumia lugha ya Kikuyu kuwazungumzia vijana huku asilimia nyingine 36 wakipendelea lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, asilimia 19 ya wazazi mijini hutumia lugha ya Kiingereza kuwazungumzia vijana na asilimia 5 ya wazazi wakitumia Sheng.

### 5.7.8 Lugha ambayo Wazazi Wako Wanatumia Wanapowasiliana Nyumbani

Zaidi, utafiti huu ulitaka kufahamu kutoka kwa vijana lugha ambayo wazazi wao walipendelea kutumia wanapowasiliana wao kwa wao pale nyumbani. Matokeo haya yanaangaziwa na jedwali 33 lifuatalo.

**Jedwali 33: Lugha ambayo Wazazi Wako Wanatumia Wanapowasiliana Nyumbani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kikuyu | 158 | 53.8% | 86.0% |
| Kiswahili | 141 | 29.4% | 47.0% |
| Kiingereza | 65 | 13.5% | 21.7% |
| Sheng | 16 | 3.3% | 5.3% |
| Jumla | 480 | 100.0% | 160.0% |

Jedwali 33 linaonyesha kuwa asilimia 54 ya wazazi huzungumza lugha ya Kikuyu wanapowasiliana pale nyumbani. Vile vile, ilibainika kuwa asilimia 29 ya wazazi hutumia Kiswahili kuwasiliana baina yao, asilimia 14 hutumia Kiingereza huku asilimia 3 wakitumia Sheng.

### 5.7.9 Lugha Unayoitumia Unapozungumzia Watu Wazima Mtaani

Utafiti huu pia ulitaka kutambulisha lugha ambayo vijana pale mjini huwa wanatumia kuwazungumzia watu wazima pale mitaani. Jedwali 34 linaonyesha matokeo haya ifuatavyo:-

**Jedwali 34: Lugha Unayoitumia Unapozungumzia Watu Wazima Mtaani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 250 | 53.4% | 83.3% |
| Kiingereza | 94 | 20.1% | 31.3% |
| Kikuyu | 68 | 14.5% | 22.7% |
| Sheng | 56 | 12.0% | 18.7% |
| Jumla | 468 | 100.0% | 156.0% |

Ilibainika kuwa asilimia 53 ya vijana hutumia Kiswahili kuwazungumzia watu wazima mitaani. Asilimia 20 ya vijana walitumia Kiingereza, asilimia 15 Kikuyu na asilimia nyingine 12 wakitumia Sheng.

### 5.7.10 Lugha Wanayoitumia Watu Wazima Wanapokuzungumzia Mtaani.

Katika kujaribu kutambulisha lugha ambayo watu wazima hutumia katika kuwazungumzia vijana, tuliwahoji vijana na kupata matokeo yafuatayo katika jedwali 35.

**Jedwali 35: Lugha Wanayoitumia Watu Wazima Wanapokuzungumzia Mtaani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 235 | 44.8% | 79.1% |
| Kikuyu | 126 | 24.0% | 42.4% |
| Kiingereza | 107 | 20.4% | 36.0% |
| Sheng | 56 | 10.7% | 18.9% |
| Jumla | 524 | 100.0% | 176.4% |

Asilimia 45 ya watu wazima hutumia Kiswahili wanapowazungumzia vijana pale mitaani huku asilimia 24 ikitumia lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, asilimia 20 ya watu wazima hutumia Kiingereza wanapowazungumzia vijana pale mtaani nayo asilimia 11 wakitumia Sheng.

### 5.7.11 Lugha Unayoitumia Unapomzungumzia Babu au Nyanya Yako.

Utafiti huu hali kadhalika ulichunguza kuhusu lugha ambazo vijana kutoka miji hii teule hupenda kuzitumia wanapomzungumzia nyanya na babu yao hasa wanapowatembelea sehemu za mashambani. Jedwali 36 linaonyesha matokeo haya.

**Jedwali 36: Lugha Unayoitumia Unapomzungumzia Babu au Nyanya Yako.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kikuyu | 226 | 54.6% | 75.3% |
| Kiswahili | 176 | 42.5% | 58.7% |
| Kiingereza | 6 | 1.4% | 2.0% |
| Sheng | 6 | 1.4% | 2.0% |
| Jumla | 414 | 100.0% | 138.0% |

Matokeo ya jedwali 36 yanaonyesha kuwa asilimia 55 ya vijana kutoka mijini huwazungumzia nyanya na babu zao kwa kutumia lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, asilimia 43 ya vijana huwazungumzia nyanya na babu zao kwa lugha ya Kiswahili. Kisha kuna asilimia 1 ya vijana waliosema kuwa wao hutumia lugha ya Kiingereza wanapowazungumzia nyanya na babu yao huku asilimia 1 wakitumia lugha ya Sheng.

### 5.7.12 Lugha Anayoitumia Nyanya au Babu Anapokuzungumzia

Kwa upande mwingine, utafiti wetu ulitaka kubainisha lugha ambayo nyanya au babu hutumia wanapowazungumzia vijana kama jedwali 37 linavyoonyesha.

**Jedwali 37: Lugha Anayoitumia Nyanya au Babu Anapokuzungumzia.**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kikuyu | 284 | 66.5% | 95.9% |
| Kiswahili | 124 | 29.0% | 41.9% |
| Kiingereza | 14 | 3.3% | 4.7% |
| Sheng | 5 | 1.2% | 1.7% |
| Jumla | 427 | 100.0% | 144.3% |

Matokeo hapa yabainisha kuwa asilimia 67 ya kizazi cha akina nyanya na akina babu hutumia lugha ya Kikuyu wanapowazungumzia vijana kutoka mijini. Nayo asilimia 29 ya vijana walisema kuwa nyanya na babu zao hutumia lugha ya Kiswahili wanapowazungumzia, asilimia 3 hutumia Kiingereza huku asilimia 1 wakitumia Sheng.

### 5.7.13 Watoto Kwanza Hujifunza Lugha Gani Mtaani

Utafiti huu pia ulichunguza kuhusu lugha ambayo vijana hupokea kama lugha yao ya kwanza pale mijini kati ya lugha hizi nne yaani Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo katika jedwali 38.

**Jedwali 38: Watoto Kwanza Hujifunza Lugha Gani Mtaani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 218 | 43.5% | 72.7% |
| Sheng | 169 | 33.7% | 56.3% |
| Kiingereza | 77 | 15.4% | 25.7% |
| Kikuyu | 37 | 7.4% | 12.3% |
| Jumla | 501 | 100.0% | 167.0% |

Matokeo yanaonyesha kuwa asilimia 44 ya vijana mijini hujifunza kwanza lugha ya Kiswahili huku asilimia 34 ikijifunza kwanza lugha ya Sheng. Aidha, ni asilimia 15 ya vijana mijini ambao kwanza hujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha yao ya kwanza nayo asilimia 7 pekee ya vijana wakijifunza kwanza lugha ya Kikuyu.

### 5.7.14 Lugha Inayotumiwa Kuhubiri Kanisani au Msikitini Nyumbani

Hatimaye, utafiti huu ulilenga kubainisha lugha ambayo hutumika Kanisani na msikitini mijini ambako kuna mtagusano wa lugha mbalimbali. Matokeo yalikuwa ifuatavyo kama yanavyoonyeshwa na jedwali 39.

**Jedwali 39: Lugha Inayotumiwa Kuhubuiri Kanisani au Msikitini Nyumbani**

| Lugha | Majibu | | Asilimia ya Visa |
|---|---|---|---|
| | Mirudio | Asilimia | |
| Kiswahili | 245 | 41.4% | 81.9% |
| Kiingereza | 238 | 40.2% | 79.6% |
| Sheng | 68 | 11.5% | 22.7% |
| Kikuyu | 41 | 6.9% | 13.7% |
| Jumla | 592 | 100.0% | 198.0% |

Matokeo ya jedwali 39 yanaonyesha kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ndizo hutumiwa kwa wingi zaidi Kanisani na Miskitini kwa asilimia 41 na 40 mtawaliwa. Lugha za Sheng na Kikuyu nazo hutumika kwa asilimia 12 na 7 mtawaliwa.

## 5.8 Umilisi wa Lugha Miongoni mwa Vijana Mijini.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kubaini viwango vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji

teule ya Nairobi, Kiambu na Thika kupitia stadi za kuandika, kusoma na kuongea. Ili kupima viwango vya umilisi wa lugha hizi miongoni mwa vijana katika miji hii, vifaa mbalimbali vilitumiwa ili kusaidia mtafiti kupata matokeo aliyoyataka katika stadi hizi tatu za lugha. Vifaa vilivyotumiwa ni mitihani mifupi ya kupima umilisi katika stadi ya kusoma, kuandika na kuongea kila mtihani ukiwa na jumla ya alama 20. Mitihani hii ilihusisha mambo kama vile uandishi wa insha fupi kwa kutumia lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ili kupima umilisi wa lugha hizi kupitia stadi ya kuandika. Vifungu vifupi vya ufahamu vilitumiwa kupima stadi ya kusoma katika lugha hizi nne ilhali vijana hawa waliulizwa waeleze kwa kifupi mada walizopewa ili kupima viwango vyao vya umilisi katika stadi ya kuongea.

### 5.8.1 Kuandika kwa Kikuyu.

Katika stadi ya kuandika kwa lugha ya Kikuyu, wahojiwa walitakiwa kuandika insha fupi kwa kutumia lugha ya Kikuyu kuhusu mada iliyotolewa na mtafiti. Insha hizi zilitumika kupima uwezo wa wahojiwa wa kujieleza kimaandishi kupitia lugha ya Kikuyu. Baadhi ya mambo yaliyotahiniwa ni kama vile uwezo wa kuandika maneno ya Kikuyu ipasavyo, kiwango cha matumizi ya msamiati wa lugha ya Kikuyu na kiasi ya athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika maandishi ya Kikuyu. Baada ya insha kusahihishwa na kutunzwa alama kutoka kwa jumla ya alama ishirini, matokeo yalikuwa yafuatayo kama yanavyoonyeshwa katika jedwali 40:-

**Jedwali 40: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Kikuyu.**

| | Kuandika |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **5.43** |
| **Kati** | **5.00** |
| **Modi** | **5.00** |
| **Upeo chini** | **4.00** |
| **Upeo juu** | **10.00** |

Matokeo katika jedwali 40 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuandika Kikuyu ilikuwa asilimia 5. Alama ya chini zaidi katika zoezi la uandishi wa Kikuyu ilikuwa 4 na ya juu zaidi ilikuwa 10 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.2 Kusoma kwa Kikuyu.

Katika stadi ya kusoma kwa lugha ya Kikuyu, wahojiwa walitakiwa kusoma makala fupi iliyoandikwa kwa Kikuyu. Masuala yaliyochunguzwa katika usomaji wa Kikuyu ni kama vile uwezo wa kusoma kwa mfululizo mzuri bila kutatizika kuyasoma maneno ya Kikuyu, matamshi bora ya maneno ya Kikuyu na athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika matamshi ya maneno ya Kikuyu. Matokeo ya stadi ya usomaji kwa Kikuyu yalikuwa yafuatayo katika jedwali 41:-

**Jedwali 41: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kikuyu.**

| | Kusoma |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **5.40** |
| **Kati** | **5.00** |
| **Modi** | **5.00** |
| **Upeo chini** | **5.00** |
| **Upeo juu** | **8.00** |

Matokeo katika jedwali 41 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kusoma Kikuyu ilikuwa asilimia 5. Alama ya chini zaidi katika zoezi la usomaji wa Kikuyu ilikuwa 5 na ya juu zaidi ilikuwa 8 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.3 Kuongea kwa Kikuyu

Aidha, katika stadi ya kuongea kwa lugha ya Kikuyu, wahojiwa walitakiwa kuzungumza kwa kutumia Kikuyu. Kwa mfano wahojiwa walipewa dakika tano kila mmoja kujieleza wao ni nani na usuli wao. Baadhi ya mambo yaliyochunguzwa hapa ni uwezo wa mhojiwa wa kuzungumza Kikuyu kwa ufasaha bila kutatizika kupata msamiati wa Kikuyu wa kuelezea usuli wake. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 42:-

**Jedwali 42: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kikuyu.**

| | Kuongea |
|---|---|
| Mirudio | 300 |
| Wastani | 5.52 |
| Kati | 5.00 |
| Modi | 5.00 |
| Upeo chini | 4.00 |
| Upeo juu | 8.00 |

Matokeo katika jedwali 42 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuongea Kikuyu ilikuwa asilimia 5. Alama ya chini zaidi katika zoezi la kuongea kwa Kikuyu ilikuwa 4 na ya juu zaidi ilikuwa 8 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

Kwa jumla, matokeo haya yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kusoma, kuandika na kuongea. Hali hii hatimaye inapelekea lugha ya Kikuyu kuwa na

viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

### 5.8.4 Kuandika kwa Kiswahili.

Katika stadi ya kuandika kwa Kiswahili, wahojiwa walitakiwa kuandika insha fupi za Kiswahili kuhusu mada iliyotolewa. Insha hizi zilitumika kupima uwezo wa wahojiwa wa kujieleza kimaandishi kupitia lugha ya Kiswahili. Baadhi ya masuala yaliyotahiniwa ni kama vile uwezo wa kuandika maneno ya Kiswahili vyema, kiwango cha matumizi ya msamiati wa lugha ya Kiswahili katika maandishi na kwa kiasi athari za Kikuyu, Kiingereza na Sheng katika maandishi ya Kiswahili. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 43:-

**Jedwali 43: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Kiswahili.**

| | **Kuandika** |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **15.04** |
| **Kati** | **15.00** |
| **Modi** | **15.00** |
| **Upeo chini** | **12.00** |
| **Upeo juu** | **18.00** |

Matokeo katika jedwali 43 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuandika Kiswahili ilikuwa asilimia 15. Alama ya chini zaidi katika zoezi la uandishi wa Kiswahili ilikuwa 12 na ya juu zaidi ilikuwa 18 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.5 Kusoma kwa Kiswahili.

Katika stadi ya kusoma kwa lugha ya Kiswahili, wahojiwa walipewa makala fupi zilizoandikwa kwa Kikuyu ili kuzisoma. Mambo yaliyozingatiwa katika usomaji wa

Kiswahili ni pamoja na uwezo wa kusoma kwa mfulilizo mzuri bila kutatizika kuyasoma maneno ya Kiswahili, matamshi sahihi ya maneno ya Kiswahili na athari za lugha za Kikuyu, Kiingereza na Sheng katika matamshi ya maneno ya Kiswahili. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 44:-

**Jedwali 44: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kiswahili.**

| | **Kusoma** |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **14.16** |
| **Kati** | **14.00** |
| **Modi** | **14.00** |
| **Upeo chini** | **12.00** |
| **Upeo juu** | **18.00** |

Matokeo katika jedwali 44 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kusoma Kiswahili ilikuwa asilimia 14. Alama ya chini zaidi katika zoezi la usomaji wa Kiswahili ilikuwa 12 na ya juu zaidi ilikuwa 18 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.6 Kuongea kwa Kiswahili

Katika stadi ya kuongea kwa Kiswahili, wahojiwa walitakiwa kujieleza kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Wahojiwa walipewa dakika tano kila mmoja kueleza kuhusu somo walipendalo zaidi shuleni na sababu za kulipenda somo hilo. Mambo yaliyochunguzwa hapa ni kama vile uwezo wa mhojiwa wa kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha bila matatizo ya kupata msamiati mbalimbali wa kujieleza na ukakamavu katika kuzungumza kwa Kiswahili. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 45:-

**Jedwali 45: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kiswahili.**

| | **Kuongea** |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **14.19** |
| **Kati** | **14.00** |
| **Modi** | **14.00** |
| **Upeo chini** | **11.00** |
| **Upeo juu** | **17.00** |

Matokeo katika jedwali 45 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuongea Kiswahili ilikuwa asilimia 14. Alama ya chini zaidi katika zoezi la kuongea kwa Kiswahili ilikuwa 11 na ya juu zaidi ilikuwa 17 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

Matokeo haya ya umilisi wa lugha ya Kiswahili kupitia stadi ya kuandika, kusoma na kuongea miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yanaonyesha vijana hawa wana viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na viwango chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu.

### 5.8.7 Kuandika kwa Kiingereza.

Katika stadi ya kuandika kwa Kiingereza, wahojiwa walitakiwa kuandika insha fupi za Kiingereza kuhusu mada waliyopewa. Insha hizi zilitumika kama kipimo cha uwezo wa wahojiwa wa kujieleza kimaandishi kupitia lugha ya Kiingereza. Baadhi ya masuala yaliyotahiniwa ni kama vile uwezo wa kuandika maneno ya Kiingereza vyema, kiwango cha matumizi ya msamiati wa lugha ya Kiingereza katika maandishi na kiasi cha athari za

Kikuyu, Kiswahili na Sheng katika maandishi ya Kiingereza. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 46:-

**Jedwali 46: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Kiingereza.**

| | **Kuandika** |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **14.28** |
| **Kati** | **14.00** |
| **Modi** | **14.00** |
| **Upeo chini** | **13.00** |
| **Upeol juu** | **16.00** |

Matokeo katika jedwali 46 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuandika Kiingereza ilikuwa asilimia 14. Alama ya chini zaidi katika zoezi la uandishi wa Kiingereza ilikuwa 13 na ya juu zaidi ilikuwa 16 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.8 Kusoma kwa Kiingereza.

Katika stadi ya kusoma kwa Kiingereza, wahojiwa walitakiwa kusoma makala fupi iliyoandikwa kwa Kiingereza. Mambo yaliyozingatiwa katika usomaji wa Kiingereza ni pamoja na uwezo wa kusoma kwa mfulilizo mzuri bila kutatizika kuyasoma maneno ya Kiingereza, matamshi sahihi ya maneno ya Kiingereza na athari za lugha za Kikuyu, Kiswahili na Sheng katika matamshi ya maneno ya Kiingereza. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 47:-

**Jedwali 47: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Kiingereza.**

| | Kusoma |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **14.71** |
| **Kati** | **15.00** |
| **Modi** | **14.00** |
| **Upeo chini** | **12.00** |
| **Upeo juu** | **18.00** |

Matokeo katika jedwali 47 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kusoma Kiingereza ilikuwa asilimia 15. Alama ya chini zaidi katika zoezi la usomaji wa Kiingereza ilikuwa 12 na ya juu zaidi ilikuwa 18 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.9 Kuongea kwa Kiingereza

Katika stadi ya kuongea kwa Kiingereza, wahojiwa walitakiwa kuzungumza kwa kutumia lugha ya Kiingereza. Wahojiwa walipewa dakika tano kila mmoja kueleza kuhusu mchezo waupendao zaidi shuleni na sababu za kuupenda. Mambo yaliyochunguzwa hapa ni kama vile uwezo wa mhojiwa wa kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha na ukakamavu katika kuzungumza kwa Kiingereza. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 48:-

**Jedwali: 48: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Kiingereza**

| | Kuongea |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **14.85** |
| **Kati** | **15.00** |
| **Modi** | **15.00** |
| **Upeo chini** | **12.00** |
| **Upeo juu** | **17.00** |

Matokeo katika jedwali 48 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuongea Kiingereza ilikuwa asilimia 15. Alama ya chini zaidi katika zoezi la kuongea kwa Kiingereza ilikuwa 12 na ya juu zaidi ilikuwa 17 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

Kwa jumla, matokeo haya ya umilisi wa lugha ya Kiingereza katika stadi ya kuandika, kusoma na kuongea miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yanaonyesha kuwa vijana hawa wana viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Kiingereza kama vile tu katika lugha ya Kiswahili. Viwango hivi vya umilisi wa lugha ya Kiingereza miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni vya juu  ikilinganishwa na viwango vyao vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu.

### 5.8.10 Kuandika kwa Sheng.

Katika stadi ya kuandika kwa lugha ya Sheng, wahojiwa waliulizwa kuandika insha fupi kwa kutumia lugha ya Sheng kuhusu mada iliyotolewa. Insha hizi zilitumika kama kipimo cha uwezo wa wahojiwa wa kujieleza kimaandishi kupitia lugha ya Sheng. Baadhi ya masuala yaliyopimwa ni kama vile uwezo wa kuandika maneno ya Sheng vyema, kiwango cha matumizi ya msamiati wa lugha ya Sheng katika maandishi na kiasi cha athari za Kikuyu, Kiswahili na Kiingereza katika maandishi ya Sheng. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 49:-

**Jedwali 49: Matokeo ya Stadi ya Kuandika kwa Sheng.**

| | Kuandika |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **11.51** |
| **Kati** | **12.00** |
| **Modi** | **12.00** |
| **Upeo chini** | **9.00** |
| **Upeo juu** | **14.00** |

Matokeo katika jedwali 49 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuandika Sheng ilikuwa asilimia 12. Alama ya chini zaidi katika zoezi la uandishi wa Sheng ilikuwa 9 na ya juu zaidi ilikuwa 14 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.11 Kusoma kwa Sheng.

Katika stadi ya kusoma kwa lugha ya Sheng, wahojiwa walitakiwa kusoma makala fupi zilizoandikwa kwa Sheng. Mambo yaliyozingatiwa katika usomaji wa Sheng ni pamoja na uwezo wa kusoma kwa mfulilizo mzuri bila kutatizwa na maneno ya Sheng, matamshi sahihi ya maneno ya Sheng na athari za lugha za Kikuyu, Kiswahili na Kiingereza katika matamshi ya maneno ya Sheng. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 50:-

**Jedwali 50: Matokeo ya Stadi ya Kusoma kwa Sheng.**

| | Kusoma |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **12.16** |
| **Kati** | **12.00** |
| **Modi** | **12.00** |
| **Upeo chini** | **9.00** |
| **Upeo juu** | **15.00** |

Matokeo katika jedwali 50 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kusoma Sheng ilikuwa asilimia 12. Alama ya chini zaidi katika zoezi la usomaji wa Sheng ilikuwa 9 na ya juu zaidi ilikuwa 15 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

### 5.8.12 Kuongea kwa Sheng

Katika stadi ya kuongea kwa lugha ya Sheng, wahojiwa walitakiwa kuzungumza kwa kutumia lugha ya Sheng. Wahojiwa walipewa dakika tano kila mmoja kueleza kuhusu mwanamuziki wampendaye sana na sababu za kumpenda. Mambo yaliyochunguzwa hapa ni kama vile uwezo wa mhojiwa wa kuzungumza Sheng kwa ufasaha na ukakamavu katika kuzungumza kwa kutumia lugha ya Sheng. Matokeo yalikuwa yafuatayo katika jedwali 51:-

**Jedwali 51: Matokeo ya Stadi ya Kuongea kwa Sheng.**

| | **Kuongea** |
|---|---|
| **Mirudio** | **300** |
| **Wastani** | **15.63** |
| **Kati** | **16.00** |
| **Modi** | **15.00** |
| **Upeo chini** | **14.00** |
| **Upeo juu** | **18.00** |

Matokeo katika jedwali 51 yanaonyesha kuwa alama ya wastani katika stadi ya kuongea Sheng ilikuwa asilimia 16. Alama ya chini zaidi katika zoezi la uandishi wa Sheng ilikuwa 14 na ya juu zaidi ilikuwa 18 katika zoezi lililokuwa na jumla ya alama 20.

Matokeo ya umilisi wa lugha ya sheng kupitia stadi ya kuandika, kusoma na kuongea miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yanaonyesha

vijana hawa wana viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Sheng ikilinganishwa na viwango chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu. Hata hivyo matokeo haya zaidi yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana umilisi wa chini wa lugha ya Sheng katika stadi za kusoma na kuandika ikilinganishwa na stadi ya kuongea. (taz. majedwali 49, 50 na 51). Hii labda inatokana na ukweli kuwa wakati mwingi vijana hawa hutumia lugha ya sheng katika stadi ya kuongea wala sio katika stadi za kusoma na kuandika kwa vile lugha hii haifundishwi shuleni kama vile lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

### 5.8.13 Ulinganisho wa Viwango vya Umilisi katika Miji ya Nairobi, Kiambu na Thika

Mbali na kuonyesha viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa jumla, utafiti huu vile vile ulilinganisha viwango vya umilisi wa lugha hizi nne kupitia kigezo cha miji hii mitatu yaani Nairobi, Kiambu na Thika. Ulinganisho huu ulikuwa muhimu ili kuweza kubaini kama iwapo maingiliano ya jamiilugha ya Kikuyu katika sehemu za mjini na mashambani yalikuwa na athari zozote kwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini na hatimaye kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu kwa jumla.

Jiji la Nairobi limeachana kimasafa na mji wa Kiambu kwa takriban kilomita 20 na kwa takriban kilomita 40 na mji wa Thika. Mbali na haya, Jiji la Nairobi kama asemavyo Lewis (2009) lina hali ya wingilugha ambako kuna zaidi ya lugha 50 zinazozungumzwa. Basi jiji la Nairobi lina mwingiliano mkubwa wa lugha kuliko miji ya Kiambu na Thika

huku nayo miji ya Kiambu na Thika ikiwa na maingiliano makubwa kimawasiliano na jamiilugha ya Kikuyu kutoka sehemu za mashambani. Landweer (2000) anasema kuwa jinsi jamiilugha ilivyo mbali kimasafa na kimaingiliano na jamiilugha za mjini ndivyo jamiilugha kama hii ilivyo na viwango vya juu vya uthabiti wa kiisimujamii. Aidha, jinsi jamiilugha ilivyo karibu kimasafa na kimaingiliano na jamiilugha za mjini ndivyo jamiilugha kama hii ilivyo na viwango vya chini vya uthabiti wa kiisimujamii (taz 3.2.1).

Utafiti wetu ulilenga kubaini kama iwapo umbali wa kimasafa na kimaingiliano miongoni mwa wanajamiilugha ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa upande mmoja na sehemu za mashambani kwa upande mwingine ulikuwa na athari kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu. Matokeo ya ulinganisho wa viwango vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika miji hii mitatu unaonyeshwa katika majedwali 52, 53 na 54 ifuatavyo:-

**Jedwali 52: Viwango vya Umilisi wa Lugha Jijini Nairobi.**

| | **Kuandika** | **Kusoma** | **Kuongea** |
|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **17.61** | **17.8** | **17.62** |
| **Kikuyu** | **13.80** | **14.1** | **14.0** |
| **Kiingereza** | **18.0** | **18.5** | **18.4** |
| **Sheng** | **15.3** | **15.5** | **18.2** |

Ulinganisho wa viwango vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika jiji la Nairobi ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu wana viwango vya

chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kuandika, Kusoma na kuongea ikilinganishwa na umilisi wao wa lugha za Kiingereza, Kiswahili na Sheng. Lugha ya Kiingereza ndiyo iliyo na viwango vya juu vya umilisi ikifuatwa na Kiswahili na Kiingereza. Utafiti wetu ulibani kuwa kuna maingiliano ya kiwango cha chini kati vijana wa jamiilugha ya Kikuyu jijini Nairobi na sehemu za mashambani (taz 6.4.5-Mhojiwa II). Ukosefu wa maingiliano ya kutosha ni sababu moja inayochangia vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu.

**Jedwali 53: Viwango vya Umilisi wa Lugha Mjini Kiambu.**

| | **Kuandika** | **Kusoma** | **Kuongea** |
|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **17.8** | **17.6** | **17.5** |
| **Kikuyu** | **15.3** | **15.5** | **16.01** |
| **Kiingereza** | **17.9** | **18.0** | **18.2** |
| **Sheng** | **15.01** | **15.0** | **17.5** |

Katika mji wa Kiambu, viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu havikuwa vya chini sana kama jijini Nairobi. Hakika viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu mijini Kiambu vilikuwa karibu sawa na viwango vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea. Utafiti huu ulibaini kuwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ni vya juu kuliko jijini Nairobi kwa vile mji wa Kiambu una maingiliano ya kiwango cha juu na sehemu za mashambani ambako kuna idadi kubwa ya wakaazi wa jamiilugha ya Kikuyu.

**Jedwali 54: Viwango vya Umilisi wa Lugha Mjini Thika.**

| | Kuandika | Kusoma | Kuongea |
|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | **16.8** | **17.1** | **17.5** |
| **Kikuyu** | **16.42** | **16.02** | **16.6** |
| **Kiingereza** | **17.5** | **17.53** | **17.8** |
| **Sheng** | **15.0** | **15.0** | **17.0** |

Viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu mjini Thika vilikuwa vya juu ilikinganishwa na viwango vya umilisi wa lugha hii katika jiji la Nairobi na Mji wa Kiambu. Aidha, viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu vilikaribia sana viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza huku vikiwa juu kuliko viwango vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi ya kuandika na kusoma. Utafiti huu ulibaini kuwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ni vya kiwango cha juu mjini Thika ikilinganishwa na mijini Nairobi na Kiambu kwa vile mbali na kuwa na maingiliano mengi na jamii ya Kikuyu mashambani, pia mji wa Thika uko mbali kidogo kimasafa na jiji la Nairobi ikilinganishwa na mji wa Kiambu. Umbali wa kimasafa nao unachangia kuwa na maingilano machache kati ya vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Thika na jijini Nairobi.

Kutokana na ulinganisho wa viwango vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika miji hii mitatu, utafiti wetu ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wana viwango tofauti vya umilisi wa lugha ya Kikuyu kutokana na umbali na kiasi cha maingiliano na jamiilugha ya Kikuyu mashambani. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Landweer (2000) kuwa masafa kutoka sehemu za miji na

kiwango cha maingiliano kati ya jamiilugha za mijini na mashambani ni kigezo muhimu katika upimaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha. Matokeo haya ni muhimu kwetu hasa katika kuweka mikakati mwafaka ya kuinua viwango vya umilisi na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika (taz. 7.4.2.2).

**5.9 Hitimisho.**

Sura hii imetumiwa kuwasilisha data ya kijarabati iliyokusanywa nyanjaji kuhusu mielekeo, viwango vya umilisi wa lugha na maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Data hii ilikusanywa kwa kutumia hojaji za mielekeo na matumizi ya lugha na mitihani ya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng na iliwasilishwa kwa njia ya kijarabati kupitia histogramu na majedwali. Aidha, kuna maelezo yaliyotolewa chini ya kila mchoro na jedwali kuelezea matokeo yaliyopatikana baada ya data kuchanganuliwa kupitia programu ya S.P.S.S. Katika sura iliyofuata (sura ya 6) utafiti huu ulijishughulisha na kujadili kwa kina data ya kijarabati na kimaelezo kwa kuzingatia malengo na nadharia za utafiti huu ili kuweka wazi matokeo ya utafiti.

# SURA YA SITA

## MIJADALA KUTOKANA NA DATA YA KIJARABATI NA KIMAELEZO.

### 6.1 Utangulizi

Katika sura ya tano, utafiti huu ulijihusisha na uwasilishaji wa data ya kijarabati. Data hii ilitokana na sampuli ya utafiti wetu ambayo ilijumuisha vijana wa jamii ya Kikuyu kutoka miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Vifaa muhimu vilivyotumika kukusanya data ya kijarabati ni hojaji za mielekeo na matumizi ya lugha na vile vile mitihani ya kupima umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Katika sura hii utafiti wetu ulijikita katika mijadala iliyotokana na data ya kijarabati na kimaelezo (iliyotokana na mijadala ya kimakundi). Majadiliano katika sura hii yaliongozwa na malengo na maswali ya utafiti huu, mihimili ya nadharia za utafiti wetu ambazo ni Nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na Nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa. Sura hii imepangwa kupitia mada ndogo ndogo zilizoibuka kutokana na malengo manne ya utafiti wetu ambayo yalikuwa:-

i. Kuchunguza na kubainisha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.
ii. Kubaini viwango vya matumizi ya lugha ya Kikuyu katika maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

iii. Kubaini viwango vya umilisi wa Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu waishio mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

iv. Kubaini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii na hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika.

## 6.2 Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Mojawapo wa lengo la utafiti huu lilikuwa kubaini mielekeo walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha nne zinazozungumzwa katika miji hii ambazo ni Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hasa utafiti huu ulitaka kubaini mielekeo walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana waliounda sampuli ya utafifti huu ikilinganishwa na lugha nyingine zinazozungumzwa katika miji hii mitatu.

Makisio yetu yalikuwa kwamba huenda vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu jambo ambalo huenda lingepelekea wawe na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu. Kama asemavyo Baker (1992), mielekeo ya lugha ina athari za moja kwa moja kwa umilisi wa lugha yoyote ile na hatimaye athari hizi huathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika. Ajzen na Fishbein (2005) wanafafanua kuwa kuna mielekeo chanya na mielekeo hasi kuhusu lugha miongoni mwa wazungumzaji wake. Hali hii ya kuwa na mielekeo

chanya na hasi kuhusu lugha ndiyo iliyokuwa inachunguzwa katika utafiti huu ili kubaini kama kweli lugha za mama kama vile Kikuyu bado ziko na uthabiti wa kiisimujamii miongoni mwa vijana mijini na sababu zinazoweza kuwa zikichangia hali hii.

Katika miji hii mitatu, kuna mtagusano wa lugha mbalimbali hali inayochangia kuwepo kwa mazingira ya wingilugha. Baadhi ya lugha zinazotumiwa katika miji hii kwa wingi katika mawasiliano ni Kiswahili, Kiingereza, Sheng na lugha mbalimbali za mama kama vile Kikuyu. Kama asemavyo Bussmann (1996), ni vigumu sana kwa wazungumzaji katika jamii yenye wingilugha kujiepusha na suala la kuunda mielekeo mbalimbali kuhusu lugha zinazopatikana katika mazingira yao. Wazungumzaji huenda wakapendelea kutumia lugha moja huku wakizichukia lugha nyingine. Hali hii ndiyo iliyojitokeza miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika matumizi yao ya lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Katika kubaini mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili Kiingereza na Sheng, mtafiti alijaribu kubaini umuhimu ambao vijana hawa huambatisha na lugha hizi nne katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali muhimu katika miji hii mitatu. Baadhi ya shughuli hizi zilikuwa ni kama vile elimu, biashara, kupata kazi, kuzungumza na wazazi wao na watu wazima kwa jumla, kuzungumza na wenzao, kufanya urafiki, kuwasiliana nyumbani na kufahamu na kuhifadhi utamaduni wa jamii yao.

### 6.2.1 Mielekeo Kuhusu Lugha za Kufundishia Shuleni.

Katika shughuli za elimu, utafiti huu ulionyesha bayana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawaoni umuhimu wowote wa kutumia lugha ya Kikuyu, ambayo ni lugha yao mama, katika masuala ya elimu. Hii ni kwa sababu hakuna kijana hata mmoja aliyechagua lugha ya Kikuyu kuwa lugha ya kuendesha masomo shuleni katika miji hii mitatu. Asilimia 99 ya vijana hawa walisema kuwa lugha muhimu na zinazofaa kutumiwa katika shughuli za elimu ni Kiingereza na Kiswahili huku asilimia 1 pekee wakifikiria kuwa lugha ya Sheng ni muhimu katika shughuli za kielimu (taz. jedwali 10 na mchoro 10).

Utafiti huu ulibaini wazi kuwa kuna hali ya kutotumika kwa lugha za mama katika elimu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika. Hii ina maana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wanayo mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya elimu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Jambo hili linawafanya wasione umuhimu wa kujifunza lugha ya mama na kwa hivyo hatimaye umilisi wao wa lugha ya mama ni wa kiwango cha chini mno kama ilivyojitokeza kwingineko katika utafiti huu.

Fishman (2001) na Lewis na Simons (2009) katika vigezo vyao vya kupima uthabiti wa lugha vya GIDS na EGIDS mtawaliwa, wanafafanua vyema kuwa kigezo kimoja ambacho hutumika kuonyesha kama lugha ina uthabiti wa kiisimujamii ni iwapo lugha husika inaungwa mkono na asasi mbalimbali za kijamii kama vile kufundishia shuleni

hasa katika daraja za chini za mfumo wa elimu. Pia, mbali na kutumika kama lugha za kufundishia, maarifa kuhusu lugha husika yanafaa kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia elimu.

Aidha, shule zote zilizohusishwa katika jumuiya ya utafiti huu zilikuwa na sera maalum kuhusu matumizi ya lugha hizi nne. Lugha zilizokubaliwa kutumiwa shuleni ni lugha za Kiingereza na Kiswahili ambapo Kiingereza katika shule hizi zote ndicho hutumiwa kwa wingi huku lugha ya Kiswahili ikitengewa siku moja au mbili katika juma. Lugha za Kikuyu na sheng nazo zilikuwa zimepigwa marufuku kabisa na hazikufaa kutumiwa hata kidogo kimawasiliano.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa sera za matumizi ya lugha shuleni katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika zilichangia pakubwa katika kupunguza uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu. Utafiti huu unaunga mkono maoni ya Sheik (2011) anaposema kuwa njia moja kuu ya kuimarisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama (kama vile Kikuyu) ni kuhakikisha kuwa serikali za Afrika zimetilia maanani mapendekezo ya UNESCO ya 2005 na vipengele vya 6 na 14 vya azimio la mwaka wa 2007 la Umoja wa Mataifa vya kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama ulimwenguni kwa kuzifanya lugha za kufunzia shuleni.

Sera za matumizi ya lugha katika shule za miji ya Nairobi, Kiambu na Thika pia zilichangia pakubwa katika kuunda mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu kuhusu lugha

hizi nne. Mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza na Kiswahili na mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu na Sheng kama lugha za elimu basi ni zao la moja kwa moja la sera za matumizi ya lugha katika shule mijini. Basi inaonyesha kuwa kuna msukumo unaowafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuwa na mielekeo mbalimbali kuhusu lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Kama wasemavyo, Fishbein & Ajzen (1985), Furaha (1991) na Miller (2005) kuhusu nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa, jambo moja ambalo huchangia mtu kuwa na mwelekeo wowote ule kuhusu jambo fulani ni matarajio ya watu wengine katika jamii yake kuhusu jambo hilo. Kwa upande mmoja, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama lugha za elimu kwani watu wengine katika jamii yao kama vile walimu na wazazi wanatarajia watumie lugha hizi mbili shuleni ili wafaulu masomo. Kwa upande ule mwingine, vijana mijini wana mielekeo hasi kuhusu Kikuyu na Sheng kama lugha za elimu kwa vile walimu na wazazi hawawatarajii wazitumie lugha hizi shuleni kwani hazina faida kielimu.

Katika jedwali 20 katika sura ya tano, vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika wametoa sababu mbalimbali zinazochangia wao kutotumia lugha ya Kikuyu shuleni. Sababu mojawapo kuu ya kutotumia lugha hii ni kuwa lugha hii imepigwa marufuku shuleni na mwanafunzi anayepatikana akiitumia hupewa adhabu kali. Sababu nyingine za kutotumia lugha hii ni kama vile kuwa lugha ya Kikuyu hutatiza ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza hasa katika kiwango cha matamshi na

kuwa Kikuyu sio lugha ya taifa na basi hutatiza mawasiliano katika shule za upili mijini ambako kuna wanafunzi kutoka jamii mbalimbali nchini Kenya mbali na ule uwezakano wa kuleta ukabila shuleni. Hata hivyo, utafiti huu ulionyesha kuwa baadhi ya wanafunzi hutumia lugha ya Kikuyu kisirisiri hasa wanapowasiliana na wafanyakazi wengine shuleni na wanapotaka kujitenga kimawasiliano na wanafunzi kutoka jamii nyingine pale shuleni.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya elimu na yanakubaliana na matokeo ya utafiti wa Gachiri (2009). Gachiri alitafiti kuhusu athari za sera ya lugha nchini Kenya kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana katika kaunti ya Kirinyaga ambako alibaini kuwa sera za shule katika kaunti ya Kirinyaga kuhusu matumizi ya lugha zilisisitiza zaidi matumizi ya lugha za Kiingereza na Kiswahili huku lugha ya Kikuyu ikipigwa marufuku shuleni. Gachiri anaeleza kuwa hiki ndicho kiini mojawapo cha vijana katika kaunti ya Kirinyaga kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu jambo linalowafanya kuwa na umilisi wa viwango vya chini vya lugha ya Kikuyu.

### 6.2.2 Mielekeo Kuhusu Lugha za Kufanyia Biashara.

Mielekeo hasi ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu iliendelea kujitokeza katika shughuli nyingine muhimu za kijamii kama vile biashara. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ni asilimia 11 pekee ya sampuli yetu ya vijana mijini iliyofikiria kuwa Kikuyu ni lugha muhimu katika biashara mjini. Hii

ni asilimia ndogo ikilinganishwa na asilimia 89 ya vijana waliofikiria lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ndizo lugha mwafaka zaidi katika shughuli za kibiashara (taz. jedwali 11). Inatokea kuwa lugha ya Kiswahili (asilimia 39) ndiyo lugha inayoonyesha mwelekeo chanya zaidi miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kama lugha mwafaka ya kufanya biashara ikifuatwa na Kiingereza (asilimia 31).

Mielekeo hii ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuhusu lugha hizi nne kama lugha za biashara inakubaliana na mielekeo na matumizi ya kijumla ya lugha hizi nne kama lugha za biashara nchini Kenya. Kwa mfano, Wendo (2009) anaeleza kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ambayo hutumika kwa kiasi kikubwa katika uendeshaji wa biashara za humu nchini hasa katika sehemu za mijini ambako kuna mazingira ya mtagusano wa lugha. Naye Muaka (2005) anafafanua kuwa lugha ya Kiingereza nchini Kenya hutumika zaidi kama lugha ya kutekeleza biashara rasmi za kiserikali na kuendesha biashara za kimataifa kati ya nchi ya Kenya na mataifa ya nje. Lugha ya Kikuyu nayo kama anavyoelezea Gachiri (2009) hutumika zaidi katika kuendesha biashara katika sehemu za mashambani ambako kuna wakaazi wengi kutoka jamii ya Kikuyu na katika mitaa yenye wakaazi wengi wa jamii ya Kikuyu katika miji mikuu ya Kenya kama vile Nairobi na Nakuru. Githiora (2002) anafafanua kuwa lugha ya Sheng nayo hutumika mjini kuendesha biashara ndogo ndogo kama vile uchuuzi na uchukuzi na hasa katika mitaa iliyo na watu wengi wa vipato vya chini.

Ruwaza kama hizi za matumizi haya mbalimbali ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika biashara zilipatikana pia kuwa ndizo zilizochangia zaidi katika kujenga mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijijni Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha iliyo mwafaka zaidi katika shughuli za kibiashara mijini. Mielekeo hasi ya vijana kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha mwafaka ya biashara mijini ilisaidia katika kuelezea sababu zinazowafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kutopendelea kuizungumza lugha ya Kikuyu ambayo ndiyo lugha yao ya mama na hatimaye kuwafanya wawe na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu.

Kama asemavyo Landweer (2000) sababu moja inayoifanya lugha kuwa imara ama iwe na viwango vya juu vya uthabiti wa kiisimujamii ni kuwa na msingi imara wa kiuchumi. Hii ina maana kuwa mbali na kuwa na faida nyingine kiuchumi, lugha husika lazima iwezeshe wazungumzaji wake kushiriki kikamilifu katika biashara ili waweze kujitegemea kiuchumi. Iwapo lugha basi haitumiki katika biashara, Landweer anaelezea kuwa kundi fulani la watu huhama lugha yao na kuanza kuzituimia lugha nyingine zinazotumika katika biashara kwani zina faida kwao kiuchumi.

### 6.2.3 Mielekeo Kuhusu Lugha ya Kutafuta Kazi za Kitaaluma Baada ya Masomo.

Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu katika shughuli za kutafuta kazi za kitaaluma baada ya shule (taz. jedwali 12). Idadi kubwa ya vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu kulingana na utafiti huu walikuwa na mwelekeo kuwa lugha ambayo inaweza kuwawafaa zaidi

katika kujipatia kazi za kitaaluma baada ya kumaliza shule ni lugha ya Kiingereza (asilimia 66) ikifuatwa na lugha ya Kiswahili (asilimia 32). Ni asilimia 1 pekee ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini ambayo ilifikiria kuwa lugha ya mama kama vile Kikuyu inaweza kuwasaidia kupata kazi za kitaaluma baada ya kumaliza shule.

Muaka (2009) na Gachiri (2009) wanafafanua kuwa lugha ya Kiingereza ndiyo lugha iliyo na hadhi ya juu zaidi nchini Kenya. Hii ni kwa sababu lugha ya Kiingereza imetengewa majukumu rasmi pekee nchini Kenya na ambayo yanaambatanishwa na kazi tofauti tofauti za kitaaluma. Hii inaeleza sababu za asilimia 66 ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini waliounda sampuli ya utafiti huu kuipendelea lugha ya Kiingereza kama lugha ambayo ingewasaidia kupata kazi za kitaaluma kwa urahisi baada ya kumaliza masomo yao. Lugha ya Kiingereza inafuatwa kwa hadhi na Kiswahili. Lugha hizi mbili zina hadhi kubwa ikilinganishwa na lugha nyingine zote nchini Kenya. Mtazamo huu basi unaelezea ni kwa nini vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wana mielekeo chanya kuhusu Kiingereza na Kiswahili kama lugha za kuwasaidia kupata kazi za kitaaluma baada ya kumaliza masomo.

Aidha, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini walionyesha mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu (asilimia 1) na Sheng (asilimia 1) kama lugha za kujipatia kazi za kitaaluma baada ya kumaliza shule. Lugha za mama kama vile Kikuyu nchini Kenya zimetengewa majukumu ya kimawasilano na kibiashara katika sehemu za mashambani (Iraki 2004) na basi hazihusishwi kwa wingi na utowaji wa nafasi za kazi za kitaaluma nchini Kenya.

Kutokana na matokeo haya ni bayana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha inayoweza kuwasaidia kupata kazi za kitaaluma baada ya kumaliza masomo yao. Mielekeo kama hii ndio inawafanya wasiwe na moyo wa kujifunza na kuzungumza Kikuyu hali inayofanya viwango vyao vya umilisi wa lugha ya Kikuyu kuwa vya chini. Kama asemavyo Landweer (2000) faida moja ya kiuchumi ya lugha kwa mzungumzaji ni kumwezesha kupata ajira baada ya masomo. Iwapo lugha haiwezi kutimiza wajibu huu basi wanaofaa kuizungumza huhamia lugha nyingine na basi hufanya viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yao kuteremka. Hii ndiyo hali inayokabili lugha ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu kama utafiti huu ulivyobaini.

### 6.2.4 Mielekeo Kuhusu Lugha za Mawasiliano Mitaani na Nyumbani Baina ya Vijana na Wazazi na Baina ya Vijana Wenyewe.

Utafiti huu pia ulilenga kubaini mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha iliyokuwa mwafaka katika mawasiliano yao na wazazi na watu wazima nyumbani na mitaani mwao (taz. jedwali 13) katika sura ya tano. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa vijana wengi wa jamii ya Kikuyu mijini walipendelea zaidi lugha za Kiswahili (asilimia 44) kama lugha ya mawasilano baina yao na wazazi na watu wazima nyumbani na mitaani. Lugha ya Kiingereza (asilimia 25) ilifuata kisha lugha ya Kikuyu (asilimia 22) na Sheng (asilimia 9) mtawaliwa. Matokeo haya yanaonyesha kuwa vijana wengi wa jamii ya Kikuyu mijini wana mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili ikifuatwa na lugha ya Kiingereza kama lugha za mawasiliano

baina yao na wazazi na watu wazima nyumbani na mitaani. Katika mizani ya likati (taz. mchoro 10), ilibainika wazi zaidi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawatumii lugha ya Kikuyu kwa wingi kama wanavyozitumia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng wanapozungumza na wazazi wao nyumbani. Baadhi ya sababu za kutotumia lugha ya Kikuyu katika mawasiliano baina ya Vijana wa jamii ya Kikuyu na wazazi wao mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni kama vile kuwa lugha ya Kikuyu hufahamika tu na wazazi na wala sio vijana, wazazi hawahimizi matumizi ya lugha ya Kikuyu nyumbani, Kikuyu ni lugha ngumu kujifunza na kuwa ni lugha iliyopitwa na wakati (taz. jedwali 19).

Vile vile, utafiti huu ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kwa kiasi kikubwa hawapendelei kuitumia lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano baina yao wanapotangamana mitaani. Hakika nia wazi kutokana na matokeo ya utafiti huu kuwa lugha wanayoipendelea zaidi vijana hawa kama lugha ya mawasiliano baina yao ni lugha ya Sheng (asilimia 53), Kiswahili (asilimia 24) na Kiingereza (asilimia 19) ikilinganishwa na asilimia 3 pekee ya vijana waliopendelea kutumia lugha ya Kikuyu katika mawasiliano yao (taz. jedwali 14).

Matokeo ya utafiti huu yanaweka wazi ukweli kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wanapendelea kuzitumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng kuliko lugha ya Kikuyu katika mawasiliano yao na wazazi na watu wengine wazima na pia baina yao wenyewe. Hali hii inaashiria kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapendelei lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasiliano

ama baina yao wenyewe au na wazazi na watu wazima. Ukosefu huu wa imani katika lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya mawasiliano ndio unaochangia vijana hawa kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha hii.

Kama wasemavyo Ajzen na Fishbein (2005), mielekeo chanya au hasi kuhusu lugha ni matokeo ya imani ya mtu kuhusu faida atakazozipata akiitumia lugha fulani katika mawasiliano yake. Inatokea kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu huiona lugha kama vile Sheng ikiwa na faida nyingi kimawasiliano baina yao au lugha ya Kiswahili ikiwa na faida kwao wanapowasiliana na wazazi wao na ndio maana wanazipendelea lugha hizi kuliko lugha ya Kikuyu. Jambo hili linadhihirishwa wazi na sababu wanazozitoa vijana hawa za kutopendelea kuitumia lugha ya Kikuyu katika mawasiliano baina yao ikilinganishwa na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Baadhi ya sababu hizi ni kama vile madai kuwa Kikuyu ni lugha ambayo haina faida kielimu na haisaidii mtu kupata kazi za kitaaluma baada ya kumaliza masomo, kuwa ni duni ikilinganishwa na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng na ni ishara ya mtu asiye na ustaraabu maishani (taz. jedwali. 24).

### 6.2.5 Mielekeo Kuhusu Lugha iliyo na Hadhi Kimatumizi Miongoni mwa Vijana Mijini.

Suala la hadhi ya lugha pia lilijitokeza bayana katika ruwaza za matumizi ya lugha ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Utafiti huu ulibaini kuwa vijana wengi wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu wameipea lugha ya Kikuyu hadhi ya chini kimatumizi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng (taz.

mchoro 14). Hii ni kwa sababu asilimia 67 ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini wana mielekeo kuwa vijana wanaozungumza lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi ya juu kuliko wenzao ambao wanaizungumza lugha ya Kikuyu. Hii ni idadi kubwa ikilinganishwa na asilimia 33 pekee ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini ambao hawaoni kana kwamba vijana wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi ya juu kuliko wale wanaozungumza lugha ya Kikuyu.

Kwa mujibu wa Krauss (1992), hadhi zinazopewa lugha na wazungumzaji katika jamii huchangia pakubwa katika kubaini viwango vya umilisi walivyo navyo wazungumzaji hao katika lugha wanazozizungumza. Krauss anaendelea kufafanua kuwa wazungumzaji wa lugha huwa na umilisi wa juu katika lugha walizozipea hadhi ya juu katika jamii ikilinganishwa na lugha zile walizozipa hadhi ya chini. Hali hii ya vijana wa jamii ya Kikuyu kuzipatia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng hadhi ya juu kuliko lugha ya Kikuyu kimatumizi ndiyo inayochangia vijana hawa kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng (taz. sehemu 5.8). Aidha, Landweer (2000) anaeleza kuwa hadhi iliyopewa lugha na wazungumzaji katika jamii ni muhimu katika kubaini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hiyo. Landweer anaendelea kusema kuwa, kwa upande mmoja, jinsi lugha ilivyo na hadhi ya juu miongoni mwa wazungumzaji wake ndivyo hivyo ilivyo na kiwango cha juu cha uthabiti wa kiisimujamii. Kwa upande ule mwingine, iwapo lugha imepewa hadhi ya chini na wazungumzaji basi hata viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii ni vya chini.

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna sababu mbalimbali zinazowafanya vijana wa jamii ya Kikuyu miji Nairobi, Kiambu na Thika kuipa lugha ya Kikuyu hadhi ya chini ikilinganishwa na Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng (taz. jedwali 23). Baadhi ya sababu hizi ni kama vile suala kuwa lugha ya Kikuyu sio lugha ya kisasa kwa vile haitumikii katika teknolojia za kisasa hasa katika teknolojia ya tarakilishi kama vile zinavyofanya lugha ya Kiswahili na Kiingereza nchini Kenya. Kama asemavyo Brenzinger (2003), ueneaji wa lugha katika maeneo mapya ya kijamii kama vile matumizi ya lugha katika vyombo vya kiteknolojia huwezesha lugha hiyo kupewa hadhi ya juu na wazungumzaji katika harakati zao za kufaidi kutokana na teknolojia husika. Hata hivyo, haya ni kinyume na jinsi vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika wanavyoviona vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha ya Kikuyu. Haya yanajitokeza wazi katika mjadala wa kimakundi kama ifuatavyo:-

**Mtafiti:** ***Je, lugha ya Kikuyu hutumika katika vyombo vya habari kama vile redio, runinga na magazeti? Taja baadhi ya vyombo hivi.***

**Mhojiwa I:** ***Ndiyo. Kikuyu hutumika katika redio na hata runinga.***

**Mtafiti:** ***Idhaa hizi za redio na runinga ni zipi?***

**Mhojiwa II:** ***Kuna idhaa za redio kama vile Inooro, Coro na Kameme FM.***

**Mhojiwa III:** ***Pia kuna runinga inayotangaza kwa Kikuyu.***

**Mtafiti:** ***Je, nyinyi kama vijana huwa mnasikiliza idhaa zinazotangaza kwa Kikuyu?***

**Mhojiwa I:** ***La. Mimi huzisikiliza tu wakati watu wengine wanapozisikiliza kama vile wazazi wangu nyumbani lakini mimi mwenyewe sizisikilizi.***

**Mtafiti:** ***Kuna sababu za kutosikiliza idhaa za Kikuyu za redio na runinga?***

**Mhojiwa IV:** ***Sababu ni kuwa vijana mijini hupenda kusikiliza redio Zinazotangaz kwa Kiingereza na Kiswahili na hata Sheng kama***

***vile Ghetto redio. Lugha hizi zinafahamika na vijana wote mijini ilhali sisi hatufahamu Kikuyu.***

**Mtafiti:** ***Je, Kikuyu hutumika katika tarakilishi?***

**Wahojiwa :** ***La!***

**Mhojiwa 3:** ***Lugha ya Kikuyu haina msamiati wa kuelezea masuala ya tarakilishi kama vile Kiingereza. Sidhani lugha ya Kikuyu itawahi kuwa lugha ya tarakilishi kwa sababu ni lugha iliyopitwa na wakati.***

(Taz. kiambatisho V)

Mjadala huu wa kimakundi ulionyesha wazi kuwa hata ingawa lugha ya Kikuyu inatumika katika vyombo vya habari kama vile redio na runinga, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hawasikilizi idhaa hizi bali wao hupendelea idhaa zinazotangaza kwa lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Vile vile ni wazi kuwa lugha ya Kikuyu bado haitumiki kama lugha ya tarakailishi. Sababu kama hizi ndizo zinawafanya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuipa lugha ya Kikuyu hadhi ya chini kimatumizi ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Matokeo ya haya ni kuwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana hawa ni wa kiwango cha chini ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 6.2.6 Mielekeo ya Kijumla Kuhusu Lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa Vijana Mijini.

Utafiti huu vile vile uliweza kubainisha mielekeo ya kijumla kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika (taz. mchoro 15). Ukweli huu ulidhihirika vyema kutokana na matokeo ya utafiti huu kwani vijana wa jamii ya Kikuyu

mijini Nairobi, Kiambu na Thika walipoulizwa kuhusu mielekeo yao ya kijumla kuhusu lugha ya Kikuyu kwa upande mmoja na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa upande ule mwingine, asilimia 97 ya vijana wote wa jamii ya Kikuyu katika miji hii ilionyesha wazi kuwa hawakipendi Kikuyu kama lugha yao ya mawasiliano bali wao walizipendelea lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Ni asilimia 3 pekee ya vijana waliounda sampuli hii iliyoonekana kukipenda Kikuyu kama lugha yao ya mawasiliano.

Kuna sababu mbalimbali ambazo zilitolewa na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika zinazowafanya wasiipende lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Baadhi ya sababu hizi ni kama vile kuwa wataonekana kama ni 'washamba' yaani wasiostaarabika wakizungumza Kikuyu, Kikuyu si lugha muhimu kwa vile hawaitumii mara nyingi na katika maeneo ya kijamii mengi kama vile shuleni na katika biashara, vijana wanaozungumza kwa Kiswahili, Kiingereza na Sheng wana hadhi kuliko wale wanaozungumza Kikuyu kwa vile wana matamshi mazuri na wana ufasaha wa kuzungumza kuliko wanaofahamu Kikuyu na kuwa vijana hawapendi kujifunza Kikuyu kwani ni kigumu na wanaiona kuwa lugha duni ambayo haina haja kujifunza.

Mielekeo hii ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu lugha ya Kikuyu na sababu walizozitoa zote zilionyesha kuwa kwa kiwango kikubwa vijana hawa hawana fahari ya lugha yao ya mama yaani Kikuyu. Fahari ya lugha

hutokana na umuhimu uliopewa lugha na wanajamiilugha wenyewe. Kama aelezavyo Landweer (2000), mtazamo wa wanajamii kuhusu lugha yao ni jambo moja ambalo huathiri uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika. Landweer anaendelea kusema kuwa iwapo jamiilugha itaiona lugha yao kuwa muhimu, basi hivyo ndivyo lugha hii ilivyo thabiti kiisimujamii na iwapo jamiilugha itaiona lugha yao kuwa sio muhimu, basi uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hii utakuwa wa kiwango cha chini. Utafiti huu basi ulibaini kuwa hali ya kisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika sio thabiti kwa vile asilimia kubwa ya vijana hawa wana mielekeo kuwa lugha ya Kikuyu sio lugha muhimu katika mawasilano yao ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 6.2.7 Mielekeo Chanya Kuhusu Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana Mijini.

Hata ingawa kwa jumla utafiti huu ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha yao ya mawasiliano, bado kuna idadi ndogo (asilimia 3) ya vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu ambao waliiona lugha ya Kikuyu kuwa lugha mwafaka hasa katika utekelezaji wa shughuli nyingine zisizoweza kuendeshwa vyema kwa kutumia lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Mojawapo wa shughuli ambayo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini walionelea kuwa yafaa kuendeshwa kwa lugha ya Kikuyu ni kuhifadhi, kueneza na kuwafahamisha kuhusu utamaduni wao wa jamii ya Kikuyu. Hii ina maana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu

katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika wana mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya kueneza na kuhifadhi utamaduni wa jamii yao ya Kikuyu. Hii ni kwa sababu asilimia 63 ya vijana ambao walihojiwa ilichagua Kikuyu kama lugha mwafaka ya kueneza na kuhifadhi utamaduni wao ikilinganishwa na lugha za Kiswahili (asilimia 20), Kiingereza (asilimia 15) na Sheng (asilimia 2) ambazo kwa pamoja zilifikiriwa kuwa muhimu katika shughuli hii ya kuhifadhi, kueneza na kuwafahamisha kuhusu utamaduni wa jamii ya Kikuyu (taz. jedwali 17)

Kama wasemavyo Ruhlen (1996) na Vigdis (2003), lugha za mama ni muhimu katika kila jamii kwani zina majukumu maalum ya kutekeleza kama vile kuhifadhi na kuendeleza utamaduni na vile vile kuhifadhi historia ya jamii. Katika utafiti huu ilibainika kuwa hata ingawa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa kiasi kikubwa wana mwelekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kikuyu, bado vijana hawa wanaitambua lugha ya Kikuyu kama lugha iliyo mwafaka zaidi katika kuhifadhi, kueneza na kuwafahamisha kuhusu utamaduni wao.

Aidha, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika waliiona lugha ya Kikuyu kama lugha mwafaka katika mawasiliano yao na wenzao na watu wazima katika sehemu za mashambani. Baadhi ya vijana waliohojiwa walionyesha kuwa na mwelekeo chanya kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya mawasilino katika sehemu za mashambani wanapotembea hapo. Hata hivyo, kwa vile hawaifahamu lugha hii vyema, baadhi ya vijana (asilimia 55) waliohojiwa walionekana kujihurumia kutokana na

kushindwa kwao katika kuwasiliana kwa lugha ya Kikuyu (taz. mchoro 12). Sababu za kujihurumia ni kwa vile waliona kuwa hawana fursa ya kufahamu kuhusu utamaduni wao, hawawezi kuwasiliana vyema na watu mashambani na pia kuna uwezekana wa kudharauliwa, kusengenywa na kutengwa na vijana wenzao waishio mashambani waendapo huku (taz. jedwali 22).

### 6.2.8 Hitimisho kuhusu Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika kuhusu Lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Kwa mujibu wa Landweer (2000), mojawapo wa kigezo muhimu cha kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kule kuangalia mtazamo au mielekeo walio nayo wanajamii wenyewe na watu wengine kuhusu lugha yao. Matokeo haya kuhusu umuhimu wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kijamii yanaonyesha wazi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika kwa kiasi kikubwa wana mtazamo mbaya au mwelekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kikuyu. Hali hii imepelekea lugha hii ya Kikuyu kupewa hadhi ya chini na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini ikilinganishwa na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng ambazo wanaziona kuwa lugha mwafaka zaidi za kuwasiliana nazo katika kutekeleza shughuli muhimu kama vile elimu na biashara katika miji hii mitatu.

Landweer (2000:67) anaongezea kuwa, “kigezo kingine cha kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kwa kuangalia hadhi iliyopewa lugha katika jamii husika”. Landweer anaendelea kueleza kuwa “jinsi lugha inavyopewa hadhi ya juu katika jamii ndivyo lugha hii ilivyo thabiti kiisimujamii na jinsi lugha ilivyo na hadhi ya chini

miongoni mwa wazungumzaji wake ndivyo ilivyo na uthabiti wa kiisimujamii wa hali ya chini".

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wameathirika na matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng kimawasiliano katika shughuli zao nyingi za kijamii. Kwa mujibu wa utafiti huu basi, vijana hawa wana mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu hali inayowafanya kuwa na mtazamo mbaya kuhusu lugha ya Kikuyu na hivyo kuipa hadhi ya chini kimatumizi ikilinganishwa na lugha kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Aidha, kutokana na mielekeo yao hasi kuhusu lugha ya Kikuyu, ni wazi kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika ni ya kiwango cha chini na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hii miongoni mwao vile vile ni wa kiwango cha chini. Hali hii inasababishwa na ukweli kuwa vijana hawa hawaoni umuhimu wa kuitumia lugha ya Kikuyu katika shughuli zao nyingi za kijamii huku wakipendelea lugha nyingine kama Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kama aelezavyo Miller (2005) katika nadharia ya Vitendo Vilivyopangwa, mielekeo na matarajio ya mtu kuhusu jambo fulani ndiyo humpa nia ya kutenda jambo hilo na hatimaye hujikuta akilitenda jambo lenyewe au akiwa na tabia fulani. Katika masuala ya matumizi ya lugha kama waelezavyo Ajzen na Fishbein (2005), mielekeo ya mtu kuhusu lugha fulani na matarajio yake kuhusu faida za kutumia lugha ile kwake

ndizo humfanya awe na nia ya kutumia lugha hiyo na hatimaye yeye hujikuta akiitumia lugha hiyo katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii.

### 6.3 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubaini maeneo ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hupendelea kutumia lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha huwa muhimu katika kupima uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yeyote ile ulimwenguni (Lewis na Simons 2009). Naye Landweer (2000) ana maoni kuwa jinsi lugha inavyotumiwa kimawasiliano katika maeneo mengi ya kijamii ndivyo lugha hii ilivyo thabiti kimatumizi. Hakika utafiti huu ulilenga kubaini maeneo mbalimbali ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hutumia lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Kwa kufanya hivi utafiti huu ulizingatia zaidi maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha ya shuleni na nyumbani kama maeneo muhimu ya kutambulisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hizi miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini.

#### 6.3.1 Miktadha Mbalimbali ya Matumizi ya Lugha katika Eneo la Kijamii la Shuleni.

Eneo la kijamii la shuleni lilikuwa muhimu katika uchunguzi wetu wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa vile vijana waliounda sampuli ya utafiti huu hutumia muda mwingi wao

wakiwa shuleni ambapo pia kumewekwa sera maalum za matumizi ya lugha. Katika shule zote 12 za upili zilizotembelewa, kulikuwa na sera maalum za lugha ambapo lugha zilizoruhusiwa kutumiwa ndani ya shule ni Kiswahili na Kiingereza huku lugha za Kikuyu na Sheng zikiwemo lugha nyingine za mama zikiwa zimepigwa marufuku kimatumizi katika shule hizi. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa lugha za Kikuyu na Sheng bado zilikuwa zinatumiwa na vijana wa jamii ya Kikuyu kuwasiliana pale shuleni japo kwa njia ya siri, kwa viwango vya chini na katika miktadha maalum pekee.

Baada ya kuchunguza miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika eneo la shuleni, utafiti huu ulibaini kuwa lugha ya Kikuyu na lugha nyingine za mama kwa jumla hutumika kwa nadra sana katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la shuleni. Hii ina maana kuwa eneo la kijamii la shuleni husisitiza tu matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza kwa wingi kwani ndizo lugha rasmi za kufunzia nchini Kenya. Hali hii ina athari za moja kwa moja kwa matumizi ya lugha za mama kama vile Kikuyu kwa vile hazipati fursa ya kuzungumzwa na vijana shuleni ilhali vijana hawa hutumia muda wao mwingi pale. Miktadha ifuatayo inaonyesha hali hii kwa uwazi.

#### 6.3.1.1 Lugha ya Mawasiliano Darasani

Utafiti ulibaini kuwa lugha zilizotumika kwa wingi kuwasiliana ndani ya darasa miongoni mwa wanafunzi (vijana) ni lugha za Kiswahili and Sheng kwa asilimia 34 na 33. Asilimia 33 ya vijana nayo ilitumia Kiingereza. Hakuna mwanafunzi hata mmoja

aliyedai kutumia lugha ya Kikuyu wanapozungumza na wenzao darasani (taz. jedwali 26). Wanapozungumza na walimu pale darasani, utafiti huu ulibaini kuwa mawasiliano mengi kati ya vijana na walimu huendeshwa kwa Kiingereza kwa asilimia 53 na Kiswahili kwa asilimia 45. Ni asilimia 2 tu ya vijana ambao walidai kuwa wao huwasiliana na walimu wao kwa kutumia Sheng pale darasani. Lugha ya Kikuyu huwa haitumiki kamwe katika mawasiliano baina ya walimu na wanafunzi darasani (taz. jedwali 28). Kutokana na miktadha hii miwili, ni wazi kuwa lugha iliyoathirika kabisa na sera za matumizi ya lugha shuleni pale darasani ni lugha ya Kikuyu ambayo haitumiki kamwe. Hii ina maanisha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapati fursa ya kuzungumza lugha ya Kikuyu jambo ambalo linaathiri pakubwa uthabiti wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ambazo hutumika darasani kwa viwango tofauti.

#### 6.3.1.2 Lugha ya Mawasiliano Nje ya Darasa.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa ruwaza ya matumzi ya lugha darasani hugeuka vijana wanapotumia lugha nje ya darasa. Kwani mujibu wa matokeo ya utafiti huu, asilimia 50 ya vijana hutumia lugha ya Sheng nje ya darasa, asilimia 33 hutumia Kiswahili huku asilimia 16 ikitumia Kiingereza. Aidha, lugha ya Kikuyu hutumiwa na asilimia 2 pekee vijana nje ya darasa (taz. jedwali 27). Zaidi, ilibainika kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini huongezeka wanapozungumza na wafanyakazi wengine shuleni nje ya darasa kwani asilimia 16 ya vijana hawa hutumia lugha ya Kikuyu. Hata hivyo, hii ni idadi ndogo ikilinganishwa na vijana asilimia 57 ambao hutumia Kiswahili, asilimia 18 ambao hutumia Sheng na asilimia 9 ambao

hutumia Kiingereza kuwasiliana na wafanyakazi wa shule nje ya darasa (taz. jedwali 29). Ilitokea kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu huongezeka miongoni mwa vijana hawa katika miktadha isiyo rasmi sana kama vile nje ya darasa.

### 6.3.2 Miktadha Mbalimbali ya Matumizi ya Lugha katika Eneo la Kijamii la Nyumbani.

Gordon (2005) ana maoni kuwa eneo la kijamii la matumizi ya lugha la nyumbani ni muhimu sana katika kubaini uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yoyote ile. Hii ni kwa sababu hapa ndipo mtoto hukutana na matumizi ya lugha yake ya kwanza maishani mwake na pia eneo hili ndilo kitovu cha kupitisha lugha yoyote ile kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Landweer (2000) naye anafafanua zaidi kuwa eneo la kijamii la matumizi ya lugha la nyumbani ndilo msingi wa maeneo mengine ya kijamii ya matumizi ya lugha kwani ndilo eneo ambalo huhusika zaidi na matumizi ya kiwango cha juu cha lugha za mama ulimwenguni. Kwa hivyo, kipimo mwafaka zaidi cha kubaini iwapo lugha inaupoteza uthabiti wake wa kiisimujamii ni kwa kuchunguza jinsi lugha ile inavyotumiwa kimazungumzo katika miktadha mbalimbali pale nyumbani.

Utafiti wetu ulitalii miktadha mbalimbali ya matumizi ya lugha katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la nyumbani katika juhudi za kubaini uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamiii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Miktadha hii ni kama ifuatayo:-

#### 6.3.2.1 Lugha ya Mawasiliano Miongoni mwa Vijana katika Kiwango cha Familia.

Utafiti huu ulibaini kuwa lugha ya Kikuyu ndiyo hutumiwa na idadi ndogo zaidi ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika mawasiliano yao kama familia. Hii ni kwa sababu ni asilimia 10 pekee ya vijana waliohojiwa ambao walidai kutumia Kikuyu katika mawasiliano wakiwa nyumbani ikilinganishwa na asilimia 47 ya vijana ambao huwasiliana kwa lugha ya Sheng wakiwa nyumbani ikifuatwa na Kiswahili kwa asilimia 26 huku Kiingereza kikitumiwa na asilimia 17 ya vijana (taz. jedwali 30). Hii ina maana kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hupendelea kuzitumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng badala ya lugha ya Kikuyu ambayo ndiyo lugha yao ya mama. Hali hii basi inapelekea kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

#### 6.3.2.2 Lugha ya Mawasiliano Miongoni mwa Wazazi na Vijana Nyumbani.

Utafiti huu vile vile ulibaini kuwa japo lugha ya Kikuyu inatumiwa katika eneo la nyumbani kati ya wanafamilia, matumizi haya yalikuwa ya kiwango cha chini ilikilinganishwa na lugha nyingine kama vile Kiswahili ikizingatiwa kuwa lugha ya mama ya familia hizi ni Kikuyu. Karanja (2012) ana maoni kuwa kutoweka kwa matumizi ya lugha katika eneo la nyumbani ni dalili kuu ya kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika. Matokeo ya utafiti huu (taz. jedwali 31) yanaonyesha kuwa asilimia 46 ya vijana hutumia Kiswahili wanapowazungumzia wazazi wao pale nyumbani ilhali asilimia 24 hutumia lugha ya Kikuyu wanapowazungumzia

wazazi wao, asilimia 19 ya vijana huwazungumzia wazazi wao kwa lugha ya Kiingereza huku asilimia 12 wakitumia Sheng.

Nalo jedwali la 32 laonyesha kuwa asilimia 39 ya wazazi hutumia lugha ya Kikuyu kuwazungumzia vijana, asilimia nyingine 36 hutumia lugha ya Kiswahili, asilimia 19 Kiingereza huku asilimia 5 ya wazazi wakitumia Sheng kuwazungumzia vijana. Hapa pia lugha ya Kiswahili inatoa ushindani mkubwa kwa lugha ya Kikuyu ambayo inastahili kutumiwa kwa wingi zaidi na wazazi wanapowazungumzia vijana ili wawapitishie lugha hii. "Iwapo lugha haipitishwi kutoka kizazi kimoja hadi kingine ama inapitishwa kwa viwango vya chini, basi lugha ile imo katika hatari kubwa ya kushuka katika viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii na basi kuingia katika mkondo wa lugha zinazoangamia pole pole ulimwenguni" (Brenzinger 2003:78).

## 6.4 Umilisi wa Lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Lengo lingine la utafiti huu lilikuwa kuchunguza na kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu waishio mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Haya yalifanywa kwa kuwapa wahojiwa mazoezi ya uandishi, usomaji na uzungumzaji ili kuweza kupima viwango vyao vya umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea.

Wahojiwa kwanza walipewa mazoezi ya kusoma kwa sauti na kuandika katika lugha hizi nne ili kupima viwango vyao vya umilisi wa lugha hizi nne waliokuwa katika stadi hizi mbili yaani kusoma na kuandika. Aidha, wahojiwa walitakiwa kutoa hotuba fupi katika mada teule katika lugha hizi ili kupima viwango vyao vya umillisi wa lugha hizi katika stadi ya kuongea. Katika stadi hizi za kuongea, kusoma na kuandika, vigezo mbalimbali vilitumiwa na watafiti ili kupima viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini.

Vigezo hivi vilikuwa kama vile kusitasita katika mazungumzo na usomaji, kuchanganya na kuhamisha msimbo kusikofuata ruwaza maalum, matamshi mabaya ya maneno, maendelezo mabaya ya maneno, kiimbo kibaya na ung'amuaji wa maana ya maneno. Kigezo kingine kilihusu uwezo wa wahojiwa wa kujieleza kwa ufasaha wakitumia lugha hizi na kiwango cha msamiati katika mazungumzo na uandishi. Vigezo hivi ndivyo baadhi ya vile vilivyotumiwa na watafiti katika kupima na kubaini viwango vya umilisi walio nao vijana wa jamii ya Kikuyu mijini katika lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Aidha, Mtafiti aliwashirikisha wanafunzi katika mijadala mifupi ya kimakundi iliyoongozwa na maswali yaliyokuwa yametayarishwa awali. Mijadala hii ilihusu mada mbalimbali katika lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ikilenga kuibua data

zaidi kuhusu ujuzi wao wa kijumla wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 6.4.1 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Wahojiwa waliounda sampuli ya utafiti huu walipewa mazoezi mbalimbali ili kupima viwango vyao vya umilisi katika lugha ya Kikuyu kila zoezi likiwa na jumla ya alama ishirini. Matokeo yalionyesha kuwa vijana kutoka jamii ya Kikuyu katika miji husika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kuongea, kusoma na kuandika. Hii ni kwa sababu katika stadi hizi tatu za lugha, wahojiwa wote walipata alama za chini kutoka kwa asilimia 20. Katika stadi ya kuandika alama ya kati ilikuwa 5 huku alama ya chini zaidi ikiwa 4 na juu zaidi ikiwa 10 (taz. jedwali 40). Katika stadi za kusoma na kuongea alama ya kati ilikuwa 5 huku alama ya chini zaidi ikiwa 4 na ya juu zaidi ikiwa 8 (taz. jedwali 41). Aidha, katika stadi ya kuongea kwa Kikuyu, alama ya kati ilikuwa 5, alama ya chini zaidi ikiwa 4 na ya juu zaidi ikiwa 8 (taz. jedwali 42).

Kutokana na matokeo haya, utafiti huu uliweza kubaini kuwa hata ingawa wahojiwa wote walioshiriki katika sampuli ya utafiti huu walikuwa kutoka jamii ya Kikuyu, umilisi wao wa kiisimu wa lugha ya Kikuyu kwa jumla ni wa viwango vya chini mno. Kama aelezavyo Verhoeven (1992:22) “umilisi wa kiisimu hurejelea ule uwezo wa mzungumzaji wa kuweza kutumia sheria mbalimbali za lugha husika kuunda maneno na sentensi sahihi na zenye maana jambo linalomwezesha kushiriki vyema katika mawasilano kwa ile lugha”. Vipengele vya umilisi wa kiisimu wa lugha kwa mujibu wa

Rubin (1992) ni kama vile uwezo wa mzungumzaji wa kuunda na kutambua miundo ya sentensi sahihi na isiyo sahihi katika lugha husika (sintaksia), kufahamu msamiati mbalimbali wa lugha (leksimu), kuwa na matamshi bora (fonolojia) na kufahamu maana ya maneno (semantiki).

Matokeo ya utafiti huu yaliweza kubaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana matatizo mbalimbali katika stadi za kuongea, kusoma na kuandika kwa Kikuyu. Matatizo yaliyogunduliwa miongoni mwa vijana hawa katika lugha ya Kikuyu katika stadi za kusoma na kuongea ni kama vile kuongea kwa kusita sita kutokana na ukosefu wa msamiati wa kutosha wa lugha ya Kikuyu, matamshi mabaya ya baadhi ya maneno ya Kikuyu kutokana na athari za lugha ya Kiswahili, kushindwa kuyatamka kabisa baadhi ya maneno ya Kikuyu, kulemewa na kuzisoma na kuzitamka baadhi ya irabu za Kikuyu na kuongea lugha ya Kikuyu kwa kiimbo kibaya kana kwamba wanasoma kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

Katika stadi ya kuandika kwa Kikuyu, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walitatizika zaidi katika kuziandika irabu na konsonanti za Kikuyu kwa vile hawafahamiani vyema nazo hasa zile zinazoandikwa kwa namna tofauti na zile za Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano wengi wa wahojiwa waliiandika na kuitamka irabu *u* ya Kikuyu kama irabu *o* ya Kiswahili na kwa hivyo kuyasoma na kuyaandika maneno ya Kikuyu yaliyo na irabu *u* visivyo kwa mfano *oka* badala ya *uka* (njoo), *ora* badala ya *ura* (toroka) n.k. Pia stadi ya uandi- shi kwa lugha ya Kikuyu ilikubwa na matatizo mengi

ya uendelezaji wa maneno kwani kwa vijana wengi wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika, msamiati wa lugha ya Kikuyu ni mgeni sana kwao.

### 6.4.2 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kiswahili Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Vile vile, mtafiti aliwapa wahojiwa mazoezi mbalimbali ili kubaini viwango vyao vya umilisi wa lugha ya Kiswahili katika stadi za kusoma, kuandika na kuongea. Matokeo ya mazoezi haya yalionyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wahojiwa wote walipata alama za juu katika stadi za kusoma, kuandika na kuongea kwa Kiswahili. Katika stadi ya kuandika kwa Kiswahili alama ya kati ilikuwa 15 huku alama ya chini zaidi kati ya wahojiwa 300 ikiwa 12 na ya juu zaidi ikiwa 18 (taz. jedwali 43). Alama ya kati katika stadi ya kusoma ilikuwa 14 nayo alama ya chini zaidi ikiwa 12 huku ile ya juu zaidi ikiwa alama 18 (taz. jedwali 44). Hatimaye, katika stadi ya kuongea kwa Kiswahili, alama ya kati ilikuwa 14, alama ya chini zaidi 11 na alama ya juu zaidi ikiwa 17.

Kwa jumla, viwango vya umilisi wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu miji husika vilikuwa vya juu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa hii ni mojawapo wa lugha ambazo zinatumiwa kwa wingi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika maswasiliano yao ya kila siku katika maeneo kama vile shuleni na nyumbani na kwa hivyo wameitumia katika kuwasiliana kwa muda mrefu. Kama aelezavyo Muaka (2011) Kiswahili ni lugha ya kiasili nchini Kenya ambayo imekua na kusambaa kimatumizi hadi kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya mbali na

ukweli kuwa lugha ya Kiswahili pia ni lugha ya Kimataifa. Aidha, kama ilivyodhihirika kwingineko katika utafiti huu (taz. sura ya 5), vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji husika wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiswahili kwa jumla. Mwelekeo wao chanya kuhusu Kiswahili ni sababu moja iliyochangia vijana hawa kuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (2005) mielekeo ya lugha huwa na athari za moja kwa moja kwa umilisi wa lugha husika. Hii ina maana kuwa jinsi wazungumzaji walivyo na mwelekeo chanya kuhusu lugha yao, ndiyvo walivyo na viwango vya juu vya umilisi wa lugha hiyo.

### 6.4.3 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kiingereza Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Kuhusu umilisi wa lugha ya Kiingereza, utafiti huu uliweza kubaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa ni viwango vya juu vya umilisi wa lugha hii. Haya yalibainishwa wazi na alama za juu ambazo vijana hawa walizipata katika mazoezi waliopewa ya kupima umilisi wao wa Kiingereza katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea.

Katika stadi ya kuandika kwa Kiingereza alama ya kati ilikuwa 14 huku alama ya chini zaidi ikiwa 13 na ya juu zaidi ikiwa 16 (taz. jedwali 46). Nayo alama ya kati katika stadi ya kusoma kwa Kiingereza ilikuwa 12 wakati alama ya chini ikiwa 12 huku alama ya juu zaidi ikiwa 18 (taz. jedwali 47). Hatimaye katika stadi ya kuongea kwa Kiingereza, alama ya kati ilikuwa 15, alama ya chini mno ikiwa 12 na ile ya juu zaidi ikiwa alama 17 (taz. jedwali 48).

Kutokana na matokeo haya inabainika wazi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana umilisi wa kiisimu wa viwango vya juu wa lugha ya Kiingereza katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea. Hali hii inatokana na ukweli kuwa vijana hawa wana mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza kwa vile wanaiona lugha hii kuwa na faida na umuhimu mwingi kwao maishani. Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana imani kuwa lugha ya Kiingereza itawasaidia kupata kazi baada ya shule na kuwa mtu anayeifahamu vyema lugha ya Kiingereza huwa na hadhi ya juu katika jamii (taz. jedwali 23).

Aidha, lugha ya Kiingereza ni lugha mojawapo inayofundishwa shuleni na pia inayotumiwa kama lugha ya kufundishia. Basi umuhimu mwingi uliopewa lugha ya Kiingereza shuleni na nyumbani ulibainika kuwa umechangia pakubwa katika kuwafanya vijana hawa kuwa na mielekeo chanya kuhusu Kiingereza hali inayowafanya hatimaye kuwa na umilisi wa viwango vya juu vya Kiingereza.

### 6.4.4 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Hatimaye, Utafiti huu uliweza kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Utafiti huu ulibaini kuwa vijana hawa walikuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi ya kuongea pekee huku vijana wawa hawa wakiwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi za kusoma na kuandika. Katika stadi ya kuandika kwa Sheng, alama ya kati ilikuwa 12 huku alama ya chini ikiwa 9 na ya juu ikiwa 14 (taz.

jedwali 49). Alama ya kati katika stadi ya kusoma kwa Sheng ilikuwa 12, alama ya chini ikiwa 9 na alama ya juu ikiwa 15 (taz. jedwali 50). Hata hivyo, katika stadi ya kuongea kwa Sheng, alama ya kati ilikuwa 16 huku alama ya chini ikiwa 14 na alama ya juu ikiwa 18.

Sababu kuu ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ya kuwa na umilisi wa viwango vya juu katika stadi ya kuongea kwa Sheng ilhali wana umilisi wa viwango vya chini katika stadi ya kuandika na kusoma inaelezewa vyema na majibu ya kijana mmoja aliyeshiriki katika mjadala wa kimakundi na aliyekuwa na maoni yafuatayo:-

Mhojiwa II: ***Lugha ya Sheng haifundishwi shuleni na pia huwa hata imepigwa marufuku. Kwa hivyo hatupati fursa ya kujua jinsi ya kuandika na kusoma Sheng kama vile tunavyofundishwa Kiingereza na Kiswahili shuleni. Hata hivyo hii ndiyo lugha ambayo sisi vijana hutumia kwa wingi tunapowasiliana kati yetu tukiwa nyumbani hapa mjini na kwa hivyo tunajua jinsi ya kuizungumza Sheng kutoka kwa vijana wengine wenzetu mtaani bila ya kufundishwa na yeyote.***

(Taz. Kiambatisho V )

Kutokana na maoni kama haya, inabainika wazi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika hujihusisha na matumizi ya Sheng kwa wingi katika kiwango cha kuongea bali sio katika kiwango cha kuandika na kusoma. Hii ndiyo sababu kuu inayopelekea vijana hawa kuwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi ya Kuongea ikilinganishwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Sheng katika stadi ya kuandika na kusoma.

### 6.4.5 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kubaini viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ikilinganishwa na viwango vyao vya umilisi wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Katika kulinganisha viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu na viwango vya umilisi wa Kiswahili, Kiingereza na Sheng, utafiti huu ulibaini kuwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng ndizo hutumika kwa wingi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika katika shughuli zao nyingi shuleni na nyumbani.

Hali hii huwanyima vijana hawa fursa ya kutumia lugha ya Kikuyu katika shughuli zao mbalimbali na hii ndiyo mojawapo wa sababu zinazowafanya wawe na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea. Haya ni wazi katika maelezo yafuatayo ya wahojiwa:-

**Mtafiti:** ***Ni kwa nini nyinyi vijana mijini hamfahamu vyema lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng?***

**Mhojiwa I:** ***Hatupati fursa kamwe ya kuongea wala kujifunza lugha ya Kikuyu hapa mijini. Hii ni kwa sababu lugha hii haitumiki shuleni na hakika huwa ni kinyume cha sheria za shule kwa mwanafunzi kuzungumza kwa Kikuyu ama lugha nyingine ya mama shuleni. Pia tukiwa nyumbani mara nyingi sisi hutumia lugha ya sheng kuwasiliana.***

**Mhojiwa II:** ***Pia sisi vijana hatupati fursa ya kutembea mashambani mara kwa mara na tunapoenda mashambani huwa ni kwa muda mfupi tu. Basi huwa hatupati wakati wa kuingiliana na vijana wenzetu vijijni ambao wangetusaidia kuifahamu lugha ya Kikuyu.***

(Taz. Kiambatisho V)

Aidha, mbali na kukosa fursa ya kujifunza na kuitumia lugha ya Kikuyu, utafiti huu ulibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng kutokana na mielekeo yao kuhusu lugha hizi nne. Vijana hawa kwa kiwango kikubwa wana mwelekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu jambo linalowafanya wasione umuhimu wa kukifahamu Kikuyu. Vijana wengi wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika huiona lugha ya Kikuyu kama lugha ya kueneza ukabila, lugha iliyopitwa na wakati, lugha ambayo haina faida kielimu na ambayo haimsaidii mtu kupata kazi za kitaaluma baada ya kumaliza shule (taz. jedwali 21).

Utafiti huu basi uliweza kubaini kuwa viwango vya umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni vya chini ikilinganishwa na viwango vya umilisi wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hii ina maana kuwa kuna athari za moja kwa moja za matumizi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Hali hii pia inaashiria kuwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana hawa mijini ni wa kiwango cha chini.

### 6.5 Viwango vya uthabiti wa Kiisimujamii na hali ya Kijumla ya Kiisimujamii ya Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Utafiti huu ulibaini mambo matatu makuu kuhusu maswali matatu ya kwanza ya utafiti huu. Mambo haya ni:-

i) Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi

kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na mielekeo yao chanya kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

ii) Vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na viwango vya juu vya umilisi wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

iii) Vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapendelei kuitumia lugha ya Kikuyu katika maeneo mengi ya kijamii ya matumizi ya lugha kama vile nyumbani na shuleni bali wao hupendelea zaidi kuzitumia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Kutokana na matokeo haya, inabainika kuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha nyingine ambazo ni Kiingereza na Sheng yana athari mbalimbali kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Kwanza, matumizi ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng yamepelekea vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu. Hii ni kwa sababu, kama ilivyobainika katika utafiti, lugha ya Kikuyu haitumiki na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini katika utekelezaji wa shughuli muhimu za kijamii kama vile elimu, kupata kazi baada ya shule, kuendesha biashara, kuwasiliana baina ya vijana na wazazi wao na baina yao na wenzao.

Pili, matumizi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika maeneo muhimu ya kijamii kama vile nyumbani na shuleni yamepelekea matumizi ya lugha ya Kikuyu katika maeneo haya kuwa ya kiwango cha chini miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Shuleni, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hutumia lugha za Kiingereza na Kiswahili ambazo ndizo lugha zilizohalalishwa kutumiwa. Lugha ya Kikuyu huwa imepigwa marufuku shuleni na kwa hivyo vijana hawa hawapati nafasi nzuri ya kutumia lugha hii. Katika eneo la nyumbani lugha zinazotumiwa kwa wingi na vijana wa jamii ya Kikuyu mijini katika mawasiliano yao na watu mbalimbali ni lugha za Sheng, Kiswahili na Kiingereza. Matumizi ya Kikuyu katika mazingira ya nyumbani ni finyu sana kama utafiti huu ulivyobainisha.

Tatu, hali ya kuwa na mielekeo hasi kuhusu Kikuyu na kule kufifia kwa matumizi ya lugha ya Kikuyu katika maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha, inapelekea vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji ya Nairobi, Kiambu na Thika kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu. Vijana hawa, kama utafiti huu ulivyobainisha wana matatizo tele katika kusoma, kuandika na kuongea kwa Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Basi inatokea kuwa mielekeo chanya kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng na vile vile matumizi ya kiwango cha juu ya lugha hizi tatu katika maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha kuna athari za moja kwa moja kwa umilisi wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini.

Nne, utafiti huu ulionyesha kuwa athari nyingine ya matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng mijini Nairobi, Kiambu na Thika yameibua mpangilio

mpya wa matumizi ya lugha hizi miongoni mwa vijana. Awali, kama walivyoelezea Mkilifi (1972) na Batibo (2005) mataifa mengi ya Kiafrika yana mpangilio wa kitriglosia katika matumizi yake ya lugha. Lugha za kikoloni kama vile Kiingereza huwa na hadhi ya juu na hutekeleza majukumu rasmi kama vile shughuli za kielimu na kiserikali. Kati kati kuna lugha za kiasili za matumizi mapana kama vile Kiswahili na chini kabisa katika mpangilio huu ni lugha za mama kama vile Kikuyu. Inatokea kuwa miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini lugha ya Kikuyu ambayo ni lugha yao ya kijamii (mama) inatoweka katika mpagilio huu wa kitriglosia na nafasi yake kuchukuliwa na lugha ya Sheng. Basi mpangilio mpya wa kitriglosia miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika unahusisha lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika hali ya mpishano huru kutegemea miktadha tofauti ya matumizi ya lugha hizi tatu.

Hatimaye, utafiti huu ulibaini kuwa hali ya kijumla ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu ni kuwa hata ingawa lugha hii ndiyo lugha yenye wazungumzaji wengi zaidi nchini Kenya, viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii vinaendelea kushuka miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha wa lugha yoyote ile ni ishara ya kuonyesha kuwa lugha hiyo imeanza kuingia katika mkondo wa kuangamia pindi miaka inavyoendelea kupita. Jambo hili lafaa kuangaliwa kwa makini kwani kama asemavyo Brenzinger (1992), sio lugha ndogo tu ulimwenguni ambazo zimo katika hatari ya kuangamia kama yalivyo makisio ya wengi. Hata baadhi ya lugha kubwa ulimwenguni pia zimo katika viwango mbalimbali vya kuangamia sio kutokana na uhaba wa wazungumzaji, bali

kutokana na sababu nyingine kama vile kuathiriwa na mtagusano wake na lugha nyingine katika jamii zinazosababisha kushuka kwa uthabiti wake wa kiisimujamii.

**6.6 Hitimisho**

Sura hii ilihusu mijadala kutokana na data ya kijarabati iliyowasilishwa katika sura ya 5. Aidha, sura hii ilihusisha mijadala kutokana na data ya kimaelezo ambayo ilikusanywa kupitia mijadala ya kimakundi iliyohusisha vijana kutoka jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Data zote mbili (kijarabati na kimaelezo) zilijadiliwa kwa pamoja kwa kufuata mpangilio sambamba wa mbinu changamano ya utafiti (taz. mchoro 6) ambapo data ya kijarabati na kimaelezo hujadiliwa na kufasiriwa kwa pamoja ili kupata matokeo ya utafiti (Creswell 2011). Mijadala ya data ya kijarabati na kimaelezo iliendeshwa kwa kuzingatia vigezo vya nadharia za utafiti huu ambazo ni nadharia ya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha (Landweer 2000) na nadharia ya vitendo vilivyofikiriwa na vitendo vilivyopangwa (Fishbein na Ajzen 1975, 2005).

Data ya kijarabati na kimaelezo ilidhihirisha wazi hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ambapo ilibainika wazi kuwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu ni vya chini ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Ilitokea wazi kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapendelei kuzungumza kwa lugha ya Kikuyu bali wao hupendelea matumizi ya lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Sura hii ya sita ilianza kwa kuangazia suala la mielekeo waliyo nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika. Mijadala kutokana na data ya kijarabati na kimaelezo ilibaini kuwa vijana hawa kwa jumla wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Pili, sura hii iliangazia suala la umilisi wa lugha ya Kikuyu kupitia stadi za kusoma, kuandika na kuongea. Ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu katika miji hii mitatu wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na viwango vyao vya umilisi wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Aidha, sura hii ilibaini kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni kidogo sana katika maeneo mbalimbali ya kijamii kama vile shuleni na nyumbani. Hatimaye, sura hii ilitalii kuhusu hali ya kijumla ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miononi mwa vijana wa jamii ya Kikuyu na kubaini kuwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana hawa mijini ni wa viwango vya chini ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

# SURA YA SABA

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii ni muhtasari wa utafiti mzima kwanzia sura ya kwanza hadi ya mwisho. Vile vile, matokeo ya utafiti huu yametolewa kwa kifupi kupitia ugunduzi mbalimbali ambao umepatikana baada ya kuchunguza kwa kina kila lengo la utafiti huu kwa kuzingatia msingi ya nadharia za utafiti. Hatimaye, sura hii imetoa mapendekezo mbalimbali ambayo yakitekelezwa yatasaidia katika kuinua viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama kama vile Kikuyu nchini Kenya na basi kuziepusha na hatari ya kuingia katika orodha ya lugha duniani zilizoanza kuangamia pole pole pindi miaka inavyopita.

### 7.2 Muhtasari wa Kila Sura

Lengo la jumla la uafiti huu lilikuwa kuchunguza hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa kubaini viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii ikililinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Haya yalifanywa kwa kuzingatia vigezo vya nadharia zilizouongoza utafiti huu hasa nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha (Landweer 2000). Utafiti huu umegawika katika sura saba.

Sura ya kwanza inatoa maelezo kuhusu usuli wa utafiti huu kwa jumla ambapo suala la mtagusano wa lugha na baadhi ya athari zake zimefafanuliwa. Sura hii pia imeweka wazi masuala mengine muhimu kama vile suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na mipaka na upeo wa utafiti. Hatimye, sura hii inamalizika

kwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu nadharia zinazouongoza utafiti huu ambazo ni nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha (Landweer 2000) na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa (Fishbein na Ajzen 1975, 2005).

Sura ya pili imejihusisha na maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti huu. Masuala haya ni kama vile maelezo kuhusu asili na historia fupi ya lugha ya Kikuyu na tafiti mbalimbali za kijumla ambazo tayari zimefanywa kuhusu lugha hii. Pia, kuna mapitio ya tafiti ambazo zinazungumzia kuhusu uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu ambalo ndilo suala liloangaziwa kwa kina katika utafiti huu na hasa athari za Kiswahili na lugha nyingine kama vile Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Sura hii pia imelishughulikia suala la mielekeo ya lugha, jinsi ya kuipima mielekeo ya lugha kupitia vipimo vya moja kwa moja na visivyo vya moja kwa moja na maelezo ya tafiti mbalimbali kuhusu mielekeo ya lugha barani Afrika. Zaidi, suala la umilisi wa lugha na umilisi wa mawasiliano limejadiliwa katika sura hii na jinsi ya kupima umilisi wa lugha miongoni mwa wazungumzaji kupitia mitihani ya kupima umilisi wa lugha ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja.

Katika sura ya pili vile vile kuna maelezo kuhusu dhana ya vijana na jinsi mashirika na nchi mbalimbali ulimwenguni zinavyofafanua kizazi cha vijana kupitia vigezo mbalimbali kama vile umri, kijamii (kitamaduni), kisheria, kiuchumi na kisaikolojia (taz sehemu 2.6.1). Kuhusu vijana, sura hii pia ina maelezo kuhusu matumizi yao ya lugha

hasa katika sehemu za mijini barani Afrika na nchini Kenya. Aidha, sura hii imetoa maelezo ya kijumla ya kiisimujamii ya lugha nchini Kenya kwa kuangazia ruwaza za matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng nchini Kenya na mielekeo ya kijumla iliyoambatanishwa na lugha hizi nne. Suala la matumizi ya lugha za mama ikiwemo Kikuyu katika miktadha ya wingilugha pia limejadiliwa katika sura hii.

Katika sura ya tatu, masuala yaliyofafanuliwa yalihusu maelezo juu ya dhana ya lugha ya mama kupitia masuala kama vile asili na maana ya lugha ya mama na manufaa ya lugha za mama. Utafiti huu ulijadili kuhusu lugha za mama kama lugha zilizotengewa jukumu la mawasiliano na wanajamii mashinani ama vijijini katika taifa ambalo bila shaka lina matumizi ya lugha nyingine katika viwango vingine kama vile kiwango cha kitaifa na kimataifa. Masuala mengine yaliyofafanuliwa katika sura hii ni yale ya kinadharia yanayohusiana na uthabiti wa lugha za mama kwa jumla na juhudi za uimarishaji wa lugha za mama kupitia elimu katika nchi mbalimbali ulimwenguni. Aidha suala la matumizi ya lugha za mama katika mazingira ya wingilugha limejadiliwa katika sura hii na hasa mipagilio ya matumizi ya lugha ya diglosia na triglosia.

Sura ya nne ina maelezo kuhusu mbinu za utafiti zilizotumiwa katika utafiti huu. Kwa jumla utafiti huu ni wa kisoroveya. Muundo wa kisoroveya ni utaratibu wa kukusanya data kwa kutumia hojaji ama mahojiano kutoka kwa sampuli ili kupata data inayomwezesha mtafiti kuelezea mielekeo, maoni, tabia na sifa za jumuiya nzima kwa kutumia data inayotokana na sampuli iliyoteuliwa.

Utafiti huu ulitumia mbinu changamano ya utafiti ambao ni mtindo wa kukusanya na kuchanganua data kwa kuchanganya mbinu za kijarabati na kimaelezo katika utafiti mmoja ili kuelewa suala la utafiti vyema zaidi. Aidha, maelezo mengine katika sura hii yalihusu mahala pa utafiti, jumuiya lengwa, uteuzi wa sampuli na idadi ya sampuli. Maelezo mengine yalihusu vifaa vya utafiti, utafiti awali, mbinu za kukusanya data na hatimaye suala la uchanganuzi wa data.

Kwenye sura ya tano uwasilishaji wa data iliyokusanywa nyanjani kwa kutumia vifaa vya ukusanyaji data umefanywa. Vifaa hivi ni kama vile hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha, mitihani ya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng na hojaji kuhusu maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha. Data hii ilikusanywa kutokana na sampuli ya vijana wa jamii ya Kikuyu wanaoishi katika miji ya Nairobi, Thika na Kiambu katika kaunti za Nairobi na Thika. Hojaji ya mielekeo na matumizi ya lugha ilitumiwa ili kukusanya data muhimu ambayo ilionyesha mielekeo ambayo wahojiwa walikuwa nayo kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

Jambo lingine lililoangaziwa katika sura hii ni la umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Haya yalifanywa kupitia stadi za kuandika, kusoma na kuongea ili kupima viwango vya umilisi wa lugha hizi miongoni mwa vijana katika miji hii mitatu. Hatimaye, sura hii iliwasilisha data kuhusu maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa

jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika. Maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha yaliyozingatiwa katika sura hii ni yale ya shuleni na nyumbani katika miktadha mbalimbali. Data kutokana na hojaji ya matumizi na mielekeo ya lugha, mitihani ya umilisi wa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng na maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha iliwasilishwa kwa njia ya kijarabati kupitia majedwali na histogramu.

Sura ya sita ya utafiti huu ilijikita katika mijadala iliyotokana na data ya kijarabati na kimaelezo (iliyotokana na mijadala ya kimakundi) lengo kuu likiwa kuweka wazi matokeo ya utafiti huu. Katika sura hii, mijadala iliongozwa na malengo na maswali ya utafiti huu na mihimili ya nadharia za utafiti ambazo ni nadharia ya Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha na nadharia ya Vitendo Vilivyofikiriwa na Vitendo Vilivyopangwa. Sura hii ilianza kwa kujadili mielekeo ya vijana mijini kuhusu lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu uliweza kubaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii kama vile elimu, kupata kazi za kitaaluma baada ya shule, kuzungumza na wazazi na kuzungumza na wenzao. Hata hivyo vijana hawa walikuwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya kuhifadhi na kueneza utamaduni na historia ya jamii ya Wakikuyu.

Suala lingine katika sura hii lilihusu umilisi wa lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.

Ilibainika kuwa vijana hawa wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kusoma, kuandika na kuongea ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Aidha, suala la mwisho katika sura hii lilihusu maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha. Maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha yaliyoangaziwa katika sura hii ni yale ya shuleni na nyumbani. Ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawatumii lugha ya Kikuyu katika maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha ya shuleni na nyumbani bali wao huzitumia kwa wingi lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika miktadha tofauti ya matumizi ya lugha. Hatimaye katika sura ya saba kuna muhtasari sura zote za utafiti huu na muhtasari wa matokeo ya utafiti na mapendekezo.

**7.3 Hitimisho**

Utafiti huu kama inavyoonyeshwa katika sura ya kwanza sehemu ya 1.3.1 ulilenga kuchunguza na kubainisha mielekeo ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng na kubaini maeneo ya kijamii ambamo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hupendelea kutumia lugha za Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Aidha, utafiti huu ulilenga kubaini viwango vya umilisi wa Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu waishio mijini ikilinganishwa na Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hatimaye lengo la mwisho lilikuwa kuchunguza athari za Kiswahili na lugha nyingine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu na hivyo kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana Wakikuyu mijini Nairobi,

Kiambu na Thika. Matokeo ya malengo haya yametolewa katika sehemu zinazofuata za 7.3.1 hadi 7.3.4.

### 7.3.1 Mielekeo ya Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini kuhusu Lugha ya Kikuyu.

Kwa kurejelea lengo la kwanza la utafiti huu lililohusu mielekeo ya lugha, ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika kwa jumla wana mielekeo hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Katika kubaini mielekeo ya vijana mijini kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, utafiti huu ulitumia hojaji ya mielekeo na matumizi ya lugha.

Shughuli moja ya kijamii ilikuwa kupata elimu shuleni ambapo lugha ya Kikuyu ilionekana kutotumika shuleni rasmi isipokuwa katika miktadha michache isiyo rasmi. Katika shule zote zilizohusishwa katika jumuiya ya utafiti huu, kulikuwa na sera za matumizi ya lugha ambapo lugha zilizoteuliwa kutumiwa rasmi shuleni zilikuwa Kiingereza na Kiswahili huku lugha ya Kikuyu na Sheng zikiwa zimepigwa marufuku. Hata hivyo, utafiti huu pia ulibaini kuwa bado lugha ya Kikuyu ilikuwa ikitumiwa na vijana shuleni kwa viwango vya chini na kwa njia isiyo halali hasa wakati walipokuwa wakiwasiliana na wafanyakazi wengine shuleni. Hali ya kupigwa marufuku kwa lugha ya Kikuyu na kule kuhimizwa kwa matumizi ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili shuleni kulichangia vijana kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kama lugha ya

kujipatia masomo huku wakiwa na mielekeo chanya kuhusu lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

Katika shughuli nyingine kama vile biashara, kupata kazi za kitaaluma baada ya masomo na kuzungumza na wazazi na watu wazima, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini vile vile walionekana kupendelea matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza huku tena lugha ya Kikuyu ikikosa nafasi muhimu katika utekelezaji wa shughuli hizi. Lugha ya sheng nayo ndiyo iliyopendelewa zaidi na vijana hawa katika shughuli kufanya urafiki na kuzungumza baina yao ikifuatwa na lugha za Kiswahili na Kiingereza. Hapa pia lugha ya Kikuyu ilionekana kutengwa na vijana wa jamii ya Kikuyu katika kufanya urafiki na mazungumzo kati yao.

Kutotumiwa kwa lugha ya Kikuyu katika shughuli muhimu za kijamii kama hizi kulitoa ishara tosha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hali hii ya kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana hawa inathibitishwa zaidi na sababu mbalimabali walizozitoa za kutoitumia lugha ya Kikuyu. Sababu walizozitoa ni kama vile lugha ya Kikuyu huwa haitumiki katika maeneo mengi ya kijamii kama vile shuleni, ni lugha ambayo hueneza ukabila, imepitwa na wakati kwani kuna lugha nyingine za kisasa kama vile Sheng, haimsaidii mtu kupata kazi za kitaaluma baada ya shule na kuwa hata wazazi wao hawaitumii kwa wingi na kwa hivyo hawakupata fursa ya kujifunza lugha hii.

Hata ingawa utafiti huu ulionyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu kwa jumla, jambo la kutia moyo ni kuwa vijana hawa wanafahamu kuwa lugha ya Kikuyu ni muhimu katika kuhifadhi na kueneza utamaduni na historia ya jamii yao ya Kikuyu. Zaidi, vijana hawa walionyesha moyo wa kutaka kujifunza na kuifahamu lugha ya Kikuyu ili waweze kuwasiliana na babu na nyanya zao na vijana wenzao wanapozuru sehemu za mashambani.

### 7.3.2 Viwango vya Umilisi wa Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu.

Katika kuchunguza kuhusu lengo la pili la utafiti huu, ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wana viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea ikilinganishwa na lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Mitihani ya kupima umilisi katika stadi ya kusoma, kuandika na kuongea ilitumiwa kila mtihani ukiwa na jumla ya alama 20. Uandishi wa insha fupi katika lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ulitumiwa ili kupima umilisi wa lugha hizi nne katika stadi ya kuandika. Vifungu vya ufahamu navyo vilitumiwa kupima stadi ya kusoma katika lugha hizi nne. Aidha, vijana hawa waliulizwa watambe hadhithi fupi fupi kwa wenzao ili kupima viwango vyao vya umilisi wa lugha hizi katika stadi ya kuongea.

Matokeo ya mitihani hii yalibaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika walikuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu. Hii ni

kutokana na ukweli kuwa walipata alama za chini sana katika stadi za kuandika, kusoma na kuongea ikilinganishwa na alama walizozipata katika lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Katika stadi hizi tatu za lugha vijana wote waliofanya mazoezi ya kupima umilisi wao wa lugha ya Kikuyu walipata alama 5 kama alama ya wastani huku alama za wastani katika lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng zikiwa kati ya 12 na 15. Inatokea kuwa mielekeo walio nayo vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika ndiyo inachangia vijana hawa kuwa na umilisi wa viwango vya chini katika lugha ya Kikuyu kwa vile hawaitumii lugha hii kwa wingi katika mawasiliano yao.

### 7.3.3 Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini.

Baada ya kuchunguza kuhusu lengo la tatu la utafiti huu, ilibainika kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawapendelei kutumia lugha ya Kikuyu katika maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha bali wao hupendelea kuzitumia lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Maeneo ya kijamii ya matumizi ya lugha yaliyotiliwa umuhimu hapa ni yale ya nyumbani na shuleni ambapo tulichunguza lugha zilizotumiwa katika maeneo haya katika miktadha tofauti.

Utafiti huu ulionyesha kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini hutumia lugha za Kiingereza na Kiswahili kwa wingi (asilimia 98) shuleni wakiwa darasani wakati wa masomo kwa vile hizi ndizo lugha rasmi katika muktadha ule. Lugha ya Kikuyu haitumiki kamwe pale darasani. Nje ya darasa, utafiti huu ulibaini kuwa asilimia 98 ya vijana hawa hutumia lugha za Sheng, Kiswahili na Kiingereza. Ni asilimia 2 tu ya vijana hawa iliyotumia lugha ya Kikuyu katika mawasiliano baina yao nje ya darasa huku

asilimia 16 ya vijana ikitumia Kikuyu kuwasiliana na wafanyakazi wa shule. Utafiti huu pia ulionyesha kuwa hali ilikuwa kama hii tu katika eneo la matumizi ya lugha la nyumbani ambapo idadi kubwa ya vijana walipendelea kuzitumia lugha za Sheng, Kiswahili na Kiingereza kuwasilana baina yao na baina yao na watu wazima. Hali hii vile vile inachangia kwa njia ya moja kwa moja hali ya vijana hawa kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na viwango vyao vya umilisi wa lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng.

### 7.3.4 Hali ya Kiisimujamii ya Lugha ya Kikuyu Miongoni mwa Vijana wa Jamii ya Kikuyu Mijini.

Hatimaye, utafiti huu ulibaini kuwa hali ya kijumla ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu ni kuwa hata ingawa lugha hii ndiyo lugha yenye wazungumzaji wengi zaidi nchini Kenya, viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii vinaendelea kushuka miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika.  Kushuka kwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha yoyote ile ni ishara ya kuonyesha kuwa lugha hiyo imeanza kuingia katika mkondo wa kuangamia pindi miaka inavyoendelea kupita.

## 7.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu kuwa viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika ni vya chini ikilinganishwa na lugha nyingine wanazozitumia kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng, utafiti huu unatoa mapendekezo mbalimbali ili kubadili hali hii. Mapendekezo haya yote yamelengwa kuweka mikakati kabambe ya kuinua na kudumisha

uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama kama vile Kikuyu miongoni mwa vijana mijini.

### 7.4.1 Uimarishaji wa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha.

Uimarishaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kitendo cha kurudishia lugha uthabiti wake wa kiisimujamii ambao huenda umepunguka ama unaendelea kupunguka (Ngure 2012). Aidha, kama asemavyo Obiero (2010), uimarishaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni kitendo cha kimakusudi cha kuzuia uhamaji wa lugha ama hata utowekaji wa lugha. Obiero anazidi kueleza kuwa uimarishaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ni shughuli ambayo huhusisha wadau mbalimbali kama vile serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, jamii husika na wanaisimujamii.

Shughuli zozote za uimarishaji wa lugha huanza tu baada ya kutambulisha hali ya kiisimujamii ya lugha husika kwa kuchunguza viwango vyake vya uthabiti wa kiisimujamii kama ilivyofanywa katika utafiti huu. Utafiti wetu ulilenga kubaini hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu. Kufikia mwisho wa utafiti huu tuliweza kubaini kuwa hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Thika, Kiambu na Thika si imara. Hii ni kutokana na mielekeo hasi na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya Kikuyu walivyo navyo vijana hawa. Kwa mujibu wa Obiero (2010) shughuli zote za uimarishaji wa lugha huanza kwa shughuli ya kubaini viwango vya uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika.

### 7.4.2 Juhudi za Uimarishaji wa Uthabiti wa Kiisimujamii wa Lugha.

Kama ilivyobainika katika sura za tano na sita za utafiti huu, hali ya kiisimujamii ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika sio imara kutokana na athari za lugha za Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Utafiti huu unatoa mapendekezo kadhaa ya kubadili hali hii. Mapendekezo ya utafiti huu basi ni juhudi za kujaribu kuweka mikakati ambayo inaweza kutekelezwa ili kubadili mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu na pia kuinua viwango vya umilisi wa lugha hii miongoni mwa vijana hawa. Mapendekezo haya ni yafuatayo:-

#### 7.4.2.1 Matumizi ya Lugha ya Kikuyu katika Maeneo ya Kijamii ya Matumizi ya Lugha.

Pendekezo la kwanza la utafiti huu ni kuwa matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika yanafaa kuhimizwa katika maeneo mbalimbali ya kijamii ya matumizi ya lugha. Jambo moja ambalo utafiti huu umebainisha wazi ni kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika hawatumii lugha ya Kikuyu katika maeneo muhimu ya kijamii ya matumizi ya lugha kama vile nyumbani na shuleni bali wao hutumia lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng. Hali hii inachangia wao kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kikuyu na hatimaye kuwa na viwango vya chini vya umilisi wa lugha ya hii.

Eneo moja la kijamii la matumizi ya lugha ambapo matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijni yanafaa kuhimizwa ni eneo la nyumbani. Eneo la nyumbani ni muhimu sana katika kukuza uthabiti wa kiisimujamii wa lugha

yeyote ile. Hii ni kwa sababu hapa ndipo lugha hupokezanwa kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto. Hivyo, iwapo lugha haipitishwi kutoka kwa wazazi hadi kwa watoto pale nuymbani basi uthabiti wake wa kiisimujamii huanza kupotea. Kwa mujibu wa Landweer (2000), eneo la nyumbani ndilo msingi wa maeneo mengine ya kijamii ya lugha yoyote ile kwani ndilo ambalo huhusika na matumizi ya kiwango cha juu cha lugha za mama. Naye Karanja (2012) anaeleza kuwa kutoweka kwa matumizi ya lugha katika eneo la nyumbani ni dalili hakika ya kupungua kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha husika.

Vile vile, matumizi ya lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mjini Nairobi, Kiambu na Thika yanafaa kuhimizwa katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la shuleni. Kama ilivyojitokeza katika utafiti huu, lugha zinazotumiwa kama lugha rasmi za kufundishia shuleni ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha za mama kama vile Kikuyu zimepigwa marufuku jambo ambalo linafanya vijana hawa wasipate fursa ya kuzitumia na kuzifahamu vyema lugha hizi za mama.

Njia moja ya kuimarisha lugha za mama katika eneo la kijamii la matumizi ya lugha la shuleni ni kwa kuzifanya lugha za kufunzia shuleni kama ilivyofafanuliwa kwingineko kwenye utafiti huu (taz sehemu 3.5.1) Shirika la UNESCO (2005), lilizindua kampeni za kuziimarisha lugha za mama ulimwenguni. Tayari nchi kadhaa hapa Afrika kama vile Afrika Kusini, Nigeria na Ethiopia zimeanza kufanya majaribio ya kuzitumia lugha za mama katika ufundishaji. Hata ingawa lugha za mama zafaa kutumia kufundishia katika madarasa ya kwanza matatu nchini Kenya, bado kuna upinzani mkubwa kutoka kwa wadau muhimu katika sekta ya elimu kama vile wazazi na walimu ambao hawaonekani

kuunga mkono juhudi hizi. Basi, lugha za Kiswahili na Kiingereza ndizo bado zinazotumika kwa wingi kufundishia katika madarasa ya kwanza matatu nchini Kenya huku lugha za mama kama vile Kikuyu zikitengwa. Mapendekezo ya utafiti huu ni kuwa Wizara ya Elimu nchini Kenya inafaa kuhimiza utekelezaji kamili wa mafunzo kupitia lugha za mama katika madarasa ya kwanza matatu shuleni ili watoto wapate fursa ya kuzifahamu zaidi lugha zao za mama.

Aidha, lugha za mama kama vile Kikuyu zafaa kuanza kutumiwa kwa dhati katika maeneo mapya ya matumizi ya lugha kama vile katika uwanja wa teknolojia na mawasiliano. Kama asemavyo Sheik (2011) lugha za mama barani Afrika zafaa pia kushirikishwa katika mawasiliano ya kiteknolojia ili zipate maeneo mapya ya kijamii ya kuzitumia. Hatua hii itahakikisha kuwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama nchini Kenya umeanza kuiimarishwa kwa kuzifanya lugha za tarakilishi ili ziweze kutumika katika mtandao kwa wingi iwezekanavyo.

Vyombo vya habari vinavyotumia lugha za mama kama vile Kikuyu vyafaa kuhimiza vijana kuzitilia maanani lugha zao za mama kwa kuanzisha vipindi vya kuvutia vijana na kuwelimisha kuhusu umuhimu wa kuzifahamu lugha zao za mama. Kama ilivyojitokeza katika utafiti huu, japo vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wanafahamu kuhusu idhaa zinazotangaza kwa lugha ya Kikuyu, wengi wao hawapendi kuzisikiliza kwa vile wanavutiwa zaidi na idhaa zinazotangaza kwa Kiswahili,

Kiingereza na hata Sheng. Kwa njia hii lugha hizi zitaanza kupata hadhi ya juu katika jamii na vijana watapata njia mwafaka ya kuzifahamu na kuzitumia kwa wingi.

**7.4.2.2 Uhusiano wa Vijana wa Mijini na jamii za Mashambani.**

Pendekezo lingine la utafiti huu ni kuwa kunafaa kuwa na uhusiano wa karibu kati ya vijana wa mijini na jamii za vijijini. Utafiti huu ulibaini wazi kuwa idadi kubwa ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika huzuru sehemu za mashambani kwa nadra sana. Hali hii huwanyima fursa ya kutangamana na vijana wenzao na wakaazi wengine kule mashambani na hivyo hukosa fursa mwafaka ya kujifunza na kuifahamu vyema lugha ya Kikuyu. Kama asemavyo Landweer (2000), mazingira ya mjini ambako kuna hali ya wingilugha huchangia pakubwa katika uzorotaji wa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha nyingi. Landweer anaendelea kufafanua kuwa lugha zilizo mbali na maeneo ya mijini huwa thabiti zaidi kiisimujamii kuliko lugha zilizo katika mazingira ya mijini ambazo huathiriwa kwa urahisi na lugha nyingine zinazotumika mijini. Maingiliano kama haya ya vijana hawa kutoka mijini na jamii za mashambani basi yatatoa fursa ya kujifunza lugha hii kutoka kwa vijana wenzao mashambani na hata watu wazima wakiwemo akina babu na nyanya.

**7.4.2.3 Miradi ya kufundisha Vijana wa Mijini Lugha ya Kikuyu.**

Katika maingiliano ya vijana wa jamii ya Kikuyu mijini na jamii za Wakikuyu mashambani, kunafaa kuteuliwe baadhi ya wenyeji wa mashambani ambao watapewa jukumu la kufundisha moja kwa moja vijana wa jamii ya Kikuyu kutoka mijini kuhusu masuala mbalimbali ya lugha ya Kikuyu. Wakufunzi hawa wanaweza wakawa vijana

wenzao ambao wanaweza kuwafundisha masuala mbalimbali ya kiisimu kuhusu lugha ya Kikuyu wanapoingiliana kimazungumzo pale mashambani. Vile vile, kunafaa kuwe na wakufunzi wa lugha ya Kikuyu ambao ni watu wazima wanaoweza kuwafunza vijana hawa kuhusu tamaduni mbalimbali za jamii yao ya Wakikuyu na umuhimu wa kuifahamu lugha yao ya mama. Aidha, miradi kama hii ya kuwafunza vijana wa jamii ya Kikuyu kuhusu lugha ya Kikuyu inawezekana pia kuanzishwa mijini ambapo vijana hawa wanaweza kufunzwa kuhusu lugha ya Kikuyu hasa wakati wa likizo. Mbinu hii ya kutumia wakufunzi wa lugha ya Kikuyu yafaa kuandaliwa kwa ushirikiano wa karibu na wadau mbalimbali kama vile wazazi, vyombo vya habari vinavyotangaza kwa Kikuyu, vijana wa jamii ya Kikuyu mijini kati ya wengine.

#### 7.4.2.4 Nafasi ya Serikali za Kaunti katika Kukuza Lugha za Mama.

Serikali za kaunti nchini Kenya zafaa kuwa katika nafasi ya kwanza ya kuhimiza uhifadhi na udumuishaji wa lugha za mama kama vile Kikuyu kwa njia ya moja kwa moja. Hii ni kwa sababu serikali za kaunti ndizo zilizo karibu kiutawala na jamii mbalimbali nchini Kenya ambazo hutumia lugha za mama katika shughuli zao mbalimbali za kila siku. Njia mojawapo ni kama vile kuanzisha sherehe za kitamaduni katika kaunti zote 47 nchini Kenya. Sherehe kama hizi zitatoa fursa mwafaka ya kuelimisha wenyeji, na hasa vijana, wa kaunti hizi kuhusu lugha na tamaduni zao mbalimbali. Aidha, sherehe kama hizi za kijamii zitatumika kama jukwaa la kuhimiza haja ya kuwa na uzalendo wa lugha za mama mbali na kuhimiza matumizi ya kiwango cha juu cha lugha za mama katika kiwango cha kaunti.

Kwa kufanya hivi, lugha za mama zitaanza kupata mielekeo chanya na hadhi ya juu miongoni mwa wanakaunti mbalimbali na uthabiti wa kiisimujamii wa lugha hizi utaimarika. Kama wasemavyo Hinton na Hale (2001), njia mojawapo ya kuimarisha uthabiti wa kiisimujamii wa lugha za mama ni kupitia sherehe za kitamaduni zitakazohusisha nyimbo za kitamaduni, utambaji wa hadithi na maigizo mbalimbali kupitia lugha husika zinazotishiwa na hatari ya kuangamia pindi wakati unavyopita.

Mbali na serikali za kaunti, serikali kuu nchini Kenya nayo vile vile inafaa kutoa ufadhili wa sherehe kama hizi katika kiwango cha kitaifa ili nchi nzima iweze kupata fursa ya kufahamu kuhusu lugha za mama za jamii mbalimbali nchini Kenya. Aidha, serikali kuu inafaa kuhimiza zaidi haja ya vijana kushiriki katika tamasha hizi kupitia mashirika yanayohusika na masuala ya vijana nchini Kenya na wizara husika kama vile Wizara ya Michezo, Utamaduni na Sanaa. Hatua kama hii itasaidia pakubwa katika kuimarisha lugha za mama kama vile Kikuyu nchini Kenya miongoni mwa vijana mijini na hata mashambani.

Utafiti huu umebaini kuwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini Nairobi, Kiambu na Thika wanaichukulia lugha za mama kama vile Kikuyu kuwa lugha ya kikabila na ambazo hutumika kueneza hisia za kikabila. Kwa kukuza uzalendo wa lugha za mama kupitia sherehe za kitamaduni katika kila kaunti, mielekeo hasi kama hii kuhusu lugha za mama ikatoweka na uthabiti wake wa kiisimujamii kuanza kuimarika. Hii ni kwa sababu lugha za mama zitakuwa zimepewa jukumu maalum na muhimu la kutekeleza katika kila kaunti nchini Kenya.

## 7.5 Tamati

Sura hii, mbali na kutoa muhtasari wa kila sura pia imeyajadili masuala mbalimbali ambayo yametokana na utafiti huu. Masuala haya ndiyo yamekuwa matokeo ya utafiti huu. Hatimaye katika sura hii tumetoa mapendekezo ambayo yanafaa kutekelezwa na wadau mbalimbali kama vile serikali kuu, serikali za kaunti, mashirika ya kiutafiti na wanaisimujamii kwa jumla ili kuanzisha juhudi za dhati za kuinua viwango vya uthabiti wa lugha za mama nchini Kenya na kwa kufanya hivyo kuzifanya imara na kuziepusha na hatari yoyote ile ya kuangamia.

**Marejeleo**

Abdulaziz, M.H. (1992) 'Patterns of Language Acquisation and Use in Kenya: Rural-Urban Differences'. In: *International Journal of Sociology of Language* Vol 34 pg 95 – 120.

Abdulaziz, M. H. and K. Osinde (1997) 'Sheng and Engsh: Development of Mixed Codes among the Urban Youth in Kenya'. In: *International Journal of the Sociology of Language* (Sociolinguistic Issues in Sub-Saharan Africa), pp. 45-63.

Adams, A. (1999) 'Language Planning in the European Union and the Republic of South Africa: Parallel Cases?' In: L.Limage (ed.), *Comparative Perspectives on Language and Literacy*. Selected papers from the work of the Language and Literacy Commission of the 10th World Congress of Comparative Education Societies held in Cape Town, 1998 (pp. 533-542). Dakar: UNESCO.

Adegbija, E. (1994) 'Language Attitude in Sub – Saharan Africa: A Sociolinguistic Overview. Clevedon. U.K : Multilingual Matters Ltd.

Afolayan, A. (1976). 'The Six-Year Primary Project in Nigeria'. In: A. Bamgbose (Ed.), *Mother Tongue Education: The West African Experience* (pp. 113-134). London: Hodder and Stoughton.

Allard, R na R. Landry. (1986) 'Subjective Ethnolinguistic Vitality Viewed as a Belief System'. In: *Journal of Multilingual and Multicultural Development* 7(2) 1-12

Ajzen, I. (1991) The theory of Planned Behavior. Organizational Behavior and Human Decision Processes, 50, Prentice-Hall. pp. 179–211.

Ajzen, I. (1985) 'From Intentions to Actions: A Theory of Planned Behavior.' In: J. Kuhl & J. Beckmann (eds.), *Action Control: From Cognition to Behavior*. Berlin, Heidelber, New York: Springer-Verlag.

Ajzen, I. & M. Fishbein. (2005) The Influence of Attitudes on Behavior. In: Albarracin, D, Johnson, B.T na Zanna M.P. (eds.), *The Handbook of Attitudes*, Lawrence Erlbaum Associates.

Ajzen, I. & Fishbein, M. (1980) *Understanding Attitudes and Predicting Social Behavior*. Englewood Cliffs, NJ: Prentice-Hall.

Ajzen, I. & M. Fishbein. (1975) *Belief, Attitude, Intention, and Behavior: An Introduction to Theory and Research*. Reading, MA: Addison-Wesley.

Amatubi, M.N. (2002) 'Globalization and the Mainstreaming of Kiswahili Research in the 21st Century'. In: *Utafiti wa Kiswahili*. Maseno: Maseno University. pp. 43 – 48.

Babusa, H.O. (2010) *Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi Katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya*. Kenyatta University Ph.D Thesis (Unpublished).

Baker, C. (1992) *Attitudes and Language*. Clevedon, England: Multilingual Matter Ltd.

Batibo, H.M. (2005) *Language Decline and Death in Africa: Causes, Consequences and Challenges.* Clevedon, Multilingual Matters.

Best, W.J na J.V Kahn (2010) *Research in Education*, New Jersey U.S.A: Person Prentice

Bosire, M. (2008) *Sheng: The Phonology, Morphology and Social Profile of an Urban Vernacular*. University at Albany, State University of New York dissertation.

Borg, W. R. na M. D, Gall. (2003). *Educational Research: An Introduction* (Fifth Ed) New York: Longman.

Bradley, D. (2002) 'Language Attitudes: The Key Factor in Language Maintenance. In: Bradley D and Bradley M. *Language Endangerment and Language Maintenance*. London: Routledge.Curzon.

Brenzinger, M. (ed.) (1998) 'Endangered Languages in Africa' Köln: Rüdiger Kö http://portal unesco org/culture/es/files/8283/11195176347 Language _ Vitality_and_Endangerment.pdf [accessed 19. 03. 2013]

Brewer,J and A. Hunter (1989) *Multimedia Research: A Synthesis of Style*. Newbury Park CA: Sage

Brown, D. J.(2005). *Testing in Language Program*. New York: McGraw-Hill.

Bussmann, H. (1996) *Routledge Dictionary of Language & Linguistics*, Great Britain: Routledge

Canale, M. & M. Swain. (1980). *Theoretical Bases of Communicative Approaches to Second Language Teaching and Testing*. Applied Linguistics.Vol 1, pp1-47.

Canale, M. & M. Swain. (1981). ‘A Theoretical Framework for Communicative Competence’. In: Palmer, A., Groot, P., & Trosper, G. (eds.), *The Construct Validation of Test of Communicative Competence*, 31-36. Clevedon. Multilingual Matters.

Canale, M. (1983). ‘From Communicative Competence to Communicative Language Pedagogy’. In: Richards, J. C. & R. W. Schmidt. (eds.), *Language and Communication*, pp. 2- 27. London: Longman.

Canale, M. (1984).’A Communicative Approach to Language Proficiency Assessment in a Minority Setting’. In: Rivera, C. (ed.), *Communicative Competence Approaches to Language Proficiency Assessment: Research and Application*, 107-122.Clevedon.Multilingual Matters.

Clark, S.M. (1992) *Youth in Mordern Society*. New York: Winston Inc.

Chapelle, C. A. & G. Brindley. (2010). ‘Linguistic Competence Assessment’. In: Schmitt (ed.) *An Introduction to Applied Linguistics*. Hodder & Stoughton Ltd.pp 24 – 66.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, Massachusetts: The M.I.T. Press.

Creswell, J.W. (2003) *Research Design.* Thousand Oaks. C.A: Sage

Creswell, J.W. (2007) *Educational Research Planning and Evaluation: Qualitative and Quantitative Reserch* (2 ed) Ohio: Prentice Hall, Inc.

Creswell, J.W. na P.L.V Clark. (2011) *Designing and Conducting Mixed Method Research*. California U.S.A: Prentice Hall, Inc.

Crystal, D. (2000) *Language Death*. Cambridge: Cambridge University Press.

Crystal, D. (2010) *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cummins, J. (2009) *Bilingual Children’s Mother Tongue: Why is it Important for Education*. Toronto: Sprogforum. Online Version: http:// www. teachlearn. com/cumins/mother.htm

Denzin, K.N. & Y.S Lincoln. (2011) *The SAGE Handbook of Qualitative Research*. U.S.A: SAGE Publication, Inc.

Desai, Z. K. (1991). 'Democratic Llanguage Planning and the Transformation of Education in Post-Apartheid South Africa'. In E. Unterhalter, H. Wolpe & T. Botha (eds.), *Education in a Future South Africa* (pp 112 - 122). London: Heinemann.

Desai, Z. K. (1994). Acknowledging Diversity: The Need to Promote African Languages. *Per Linguam*, Vol.10 (1) pp. (41-49).

Desai, Z. K. (2012) *A Case for Mother Tongue Education?* South Africa. University of the Western Cape PhD thesis (Unpublished)

Deumert, A. et al. (2000). *Introducing Sociolinguistics.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Deumert, A. et al. (2005). *Language, Informal Networks and Social Protection*. *Global Social Policy, 5(3),* 303-328.

Eckert, P. (2003), Language and Adolescent Peer Groups. In: *Journal of Language and Social Psychology*, 22, 112-118
.

Evans B.A. **(**2012).*About.com's African History Site* http:// africanhistory. about.com/ od/kenya/ig/Kenya-Peoples/Kikuyu-Map.htm

Fasold, W.R. (1984) *The Sociolinguistics of Society: Introduction to Social Linguistics.* Padstow, Great Britain: T. J Press LTD.

Fielding, N. na J. Fielding. (1986) *Linking Data*. Bevery Hills: Sage

Fishman, J.A. (1991) *Reversing Language Shift: Theoretical and Empirical Foudations of Assistance to Threatened Languages*.Clevedon, England: Multilingual Matters Ltd.

Fishman, J.A. (ed) (2001) *Can Threatened Languages Be Saved? Reversing Language Revisted: A 21$^{st}$ Century Perspective*. Clevedon, England: Multilingual Matters

Flutcher, G. & F. Davidson. (2007). *Language Testing and Assessment: An Advance Resource Book.* New York, Routledge Taylor.

Frawley, W.J. (2003) *International Encyclopedia of Linguistics Vol 2*. London: Oxford University Press.

Furaha, J.H. (1991) *Matumizi ya Lugha Mjini Malindi: Jinsi Mielekeo Inavyoathiri Uteuzi wa Lugha.* M.A Thesis: Kenyatta University (Unpublished).

Gachiri, O. (2009) *Kenyan Language Ideologies, Language Endangerment and Gikuyu (Kikuyu):How Discourses of Nationalism, Education and Development have Placed a Large Indigenous Language at Risk.* Phd Thesis: The University of Arizona (Unpublished).

Gathenji, W.H. (1981) *The Morphology of the Verbal Extensions in Gikuyu*. M.A Thesis University of Nairobi (Unpublished).

Gathigia, M.G. (2010) *A Cognitive Linguistic Analysis of Gikuyu Euphemisms*. M.A Thesis Kenyatta University (Unpublished).

Giles, H. et al. (1977) 'Towards a Theory of Language in Ethnic Group Relations'. In: Giles, H. (ed) *Language, Ethinicity and Intergroup Relations*. Lodon: Academic Press. 307 – 348.

Githinji, P. (2008), Ambivalent Attitudes: Perception of Sheng and its Speakers. In: *Nordic Journal of African Studies*, 17, 2, 113-136.

Githiora, C. (2002), Sheng: Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? In: *Journal of African Cultural Studies*, 15, 2, 159-181.

Gray, D.E. (2009) *Doing Research in the Real World*. Lodon: SAGE Publication Ltd.

Green, J.C. (1989) 'Towards a Conceptual Framework for Mixed Methods Evaluation Designs'. *Education Evaluation and Policy Analysis* 11 (3) 255 - 274

Green, J.C. (2008) 'Is Mixed Methods Social Inquiry a Distinctive Methodology?' *Journal of Mixed Methods Research* 2(1). 7 – 22.

Grenoble, L. A. and J. Whaley (eds.) (2006). *Endangered Languages*. Cambridge: CambridgeUniversity Press.

Grimes, B.F. (ed). (2000) *Enthologue Language Vitality Categories.* Dallas: SIL International

Gunthrie, M. (1967) *The Classification of Bantu Languages*. Lodon: Dawson of Pall Mall.

Hale, J.L, B.J. Householder, & K.L Greene. (2002)' The Theory of Reasoned Action'. In: J.P. Dillard & M. Pfau (eds.), *The Persuasion Handbook: Developments in Theory and Practice* (pp. 259–286). Thousand Oaks, CA: Sage.

Halle, K. (1992) "On Endangered Languages and the Importance of Linguistic Diversity". In: Grenoble, L. A. and J. Whaley (eds.)(1998). *Endangered Languages*. Cambridge: CambridgeUniversity Press.

Heugh, K.et al.(2010). 'Multilingual Education in Ethiopia: What Assessment Shows About What Works and What Doesn't'. In: K.Heugh & T. Skutnabb-Kangas (eds.), *Implementing Mother Tongue Education: The Ethiopian Context.* (pp. 316-342). Clevedon: Multilingual Matters.

Hinton, L. and K. Hale. (ed). (2001) *The Green Book of Language Revitalization in Practice.* California: Academic Press

Hinton, L et al. (2002) *How to Keep Language Alive: A Common Sense Approach to One – on – 0ne Language Learning*, California: Academic Press.

Hudson, A. (2002) 'Outline of a Theory of Diglosia in International Journal of the Sociology of Language' (2002) Vol 2002 Issue 157 pg 1 – 48 Retrived from http://www.reference. global. Com/doi/abs/10.1515/ijs/2002.039.

Hymes, D. H. (1972). 'On Communicative Competence'. In: Pride, J. B., & Holmes, J. (eds.), *Sociolinguistics*, pp. 269-293. Baltimore, USA: Penguin Education, Penguin Books Ltd.

Ingram, D. E. (1985) "Assessing Proficiency: An Overview of Some Aspects of Testing." In: K. Hyltenstam & M. Pienemann (eds.), *Modelling and Assessing Second Language Acquisition.* Clevedon, Avon: Multilingual Matters Ltd.

Iraki, F. K. (2004) 'Cognitive Efficiency: The Sheng Phenomenon in Kenya'. International Pragmatics Association 14:1.55-68

Johnson, R.B. et al. (2007) '*Towards a Definition of Mixed Method Research'. Journal of Mixed Methods Research.* u.k 112 – 133.

Kamau, T.G. (1996) *The Major Phonological Processes of Kindia and Kigichugu Dialects of Gikuyu : A Comparative Study*. Kenyatta University M.A Thesis (Unpublished).

Kamwangamalu, N. (2007) 'One Language, Multi-Layered Identities: English in a Society in Transition, South Africa'. *World Englishes* Vol.26. No.3, 263-275.

Karanja, P. (2009) *Investigating Language Death: A Social Liguistic Analysis of Kiamu and Kimvita Dialects of Kiswahili in Kenya*. Koln, Germany: Lambert Academic Publishing.

Karanja, P. (2012) 'Kiswahili Dialects Endangered: The Case of Kiamu and Kimvita'. In: *International Journal of Humanities and Social Sciences*. Vol 2 No.17 pg 95-117.

Kartz, D. (1960) 'The Functional Approach to the Study of Attitudes'.*Public Opinion 24* pg 163 – 204.

Kebeya, H.U. (2008) *Lingistic Accomodation and Code Switching During Luo/Luhyia and Luo/Gussi Contact.* Kenyatta University, Ph. D Thesis (Unpublished).

Keniston. (1975) ‘Youth as a Stage of Life’ In: Havighurst, J.R and Dreyer, H.P (eds). *Youth.* U.S.A: The National Society for the Study of Education.

Kenya Institute of Education. (2011) *Kenya Primary School Syllabus Vol 2 (3rd Edition)*. Nairobi: Kenya Institute of Education

Kenya National Bureau of Statistics.(2010) 2009 Kenya Population and Housing Census:Population Distribution by Age, Sex and Adminstative Units (Vol 1c). Nairobi: Government Press.

Kerswill, P. (2000) “Children, Adolescents and Language Change”, In: *Language Variation and Change* 8.2, 177–202.

Khejeri, M. (2014) Teachers’ Attitudes Towards the Use of Mother Tongue as a Language of Instruction in Lower Primary Schools in Hamisi District, Kenya. In: *International Journal of Humanities and Social Science Vol. 4 No. 1pp. 75-85*

Kiessling, R. & M. Mous. (2004) *Urban Youth Languages in Africa*. Anthropological Linguistics Vol 46. No 3. pp 303 – 341.

Kioko, A.N. & M. J. Muthwii. (2001). ‘Demands of a Changing Society: English in Education in Kenya Today’. In: *Language, Culture and Curriculum*14(3).pp 201-213

Kombo, D.K. and D. Tromp. (2006) *Propasal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kothari, C. R. (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.

Krauss, M. (1992) “The World’s Languages in Crisis”. In: *Language* vol68.4-10: SIL International.

Kremnitz. et al. (1997) ‘The Language Continuum as a Pluridimensional Concept’. In: Amond U (ed). *Status and Functions of Language Varieties* pg 541 – 551

Lehmann, C. (2009) "Linguistic Competence: Theory and Epiry." *The Linguistic Review* 21 Germany: University of Erfurt pp175-210.

Landweer. (2000) ‘Indicators of Ethno Linguistic Vitality*’.* Notes on Sociolinguistics 5 pg 5 – 22 [ Online:http//www.s.l. org /socialx/ndg-lg-indicators.html]

Lune, H. et al. (2010) *Perspective in Social Research Methods and Analysis.* Thousand Oaks: SAGE Publication Inc.

Lewis, M.P and G.F Simons (ed). (2009) *Ethnologue: Languages of the World*, 16$^{th}$ edition. Dallas: SIL International.Online Version:http://www.ethonlogue.com

Mazrui, A.A. & A.M. Mazrui. (1998). *The Power of Babel*. Oxford, England: James Currey.

Mcmanara, T. (2000) *Language Testing*. Oxford, Oxford University Press.

Mbaabu, I. (1996) *Language Policy in East Africa: A Dependency Theory Perspective,* Nairobi: Educational Research Publication.

Mbugua,W.G. (1998) *Language and Gender: A Case Study in Social Semiotics of the Lexicon of Gikuyu Language*. Kenyatta University, M.A Thesis (Unpublished).

Mbwesa, K. J. (2006) *Introduction to Management Research: A Student Handbook*. Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi, Kenya.

McLaughlin, F. (2009), Introduction to the Languages of Urban Africa.In: F. Mc Laughlin (ed.), *The Languages of Urban Africa*, London: Continuum, 1-18.

McLaughlin, F. (2009) Senegal's Early Cities and the Making of an Urban Identity. In: F. Mc Laughlin (ed). *The Languages of Urban Africa*, London: Continuum,71-85.

Mesthrie, R. and W. Leap. (2000) *Language Contact: Maintenance, Shift and Death'.* In: Mesthrie, R, Swann. J, Deumert, A. and Leap. W. *Introducing Social Linguistic* PhiladelphiaJohn Bejamins pg 248- 278.

Michieka, M. (2012) 'Language Maintenance and Shift Among Kenyan University Students.'In: Bruce, C. and N. Rolle *Selected Proceedings of the 41st Annual Conference on African Linguistics*. pp164-170. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. www.lingref.com, document #2746.

Miller, K. (2005). *Communications Theories: Perspectives, Processes, and Contexts*. New York: McGraw-Hill.

Milroy, L. (1987) *Observing and Analyzing Natural Language*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Mkilifi, M. H. A. (1972), 'Triglossia and Swahili-English Bilingualism in Tanzania'. In: *Language in Society*. Vol. 1, No. 2 Cambridge University Press. pp. 197-213

Morse, J.M. (1991) 'Approaches to Qualitative – Quantitative Methodological Triangulation'. Nursing Research 40 pp 120 -123

Moseley, C. (ed.) (2010). *Atlas of the World's Languages in Danger, 3rd ed*. Paris, UNESCO Publishing. Online http:// www. unesco. org/culture/ en/endangered languages/atlas

Mous, M. (2009), The Development of Urban Youth Languages in Africa. In: M. C. Junyent (ed.), *Transferences: The Expression of Extra-linguistic Processes in the World's Languages*, Vic, Spain: Eumo Editorial, 215-232.

Muaka, L. (2009) *The dynamics of Language Use Among Rural and Urban Kenyan Youths*. University of Illinois. Ph.D dissertation.

Muaka, L. (2011) 'Language Perceptions and Identity Among Kenyan Speakers'. In: Eyamba, G.B et al *Selected Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics*, (ed) Somerville, MA Cascadilla Proceedings Project pp 217-230.

Muchemi, J.A. (2011) *Lexical and Morphosyntactic Attrition in Secondary School Students who Speak Gikuyu as* $L_1$. Kenyatta Universty: M.A Thesis (Unpublished).

Mugane. (1986) *Bantu Nominalization Structures (Gikuyu).* Ph.D Thesis University of Arizona (Unpublished) .

Mugenda, A.G. (2008) *Social Science Research: Theory and Principle*. Nairobi: Applied Research & Trainning Services.

Mugenda & Mugenda. (2012) *Research Methods Dictionary*. Nairobi: Applied Research & Trainning Services.

Muriuki, G. (1976) *The Kikuyu in the Pre- Colonial Period in Kenya before 1900*. Nairobi: East African Publishing House.

Muriuki, G. (1974) *A History of the Kikuyu 1500-1900*. Nairobi: Oxford University Press

Murray, S. (2002) 'Language Issues in South African Education: An Overview'. In: R. Mesthrie (ed.), *Language in South Africa* (pp. 434-438).Cambridge: C. U. P.

Mutahi, K.E. (1977) *Sound Change and the Classification of the Dialects of Southern Mt. Kenya*. Nairobi University: Ph. D Thesis (Unpublished).

Muthwii, M.J. (2002) Language Policy and Practices in Education in Kenya and Uganda: Perception of Parents, Pupils and Teachers on the Use of Mother Tongue, Kiswahili and English in Primary Schools. Nairobi:Phoenix.

Mwaro, A.G. (2002) ‘Mchango wa A.S Nabhany katika Utafiti na Utandaridhi wa Istilahi za Kiswahili’. Ktk: *Utafiti wa Kiswahili*. Maseno: Maseno University. Uk 49-56.

Mwihaki, A.N. (1998) *Loan Words and Nativization: A Generative View of the Phonological Adaptation of Gikuyu Loan Words*. Kenyatta University M.A Thesis (Unpublished)

Ngechu. M. (2004) Understanding the Research Process and Methods. An Introduction to Research Methods. Nairobi: Acts Press,

Ngure, K.K. (2012) *From Rendille to Samburu: A Language Shift Involving Two Mutually Unitwlligible Languages of Northern Kenya.* University of Nairobi: Ph.D Thesis (Unpublished).

Nicuolo, G. (1991) *Problems of Testing Communicative Performance*. Baltimore: University Park Press.

Njoroge, D. (1978) *Kikuyu Deverbatives and other Nominalizations*. Nairobi University M.A Thesis (Unpublished)

Nunn, R. (2005) "Competence and Teaching English as an International Language." *Asian EFL Journal* 7(3(6)). < http://www.asian-efl- journal.com/ September _05_rn.php>

Paton, M. Q. (2002) “*Qualitative Research and Evaluation Methods (3rdEdition)”.* London: Sage Publications.

Patrick, P. L. (2005) *Sociolinguistic Methods*. England: University of Essex

Pokorn, N. (2005) Challeging the Traditional Axioms: Translation into Mother Tongue. New York : John Bejamins.

Obiero, J.O. (2010) From Assessing Language Endangerment or Vitality to Creating and Evaluating Language Revitalization Programmes. In: *Nordic Journal of African Studies* 19(4) Leipzig, Germany pg 201-206.

Ochieng, W. R. (ed). (1989) *A Modern History of Kenya, 1895-1980*. Nairobi: Evans Brothers (Kenya) Ltd.

Ogula, P. A. (2005). *Research Methods.* Nairobi: CUEA Publications.

Okombo, O. (1993). “Language and Culture”. In: Kenya National Commission for UNESCO’s Seminar Paper on Culture (September, 1993).

Okwany, L. (1993) *Attitude of High School Students in Kenya Towards Learning of Kiswahili*. Canada: University of New Brunswick.

Omulando, C. (2004). *The Effect of Kiswahili on the Use of English as a Medium of Instruction in Kenya Secondary Schools.* Moi University M.Phil Thesis. (Unpublished)

Onweugbuzie et al. (2004) *Mixed Method Research: A Research Pradigim Whose Time Has Come.* Educational Reseacher 33(7) u.k 14-26.

Orodho, A. J. (2003) *Essentials of Educational and Social Sciences Research Method*. Nairobi: Masola Publishers.

Orodho, A. J. (2009) *Elements of Education and Social Science Research Method*. Maseno: Kanezja Publishers.

Rallis, S.F. (1994) ‘Qualitative and Quantitative Inquiries Are Not Incompatible: A Call for New Partnership’. In: Reichardt, C.F and S.F Rallis (eds) *The Qualitative – Quantitative debate:New Perspective* uk 85-95. SanFrancisco: Josey Bass

Republic of Kenya. (2009) *Kenya Population Census: Kenya National Bureau of Statistic, Nairobi*: Government Press.

Republic of Kenya. (2010). *The New Constitution of Kenya*. Nairobi: Government Press.

Ritchie, J & J. Lewis. (2003) *Qualitative Research Practice: A Guide for Social Sciences Students and Researchers*. Sage Publications: London.

Rubin, R.B. (1992) *Assessing Speaking and Listening Competence at the College Level: The Communication Competency Assessment Instrument*. Communication Education Vol 31, pp 9-18.

Ruhlen, M. (1996) *The Origins of Language: Tracing the Revolution of Mother Tongue*. Canada: John Wiley & Sons Inc

Sallabank, J. (2004) Language Revitalization: Issues and Outcomes. London: SOAS

Sankoff, G. (2001) ‘Linguistic Outcomes of Language Contacts’. In: Peter, T (ed) *Handbook of Sociolinguistics*. Oxford: Basil Blackwell (2001) pg 638 – 668

Savignon S,G. (1972) *Communicative Competence: An Experiment in Foreign Language Teaching*. Philadelphia: Center for Curriculum Development.

Sebba, M. (2011) 'Societal Biligualism'. In: Wodak, R (ed) *The SAGE Handbook of Sociology*, Lodon: SAGE Publication Ltd

.

Schilling, N. (2013) *Sociolinguistic Fieldwork*. Cambridge: Cambridge University Press.

Sheppard, B.H, J. Hartwick, & P.R .Warshaw.(1988) 'The theory of Reasoned Action: A Meta- Analysis of Past Research with Recommendations for Modifications and Future Research'. *Journal of Consumer Research*, 15, 325–343.

Skutnabb-Kangas, T. (1981) *Linguistic Genocide.* UK: Lawrence Erlbaum Associates.

Smeets, R .(2005) *UNESCO Activities for Safeguarding of Endangered Languages Intangible Heritage Section*: UNESCO. Paris [online:http://www. UNESCO. ru/files/docs/smeets text eng.pdf]

Sprenger-Tasch, M. (2003) "Attitudes Towards Luganda, Kiswahili, English, and Mother Tongue as Media of Instruction in Uganda". In: Thomas B. & Klaus-Uwe P. (eds.), *Motivation in Language: Studies in Honor of Günter Radden et al,* pp.347–366.

Thiba, M. (2000) 'We Speak Eleven Tongues: Reconsructing Multilinguisim in South Africa. In: Brock – Utne & R.K. Hopson (eds) Language of Instruction forAfrican Emanicipation: Focus on Postcolonial Context and Construction. pp 147 – 175 Cape Town: CASAS.

Thomason, J.A. (2005) *Language Contact: An Introduction*. Edinburgh: University Press Edinburgh.

Triandis, H.C. (1971) *Attitude and Attitude Change*. Illinois: John Willey and Sons Inc.

Tsunoda, T. (2006) *Language Endangerment and Language Revitalization: An Introduction*. German: Mouton De Gruyter.

United Nations. (2007) *Internatinal Conference on Language Development, Revitilization and Mulitilingual Education*. New York: United Nations.

UNESCO. (1953) *The Use of Vernacular Languages in Education*. Monographs on Foundations of Education.Paris:UNESCO.

UNESCO. (2005) 'Advocacy Kit for Promoting Multilingual Education: Including the Excluded Bangkok'. Bangkok: UNESCO http://unesdoc. unesco.org /015/ 0001541/152178. [accessed 25/08/2013]

UNESCO. (2007) 'Mother Tongue Based Literacy Programmes:Case Study of Good Practice in Asia'. Bangkok: UNESCO Asia and Pacific Regional Bureau for Education

UNESCO. (2009) Atlas on the World's Languages in Danger. http://www.unesco.org/culture/ich/index.php?=0026. [accessed 4/9/2013]

UNESCO. (2010) 'Why and How Africa Should Invest in African Languages and Multilingual Education: An Evidence and Practical Based Advocacy Brief'. Hamburg: UNESCO Institute of Longlife Learning.

Varennes, F. (1996) Language Minorities & Human Rights. Nertherlands: Martinus Nijhoff Publishers.

Varennes, F. (2001) A Guide to the Rights of Minorities & Language. Nertherlands: Martinus Nijhoff Publishers.

Verhoeven, L. (1992) "Assessment of Bilingual Proficiency."In: L. Verhoeven & J. H. A. L. de Jong (Eds.), *The Construct of Language Proficiency: Applications of Psychological Models of Language Assessment* (pp.124-136). Amsterdam: John Benjamins Pub.

Vigdis, F. (2003) *Plight of Mother Tongue in a Multiligual World*. Paris, UNESCO Publishing.

Wa Thiong'o, Ngugi. (1986) *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature.* London: James Currey.

Walker, R. (1982) " Measuring Language Attitude and Language Use". In: Notes on Linguistics Special Publication No. 2. Sociolinguistic Survey Conference.

Waithaka, M.N. (2010) *Mofolojia ya Manenomkopo ya Gikuyu kutoka Kiswahili: Mtazamo wa Fonolijia Leksia,* Kenyatta University M.A Thesis (Unpublished).

Wangechi, N.R. (1991) *The Acquisation of Gikuyu Syntactic Structures by Gikuyu Children Aged Between 3 and 5 years.* Kenyatta University M.A Thesis (Unpublished).

Wanyoike, K.S. (2002) *A Morphophonological Analysis of Gikuyu Verbal Affixes within Lexical Phonology.* Kenyatta University M.A Thesis (Unpublished).

Wendo, N. (2009) 'Language Policy in Kenya: Negotiation with Hegemony' *The Journal of Pan African Studies,* vol.3, no.1. pp 121 - 138

Wurum, S.A. (2002) ‘Strategies for Language Maintenance and Revival’.In: Bradley D and Bradley M. *Language Endangerment and Language Maintenance.* London: RoutledgCurzon.

Wyman, T.L. (2012) *Youth Culture*, *Language Endangerment and Linguistic Survivance*. Clevedon: Multilingual Matters..

Zuckermann, G. and M. Walsh (2011) ‘Stop, Revive, Survive: Lessons from the Hebrew Revival Applicable to the Reclamation, and Empowerment of Aboriginal Languages and Cultures’. Australian Journal of Linguistics Vol 3.

## Viambatisho

Kiambatisho I

**UMILISI WA LUGHA**

**MWONGOZO WA MASWALI YA MIJADALA YA KIMAKUNDI KWA WANAFUNZI**

1) a. Kati ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, ni lugha ipi ambayo mnaifahamu vyema zaidi au kuitumia kwa ufasaha zaidi katika mazungumzo. Toa sababu za kuifahamu lugha hii vyema.

   b. Je, ni lugha ipi ambayo hamfahamu vyema kati ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng? Toa sababu za kutoifahamu lugha hii vyema?

2) a. Je, nyote mnaweza kuzungumza kwa lugha ya Kikuyu kwa ufasaha?

   b. Iwapo jibu ni la, ni sababu zipi zinazomfanya msiifahamu lugha ya Kikuyu vyema? Toeni sababu zote zinazochangia hali hii.

   c. Je, mnafikiri matumizi yenu ya Kiswahili, Kiingereza na Sheng katika mawasiliano yanachangia kutofahamu kwenu vyema kwa lugha ya Kikuyu?

3) Ni stadi gani kati ya kuongea, kusoma na kuandika inayowatatiza zaidi mnapotumia lugha ya Kikuyu?

4) a. Je, lugha ya Kikuyu hutumika katika vyombo vya habari kama vile redio, runinga na Magazeti? Taja baadhi ya vyombo hivi.

   b. Je, nyinyi husikiliza, husoma ama hutazama idhaa za redio na runinga ama magazeti ya Kikuyu.

   c. Toa sababu za jibu lako kwa 4b.

5) Kunao umuhimu wowote wa kuifahamu vyema lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana mijini? Taja baadhi ya umuhimu huo.

Kiambatisho II

**MAZOEZI YA KUPIMA UMILISI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUONGEA**

**STADI YA KUSOMA**

1. Someni vifungu hivi vya ufahamu vilivyoandikwa kwa lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. (alama.20)

**STADI YA KUSIKILIZA na KUANDIKA**

2. Sikizeni kwa makini na mnakili vifungu vifuatavyo vya imla kama mtakavyosomewa katika lugha ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng. (alama. 20)

**STADI YA KUONGEA**

3. Wanafunzi watashirikishwa katika mijadala mifupi kuhusu mada itakayochaguliwa na mtafiti ili kupima uwezo wao wa kuongea na kujieleza katika lugha ya Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng. (alama. 20)

Kiambatisho III

**HOJAJI YA WANAFUNZI KUHUSU MIELEKEO NA MATUMIZI YA LUGHA.**

Mimi ni mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu athari za mielekeo ya lugha ya Kiswahili na lugha nyinine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Majibu yako kwa maswali yafuatayo yatasaidia sana utafiti huu.

Habari zozote utakazozitoa kwenye hojaji hii hazitafichuliwa kwa yeyote yule. Tafadhali yajibu maswali yote kikamilifu na kwa uaminifu uwezavyo.

**SEHEMU YA A: MAELEZO YA KIBINAFSI**

**1.KIDATO____________________** **TAREHE_____________________**

**2. UMRI** (Andika kwenye nafasi iliyotengwa)

------------------------------------------

**3. JINSIA**

☐ Msichana

☐ Mvulana

**4. LUGHA i) Lugha ya mama_______________________**

**ii) Nyingine 1.________________ 2. _____________ 3.________________**

**5. PAHALI PA KUZALIWA**

Mji /Mtaa ___________________________

## SEHEMU YA B: MIELEKEO YA LUGHA

**1. Onyesha kwa kuweka alama (√) kwenye lugha unayofikiria ni muhumu kwa shughuli zifuatazo.**

| | LUGHA | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **KIKUYU** | **KISWAHILI** | **KIINGEREZA** | **SHENG** |
| a. Kupata elimu au mafunzo shuleni. | | | | |
| b. Katika shughuli za biashara. | | | | |
| c. Kupata kazi baada ya shule | | | | |
| d. Kuzungumza na wazazi, watu wazima mtaani | | | | |
| e. Kuzungumza na wenzako. | | | | |
| f. Kufanya urafiki. | | | | |
| g. Mazungumzo nyumbani kwenu. | | | | |
| h. Kufahamu kuhusu utamaduni wako. | | | | |
| | | | | |

**2. Hapa kuna maelezo kuhusu Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng. Tafadhali sema kama unakubali au kutokubali maelezo haya. Weka mabano kwa nambari uliyochagua ifuatavyo:-**

**(1) Nakubali kabisa. (2) Nakubali. (3) Sikubali. (4) Sikubali kabisa.**

**Maswali**

**a**. Ni muhumu kwa vijana kufahamu lugha ya Kikuyu. **1 2 3 4**

Toa sababu za jibu lako

**b**. Kikuyu hutumika nyumbani kwetu kuliko Kiswahili, Kiingereza na Sheng. **1 2 3 4**
Toa sababu.

**c.** Hatutumii Kikuyu hata kidogo shuleni. **1 2 3 4**
Kwa nini? Fafanua.

**d**. Ni muhimu kufahamu Kiswahili, Kiingereza au Sheng kuliko Kikuyu **1 2 3 4**
Toa sababu za jibu lako.

**e.** Nahurumia vijana ambao hawakifahamu Kikuyu. **1 2 3 4**

Eleza sababu za jibu lako.

**f**. Vijana wanaozungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng wana hadhi ya juu **1 2 3 4**
kuliko wale wanaozungumza Kikuyu. Toa sababu za jibu lako.

**g.** Kuna wenzangu ambao hawakifahamu Kikuyu vyema vile wanavyofahamu **1 2 3 4**
Kiswahili, Kiingereza au Sheng.

Kiambatisho IV

**HOJAJI YA WANAFUNZI KUHUSU MAENEO YA KIJAMII YA MATUMIZI YA LUGHA.**

Mimi ni mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, idara ya Kiswahili. Ninafanya utafiti kuhusu athari za mielekeo ya lugha ya Kiswahili na lugha nyinine kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Majibu yako kwa maswali yafuatayo yatasaidia sana utafiti huu.

Habari zozote utakazozitoa kwenye hojaji hii hazitafichuliwa kwa yeyote yule. Tafadhali yajibu maswali yote kikamilifu na kwa uaminifu uwezavyo.

**SEHEMU YA A: MAELEZO YA KIBINAFSI**

**1.KIDATO____________________ TAREHE_____________________**

**2. UMRI** (Andika kwenye nafasi iliyotengwa)

------------------------------------------

**3. JINSIA**

☐ Msichana

☐ Mvulana

**4. LUGHA i) Lugha ya mama_______________________**

**ii) Nyingine 1._______________ 2. _____________ 3.________________**

**5. PAHALI PA KUZALIWA**

Mji /Mtaa __________________________

## SEHEMU YA B: MAENEO YA KIJAMII YA MATUMIZI YA LUGHA

**Onyesha kwa kuweka alama (√) kwenye lugha unayoitumia katika maeneo yaliyoorodheshwa hapa chini.**

**1. Ni lugha gani unayoitumia au watu wengine wanaitumia katika maeneo yafuatayo:**

| ENEO | LUGHA | | | |
|---|---|---|---|---|
| | KIKUYU | KISWAHILI | KIINGEREZA | SHENG |
| a. Unapozungumza na marafiki zako darasani pale shuleni. | | | | |
| b. Unapozungumza na marafiki zako nje ya darasa pale shuleni. | | | | |
| c. Unapozungumza na walimu pala darasani. | | | | |
| d. Unapozungumza na wafanyakazi wengine wa shule. | | | | |
| e. Unapozungumza na marafiki zako nyumbani. | | | | |
| f. Unapozungumzia wazazi wako nyumbani. | | | | |
| g. Wazazi wanapokuzungumzia pale nyumbani. | | | | |
| h. Wazazi wako wanapowasiliana pale nyumbani. | | | | |
| i. Unapozungumzia watu wazima mtaani. | | | | |
| j. Watu wazima wanapokuzungumzia mtaani. | | | | |
| k. Unapozungumza na babu au nyanya yako | | | | |
| l. Nyanya au babu anapokuzungumzia. | | | | |
| m. Watoto hujifunza lugha gani kwanza pale mtaani. | | | | |
| n. Mnatumia lugha gani mnapoenda kanisani ua mskitini pale nyumbani? | | | | |

**ASANTE**

Kiambatisho V

**MJADALA WA KIMAKUNDI**

Mtafiti: Hamjabo nyote?

Watafiti: Hatujambo sana.

Mtafiti: Asante sana….na karibuni katika kikao hiki. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja wenu amefika. Kuna yeyote ambaye hayupo?

Wahojiwa: La.

Mhojiwa III: Kila mtu amefika …tuko kumi na watano tayari.

Mtafiti: Nashukuru kila mmoja wenu kwa kufika kwa wakati tuliokubaliana. Pia ni matumaini yangu kuwa kila mtu atakuwa huru kushiriki na kuchangia katika majadiliano haya. Ama ni vipi?

Watafiti: Sawa.

Mtafiti: Haya basi wacha tuanze. Mimi naitwa Stephen Njihia Kamau, mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Niko katika idara ya Kiswahili na ninafanya utafiti kuhusu athari za Kiswahili, Kiingereza na Sheng kwa uthabiti wa kiisimujamii wa lugha ya Kikuyu miongoni mwa vijana wa jamii ya Kikuyu mijini. Kwa hivyo mjadala wetu jioni ya leo utahusu mada hii. Natumai kila mtu ako tayari kufikia sasa.

Watafiti: Tuko tayari.

Mtafiti: Haya basi… hebu tuanze. Hebu nifahamisheni, kati ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng ni lugha gani unayoifahamu vyema zaidi?

Mhojiwa I: Eeh….mimi nadhani ni Kiingereza.

Mtafiti: Huna uhakika ama…

Mhojiwa I: Nina uhakika …ni Kiingereza

Mtafiti: Kwa nini ? Kwa nini iwe ni Kiingereza wala sio Kiswahili, Sheng au hata Kikuyu?

Mhojiwa I: Hii ni kwa sababu…. Eeh …kusema kweli lugha ya Kiingereza ndiyo ninayoitumia kwa wingi shuleni tangu niliopokuwa mchanga kwanzia shule ya chekechea. Masomo mengi shuleni isipokuwa Kiswahili hufunzwa kwa Kiingereza. Hivi ndivyo nilipata kuifahamu lugha ya Kiingereza vyema zaidi kuliko lugha za Kiswahili, Kikuyu na Sheng.

Mtafiti: Asante kwa jibu lako la kina. Kuna mwingine kati yenu aliye na sababu tofauti ya kuifahamu lugha ya Kiingereza kuliko lugha za Kiswahili, Kikuyu na Sheng?

Mhojiwa II: Ndiyo. Mtu akiizungumza lugha ya Kiingereza kwa ufasaha huonekana akiwa wa 'class ya juu' miongoni mwa marafiki zake na hii ndiyo sababu iliyonifanya nipende kuitumia lugha ya Kiingereza kuliko lugha zile nyingine.

Mtafiti: Nini maana ya 'class ya juu'?

Mhojiwa II: Eee…hiyo…hadhi ya juu.

Mtafiti: Sawa. Inaitwa hadhi sio 'class'. Mwingine mwenye maoni tofauti?

Mhojiwa III: Mimi huifahamu lugha ya Kiswahili vyema zaidi kuliko lugha za Kiingereza, Kikuyu na Sheng.

Mtafiti: Aaa….Huyu naye anakifahamu Kiswahili zaidi. Kuna sababu zozote za kuifahamu lugha ya Kiswahili vyema zaidi kuliko lugha nyingine?

Mhojiwa III: Sababu kuu ya kuifahamu lugha ya Kiswahili vyema zaidi ni kuwa ndiyo lugha ambayo tunaitumia kwa wingi nyumbani kwetu na pia lugha hii inatumika hapa shuleni kwa wingi hasa nje ya darasa.

Mtafiti: Kuna mwingine kati yenu anayeifahamu zaidi lugha nyingine isipokuwa Kiingereza na Kiswahili?

Mhojiwa IV: Ndiyo. Sheng.

Mtafiti: Kwa nini?

Mhojiwa IV: Sheng ndiyo lugha ambayo huwa natumia zaidi nikiwa nyumbani tangu utotoni na ni lugha tamu kuzungumza. Hata hapa shuleni tunaitumia hata ingawa ni marufuku kuitumia. Pia Sheng inasaidia sana wakati tunaongea na marafiki zangu na hatutaki wazazi au watu wengine wazima waelewe kile tunachokisema.

Mtafiti: Imepigwa marufuku na bado unaitumia shuleni?

Mtafiti IV: Hahaha….wakati mwingine inabidi…ama ni aje nyinyi?

Mtafiti: Sawa. Naelewa. Haya. Swali lingine. Je? Kati ya Kikuyu, Kiswahili, Kiingereza na Sheng, ni lugha gani ambayo huifahamu vyema?

Wahojiwa: Kikuyu.

Mtafiti: Mnataka kusema kuwa nyote hamfahamu lugha ya Kikuyu hata kidogo?

Mhojiwa I: Sio hivyo…. Nafikiri si eti hatuifahamu lugha ya Kikuyu hata kidogo. Ukweli ni kwamba kati ya lugha za Kiswahili, Kikuyu, Kiingereza na Sheng, lugha ya Kikuyu ndiyo haifahamiki vyema na vijana wengi.

Mtafiti: Ok…Kunazo sababu maalum zinazokufanya usiifahamu lugha ya Kikuyu vyema kama unavyozifahamu lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng?

Mhojiwa: V: Kwanza kabisa mimi sijawahi kuitumia lugha ya Kikuyu tangu nilipozaliwa. Lugha ambayo nilijifunza kwanza ilikuwa Kiswahili kisha Sheng na baadaye Kiingereza nilipoenda shuleni.

Mtafiti: Unataka kusema kuwa hujawahi kuitumia lugha ya Kikuyu hata kidogo tangu ulipozaliwa? Inawezekana kweli?

Mhojiwa X: Ni kweli…

Mtafiti: Sawa lakini wacha aeleze yeye.

Mhojiwa V: Si eti sijawahi kuzungumza lugha ya Kikuyu. Nina maana kuwa mara nyingi mimi huzungumza Kiswahili, Kiingereza au Sheng kutegemea pahali nilipo ama wale ninaozungumza nao.

Mtafiti: Basi ni wapi wewe hutumia lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa V: Mimi huitumia lugha ya Kikuyu kwa nadra sana nikienda *ocha* (Neno la Sheng kumaanisha mashambani). Hata hivyo huwa sipendi kuzungumza Kikuyu kwa vile sikifahamu vyema na vijana wenzangu huko *ocha* hunicheka wanaposikia jinsi ninavyozungumza Kikuyu kisicho sanifu.

Mtafiti: Pole kwa hayo. Kuna mwingine kati yenu aliye na sababu tofauti ya kutoifahamu vyema lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa XI: Mimi nadhani kuwa siifahamu vyema lugha ya Kikuyu kwa vile kati ya hizi lugha nne Kikuyu ndiyo lugha ambayo ni ngumu kujifunza hasa kuongea na Kuandika.

Mtafiti: Ni ngumu kweli?

Mtafiti XI: Eeh….wewe hujui…ni ngumu sana. Kwa hivyo afadhali nitumie lugha nyingine ambazo ni rahisi kujifunza kama vile Kiswahili na Sheng.

Mtafiti: Kuna maoni mengine tofauti na haya?

Mhojiwa VI: Wazazi wangu hata ingawa wote ni Wakikuyu hupenda kutumia sana lugha ya Kiswahili na wakati mwingine Kiingereza wanapowasiliana nami au kati yao pale nyumbani. Basi sijawahi pata fursa ya kujifunza lugha ya Kikuyu hata ingawa mara kwa mara mimi hutamani kuifahamu vyema lugha ya Kikuyu.

Mtafiti: Inatokea wengi wenu hamkifahamu Kikuyu. Ni kwa nini nyinyi vijana mijini hamfahamu vyema lugha ya Kikuyu ikilinganishwa na lugha nyingine kama vile Kiswahili, Kiingereza na Sheng?

Mhojiwa I: Hatupati fursa kamwe ya kuongea wala kujifunza lugha ya Kikuyu hapa mijini. Hii ni kwa sababu lugha hii haitumiki shuleni na hakika huwa ni kinyume cha sheria za shule kwa mwanafunzi kuzungumza kwa Kikuyu ama lugha nyingine ya mama shuleni.

Mhojiwa XIV: Pia tukiwa nyumbani mara nyingi sisi hutumia lugha ya sheng kuwasiliana.

Mtafiti: Haya. Sababu nyingine..

Mhojiwa II: Pia sisi vijana hatupati fursa ya kutembea mashambani mara kwa mara na tunapoenda mashambani huwa ni kwa muda mfupi tu. Basi huwa hatupati wakati wakutosha wa kuingiliana na vijana wenzetu vijijini ambao wangetusaidia kuifahamu lugha ya Kikuyu.

Mtafiti: Je, matumizi ya lugha za Kiswahili, Kiingereza au Sheng yanachangia vipi kutofahamu kwako kwa lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa VII: Ndio. I mean…eee..Kwangu naona yanachangia kwa kiasi kikubwa.

Mtafiti: Fafanua. Kwa nini unayo maoni kama haya?

Mhojiwa VII: Hii ni kwa vile matumizi ya lugha nyingine kama vile Kiingereza na Kiswahili yanahimizwa sana hasa shuleni na hata wakati mwingine nyumbani. Jambo hili linatufanya kuwa na mielekeo kuwa hizi ndizo lugha muhimu tunazofaa kuzifahamu na hivyo lugha za mama kama Kikuyu hazina faida hata ukizifahamu.

Mtafiti: Ni stadi gani ya lugha kati ya kuongea, kusoma na kuandika inayokutatiza zaidi unapotumia lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa V: Sana sana ni stadi ya kuandika ikifuatwa na kusoma.

Mtafiti: Unakabiliwa na matatizo gani katika stadi hizi mbili unapotumia lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa V: Vokali nyingine za Kikuyu ni tofauti na zile za Kiswahili na Kiingereza ambazo tumezoea kuzitumia. Hivyo basi mtu hutatizika kuziandika na kuzisoma

Mtafiti: Vokali kama zipi hutatiza?

Mhojiwa V: Kwa mfano irabu kama vile i na i na u na u hukanganya mtu kwa vile hutamkwa karibu sawa lakini vokali i na u ni tofauti na zile za Kiswahili na Kiingereza. Tena hatujawahi kufundishwa jinsi ya kuziandika sauti za Kikuyu.

Mhojiwa II: Vile vile katika kusoma na kuongea mtu huathirika na kiimbo cha lugha ya Kiingereza na kwa hivyo yeye husoma lugha ya Kikuyu kama Kiingereza jambo ambalo hufanya mtu kuchekwa na watu.

Mtafiti: Je, kila mmoja wenu huelewa yanayosemwa akizungumziwa kwa Kikuyu?

Watafiti: Ndio......kusikia tunasikia

Mtafiti: Inatokeaje mko na shida katika stadi nyingine za lugha mnapotumia Kikuyu bali sio stadi ya kusikiliza?

Mhojiwa I: Siwezi kuelezea hayo.....sijui nilijifunzaje... lakini mimi husikia kile mtu anasema anaponizungumzia Kikuyu lakini siwezi kumjibu kwa Kikuyu. Mara nyingi mtu akiniuliza swali akitumia Kikuyu mimi humjibu kwa Kiswahili ama Kiingereza.

Mhojiwa IV: Mimi huwasikiliza wazazi wangu wakizungumza Kikuyu nyumbani na kwa hivyo nikaja kufahamu Kikuyu isipokuwa siwezi nikaandika, kusoma ama kuongea vyema nikitumia Kikuyu.

Mhojiwa III: Pia mtu husikia lugha ya Kikuyu ikizungumzwa katika redio.

Mtafiti: Redio kama zipi?

Wahojiwa: Inooro......

Mtafiti: Eii....mmoja mmoja..

Mhojiwa XV: Eeee....kama vile Coro, Kameme na Inooro...pole pole ukisikiliza unaanza kufahamu kile mtu anasema apozungumza kwa Kikuyu.

Mtafiti: Je, ni lugha gani nyingine ambayo hukutatiza unapoitumia?

Mhojiwa II: Lugha ya Sheng.

Mtafiti: Vipi? Fafanua.

Mtafiti II: Sheng hunitatiza katika stadi ya kuandika na kusoma.

Mtafiti: Fafanua jawabu lako tafadhali. Kwa nini stadi za kuandika na kusoma zinakutatiza unapotumia lugha ya Sheng?

Mhojiwa II: Lugha ya Sheng haifundishwi shuleni na pia huwa hata imepigwa marufuku. Kwa hivyo hatupati fursa ya kujua jinsi ya kuandika na kusoma Sheng kama vile tunavyofundishwa Kiingereza na Kiswahili shuleni. Hata hivyo hii ndiyo lugha ambayo sisi vijana hutumia kwa wingi tunapowasiliana kati yetu tukiwa nyumbani hapa mjini na kwa hivyo tunajua jinsi ya kuizungumza Sheng kutoka kwa vijana wengine wenzetu mtaani bila ya kufundishwa na yeyote.

Mtafiti: Je, lugha ya Kikuyu hutumika katika vyombo vingine vya habari kama vile runinga na magazeti? Taja baadhi ya vyombo hivi.

Mhojiwa XI: Ndiyo. Kikuyu hutumika katika redio na hata runinga.

Mtafiti: Idhaa hizi za redio na runinga ni zipi?

Mhojiwa II: Kuna idhaa za redio kama vile Inooro, Coro na Kameme FM.

Mhojiwa XIII: Pia kuna runinga inayotangaza kwa Kikuyu.

Mtafiti: Je, nyinyi kama vijana huwa mnasikiliza idhaa zinazotangaza kwa Kikuyu?

Wahojiwa: Hahaha......hapana...

Mtafiti: Hebu mmoja wenu afafanue.

Mhojiwa I: La. Mimi huzisikia tu wakati watu wengine wanapozisikiliza kama vile wazazi wangu nyumbani lakini mimi mwenyewe sizisikilizi.

Mtafiti: Kuna sababu za kutosikiliza idhaa za Kikuyu za redio na runinga?

Mhojiwa IV: Sababu ni kuwa vijana mijini hupenda kusikiliza redio zinazotangaza kwa Kiingereza na Kiswahili na hata Sheng kama vile Ghetto redio. Lugha hizi zinafahamika na vijana wote mijini ilhali sisi hatufahamu Kikuyu.

Mtafiti: Je, Kikuyu hutumika katika tarakilishi?

Wahojiwa : La!

Mhojiwa III: Lugha ya Kikuyu haina msamiati wa kuelezea masuala ya tarakilishi kama vile Kiingereza. Sidhani lugha ya Kikuyu itawahi kuwa lugha ya tarakilishi kwa sababu ni lugha iliyopitwa na wakati.

Mtafiti: Kunao umuhimu wa vijana kama nyinyi kuifahamu lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa II: Ndiyo. Lugha ya Kikuyu ina umuhimu mwingi hata kwetu vijana mijini. Hii ni kwa sababu lugha hii inaweza kutufahamisha kuhusu historia yetu kama vijana wa jamii ya Kikuyu. Kwa njia hii tunaweza kufahamu kuhusu asili yetu.

Mhojiwa V: Pia lugha ya Kikuyu ndiyo ambayo tunaweza kutegemea tunapoataka kufahamu kuhusu utamaduni wetu.

Mtafiti: Ni vipengele vipi vya lugha hii ambavyo vitakufahamisha kuhusu utamaduni wako?

Mhojiwa V: Kunavyo vipengele kama vile nyimbo za kitamaduni, hadithi, methali na vitendawili.

Mtafiti: Kunao umuhimu mwingine wa kuifahamu lugha ya Kikuyu?

Mhojiwa I: Umuhimu mwingine wa lugha ya Kikuyu ni kuwa lugha hii ndiyo tunayoitumia tunapotembelea sehemu za mashambani. Hii ni wakati tunapowasiliana na babu au nyanya, watu wazima na vijana pale mashambani ambao wengi wao husisitiza kutuzungumzia kwa Kikuyu.

Mhojiwa IV: Mara nyingi mtu huchekwa na vijana wenzetu kutoka mashambani kwa kushindwa kuzungumza Kikuyu inavyostahili jambo ambalo hunifanya niudhike.

Mtafiti: Pole kwa hayo lakini nanyi tieni bidii kuifahamu lugha ya Kikuyu ili kujiepusha na aibu kama hiyo. Mahojiano yetu yatafikia mwisho hapo. Asanteni.